

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 1 Juni, 2017**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI):**

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI):**

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Nishati na Madini juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu tutaanza na Mheshimiwa Devotha Mathew Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa ni sera ya Serikali kuboresha kilimo hapa nchini, ikizingatiwa kwamba kilimo kinatoa ajira kwa Watanzania kwa zaidi ya asilimia 80 na kilimo kimekuwa kikihudumia Watanzania kwa maana ya kujitosheleza kwa chakula, lakini kwa pia ni sera Serikali iliamua kuja na mikakati ya kuboresha sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na kutoa majukumu kwa mawakala wa pembejeo hapa nchini ili waweze kutoa huduma hizo za pembejeo kwa wakulima wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mawakala wa pembejeo wamefanya kazi yao kwa uadilifu mkubwa toka mwaka 2014/2015; 2015/2016 lakini mpaka sasa hivi mawakala hao hawajalipwa fedha zao.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sera ya Serikali kuwarusha mawakala ambao wamefanya kazi yao vizuri?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Watanzania, pia kwa Kambi ya Upinzani

inayoongozwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbewe, kwa kifo cha kiongozi wetu wa kisiasa toka Kambi ya Upinzani toka Chama cha CHADEMA Mheshimiwa Philemon Ndesamburo ambaye jana alitangulia mbele za haki, nitoe pole pia kwa mke na watoto wa marehemu, nitoe pole pia kwa Wabunge wenzangu kwa sababu Mheshimiwa Marehemu Ndesamburo tulikuwa naye hapa ndani ya Bunge. Nitoe pole pia kwa Watanzania wote kwa sababu tumempoteza kiongozi ambaye alionesha uwezo mkubwa wa kulitetea Taifa, alionesha uwezo mkubwa wa kusemea Watanzania kwa ujumla wake. Sote kwa pamoja tumuombe marehemu Mzee wetu Ndesamburo ili Mwenyezi Mungu aweze kuiweka roho yake mahala pema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kujibu swalii la Mheshimiwa Devotha Ninja, Mbunge wa Morogoro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba sera ya Serikali, moja kati ya mambo muhimu ni kuboresha kilimo na Serikali za awamu zote zimeendelea kufanya vizuri kwenye eneo hili kwa kusitiza kilimo na Serikali tunatambua kwa asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania tunategemea kilimo. Hata mpango wetu wa sasa wa Tanzania ya viwanda na uchumi wa viwanda unategemea kilimo zaidi ili kuendesha viwanda vyetu. Nikiri kile ambacho umesema Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapata msaada sana na Watanzania ambao wanajitoa katika kuunga mkono jithhada za Serikali kwa usambazaji wa pembejeo, kufanya kazi mbalimbali za kilimo na namna ambavyo wanajitahidi kuwa wavumilivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakiri kwamba ni kweli wanatudai, lakini katika hili nataka niseme ukweli kwamba tulipoanza mfumo wa utoaji wa pembejeo kwa njia ya vocha na kuwatumia hawa mawakala kutupelekea pembejeo hizi kwa wakulima kule vijijini, zipo dosari kadhaa ambazo tumeziona. Moja ya dosari kubwa ambayo tumeiona ni kwamba baadhi ya mawakala, wachache wamekuwa siyo waaminifu sana. Kwamba walikuwa wanashirikiana na watendaji wetu wa vijiji kule katika

kuorodhesha majina ya wakulima ambao si wakulima na hawapo, wamewapa mbolea, madawa na kudai fedha nyingi sana ambazo hazipo na tukajikuta tuna deni ya zaidi ya shilingi bilioni 65. Ninazo kumbukumbu kwa sababu hao mawakala wote nimekutana nao, tumekaa nao hapa tumejadili namna nzuri lakini tuliwaambia dosari hii kwa wachache wao na kwamba tumewahakikishia Serikali itawalipa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka tufanye jambo moja lazima tujiridhishe tuende kwenye vijiji kuititia watendaji ambao ni waaminifu kufanya uhakiki wa kama kweli pembejeo hizi ziliwafikia wakulima ili tueze kujua deni halisi. Nataka nikuhakikishie baada ya kuwa tumeanza uhakiki huo maana yake tumeshafanya uhakiki awamu ya kwanza. Kati ya shilingi bilioni 35 zilizookeana kwenye orodha ya madeni ya awali tulipata shilingi billioni sita tu ambazo Serikali inadaiwa. Lakini bado tuna shilingi billioni 30 nydingine ambazo sasa na kwa mujibu wa mazungumzo yangu na mawakala wote ambao walikuja hapa wiki mbili zilizopita tumekubaliana. Kimsingi kwanza, tumewasihi waendelee kuwa wavumilivu pia tumeshukuru kwamba wamekuwa wavumilivu kwa kiasi hicho. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu tufanye huo uhakiki ili tujue Serikali hasa inadaiwa kiasi gani ili tuweze kuwalipa. Nataka nikuhakikishie kwamba kazi hiyo inaendelea na tuko kwenye hatua za mwisho na tutawalipa madeni yote. Kila aliyefanya kazi vizuri kwa uaminifu, deni lake atalipwa kwa sababu hiyo ni stahili yake na kweli umefanya kazi nzuri ya kufikisha pembejeo kwa wakulima na tunatambua mchango wao na tutaendelea kuheshimu mchango wao. Ahsante sana. (*Makof*)

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, umekiri kwamba ni kweli Serikali inadaiwa, lakini umesema kwamba kuna dosari ambazo zimejitokeza katika uhakiki wa zoezi hilo na toka

mwaka 2014/2015 – 2015/2016 ni muda mrefu. Serikali kwa nini haiwezi kuona kwamba kuna haja sasa ya kuharakisha zoezi hilo kama watu wanastahiki zao wakalipwa kwa maana hivi sasa ninavyozungumza ziko taarifa kwamba kuna baadhi ya mawakala hivi sasa wameuziwa nyumba zao, kuna baadhi ambao hivi sasa wanashindwa kusomesha watoto wao shule na kuna baadhi ya mawakala ambao wamefariki kwa mshituko baada ya kuona nyumba zao zinauzwa na mabenki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kazi hii kama hawa watu mmewatambua na wamefanya kazi yao kwa uadilifi. Serikali kwenye hii Kamati ya kuandaa mawakala ilijumuisha Serikali wakiwemo wa TAKUKURU, Polisi, Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya. Sioni ni kwa nini uhakiki wa namna hii na ucheleweshaji wa namna hii kwa hawa watu ambao wamefanya kazi yao kwa uadilifi. Mheshimiwa Waziri Mkuu umetoa *commitment* kwa mawakala hawa kwa siku....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Minja muda wako unakwisha naomba uulize swali sasa ili uweze kujibiwa.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ultioa siku 25 kwamba zoezi hili la uhakiki liwe limefanyika Tanzania nzima kwa mawakala zaidi ya 940. Ni kwa nini mpaka sasa kwa miaka hiyo toka mwaka 2014 watu hawa Serikali haitaki kuwalipa haki yao ya msingi? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kupitia mazungumzo yetu kwa pamoja na mawakala wote tulitoa muda ambao tumejipanga kufanya uhakiki wa madeni yaliyobaki ili tuweke utaratibu wa kulipa na tarehe hiyo imeishia jana tarehe 31. Kwa hiyo, sasa nasubiri taarifa kutoka Halmashauri za Wilaya zote zitakazokusanywa kwenye ngazi ya Mikoa na Mikoa itatuletea takwimu na baada ya kupeleka Wizara ya Kilimo ikishapitia watapeleka Wizara ya Fedha na malipo hayo yatalipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba baadhi ya mawakala kwa mujibu wa mazungumzo yetu walieleza adha

hiyo ambayo wanaipata, lakini kupitia kauli hii wanaskia pia hata wale wadai kwamba, wale wote ambao watakuwa na madeni sahihi baada ya kuhakikiwa ni watu wema na ndio ambao pia tunajua tunatakiwa tuwalipe. Kwa hiyo, hakuna umuhimu wa kuharakisha kunyang'anya nyumba, na kufanya vitu vingine ni jambo la kuona kwamba taratibu hizi tunazozitumia ni taratibu ambazo zinaleta tija kwa Watanzania, zinaleta tija kwa Serikali kwa sababu tungeweza kupoteza mabilioni ya fedha ambayo yangeweza pia kusaidia kwenye miundombinu nyingine, lakini sasa tumbaini kwamba hayakuwa ya ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kutoa wito kwa watumishi wa Serikali wote ambao wamehusika katika hili ambao pia tutawabaini kwamba wao walihusika kwenye wizi, ubadhirifu na udanganyifu huo wote tutawachukulia hatua kali, hilo moja.

Pili, wale wote ambao wameshiriki katika hili, nirudie tena kuwashakikishia kwamba madeni hayo yakishathibitishwa kwamba fulani anadai kiasi fulani tutawalipa kama ambavyo tumetangaza, ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, baadhi ya walimu wenye ulemavu kutegemeana na ulemavu walionao wanahitaji vifaa maalum vya kujifunzia na kufundishia katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Vifaa hivyo ni pamoja na mashine za maandishi ya nukta nundu, shime sekio pamoja na vifaa vingine. Natambua kazi nzuri iliyofanywa ofisi yako pia Wizara ya Elimu kwa kutoa vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Bado tatizo lipo kwa walimu hasa kwa kuzingatia kwamba sio walimu wote wenye ulemavu wanaopangiwa kwenye shule zenye mahitaji maalum ambazo shule hizo zina vifaa hivi.

Je, wewe kama Baba na hasa kwa kuzingatia masuala haya ya watu wenye ulemavu yako chini ya ofisi yako, nini kauli yako ili kuhakikisha kwamba walimu hawa wanatekelezewa mahitaji yao na kutimiza majukumu yao pasipo matatizo yoyote? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina uratibu mzuri sana wa kuahakisha kwamba Watanzania wenzetu wenye mahitaji maalum wanapata huduma stahiki ili waweze kukamilisha shughuli zao za siku katika nyanja mbalimbali. Moja kati ya ushahidi kwamba jambo hili limeratibiwa vizuri Serikali zote zilizopita pamoja na hii ya Awamu ya Tano tumeweza kutenga Wizara inayosughulikia Watanzania wenzetu ambao wana mahitaji maalum. Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo mimi mwenyewe nipo, ndio hasa Wizara ambayo inashughulikia kwa ujumla wake, lakini tuna Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) zote hizi zinaratibu kwa namna ambavyo tumepanga utaratibu wa kufikisha huduma hii mahali hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hawa wote ambao wana mahitaji maalum, tunatambua kwamba wakati wote wanahitaji kujielimisha, kuititia taasisi na shule mbalimbali na kule wako waelimishaji ambao wanafanya kazi hiyo kila siku. Sisi tuna utaratibu kwenye maeneo haya ya vyuo, taasisi na shule mpango wa kwanza tumepeleka fedha za kuwahudumia pale ambapo wanahitaji huduma kulingana na mahitaji yake. Wako wale ambao hawana usikivu mzuri, uono hafifu, ulemavu wa viungo, wote hawa tumewaandalia utaratibu kwa kupeleka fedha kwenye Halmashauri ili waweze kuhudumiwa. Pia walimu ambao wanatoa elimu hii nao pia tumeweza kuwawezesha kwa kuwapa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kulingana na aina ya mahitaji ambayo tunayo.

Pia walimu hawa tunawapeleka semina mara nyingi kuhakikisha kwamba na wao pia wanapata elimu ya kisasa zaidi ili kuweza kuwahudumia vizuri hawa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lini Serikali itajiimarisha katika kutoa huduma hii ni kwamba Serikali imeandaa kituo cha *Msimbazi Center* kuwa ni eneo la kukusanya vifaa ambavyo tunavisambaza kwenye shule na taasisi zote ili viweze kutumika katika kufundishia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie pia Jumanne wiki ijayo napokea vifaa vingi sana vya elimu kule Dar es Salaam ambavyo vimeletwa kwa ajili ya kupeleka kwenye shule zetu za msingi. Miongoni mwa vifaa ambavyo pia tutakabidhiwa siku ya Jumanne ni pamoja na vifaa vya Watanzania wenzetu walioko vyuoni, kwenye shule ambao wana mahitaji maalum.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Amina Mollel na tunajua jitihada zako za kusemea sana eneo hili kwamba Serikali iko pamoja, Serikali inaendelea kuratibu vizuri na niendelee kuhakikishia kwamba Serikali itaendelea kuratibu na kuhakikisha kwamba vifaa vya kujifunzia na kufundishia vitapatikana na hawa waelimishaji wanapata elimu ya mara kwa mara ili waweze kuwasaidia hawa wenzetu ambao wana mahitaji maalum. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, vilevile naishukuru sana Serikali yangu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri yenyenye kutia moyo na faraja kwa watu wenyenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swalii dogo la nyongeza na swalii hili ni kwa mujibu wa Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu ambao katika kifungu cha 3 (12) chenye vipengele vya (a), (b), (c) na (d) vinatambua na vinasisitiza na kusema kwamba, nitanukuu kidogo; "kutambua kuwa ni haki ya watumishi wenyenye ulemavu kupatiwa mahitaji yao muhimu kama vile vifaa vya kuwaongezea uwezo, fedha kwa ajili ya matibabu na ukarabati wa afya zao (*rehabilitation*), nyenzo na vifaa hivi vitolewe na waajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninataka kupata kauli yako Mheshimiwa Waziri Mkuu, baadhi ya waajiri hawatekelezi majukumu haya kwa watumishi wa umma wenye ulemavu. Kama baba mwenye dhamana, nini kauli yako kwa waajiri wasiotimiza wajibu wao kama Mwongozo wa Utumishi wa Umma unavyowataka kutekeleza mahitaji hayo kwa watumishi wa umma wenye ulemavu? Ahsante.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo ameeleza kwamba, uko mwongozo wa Serikali juu ya Watumishi wa Umma wanaofanya kazi kwenye taasisi zetu za Serikali, lakini pia sio Serikali tu, hata taasisi zisizokwu za kiserikali, unawataka waajiri wote wanapowaajiri wenzetu ambao wana mahitaji maalum lazima watekelezewehi mahitaji yao ili kuwawezesha kufanya kazi yao vizuri. Kwa maana hiyo, kwa upande wa Serikali Wizara zote ziko hapa, Mawaziri wako hapa, Makatibu Wakuu wanaisikia kauli hii na kwamba lazima sasa watekeleze mahitaji na matakwa ya Serikali ya kuwashudumia hawa watumishi wenye mahitaji maalum kulingana na sekta zao. Kama yeye yuko upande wa ukarani, basi wahakikishe ana vifaa vyakatosha kumwezesha kufanya kazi hiyo vizuri na hivyo kila sekta lazima apate huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa wito kwa sekta binafsi kutoa nafasi zaidi za ajira kama ambavyo Serikali tunawaajiri wenye mahitaji maalum. Hakuna sababu ya kukwepa kuwaajiri ati kwa sababu unatakiwa kuwashudumia. Wote ni Watanzania na wote wana uwezo na tumethibitisha uwezo wao, pia hata Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, kuthibitisha kwamba sera hii ni yetu ndani ya Serikali ametoa ajira, ameteuwa watumishi ambao wana mahitaji maalum na hawa wote mahali pao pa kazi wanawezeshwa kwa vifaa vitakavyowawezesha kufanya kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie tutaeendelea kuajiri ndani ya Serikali na ninatoa wito kwa sekta binafsi ziaziji Watanzania wenzetu wenye mahitaji maalum wote ambao tunaajiri, wenye mamlaka ya kuajiri, na

Mwenyekiti wa Tume ya Ajira yuko hapa wa Chama cha Waajiri yuko hapa, asikie ili awaelekeze wenzake kwamba, ni wajibu wa kila muajiri kuwawezesha wenyewe mahitaji maalum kufanya kazi zao baada tu ya kuajiri, kama ambavyo Sera ya Serikali inahitaji kufanya hivyo. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Naomba kwanza kabla sijaauliza swali langu niipongeze Serikali chini ya Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi illvyoshughullikia suala zima la vyeti *fake* pamoja na watumishi hewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Serikali ilifanya maamuzi ya kuzuia kusafirisha mchanga wa dhahabu nje ya nchi, katika kufanya hivyo Serikali itakuwa imepoteza dira katika demokrasia ya kiuchumi duniani, lakini si hivyo tu itakuwa pia imeleta mahusiano ambayo si mazuri na nchi mbalimbali duniani. Nini tamko la Serikali kuhusu jambo hili? (*Makofii*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli sasa tuko kwenye matarajio ya kupata taarifa iliyo kamili kwenye sakata la mchanga na nataka nizungumzie eneo ambalo umehitaji zaidi la nini Serikali inatamka juu ya hili ili kuwaondolea hofu wawekezaji wetu wale waliowekeza kwenye maeneo ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni Watanzania wenye waliordesha hofu kubwa kwa kipindi kirefu, hata Waheshimiwa Wabunge katika michango yenu mbalimbali

kwa miaka iliyopita, hata pia katika kipindi hiki cha Serikali hii ya Awamu ya Tano mmeendelea kuitaka Serikali ichukue hatua thabiti na kutaka kufanya uchunguzi wa kina juu ya mchanga unaotoka nchini kupeleka nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli amelitekeleza hilo pale ambapo alinituma mimi mwenyewe kwenda Kahama, kwenda kuona zoezi la ufungashaji wamchanga na kuuona mchanga huo, lakini nilipompletea taarifa akaamua kuunda Tume na aliunda tume mbili, moja ya kwenda kuukagua mchanga wenyewe na kujua ndani kuna nini, lakini ya pili, ni ile Tume ambayo inahakiki, itatoa taarifa ya madhara ya kiuchumi, lakini pia madhara ya kisiasa kwa ujumla na mahusiano kwa ujumla wake. Mpaka sasa tumepata taarifa moja na bado tunasubiri taarifa ya pili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nataka nitumie nafasi hii kuwasihii wawekezaji wote, kwanza wasiwe na mashaka kwa sababu, lengo la Serikali ni kujiridhisha tu kwamba, je, mchanga huu unaosafirishwa kwenda nje una nini? Na wala hatubughudhi uzalishaji wao. Baada ya kuwa tumepata taarifa ya kwanza, bado hatua kamili hazijachukuliwa, tunasubiri taarifa ya kamati ya pili, baada ya hapo sasa Serikali itakaa chini na kutafakari kwa kupata ushauri kutoka sekta mbalimbali za kisheria, za kiuchumi na maeneo mengine hatua gani tuchukue. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niendelee kuwatoa hofu wawekezaji wale walioko kwenye sekta ile ya madini wawe watulivu. Hatuna jambo ambalo tumelifanyia kazi dhidi ya hatua ambazo tumechukua ndani ya nchi kwa watu wetu ambao tunao ambaao tuliwapa dhamana ya kusimamia hilo, lakini wawekezaji wote waendelee na shughuli zao za uwekezaji kama ambavyo tumekubaliana, wale ambaao wako kwenye mchanga kwa sababu juzi wameambiwa watulie, watulie, hakuna jambo ambalo litafanywa ambalo halitatumia haki, ama litaenda nje ya haki au stahili ya mwekezaji huyo na kila kitu kitakuwa wazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pia nitoe pia rai hata kwa Watanzania wawe watulivu. Tumeona watu wanatoa matamko wakidhani labda kuna uonevu, hapana! Watu watulie wasubiri majibu ya Serikali ambayo yatalinda haki ya kila mwekezaji, lakini na sisi pia Watanzania ambao tunaona tuna rasilimali zetu, hatuhitaji hizi rasilimali zipotee hovyo, lazima tuwe na uhakiki. Katika hili naomba mtuunge mkono Serikali kwa sababu kazi tunayoifanya ni kwa manufaa ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakiki huu ni kwa manufaa yetu Watanzania, ili tuwe na uhakika wa matumizi sahihi ya rasilimali zetu nchini. Kwa kufanya hilo tutakuwa tunajua tunapata nini na pia tujue tunaratibu matumizi yake na sisi Wabunge nadhani ndio hasa wahusika kama wawakilishi wa wananchi, twende tukawatulize wananchi waache kutoa matamko wasubiri Kamati zile. Pia tuzungumze na wawekezaji wetu ili nao pia wawe watulivu, bado Kamati ya pili hajatoa taarifa, baada ya hiyo maamuzi yatafanyika. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwa kuwa tatizo hili la upimaji wa mchanga linaanzia kule ambako ndiko kuna machimbo yenye. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kule *origin source* kunawekwa mashine ambazo sasa tatizo hili halitajirudia tena? (*Makofii*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja katika ya mikakati ambayo tunayo ni kupokea wawekezaji na tumeanza kuona wawekezaji kadhaa wakija kuonesha nia ya kuwekeza kwenye eneo hili. Awali kulikuwa na usiri mkubwa wa namna ya kuwakaribisha wawekezaji hawa kuwekeza kujenga mitambo hii na ndio kwa sababu Serikali imeanza kuchukua hatua za awali kwa vile tunajua kwamba, kuna maeneo ambayo yalikuwa hayaoneshwi wazi ikiwemo na eneo la kuwakaribisha wawekezaji wa kujenga mitambo hii hapa nchini.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Baada ya muda mfupi kama ambavyo mambo yameanza kujitokeza tutaamua kuwekeza, kujenga mashine zetu hapa hapa nchini au kuwakaribisha wawekezaji au kuona uwezo wa Serikali kama tunaweza ili sasa tuweze kutatua tatizo ambalo linatukabili sasa la kupoteza mchanga ambao tunautoa hapa na kupeleka nje kwa ajili ya uyeyushaji na kupata aina mbalimbali za madini. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa majibu, ahsante sana. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaeendelea na maswali ya kawaida, tunaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 317

**Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji Kulipwa  
Mishahara au Posho**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Serikali ina mpango gani wa kuwalipa posho au mishahara Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ili kurahisisha ufanisi wa shughuli zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA  
SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inathamini na kutambua kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa katika maendeleo ya Taifa. Serikali imezingatia na kuweka utaratibu wa kushirikisha viongozi hawa wanaolipwa posho maalum kwa motisha kupitia asilimia 20 ya mapato yanayorejeshwa na Halmashauri kwenye vijiji. Asilimia 17 ya fedha hizo zinatakiwa kutumika kwa shughuli za utawala, ikiwemo kulipa posho ya Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa na asilimia tatu kwa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kuboresha utaratibu huu kwa kuingiza katika mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ili kuweka utaratibu mzuri wa urejeshaji wa asilimia 20 kwenye vijiji na kuwanufaisha walengwa. Aidha, tumeimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri zote ili kujenga uwezo wa kutenga asilimia 20 kwenda kila kijiji.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wanafanya kazi nzuri na imekuwa ikiwategemea kwenye kazi zote na hata kualika mikutano yote ya Wabunge, Madiwani na kufanya kazi kubwa, asilimia 20 ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja katika majibu yake ya msingi haijawahi kupelekwa hata siku moja.

Je, kwa nini sasa Serikali isilet namna nzuri ya kuwalipa moja kwa moja hawa Wenyeviti kwa sababu, ni viongozi ili pasiwe na utaratibu huu wa asilimia ambayo haijawahi kupelekwa tangu wameanza kazi hizi mpaka sasa? (*Makof*)

Swali la pili, kwenye swali langu la msingi nilieleza habari ya Madiwani. Madiwani kimsingi wanapata posho ndogo ya shilingi 300,000 na kitu kama sikosei. Je, ni lini sasa mnaongeza posho hizi ili walau basi wafanye kazi nzuri katika chini ya Halmashauri zetu huko Wilayani? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nafahamu *concern* ya Mheshimiwa Flatei, lakini jambo hili sio la Mheshimiwa Massay peke yake, naamini Wabunge wengi sana wanaguswa na jambo hili. Na ndio maana unaona Mheshimiwa Massay alivyosimama hapa watu wengi sana, kila mtu alismama kutaka kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu naomba niseme ni kweli, kuna baadhi ya Halmashauri hizi posho hazirudi, lakini Halmashauri nyingine zinafanya vizuri katika urejeshaji wa posho hii ya asilimia 20. Ndiyo maana sasa tumesema katika mpango wetu wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura Namba 290, tumeweka kifungu maalum ambacho kinampa Waziri mwenye dhamana na jambo hilo kuweka suala zima la *regulation* maalum ya kulisazimisha suala hili sasa liwe suala la kisheria sio suala la kihiyari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni kwamba utaratibu wetu katika jambo hili mimi ninaamini si muda mrefu sheria hiyo ya fedha itakuja hapa, tutaifanyia marekebisho, sasa itakuwa ni muarobaini na katika hili naomba niwasihii kwa hali ya sasa hasa Wakurugenzi wetu wote kwamba asilimia 20 kupeleka kila kijiji sio jambo la hiyari ni jambo la lazima sasa tulipeleke ili wananchi wetu kule chini waweze kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ajenda ya posho ya Madiwani, ninakumbuka kwamba tulikuwa na Tume Maalum hapa ilikuwa maarufu kama Tume ya Lubeleje ambayo ilipitia maeneo mbalimbali na bahati nzuri Mheshimiwa Mzee Lubeleje amerudi tena Bungeni kama *Senior MP*, ilipendekeza mapendekezo mbalimbali, ndio maana tumesema kwa nyakati mbalimbali kwamba, Serikali inaangalia jambo hili na jinsi gani utaratibu wetu wa mapato utakuwa vizuri basi tutafanya marekebisho kwa kadri itakavyowezekana. (*Makofii*)

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Na mimi niseme tu kwamba mimi ni mionganoni mwa Wenyeviti wa Tanzania wa Serikali ya Mtaa wa *Vodacom* Kata ya Chanji kwa hiyo, ninaloliuliza ninalijua na changamoto zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya Serikali inayotengwa watekelezaji wa kwanza ni Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji, kauli hii ya kwamba wataanza kulipwa posho sio mara ya kwanza ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba *time frame* ni lini sheria italetwa hapa ili Wenyeviti waanze kulipwa posho kwa sababu sio hisani wanafanya kazi kubwa? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Dada yangu, Mheshimiwa Aida, Mbunge wa Viti Maalum, Iakini Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, kama walivyokuwa Wenyeviti wengine wa Jimbo la Ukonga kule nikifahamu hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema hapa kwamba kwanza kulikuwa na uzembe. Naomba niseme kwamba hata ile asilimia 20 kama kungekuwa na *commitment* ya kurudi vizuri katika Halmashauri zetu, maana sasa hivi tunapozungumza kuna Halmashauri nyingine zinafanya vizuri katika hilo. Tuna baadhi ya ushahidi kuna Halmashauri nyingine Wenyeviti wake wa vijiji wanalipwa vizuri kutokana na kwamba wameweka *commitment* ya asilimia 20 lazima irudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la *time frame* ni kwa sababu ni suala la sheria ni suala la kimchakato na taratibu zote sheria hii imeshapitia hivi sasa inaenda nadhani katika Baraza la Mawaziri kupitia katika vifungu mbalimbali, ikishakamilika itakuja humu Bungeni. Sasa niwaombe Waheshimiwa Wabunge sheria ikija humu tunawaomba tushiriki wote kwa pamoja vizuri kwa sababu,

ina vifungu vingi sana vinazungumzia suala la mapato katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kwamba tutajadili kwa kina tuje kuangalia jinsi gani tutafanya marekebisho mazuri ambayo yataenda kuwagusa Wenyeviti wetu wa Serikali za Vijiji kuweza kupata ile posho yao kwa kadiri inavyostahiki. (*Makof*)

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwa na sheria ni zuri kwa upande mmoja, lakini kwa upande wa pili Halmashauri zetu zinakabiliwa na matatizo makubwa ya kiuchumi. Sasa Serikali inatoa tamko gani kuhusu kuziwezesha Halmashauri zetu hizi kuweza kukusanya pesa za kutosha illi ziweze kuwalipa watu hawa ambao ni muhimu sana kwenye maendeleo ya vijiji vyetu? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la ukusanyaji wa mapato la Halmashauri kuwa katika hali ngumu ya uchumi, kwanza ni *commitment* yetu wote Wabunge na Madiwani kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu zikusanye vizuri. Kwa sababu, mionganoni mwa kigezo kimojawapo cha *existence* ya Halmashauri lazima iweze kukusanya mapato ndiyo maana imepewa ridhaa kuwa Halmashauri kamili. Katika hili sasa ndiyo maana katika kipindi hiki kilichopita tumetoa maelekezo mbalimbali katika suala zima la ukusanyaji wa mapato, hasa kutumia mifumo ya *electronic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, katika maeneo mbalimbali tunasuccess story kwamba leo hii kwa kutumia mifumo ya *electronics* tumepata mafanikio makubwa. Sasa maelekezo yangu nadhani twende katika *compliance* vizuri katika matumizi mazuri ya hii mifumo, kuna mahali pengine mifumo ipo, lakini haitumiki vizuri, watu wana-divert kutoka katika

mifumo ya ukusanyaji wa mapato hivi, mifumo ile sasa inajukana ipo, lakini wengine hawapati manufaa katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwasih sana Wakurugenzi wote katika Halmashauri zote twende kuhakikisha kwamba katika idara zetu za fedha tunazisimamia vizuri. Lengo kubwa ni kwamba, mapato yaliyopangwa kuititia Mabaraza ya Madiwani yaende kukusanya vizuri ili tukuze mapato katika Halmashauri zetu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso

Na. 318

### **Wilaya ya Chemba Kutokuwa na Hospitali**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO (K.n.y. MHE. JUMA S. NKAMIA)**  
aliuliza:-

Wilaya ya Chemba haina hospitali jambo linalowalazimu wananchi wake zaidi ya laki tatu kwenda kupata huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Kondoa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuhakikisha Wilaya hiyo inapata hospitali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba imetenga kwa kupima eneo la ekari 23.7 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali ya Wilaya. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri imeomba maombi maalum ya

shilingi bilioni mbili ili kuanza ujenzi wa hospitali hiyo. Aidha, upo mpango wa kukopa kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kufanikisha ujenzi wa hospitali hiyo kwa awamu. Ofisi ya Rais - TAMISEMI itashirikiana na Halmashauri ya Chemba ili kuhakikisha mipango ya ujenzi wa hospitali hiyo unafanikiwa. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Moshi Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kwa majibu ya Serikali ambayo yana matumaini ya ujenzi ya Hospitali ya Wilaya.

Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali iliahidi na mipango yake inachukua muda mrefu, je, Serikali ina mpango gani wakati inajipanga kuweza kukiboresha kituo cha afya cha Hamai ili kiweze kutoa huduma nzuri sambamba na kuchimba kisima ambacho ni tatizo kwenye eneo la kituo hicho cha afya?

Swali la pili, kwa kuwa matatizo ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ni sawa na tatizo lilioko kwenye Wilaya ya Tanganyika na Naibu Waziri analifahamu hili. Serikali iliahidi kujenga kituo cha afya Majalila. Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa kujenga kituo hicho cha Majalila?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi Rais - TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Halmashauri ya Chemba tunao huu mpango wa kuhakikisha tunajenga Hospitali ya Wilaya. Kwa vile changamoto ya Jimbo la Chemba ni kubwa ndiyo maana Serikali katika mpango wake wa kuboresha vile vituo vya afya 100, kituo cha afya cha Hamai ni mionganoni mwa vituo vya afya ambacho tunaenda kukiwekea ufanisi mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ambapo imani yangu ni kwamba si muda mrefu mchakato huo utaanza.

Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie kwamba kwa wananchi wa Chemba na hili tumeshaongea na Mheshimiwa Nkamia kwamba tutafanya kila liwezekanalo katika kipindi kifupi kijacho tutaenda kukiboresha kile kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la Wilaya ya Tanganyika Mheshimiwa Mbunge unafahamu tulikuwa wote Tanganyika nilivyokuja Jimboni kwako. Tuliitembelea Makao Makuu yako na Wilaya yako ya Tanganyika ambayo ni mpya, ndiyo maana tumpanga katika mpango wa kuboresha Wilaya hii katika eneo la Majalila kile kituo cha afya ambacho kinasuasua sana tutamekiingiza katika mpango wa vituo vya afya 100.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba nikuhakikishe kwamba wananchi wa Tanganyika wawe na imani kwamba Serikali inaenda kufanya *investment* kubwa eneo lile ili wananchi wa Tanganyika wapate huduma nzuri za afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda swali la nyongeza.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwa kuniona.

Matatizo yanayowakabili wananchi wa Wilaya Chemba kwa kukosa huduma za Hospitali za Wilaya yanalingana kabisa na ya Wilaya ya Malinyi ambapo wananchi hawana Hospitali ya Wilaya. Halmashauri ya Malinyi imeweka utaratibu kuomba TAMISEMI kuifanya Hospitali ya Lugala ambayo inamilikiwa na taasisi ya kidini kuwa Hospitali ya Wilaya, lakini ombi hilo na utaratibu huu TAMISEMI wamesimamisha.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa haraka wa kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Malinyi kupata hospitali ya Wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ukiangalia Ulanga, Malinyi wana changamoto kubwa ya sekta ya afya. Katika mpango wa haraka Mheshimiwa Mponda, naomba nikuhakikishie kwamba kuna kituo cha afya cha Mtimila ambacho tumekiwekea kipaumbele tunakuja kukiwekea miundombinu muda si mrefu, kuanzia huu mwezi wa sita kwenda mwezi wa saba inawezekana mchakato huo utanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishe wananchi wa Malinyi kwamba Serikali imewaona, tutaenda kufanya kazi kubwa pale ambayo mtakuja kuona ikifika mwezi wa nane hapo Mungu akijalia, inawezekana hali ikawa ni tofauti wananchi watakwenda kupata huduma nzuri sawa sawa na kituo cha afya cha Lupilo katika Jimbo la Ulanga (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi swalii la nyengeza.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuwa hii hospitali ya Wilaya ya Kondoia inahudumia Halmashauri tatu; na kwa kuwa imepata ufinyu mdogo sana wa bajeti na kuleta changamoto katika madawa na vifaa tiba. Sasa Serikali inaona lini wakati inafikiria kuwapatia watu wa Chemba hospitali yao, hospitali hii ikaongezewa bajeti ili kuweza kuhudumia vyema Wilaya hizi tatu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kondoia changamoto ni kubwa na ndiyo maana ukiangalia kuna Majimbo matatu tofauti ambayo ni Chemba, Kondoia Vijijiini na Kondoia Mjini lakini hospitali inayotumika sasa hivi ni Hospitali ile ya Kondoia na ukiangalia *population* mpaka watu wengine kutoka katika wilaya *especially* kama Wilaya ya Hanang' walioko mpakani wengine wanakuja hapa Kondoia.

Kwa hiyo, jambo hili ni kubwa na tumeliona ndiyo maana katika mpango wetu wa bajeti wa mwaka huu sasa hasa ukiangalia *basket fund* tumebadilisha utaratibu wa *basket fund* tumeongeza bajeti katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kuangalia ni jinsi gani tutafanya ili wananchi wapate huduma. Hata hivyo tumetoa maelekezo maeneo mbalimbali, kwa mfano tuna Halmashauri ya Kondo Mji na Halmashauri ya Kondo Vijiji lakini hospitali ni moja. Nimewahitaji Wakurugenzi wa maeneo yale waangalie katika suala zima la *basket fund* katika Halmashauri ambapo ile hospitali iko na jinsi gani kufanya kwa kuweka utaratibu wa kusaidia ile hospitali angalau kwa hali ya sasa iweze kufanya vizuri kwa sababu wananchi wote wanaohudumiwa ni watu kutoka maeneo hayo ambapo ni hospitali yetu lazima tutakuja kuweka nguvu wananchi wapate huduma nzuri. Kwa hiyo, nikushukuru sana Serikali inaifanya kazi jambo hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto,

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nataka kuongeza kwenye swali la Mheshimiwa Sware.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kugawanya fedha kwa ajili ya dawa, vifaa na vifaa tiba tunazingatia vigezo vikuu vitatu. Kigezo cha kwanza ni idadi ya walengwa wanaopewa huduma katika hospitali hiyo (*service population*) ambapo inachukua asilimia 70, kigezo cha pili ni hali ya umaskini katika eneo husika ambacho kinabeba asilimia 15 na kigezo cha tatu ni hali ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano. Kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Sware Halmashauri hizi tatu ambazo zinatumia Hospitali ya Wilaya ya Kondo wakae pamoja watuletee mapendekezo yao Wizara ya Afya kwamba hospitali hii inahudumia Halmashauri tatu na sisi tutazingatia katika kuwaongezea bajeti ya dawa. Ninakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kuwa swali la msingi linafanana kabisa na Wilaya mpya za Mkalama pamoja na Ikungi na wanatimiza vigezo vyote ambavyo Waziri amevitaja hapa.

Je, Serikali ni lini sasa italeta huduma za hospitali za Wilaya katika Wilaya hizo za Mkalama na Ikungi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mkalama ni Halmashauri mpya na imegawanyika kutoka Halmashauri ya Iramba, tunaenda kuhakikisha tunaboresha kile kituo cha afya cha Inimbila kwa sasa lengo kubwa ni kwamba kiweze kuwa na suala zima la upasuaji kuondoa haya mambo ya *referral system*, ambapo tunajua kwamba jambo hili tukilifanya litasaidia sana wananchi wa Jimbo la Mkalama kuweza kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika katika kituo cha afya cha Ikungi tunaenda kuweka uboreshaji mkubwa wa miundombinu ya afya ambayo kwa wananchi wa eneo lile wataweza kupata huduma mzuri hivi sasa ambapo kama nilivyosema awali tumeingiza katika mpango ule wa vituo vya afya 100 ambao Serikali iko katika hatua za mwisho kwa sababu kila kitu kimeshakamilika, tegemeeni Waheshimwa Wabunge katika maeneo hayo Serikali imewasikia na itafanya mambo hayo kwa kadri iwezekanavyo. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul swali fupi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Waziri ulifika Babati ukaona hospitali yetu ya Mrara na tukakueleza kwamba tunapata

wagonjwa kutoka Kondoa ambalo ndiyo swali la msingi siku ya leo. *RCC* tulishakaa kwamba hospitali yetu ipandishwe hadhi kutoka kituo cha afya kwenda hospitali ya Wilaya naomba nifahamu Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini pendekero letu hilo la *RCC* mtalifanya kazi maana hospitali ya Mrara ina hali mbaya na wagonjwa ni wengi tunashindwa kuwashudumia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nimefika na Mheshimiwa Mbunge tuliambatana pamoja siku ile tukitembea. Ni kweli wanachangamoto kubwa sana ni kwa vile utaratibu wa upandishaji wa vituo uko kwa mujibu wa sheria na utaratibu ambao nilnyi mmeshakamilisha jambo hilo lote na hivi sasa liko Wizara ya Afya katika *final stages*, nadhani Wizara ya Afya itakapokamilisha hilo jambo mtapata mrejesho, kwa sababu dhamira ya Serikali ni kuwashudumia wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kama mambo yote katika Mkoza yamekamilika naamini Wizara ya Afya ita-finalizes hilo jambo lengo kubwa ni kuwasaidia wananchi wa Babati waweze kupata huduma vizuri. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Saumu Heri Sakala Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 319

#### **Kurasimisha Bandari Bubu-Tanga**

**MHE. SAUMU H. SAKALA** aliuliza:-

Kando kando mwa Bahari ya Hindi Mkoani Tanga, pameibuka bandari bubu ambazo nyingine zinakuwa kubwa

na kuhudumia watu wengi zaidi na askari wasio waaminifu hufanya bandari bubu hizo kuwa vyanzo vyao vya mapato kwa kuchukua rushwa kwa watu wanaopitisha mizigo yao katika bandari hizo.

Je, ni lini Serikali itazirasimisha bandari hizo na kuzifanya zitambulike ili wafanyabiashara wanaozitumia wawe huru?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Saumu Heri Sakala, Mbunge wa Viti Maalum, swalii lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina taarifa ya uwepo wa bandari bubu katika mwambao wa Pwani ikiwa ni pamoja na maeneo ya Tanga. Aidha, kuibuka kwa bandari hizi bubu kumeleta changamoto za kiusalama, kiulinzi na kiuchumi. Hivyo, ili kudhibiti matumizi ya maeneo haya mamkala zinazohusika za pande zote mbili za Serikali ya Muungano zinashirikiana na kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mikakati ya pamoja na vikao vya kiutendaji ambavyo vimeduwa vikifanyika kwa kuwahusisha Wakuu wa Mikoa yote ya mwambao na visiwani, Wizara zinazohusika kutoka Bara na Visiwani, Mamlaka ya Usafiri Baharini ya Zanzibar (ZMA) Mamlaka ya Usafiri Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*), Shirika la Bandari la Zanzibar (ZPC), Mamkala ya Usimamizi wa Bahari Tanzania (*TPA*), Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), Uhamiaji, Halmashauri na vyombo vyote vya ulinzi na usalama nchini. Mikakati ya pamoja iliyowekwa ni pamoja na:-

(i) Kutambua bandari zenye umuhimu kwa wananchi kiuchumi na kijamii ili kuzirasimisha kwa kuziweka chini ya uangalizi wa vijiji vilivyo kwenye maeneo husika;

(ii) Kuimarisha ushirikiano na Serikali za Mitaa kwa kutumia Kamati za Ulinzi na Usalama ili zihusike katika

kudhibiti matumizi mabaya ya bandari bubu katika maeneo ambayo mamlaka husika hazina uwakilishi wa moja kwa moja;

(iii) Kuwa na kaguzi za mapoja kwa lengo la kuongeza ufanisi katika matumizi ya vifaa kama vile boti za ukaguzi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa suala hili, Serikali kuitia mamlaka nilizokwishazitaja, inasimamia kuhakikisha mikakati hii iliyowekwa inatekelezwa kwa wakati ili bandari bubu hizi zikiwemo za mwambao wa Mkoa wa Tanga zirasimishwe na kuwekwa chini ya uangalizi wa mamlaka husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saumu Sakala swali la nyongeza.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mrefu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ambayo Naibu Waziri ameielezea inaonyesha kabisa nia ya muda mrefu na bado iko ndani, lakini tatizo hili huku nje bado linaendelea kuwa kubwa yaani watu bado wanaendelea kuathirika sana na bandari hizi bubu.

Swali la kwanza, je, Serikali haioni kwamba kwa kuendelea kuweka mikakati hiyo mirefu ndani wananchi wanaathirika na pengine sasa ingefika wakati ikachukua mkakati wa kudhibiti angalau wakati ile mikakati ya muda mrefu ikiwa inaendelea?

Swali la pili, bandari bubu hizi ziko katika vijiji vinavyozunguka mwambao wote wa pwani. Kwa kufanya mikutano na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Bandari na watu wengine haoni kama anawatenga wale wanakijiji au wale ambaao wanazitumia zile bandari na ambaao wanaishi karibu

na zile bandari na sasa pengine ingekuwa ni vizuri Serikali ikaenda kwa wahusika moja kwa moja kuzungumza nao ikaangalia? Kuna athari pia za mazingira uchafuzi wa mazingira ni mkubwa sana katika bandari hizi bubi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii mikakati siyo mirefu sana nimejaribu tu kuisoma kwa kirefu lakini siyo mirefu sana. Ni mikakati mitatu tu maalum isipokuwa nimeileza kwa undani ndiyo maana inaonekana kama ni mikakati mirefu au ya muda mrefu.

Hata hivyo nadhani kitu cha kufahamu hapa ni kwamba bandari bubu inaanizishwa katika maeneo ambayo maeneo ya karibu tu kuna bandari ambayo ni rasmi. Kwa hiyo ni tabia ya watu kukimbia bandari rasmi na kujanzishia bandari bubu pembeni.

Kwa hiyo suala la kuahusisha walioanzisha bandari bubu tutalifanya katika maana ya kudhibiti, lakini siyo kwa maana ya kumshirika wakati yeye aliyeanzisha hiyo bandari bubu huku akijua kwamba anafanya makosa na anatafuta fedha kwa njia ambayo siyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, ni kweli wanaohudumia hizo bandari bubu kama nilivyosema ni watu ambao wamejanzishia uratatibu wao nje ya utaratibu wa Serikali na tutafanya kila njia kuhakikisha kwamba tunawashirikisha katika kudhibiti lakini wakati wa kurasimisha hata vile vijiji tunavyowapa mamlaka wanawatumia wale ambao wana uzoefu wa kuendesha hizi bandari na hivyo tukifanya hivyo masuala ya usafi na mazingira wa bandari hizo yatashughulikiwa kikamilifu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuwa matatizo yaliyopo kwenye mwambao wa Pwani hayana tofauti sana na matatizo yaliyoko kule Geita. Mkoaa wa Geita unayo bandari bubu inaitwa Nungwe ambayo inatumiwa na Mgodi wa *GGM* kushusha shehena kubwa.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari baada ya kumaliza shughuli za Bunge afuatane na Wabunge wa Geita akalione lile eneo ili Serikali iweze kuipitisha kuwa bandari halali na watumiaji wengine waweze kupita pale? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kwa hiyo taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma kuhusu hiyo bandari bubu ya Nungwe na niko tayari kufuatana nae pamoja na Wabunge wengine wa Geita ili tukaiangalie hiyo kwa undani na tuone kama ipo katika orodha ambayo inashughulikiwa na viongozi wa Mikoa wa Ziwa Victoria katika kushughulikia suala la kudhibiti bandari bubu. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masoud swali la nyongeza.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru taarifa ya Serikali inaeleza kwamba kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo kuna bandari bubu 32. Serikali muda wote imekuwa ikisema kwamba iko katika mikakati ya kuhakikisha kwamba bandari bubu hizi zinaweza kudhibitiwa, lakini tatizo linaloendelea la kuingia kwenye nyaya za umeme, matairi ya magari *fake* pamoja na maziwa ya watoto *fake* yanaendelea kuadhiri afya za binadamu na matukio mengine ya hapa na pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anaweza akawaambia nini Watanzania juu ya mkakati wa ziada kuhakikisha kwamba matairi ya magari *fake*, nyaya za umeme, maziwa ya watoto *fake* yanadhibitiwa katika

bandari bubu kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo? Naomba majibu ya haraka. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Unaomba majibu ya haraka au majibu ya uhakika? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZINA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli katika bandari bubu zilizoko katika mwambao wa Pwani kuanzia Tanga hadi Bagamoyo na Kunduchi tuna kazi kubwa sana tunafanya pale ya intelijensia pamoja na kazi ya kuhakikisha kwamba chochote kinachotoka pale hakingii katika soko kabla hakijakamatwa na Serikali. Nadhani unakumbuka ni mara nydingi tu tumeshika bidhaa mbalimbali zinazotoka upande wa pili kuingia upande huu mwingine wa nchi kwa maana inatoka Zanzibar kuingia huku kuititia hizi bandari bubu tumefanyakazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba zinasimamiwa haziathiri soko la nchi yetu na pili, hawaleti bidhaa ambazo ni *fakekama* ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya kazi hiyo na kwa kweli nichukue nafasi hii kuwapongeza sana vyombo vya ulinzi na usalama vya maeneo hayo kwa kazi kubwa wanayofanya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ajali Akbar.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matatizo yanayoikumba Tanga pamoja na Bagamoyo ya bandari bubu yanafanana sana na mpaka kati ya Newala na Msumbiji ambapo wananchi wa Msumbiji wanakuja kutibiwa pale Newala. Ni lini sasa Wizara ya Ujenzi itakuja kufanya iwe rasmi badala ya kuwaachia polisi wale wananchi wanaokuja kutoka Msumbiji wanakimbizana nao. Kwa nini sasa Wizara ikaja na ikarasimisha na ikawa ni rasmi? Naomba jibu lako Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge ambaye ametoa taarifa hii. Alitupa taarifa mapema na nimpe tu taarifa kwamba suala hili tumeanza kulifanyia kazi kwa nguvu zote na matokeo yatakapokuwa tayari tutakuja tumfahamishe.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Yosepher swali fupi.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, tatizo la ongezeko la bandari bubu katika Mkoa wa Tanga ni kutokana na uwezo mdogo wa Bandari ya Mkoa wa Tanga. Je, Waziri anatuambia nini kuhusu kuboresha Bandari ya Tanga kwa maana ya kina na miundombinu ili ongezeko hili la bandari bubu liweze kupungua? (*Makof!*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna mradi ambao sasa hivi unaendelea, unatarajiwa kukamilika karibuni wa kuongeza kina katika lile eneo ambalo sasa hivi tunalitumia. Vilevile unafahamu kwamba tuna nia pia ya kuanzisha bandari kubwa zaidi ya Mwambani na kama sehemu ya mradi ule mkubwa wa kuhakikisha mizigo ya kutoka Uganda inapita katika reli ile ya kutoka Tanga – Musoma na Bandari ya Mwambani. Mipango hii ya Serikali ni thabiti na tumeanza kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hilo la kuongeza kina ni karibuni tu mwezi ujao kazi hiyo itakuwa imekamilika.

Na. 320

**Bodi ya Kusajili Makandarasi (CRB)**

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Serikali iliunda Bodi ya Kusajili Wakandarasi (CRB)

ambayo ina jukumu la kusajili, kuratibu na kusimamia mwenendo wa makandarasi nchini.

(a) Je, tangu kuanzishwa kwa *CRB* ni wakandarasi wangapi Watanzania wamesajiliwa na taasisi hiyo?

(b) Je, Serikali Kuu na Halmashauri za Wilaya zinatumia vigezo gani kutoa kazi kwa wakandarasi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ka niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Usajili wa Makandarasi tangu ilipoanzishwa mwaka 1997 imesajili jumla ya makandarasi wa Kitanzania 13,523. Kati ya makandarasi hao, makandarasi 8,935 usajili wao uko hai na makandarasi 4,578 wamefutiwa usajili kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kushindwa kulipia ada ya mwaka na kukiuka taratibu nyininge zinazoongoza shughuli za ukandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vinavyotumiwa na Serikali katika utoaji wa zabuni kwa makandarasi vinazaingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013. Vigezo hivyo ni pamoja na kampuni kusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi, ukomo wa ukubwa wa kazi kulingana na daraja la usajili, mahitaji maalum ya mradi husika, wataalam, vitendea kazi, uzoefu wa utekelezaji wa miradi ya aina hiyo na uwezo wa ampuni kifedha wa kutekeleza mradi husika. (*Makofii*)

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na ukweli kwamba wakandarasi 13,000 ni kidogo sana ukilinganisha na idadi ya Watanzania, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kigezo kimoja wapo kinachotumika kutoa kazi wanaangalia uzoefu wa kufanya kazi hiyo hiyo kwa yule anayeomba na kwa kuwa tumekuwa tukisisitiza kutoa ajira kwa vijana wetu, *graduates wanapo-graduate* tunawaambia waanzishe makampuni.

Swali la kwanza, je, vijana hawa wanapo-*graduate* kwenye vyuo vikuu wakaanzisha kampuni, wakiomba kazi wataweza kupata kazi kwa utaratibu huu? (*Makofii*)

Swali la pili, ukiangalia sifa mojawapo inayotumika kazi ni kwamba uwezo wa kifedha wa Mkandarasi lakini uzoefu unaonyesha uwezo wa kifedha wa wakandarasi wetu ni mdogo, wengine wanafutiwa hata kwa kushindwa kulipa ada na wengine wanashindwa hata ku-access mabenki kwa sababu ya utaratibu mbovu wa mabenki tulionao.

Je, Serikali haioni wakati umefika wa kuanzisha Benki ya Wakandarasi na kuboresha taratibu ili kuwezesha Wakandarasi wetu waweze kujikomboa na kupambana na umaskini. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunawahamisha *graduates* wa fani ya uhandisi pamoja na ubunifu wa majenzi waanzishe kampuni na Serikali ina *window maalum*. Tumeweka *window maalum* ya kuhakikisha hawa watu tunawapa *training*, nadhani mfano utagundua pale Daraja la Mbutu tulifanya hivyo, hatukuzingatia uzoefu bali tulifanya pale ya majaribio, vilevile barabara ya kule Bunda kwenda Serengeti nayo vilevile kuna kilometra 50 tuliziweka kwa hawa *Mbutu Joint Venture*, tunaona kwamba kumbe hilo linawezekana na ndani yao ameshajitokeza mkandarasi mmoja sasa amepata uwezo mkubwa zaidi, Kampuni ya Mayanga ambayo sasa inajenga uwanja wa ndege wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutalifanya hilo na tutaendelea kulifanya lakini lazima tuzingatie sheria kwa sababu tukienda kinyume cha sheria tutakwenda kinyume

na kile ambacho tulikubaliana humu Bungeni. Tutatafuta kila aina ya mwanya kujaribu suala hili za uzoefu lisitukwamishe sana kuhamasisha wakandarasi wa kizalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uwezo wa kifedha ni suala la wakandarasi wenyewe na nadhani Mheshimiwa Balozi Buberwa Kamala unafahamu kwamba wakandarasi wana mpango huo wa kuanzisha benki yao na Serikali tutaendelea kuhamasisha mpango huo ukamilike.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso swalii la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swalii dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ni ukweli kwamba wakandarasi hapa nchini pamoja na wazabuni mbalimbali ambaao wamekuwa wakitoa huduma kwa Serikali, wamekuwa wakiidai Serikali fedha nydingi na Serikali imekuwa haflili kwa wakati.

Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba wakandarasi hao wakimaliza kazi na wazabuni wakimaliza huduma wanazotoa waweze kulipwa kwa wakati bila kuhatarisha kazi ambazo wanafanya?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wakati tunaingia tulirithi deni la shilingi trilioni 1.215 la makandarasi. Nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara ya Fedha wametuwezesha kati ya hizo tumeshalipa shilingi bilioni zaidi ya 790, sasa hivi tumbakiza deni dogo sana katika yale madeni ya nyuma makubwa. Ingawa kwa kulipa madeni hayo, makandarasi wameendeleza kuongeza nguvu ya kuongeza kazi na wameongeza tena madeni mengine, lakini hayo madeni mengine walau sasa hivi yanashughulikiwa kwa namna ambayo hayazalishi tena *idle time* ambayo ni fedha ambazo tunalazimika kuzilipa wakati kazi haifanyiki kwa sababu tu ya kuchelewa kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwamba sasa suala hilo halipo tena na kwa kweli tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi hii, naomba mtupongeze na tutaendelea kukamilisha deni lililobakia ili hatimaye wakandarasi hawa wasiwe tena na madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine miradi yote ya wakandarasi wazalendo tumekuwa tukilipa kikamilifu kabisa, huwa haichelewi kwa sababu tunajua uwezo wao ni mdogo na kwa kulipa mara deni linapo-*accrue* lengo ni kuwawezesha hawa wakandarasi wa kizalendo waweze kukua zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Mtuka swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa sana katika nchi hii hasa katika utekelezaji wa miradi mikubwa, mkandarasi kupewa Mikoa zaidi ya miwili ama mitatu. Jambo hili limekuwa likifanya miradi kuchukua muda mrefu, kwa mfano miradi ya *REA*.

Je, hatuna wakandarasi wa kutosha kwa mfano katika miradi ya *REA* ili kila mkoa uwe na mkandarasi mmoja kuokoa muda? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miradi ya *REA* kuna sababu maalum ya kufanya hivyo na imetokana na uzoefu wa nyuma. Lakini kimsingi katika miradi ya masuala ya ujenzi iwe majengo, barabara au reli tunafuata *qualification/sifa ambazo* huyu mkandarasi amefuata na kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi inavyotuongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tufuate hivyo, inawezekana kabisa mkandarasi wa Mkoa mwengine

akapata kazi mkoala mwagine ni kitu cha kawaida kabisa kama ilivyo mkandarasi wa nje ya nchi anapopata ndani ya nchi yetu ni kitu cha kawaida kinachoangaliwa ni sifa ya mkandarasi aliyeomba hiyo kazi na kwa mujibu wa taratibu za zabuni.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi limeongelea vigezo na kwa kuwa Rais aliyepo madarakani wakati akiwa Waziri wa Ujenzi, aliweka kigezo kwamba kazi zinapotangazwa walau kampuni moja ya mwanamke ipate kazi ili kuwainua wanawake na jambo hilo kwa sasa linafifia.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuambia ana mkakati gani wa kutoa walau waraka *TANROADS* na Halmashauri kwamba wanawake wanapopata kazi wame-*qualify* wapewe kazi hizo ili kuwainua wanawake? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Munde kwa swali hili la nyongeza kwa sababu ananipa fursa ya kuelezea nini Wizara yangu inafanya katika kuwainua wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu tuna mradi maalum wa kuhakikisha kwamba wakandarasi wanawake kwanza wanapatikana kwa sababu ili wapatikane kwanza lazima wajisajili na Bodi ya Usajili wa Wahandisi. Ndani ya Bodi ya Usajili wa Wahandisi tuna programu maalum kwa ajili ya wanawake tu na nashukuru wenzetu wa *NORAD* wanatusaidia fedha kwa ajili ya kuhakikisha hawa wahandisi wanawake wanasajiliwa, wakishasajiliwa wanaanzisha kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida kampuni hizo zinazoanzishwa na akina mama tunazilea kama nilivyosema, kila wanapopata kazi na wamekuwa wakipata kazi

mbalimbali ingawa kwa sasa bado ni kampuni chache zilizoanzishwa kupitia njia hiyo na tutaendelea kuzihamasisha nydingi zaidi zianzishwe. Kila wanapopata kazi wanalipwa malipo yao yote wanayostahili ili waweze kuendelea kukua, huwa hatuwaachii deni la aina yoyote katika wakandarasi hawa wazalendo na hasa hawa wakandarasi akina mama. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, tutamalizia swali letu la mwisho Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 321

### **Changamoto Zinazokabili Kazi za Wasanii**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA** aliuliza:-

Mchango wa kazi za wasanii umeonekana katika kutoa ajira lakini bado wasanii wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kuhujumiwa kazi zao ambapo Mheshimiwa Rais ametoa maagizo mbalimbali ya kushughulikia watu wanaohujumu kazi za wasanii.

Je, mpaka sasa ni hatua gani zimechukuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Devotha naomba kwa ruhusa yako nichukue nafasi hii kutoa taarifa fupi ya mafanikio ya mrembo Aisha Mabula ambaye tulimuona hapa hivi karibuni Bungeni, aliewezeshwa na Waheshimiwa Wabunge kushiriki mashindano ya ulimbwende ya *Miss World Super Model* nchini China.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya washiriki walikuwa 52 kutoka nchi mbalimbali duniani lakini kutoka Afrika ni

wawili ambapo mmoja wao ni huyo Bi. Aisha Mabula na Aisha Mabula alifanikiwa kuingia 14 bora kama fainali na katika fainali hiyo alishika nafasi ya tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Bi. Aisha kwa kuiwakilisha vizuri nchi yetu ya Tanzania pamoja na Bara la Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa moyo wenu wa ukarimu ambapo mlimchangia na kumuwezesha kushiriki katika mashindano hayo ya kidunia ambayo naamini kabisa mafanikio haya yatamuwezesha kupata ajira na kuendelea kuitangaza nchi yetu Kimataifa na hasa katika sekta ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu mfupi naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Kamati ya Urasimishaji wa Kazi za Filamu na Muziki nchini inayojumuisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), Baraza la Sanaa la Taifa (*BASATA*), Bodi ya Filamu Tanzania (*TFB*) na Chama cha Hakimiliki Tanzania (*COSOTA*) hutoa miongozo mbalimbali kuhusiana na masuala ya ulinzi na kazi za sanaa.

Aidha, kwa kushirikiana na *COSOTA* Wizara kupitia *BASATA* na Bodi ya Filamu Tanzania (*TFB*) hutoa *copyright clearance certificate* kwa mmiliki wa kazi yoyote ya sanaa kabla ya kupewa stempu ya kodi ya *TRA*. Lengo la stempu hizo ni kurasimisha sekta ya filamu na muziki katika uuzaji wa *CD, DVD*, kanda na kadhalika na hivyo kukabiliana na hujuma katika kazi za wasanii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo sheria na taratibu za forodha na za kulinda hakimiliki zinakiukwa na hivyo kuathiri maslahi ya wasanii, Serikali huendesha

operesheni za kukamata kazi hizo za sanaa zenye utata. Hadi kufikia Machi 2017, Wizara ilifanya operesheni kubwa mbili na za kawaida sita dhidi ya filamu zinazoingia sokoni bila kufuata utaratibu ambapo jumla ya kazi 2,394,059 zilikamatwa zikiwemo kazi za nje ya nchi 2,393,529 zenye thamani ya zaidi ya shilingi 3,590,293,500 na za ndani 530 zenye thamani ya shilingi 1,590,000.

Aidha, mitambo ya kufyatua kazi za filamu (*duplicators*) 19, *printers* za CD/DVD nane, *DVD writers* 31, kompyuta tatu na *UPS* saba zilikamatwa katika operesheni hizo.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoeleza Naibu Waziri, kazi za wasanii ni kuburudisha, kuelimisha, kuonya na kukosoa, wasanii wamekuwa wakifanya kazi hizi hata wakati wa kampeni tulishuhudia wasanii walivyofanya kazi yao vizuri na wakati mwingine waliimba nyimbo za kuponda upinzani na mlikuwa mkishangilia. Jambo la kushangaza hivi sasa wasanii wakiimba nyimbo za kukosoa Serikali wanashughulikiwa na mfano mzuri ni Ney wa Mitego pamoja na Roma Mkatoliki.

Swali la kwanza, je, ni wakati gani sasa kazi hizi za wasanii zinathaminika?

Swali la pili, kwa bahati mbaya sana Rais ametoa maagizo ya wale ambao wamehujumu kazi za wasanii na kuacha kabisa kuawajibisha Serikali yake ambayo imeshindwa kabisa kuthamini kazi nzuri iliyofanywa na Marehemu Mzee Francis Ngosha ambaye amekufa akiwa maskini wa kutupwa.

Je, Serikali inataka kukamata kazi za wasanii wakati ninyi wenyewe mmemuhujumu Mzee Francis Ngosha ambaye mpaka sasa hivi hana lolote, amekufa na hakuacha alama yoyote katika familia yake? (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha, naamini kwamba saa ya Mwongozo hutaomba Mwongozo kwamba maswali yako hayajajibwa kikamilifu, kwa sababu hakuna swali hata moja kati ya hayo mawili linalotokana na swali lako la msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maswali yake yako nje kidogo na swali la msingi, lakini kwa sababu tu ya kumbukumbu tulizonazo, swali lake la kwanza linalouliza kwamba ni wakati gani kazi za wasanii zinathaminiwa? Kama alivyosema mwenyewe, kwamba kazi ya sanaa ni kuburudisha, kuelimisha, kuonya, kukosoa na kadhalika, niseme tu kwamba kazi za wasanii tunazithamini wakati wote hasa wakati zinapoelimisha, zinapoburudisha na kufanya kazi zile ambazo zinalijenga Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kusema kwamba wasanii huwa wanashughulikiwa wakiikosoa Serikali, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hizi za sanaa zinasimamiwa na sheria. Tunayo Sheria ya BASATA Namba 23 ya mwaka 1984, tuna Sheria nydingine Namba 4 ya Bodi ya Filamu ya mwaka 1976 na tuna Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Namba 7 ya mwaka 1999. Kwa hiyo, tunachohitaji ili tuweze kuzithamini kazi hizi ni kwamba wasanii wazingatie sheria, wafuate sheria na taratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wasanii ambao tunaona kwamba wameenda kinyume, hatua huwa zinachukuliwa na hatua zenyewe, kwa mfano kuna msanii mmoja anaitwa Nikki Mbishi ambaye alipewa tu onyo kutokana na kuweka picha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne katika wimbo wake *I am sorry JK*. Hizo ni hatua tu ambazo huwa tunazichukua ili wasanii hawa wafuate sheria. Sheria ya BASATA inahitaji wasanii hawa wapitishe nyimbo zao BASATA ili ziweze kukaguliwa kabla hazijatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakiwa wamepitia kule ina maana kwamba watatoto kitu ambacho kinazingatia sheria na kinafuata maadili, sasa huu ni ukiukwaji wa maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwingine ambaye ameshawahi kupewa onyo ni Diamond kupitia kwa Meneja wake, ambaye alitumia majina ya viongozi bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ney wa Mitego, huyu aliimba wimbo wake wa Wapo ambapo ulifungiwa na BASATA kwa muda, lakini baadaye ulifunguliwa baada ya kuwa na makubaliano ya jinsi ya kuuboresha huo wimbo. Huyo mwingine Roma, hakuna hatua ambayo imechukuliwa na Serikali kwa mwaka huu kuhusu msanii huyo na ninadhani ninyi ni mashahidi kwamba alijieleza yeye mwenyewe kwa vyombo vyaa habari na Mheshimiwa Waziri pia alikuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ambalo linamhusu Marehemu Francis Ngosha na Mheshimiwa Devotha anadai kwamba Serikali imemhujumu, hii siyo kweli, hakuna hujuma. Kimsingi yapo majina mezani mpaka sasa kama matatu hivi yanayohusiana na ubunifu wa nembo tunayoitumia, ambayo ni nembo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mpaka sasa bado haijajulikana ni nani hasa ambaye ni mbunifu wa nembo hii. Kwa sababu kwa mfano, yupo Marehemu ambaye alishatangulia mbele za haki muda mrefu anayeitwa Abdallah Farhan wa Zanzibar, yeye vielelezo tayari vimeshakutwa katika kumbukumbu zake jinsi alivyokuwa akibuni nembo yetu ya Taifa, nembo ya Kenya pamoja na nembo ya *OAU* kipindi hicho alipokuwa aksoma *Makerere University*. Kwa hiyo, yapo majina ambayo yanadaiwa kwamba yalishiriki katika kutengeneza nembo hii. Ninaomba sana... (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo, tafadhalii. Mheshimiwa Waziri, malizia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA**

**MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wataalam wafanye kazi ya kutambua ni nani hasa ambaye alishiriki kubuni. Kwa sababu Marehemu Francis yeye anajulikana kama ni mchoraji, lakini siyo mbunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kwamba labda swali la Mheshimiwa Devotha Minja ni ishara ya wazi kwamba kuna uhitaji mkubwa sana wa kuwa na orodha ya wasanii na kazi ambazo wamezifanya na ni kitu ambacho sasa hivi Wizara tumeanza kukifanya ili kusudi tuwe na orodha ya wasanii wote katika nchi yetu na kazi ambazo wanazifanya ili mwisho wa siku utata kama huu usiweze kutokea tena. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Haule.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Moja kati ya changamoto kubwa za wasanii wa Tanzania ni kuibiwa kazi zao, lakini pia kutonufaika na kazi zao kwa sababu ya kazi hizo kutolindwa ipasavyo. Tunaona kuna upungufu mkubwa sana kwenye Sheria Namba 7 ya mwaka 1999, Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki.

Je, Serikali haioni kwamba huu sasa ni muda muafaka wa kuileta sheria hii kwenye Bunge lako Tukufu tuweze kuibadilisha na kuirekebisha ili iweze kusaidia wasanii wa Tanzania waweze kupata haki zao, kwa sababu wengi wanakufa masikini, wanaabiwa kazi zao mtaani lakini wanaowaibia tunawajua?

**NAIBU SPIKA:** Umeshaeleweka Mheshimiwa Profesa Jay, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA**

**MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hili suala tayari *COSOTA* imeshalionna, hii ni Sheria ya Hakimiliki na

Hakishiriki. Kwa kuanzia imeanza kufanya utaratibu wa kubadilisha kifungu namba 46. Kwa hiyo, mchakato huu unaendelea, tuwe na subira ili marekebisho yaweze kufanyika ikiwa ni pamoja na kanuni zake. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu kwa siku ya leo. Matangazo yaliyopo mezani yanahusu wageni.

Tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika na hawa ni wageni 75 wa Wizara ya Nishati na Madini ambao ni Profesa James Mdoe ambaye ni Kaimu Katibu Mkuu, tunaye pia *Engineer* Dkt. Julian Pallangyo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu - Nishati, yupo pia *Engineer* Benjamin Mchwampaka ambaye ni Kamishna wa Madini, yupo pia *Engineer* Innocent Luoga ambaye ni Kaimu Kamishna wa Nishati na Masuala ya Petrolli. (*Makofii*)

Pia wapo Wenyeviti wa Bodi kutoka taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo, yupo Dkt. Alexander Kyaruzi ambaye ni Mwenyezekiti wa Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*), yupo pia Profesa Sufian Bukurula ambaye ni Mwenyezekiti wa Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (*TPDC*), yupo pia Dkt. Gideon Kaunda ambaye ni Mwenyezekiti wa Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) na Dkt. Adelardus Kilangi ambaye ni Mwenyezekiti wa Mamlaka ya Udhhibit wa Mkondo wa Juu wa Petrol (*PURA*). (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, pia yupo vilevile Balozi Alexander Muganda ambaye ni Mwenyezekiti wa Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*), yupo Profesa William Mwegoha ambaye ni Mwenyezekiti Chuo cha Madini, Profesa Shukrani Manya ambaye ni Mwenyezekiti wa Wakala wa Jiolojia Tanzania (*GST*), Dkt. Stephen Mdachi ambaye ni Mwenyezekiti Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*PBPA*), yupo pia Profesa Jamidu Katima ambaye ni Mwenyezekiti wa Mamlaka ya Udhhibit wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*), yupo pia Ndugu Beatus Segeja ambaye ni Mwenyezekiti wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (*TGDC*) na hawa wameambatana na Wakuu wa Idara, Vitengo na

Taasisi pamoja na Maafisa wa Wizara ya Nishati na Madini.  
*(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 31 wa Mheshimiwa Pauline Gekul ambaao ni Waheshimiwa Madiwani, Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jimbo kutoka Babati Mjini, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 66 wa Mheshimiwa Joseph Haule ambaao ni wanafunzi 60 na walimu sita wa Shule ya Msingi Kantui kutoka Ruaha, Mikumi Mkoani Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambaao ni wanafunzi 21 kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, Tawi la Dar es Salaam. Karibuni sana wageni wetu Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, tutaendelea na shughuli zilizo mbele yetu. Katibu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mwongozo wa Spika.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) kwa ruhusa yako. Kuna suala linaloendelea, nataka kupata Mwongozo wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Bungeni tumekuwa tukipiga marufuku sana tabia za uhamasishaji hasa kwa masuala yanayohusiana na watoto, mambo ya mimba za utotonu na mambo mengine, lakini kuna tangazo linaendelea kwenye vyombo vya habari linasemajaza ujazwe na katika lile tangazo amechorwa mtoto wa shule

amewekwa pale juu ana mimba halafu hapa chini yanaendelea matangazo yanasema jaza ujazwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili sisi tunaotoka kule vijijini hatujui vizuri Kiswahili cha Pwani, tunalitafsiri vibaya; na imekuwa lugha hata kwa watoto wa shule sasa kule mitaani wanasema nijaze nikujaze. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Mwongozo wako, kwa nini Serikali isipige marufuku maneno haya ya jaza ujazwe? Hayaendani na utamaduni wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Na mimi nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) kwa jambo lilitokea mapema hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo akimjibu Mheshimiwa Devotha Minja, lilzungumzwa suala la Marehemu Mzee Ngosha aliyefariki katika Hospitali ya Muhimbili tarehe 28 Mei. Sasa naomba Mwongozo wako kujua, pamoja na kwamba hadi leo kwanza kwa masikitiko makubwa, Serikali haijui mpaka leo aliyetuchorea nembo ya Taifa ni nani na pia mpaka leo hii sisi Tanzania hatuna Vazi Rasmi la Taifa, naomba Mwongozo wako. Je, Serikali ina mpango gani wa kuisaidia au kuifanyia nini familia ya Mzee Ngosha ili ibaki kama kielelezo kwa kuwa inasadikika kwa maelezo yake mwenyewe yule Mzee Ngosha alisema alianza kubuni nembo ya Taifa mwaka 1957 akiwa katika mashamba ya Mkonge Mkoani Tanga?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, vilevile Serikali imejifunza nini katika kuwaenzi watu maarufu na mashuhuri hapa Tanzania ili yasije yakajitokeza matatizo na kasoro kama kwenye suala la Mzee Ngosha? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo ambalo nataka unisaidie kunipa Mwongozo wako kwa sababu inaweza ikatugombanisha na sisi hasa upande wa Upinzani hapa; inaonesha kwenye kumbukumbu zenu kutoka kwenye Kiti chako hapo kwamba mimi kwenye hili Bunge nimechangia mara tatu.

Mimi nimechangia mara mbili, siyo mara tatu na kitendo cha kuongeza siku ya kuchangia kinanifanya kwenye Wizara kama ya leo muhimu sana ambayo nimejipanga mwezi mzima kuchangia, sitapata nafasi kwa sababu tunaangalia umechangia mara ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuepuka kutugombanisha, sisi na viongozi wetu wa Kambi ya Upinzani hapa, ni muhimu nipate Mwongozo wako. Mimi nimechangia dakika kumi kwenye Wizara ya Elimu na dakika tano ambazo niliomba heshima ya Kiti nikachangia Wizara ya Ardhi. Sikuchangia tena, ila kama niliomba Mwongozo ukabadilishwa kwamba nilichangia, ndiyo naomba Mwongozo wako ili uweze kunisiaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Catherine Magige.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Nasimama kwa Kanuni hiyo hiyo ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge za Leo kwenye Hoja za Serikali, leo tutajadili hotuba

ya Wizara ya Nishati na Madini na ukirudi kwenye ratiba mpya kabisa iliyotolewa tarehe 24 Mei, 2017, inaonesha kwamba siku ya Alhamisi tarehe 1 Juni yaani leo mpaka Ijumaa ndiyo utakuwa huo mjadala wa Nishati na Madini unaendelea. Ukishuka chini ya hii ratiba imeandikwa pia siku ya Ijumaa, tarehe 2 Juni Ijumaa hiyo hiyo ambayo ipo kwenye Nishati na Madini inarudiwa tena kwamba mpaka Jumatano Kamati ya Bajeti itakuwa inakaa na Serikali kujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hii ratiba iko sahihi, naomba Mwongozo wako kwamba je, huu mjadala wa Wizara ya Nishati na Madini utakuwa ni wa siku mbili au wa siku moja na nusu? Kwa sababu tunapanga wachangiaji kutokana na uwiano ule wa vyama, kwa hiyo, tunafahamu kama mjadala ni wa siku moja sisi hapa tunakuwa na dakika 10, lakini kama ni wa siku mbili maana yake tunakuwa na dakika 40.

Sasa kama siku ya Ijumaa ina majukumu mawili tofauti, maana yake itatuvuruga pia katika kupanga wachangiaji. Vilevile shughuli ya Kamati ya Bajeti kukaa na Serikali ni takwa la Sheria ya Bajeti ambayo inataka ni lazima ziwe siku sita. Sasa ukiitoa hiyo Ijumaa maana yake zile siku sita hazitimii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako hapa, hii ratiba ikoje ili tuweze kujipanga vizuri? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako. Wiki iliyopita kuna Mwongozo ulitolewa hapa Bungeni na Mwenyekiti, Mheshimiwa Zungu ndiye alikuwepo hapo kwenye Kiti na akasema kuwa Mwongozo huo utatolewa maamuzi na Kiti cha Spika, lakini hadi sasa hivi ni kimya. Mwongozo huo unahu Shule ya Butwa iliyopo Geita ambapo tulipoteza watoto watatu, boti ilizama. Mpaka sasa hivi ni wiki ya pili watoto hawaendi shule wala hawajui hatma yao ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wazazi, naomba Waheshimiwa Wabunge, nimeulizia boti ni shilingi milioni 15 tu, ikiwezekana, hata tukatwe kwa siku shilingi 30,000 kila Mbunge ili watoto wale waweze kununuliwa boti ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma kuhusu tangazo ambalo limesikika ama kuonekana katika vyombo vya habari na kwa maelezo ya Mheshimiwa Musukuma anaomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) na ametoa maelezo ambayo sina haja ya kuyarudia juu ya maneno yanayotumika katika tangazo la simu ama matangazo ya simu ama makamupuni ya simu. Wakati akimalizia kuomba Mwongozo wake, amesema kwa nini Serikali isipige marufuku tangazo kama hilo?

Waheshimiwa Wabunge wote tunaelewa zipo changamoto mbalimbali, kimsingi hili jambo kwa mujibu wa Kanuni aliyotumia Mheshimiwa Musukuma siyo jambo linaloweza kuombewa mwongozo Bungeni kwa sababu halijatokea hapa ndani. Hata hivyo kwa sababu hilo tanganzo pengine lipo kwa wale walilionna ama kulisikia, ziko namna mbalimbali ambazo matangazo mengine hutolewa pengine siyo na kampuni husika, lakini ni kwa ajili ya uchafuzi. Sasa Bunge lisije likaingizwa katika mazingira ambayo tangazo linahusishwa na kampuni fulani ikaonekana kampuni hiyo ndio iliyotengeneza tangazo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, yapo mazingira mbalimbali nanyi ni mashahidi, makampuni yanayogombana ama yanayokuwa mahasimu hasa kwenye eneo la dawa, wanatoa matangazo kwamba dawa hii ina madhara haya kwa sababu dawa hiyo inatoka kiwanda fulani na Mheshimiwa Waziri wa Afya amekuwa akiwasiliana na *TFDA* kila wakati kutoa ufanuzi.

Kwa hiyo, hata hili aliloomba Mheshimiwa Musukuma tuwe makini katika kuyaangalia haya mambo, lakini hata

hivyo *TCRA* iwe inatazama haya mambo kwa haraka. Kama Kampuni hajatoa hilo tangazo, yule aliyelianzisha achukuliwe hatua ili kuzuila matangazo kama hayo ya kuchafuliana biashara, kwa sababu wote tunajua katika biashara yako mambo mengi.

Kwa hiyo, upande wa Serikali, *TCRA* iliangularie jambo hilo kama ni kweli na limeleta taabu katika jamii lifanyiwe kazi kwa haraka ili lisilete mkanganyiko uliopo.

Vile vile nimeombwa pia mwongozo wa pili na Mheshimiwa Mussa Mbarouk kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Mheshimiwa Mbarouk wakati akieleza ametoa maelezo kuhusu swali la nyongeza lilitolizwa na Mheshimiwa Devotha Minja kuhusu Marehemu Ngosha na kwamba anasikitika Serikali haimjui mtengeneza nembo na pia akauliza hapo maswali mawilli kwamba Serikali ina mpango gani wa kutunza familia ya Marehemu Ngosha na pia Serikali imejifunza nini katika kutunza kumbukumbu?

Waheshimiwa Wabunge, haya ni maswali ambayo Mheshimiwa Mussa Mbarouk ana uwezo wake yeye kuiuliza Serikali ili imjibu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbarouk hayo ni maswali ambayo unapaswa kuiuliza Serikali na siyo Kiti ili kitoe mwongozo. Ni Serikali ndiyo inayopaswa kujibu na wewe unajua utaratibu wa namna ya kuiuliza Serikali. Aidha, unapeleka swali lako la msingi ili upate nafasi ya kuliuliza kikamilifu ama swali la namna hiyo likitokea, basi utaliuliza kama nyongeza ili Serikali ikupe majibu na siyo Kiti ndiyo ikupe mwongozo.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf, tafadhal!

Waheshimiwa Wabunge, pia nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Mwita Waitara akizungumza kuhusu michango ya leo na kwamba yeye katika karatasi ambayo imetayarishwa na upande wa Ofisi ya Bunge

inaonesha kwamba amechangia mara tatu, lakini yeye kachangia mara mbili tu na ana hofu kwamba anaweza asipate nafasi katika chama chake kwa sababu kumbukumbu zinaonesha amechangia mara tatu badala ya kuonesha amechangia mara mbili ili apewe fursa ya kuchangia leo.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza ujumbe huo Mheshimiwa Waitara alishaniletea, na mimi nimeshapeleka ili Ofisi iweze kuangalia ameshachangia mara ngapi, maana wakati mwingine hata sisi wenyewe Wabunge tunasahau tumechangia mara ngapi ikiwa ni pamoja na hata maswali huwa tunasahau kwamba tumeshauliza mara ngapi?

Kwa hiyo, Ofisi itaniletea hapa majibu nami nitatoa taarifa ka chama chake kwamba amechangia mara ngapi. Lakini na vyama navyo viangalie namna nzuri ya kuweka wachangiaji kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wa vyama vyote vilivyoko humu Bungeni wanayo malalamiko.

Kwa hiyo, ma-*Chief Whip* wa vyama hivi waangalie namna nzuri ya kuweka wachangiaji ili kusiwe na haya malalamiko yanayotokea kwamba wengine wanachangia na wengine hawachangii. Kwa hiyo, Chama cha CHADEMA kitapokea taarifa nikishapata kutoka ofisini, sasa mtaamua kama mtampa nafasi ama hamumpi nafasi.

Mwongozo mwingine nilioombwa ni kutoka kwa Mheshimiwa Abdallah Mtolea ambaye ameomba kuhusu orodha ya shughuli za leo ambapo ratiba aliyonayo inaonesha shughuli inayoanza leo yaani mjadala wa Wizara ya Nishati na Madini utakuwa leo na kesho naye anauliza kwamba ikiwa ni leo na kesho kwa mujibu wa ratiba ambayo ilikwishatolewa mapema, basi siku sita ambazo ni matakwa ya kisheria ya bajeti, Kamati ya Bajeti itashindwa kufanya kazi yake kisheria, kwa maana ya kwamba itafanya kazi pungufu ya siku sita ikiwa haitaanza kesho na kwa kuwa kesho ratiba inaonesha kwamba tutaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, basi yeye ana wasiwasi huo.

Sasa kwa kuwa ameomba mwongozo wa Kiti, Mheshimiwa Mt Olea usiwe na wasiwasi juu ya hilo, Bunge hili linapenda kufuata sheria, kwa hiyo, siku ya kesho itapangwa kwa namna ambayo Sheria ya Bajeti haitapungukiwa matakwa yake na kwa hiyo, tutaianglia hiyo orodha ya kesho itaonesha namna nzuri ambayo tutalifanya hilo suala ambalo linatakiwa kisheria la kuwa la siku sita ambazo zitaanza kuhesabiwa kuanzia kesho. Kwa hiyo, orodha ya matukio mtaiona kwenye orodha ambayo ni ya kesho sasa na siyo ya leo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mt Olea usiwe na wasiwasi, Bunge halina mpango wa kuvunja Sheria ya Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, pia nimeombwa mwongozo wa mwisho na Mheshimiwa Catherine Magige ambaye ameeleza kuhusu watoto watatu waliozama wa Shule ya Butwa na kwamba mpaka sasa watoto hawa waliobaki sasa wanashindwa kwenda shule kwa sababu boti waliyokuwa wakisafiria inaonekana haiko salama kwa ajili ya kuvusha watoto kwenda shule na kuwarudisha na wakati akiendelea kuomba mwongozo huo ametoa maelezo kwamba leo siyo siku ya kwanza kuomba mwongozo huu, ulishaombwa wiki iliyopita na maelezo yakatolewa kwamba Mheshimiwa Spika atatoa mwongozo juu ya jambo hilo lifanywe vipi.

Mheshimiwa Catherine Magige ameendelea na kutoa mapendekezo kwamba Waheshimiwa Wabunge tukatwe shilingi 30,000 ili boti ambayo kwa taarifa aliyoitao inayouzwa shilingi milioni 15 iweze kununuliwa na watoto hawa waweweze kwenda shule. Pamoja na mambo mengine, imekuwepo miguno mingi sana humu ndani baada ya kusikia pendekizo hili la kukatwa shilingi 30,000.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa mwongozo ulishatolewa na Mheshimiwa Zungu kwamba Mheshimiwa Spika atatoa maelezo, basi mwongozo huu ulioombwa na Mheshimiwa Catherine Magige ni wa kukumbusha Kiti kuhusu mwongozo unaosubiriwa aliokuwa ameahidi Mheshimiwa Zungu. Kwa hiyo, utafanyiwa kazi na majibu yataletwa. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo tunaendelea, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2017/2018**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini. (*Makofî*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI - K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba ruhusa yako kulingana na ukubwa wa kitabu hiki basi hotuba yetu yote kama ilivyo kwenye kitabu iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ombi lingine naomba uniruhusu nichukue fursa hii kuwatakitia funga nzuri, yenye rehema ndugu zangu wote waislamu waliofunga Tanzania na duniani kote na hasa Jimbo la Muleba ya Kaskazini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema sisi Waheshimiwa Wabunge wote na hivyo kutuwezesha kuendelea na utekelezaji wa majukumu yetu ya Kitaifa ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa dhati kuwapongeza viongozi wetu wote wa Kitaifa kwa jinsi wanavyojituma katika kutatua matatizo na changamoto mbalimbali za Taifa letu na hatimaye kuwaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake kwa jinsi anavyochukua hatua za kusimamia na kulinda rasilimali za Taifa hasa Madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kazi yake nzuri anayoendelea kuifanya tangu alipoteuliwa. Aidha, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa jinsi anavyoendelea kusimamia shughuli za Serikali kwa nguvu zake zote. Tuwaombee wote Mwenyezi Mungu ili waendelee na kasi hiyo na hatimaye nchi yetu iweze kupiga hatua za kimaendeleo kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge lako Tukufu pamoja na watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge letu Tukufu kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukurani za kipekee pia kwa Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Mwenyezekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini; na Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Makamu Mwenyezekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa maoni na ushauri wao waliokuwa wakiutoa katika utekelezaji wa shughuli za Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa wote walioteuliwa katika

kipindi hiki na kupata Ubunge. Kwa namna ya kipekee nimpongeze Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Kabudi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Sheria na Katiba. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika Mashariki na ni matarajio yetu kuwa watatuwakilisha kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupa pole wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza mwenzetu, Marehemu Samuel Sitta aliyekuwa Mbunge Mstaifu wa Jimbo la Urambo Magharibi, Spika Mstaifu wa Bunge la Tisa na Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Vilevile nitoe pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuwapoteza Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani - Zanzibar pamoja na Mheshimiwa Elly Marko Macha, Mbunge wa Viti Maalum wa CHADEMA. Pia natoa pole nyngi kwa wazazi, walezi, ndugu na familia za wanafunzi waliopata ajali kule Arusha. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wote wenzangu kutoa pole kwa familia za Marehemu na kumwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa shughuli kwa mwaka 2016/2017 pamoja na mpango wa bajeti wa 2017/2018. Maeneo yaliyopewa Kipaumbele kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 katika sekta ya nishati ni pamoja na kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme nchini, kuendelea na utekelezaji wa mpango wa kuboresha sekta ndogo ya umeme, kuendeleza nishati jadidifu, kuvutia uwekezaji katika sekta ya nishati hususan kwenye uzalishaji wa umeme na katika utafiti wa mafuta na gesi asilia. Aidha, Wizara ilifanya mapitio (*updates*) ya PSMP 2016 kwa lengo la kutumia vyanzo vyaa nishati

vilivyopo nchini ambapo gesi asilia itachangia asilimia 40, makaa ya mawe yamepangwa kuchangia asilimia 35, umeme wa maji tunalenga kuchangia asilimia 20 na vyanzo vingine asilimia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara ilitoa kipaumbele katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali za madini, kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini, kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani za madini, kuendelea na utafutaji wa *graphite* na madini mengineyo yanayohitajika katika teknolojia za kisasa na kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa afya, usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa. Sambamba na hayo, Wizara iliweka msisitizo katika kuwajengea uwezo watumishi katika fani mbalimbali na pia kusimamia, kufuatilia na kuboresha sera, sheria, kanuni, mipango na mlongozo mbalimbali ili kuboresha ufanisi na tija katika sekta ya nishati na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Wizara itaendelea kutekeleza maeneo ya vipaumbele mbalimbali yakiwemo kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini; kuimarisha ukusanyaji wa na mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali za gesi asilia na madini; kusimamia uingizaji, utunzaji na usambazaji wa mafuta nchini; kuwezesha uwekaji wa mtandao wa usambazaji wa gesi asilia viwandani na majumbani pamoja na uendelezaji wa mradi wa kusindika gesi asilia (*LNG*).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara pia itatekeleza maeneo mengine mapya ambayo ni pamoja na kuendeleza utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania; ujenzi wa bomba la mafuta safi kutoka Dar es Salaam, Tanzania hadi Ndola, Zambia; kukamilisha mazungumzo kuhusu ujenzi na upatikanaji wa gesi asilia kwenye viwanda vya mbolea vinavyotarajiwa kujengwa katika maeneo ya Kilwa Masoko, Lindi na Mtwara na

kuendelea na utekelezaji wa agizo la Serikali la kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati na Madini katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 330.68. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi, 2017 Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 266.21 sawa na asilimia 72. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 727.50 sawa na ongezeko la asilimia 96.3 ikilinganishwa na mwaka 2016/2017. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na mauzo ya gesi asilia ambayo mwaka 2017/2018 yanakadiriwa kufikia shilingi bilioni 477.36 ikilinganishwa na shilingi bilioni 115.13 kwa mwaka 2016/2017. Hii ni kutokana na kukamilika kwa bomba la gesi ambapo viwanda vingi vinatarajia kuunganishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyopitishwa kwa ajili ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2016/2017 ni jumla ya shilingi triliuni 1.122 ambayo inajumuisha fedha za miradi ya maendeleo shilingi triliuni 1.056, sawa na asilimia 94 ya bajeti yote. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa shilingi bilioni 66.23 sawa na asilimia sita. Hadi kufikia tarehe 25 Mei, 2017 Wizara ilishapokea jumla ya shilingi bilioni 591.39 sawa na asilimia 52.71.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) hadi kufikia tarehe 25 Mei, 2017 ulikuwa umepokea jumla ya shilingi bilioni 448.87 sawa na asilimia 76.39 ya bajeti yake kwa mwaka 2016/2017. Sambamba na hatua hiyo, Wizara imeendelea kusimamia kwa umakini mkubwa matumizi ya fedha za umma na kulingana na ukaguzi uliofanywa na *PPRA* katika kipindi cha mwaka 2015/2016 Wizara ya Nishati na Madini imekuwa miongoni mwa Wizara tatu bora kwa kupata alama ya asilimia 88.85. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2016/2017 Wizara ilitekeleza mipango na shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni mpango kabambe wa uendelezaji wa sekta ndogo ya umeme na matumizi ya gesi asilia. Mwezi Desemba, 2016 Serikali ilikamilisha mapitio ya mpango kabambe wa uendelezaji wa sekta ndogo ya umeme. Mpango huo umebainisha utekelezaji wa miradi ya uzalishaji na usafirishaji wa umeme katika kipindi cha muda mfupi, kati na mrefu. Mpango huo umezingatia ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini, gharama nafuu ya uwekezaji na uchangiaji wa vyanzo mbalimbali vya nishati (*energy mix*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia imeandaa rasimu ya mpango kabambe wa matumizi ya gesi asilia (*Natural Gas Utilization Master Plan*) chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (*JICA*). Mpango huu unatoa mwongozo kuhusu matumizi bora ya gesi asilia pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya gesi asilia. Aldha, mpango huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka 30 kuanzia 2017 hadi 2046 ambapo jumla ya futi za ujazo trilioni 18.7 za gesi asilia zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na jitihada za makusudi za kuongeza Idadi ya wananchi wanaopata huduma ya umeme nchini. Hadi kufikia Machi, 2017 idadi ya wananchi waliofikiwa na huduma ya umeme (*overall electricity access level*) imefikia asilimia 67.5 kulinganisha na asilimia 40 iliyo fikiwa mwezi Aprili, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, idadi ya wananchi wanaopata huduma ya umeme (*urban electricity access level*) imefikia asilimia 97.3 ikilinganishwa na asilimia 63.4 iliyo fikiwa mwaka 2014/2015, wakati wanaopata huduma ya umeme vijiji (*rural electricity access level*) imefikia asilimia 49.5 ikilinganishwa na asilimia 21 ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2017 idadi ya wananchi waliounganishiwa umeme (*overall electricity connection level*) imefikia asilimia 32.8 ikilinganishwa na asilimia 30 ya mwaka 2015/2016. Aidha, idadi ya wananchi

waliounganishiwa umeme mijini (*urban electricity connection level*) imefikia asilimia 65.3 wakati waliounganishiwa umeme vijijini (*Rural electricity connection level*) imefikia asilimia 16.9

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango ya kuongeza uzalishaji wa umeme nchini, Wizara imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo *Kinyerezi I megawatts 240, Kinyerezi I extension megawatts 185* na Mradi wa Rusumo *megawatts 80*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu wa Rusumo wa MW 80, Tanzania itapata MW 26.6. Katika kuendelea na utekelezaji wake, wakandarasi walisaini mkataba tarehe 9 Novemba, 2016. Aidha, malipo ya awali kwa Wakandarasi, kiasi cha dola za Marekani milioni 16.3 sawa na takribani shilingi bilioni 37.67 yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzinduzi rasmi wa kuanza ujenzi huo (*ground breaking ceremony*) ulifanywa na Mawaziri wanaosimamia masuala ya nishati wa nchi za Tanzania, Rwanda, Burundi, pamoja, Maafisa kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Afrika walihudhuria shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na miradi hiyo, Serikali pia ipo katika hatua mbalimbali za maandalizi ya utekelezaji wa miradi mingine ya uzalishaji umeme ikiwemo Mradi wa Malagarasi MW 45, Mradi wa Kakono (Kagera) MW 87, Mradi wa Somanga Fungu (Lindi) MW 300, *Kinyerezi III MW 600* na *Kinyerezi IV MW 330*, Mradi wa Mtwara MW 300, Mradi wa Kiwira MW 200 na Miradi ya uzalishaji ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miundombinu ya usafirishaji umeme, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ambayo ni pamoja na Mradi wa Msongo wa KV 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga ambao ulikamilika mwezi Desemba, 2016. Mradi wa Msongo wa KV 220, kutoka Makambako hadi Songea, Mradi wa Njia ya Umeme ya Msongo wa KV 400 wa Singida, Arusha, Namanga.

Aidha, miradi mingine ya usafirishaji umeme itakayoendelea kutekelezwa kwa mwaka 2017/2018 ni pamoja *North - West* kutoka Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi wa KV 400; Mradi wa *North - East* kutoka Kinyerezi hadi Arusha kuititia Chalinze na Segera wa KV 400, Somanga Fungu hadi Kinyerezi KV 400, Rusumo hadi Nyakanazi KV 220 pamoja Bulyanhulu hadi Geita KV 420. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kupeleka umeme vijiji awamu ya pili na kuanza awamu ya tatu ya miradi hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, hapo ndio niwaombe Waheshimiwa Wabunge mnapochangia, kumbuka kuandika vijiji vyenu ambavyo havijapata umeme kusudi kwa mamlaka nilliyonayo leo niweze kuwakumbuka. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijiji awamu ya pili (*REA Turnkey Phase II*); katika kipindi cha mwaka 2016/2017 Serikali kuititia *REA* imekamilisha kazi ya ujenzi wa vituo sita vya kuongeza nguvu ya umeme kutoka msongo KV 11 hadi KV 33 katika miji ya Kasulu, Kibondo, Kigoma, Mbinga, Ngara na Tunduru; ujenzi wa kusambaza umeme wa msongo wa KV 33 zenyen urefu wa kilometra 17,740; ujenzi wa vituo vidogo vya kupoozea na kusambaza umeme 4,100 na ujenzi wa njia ndogo ya usambazaji umeme zenyen urefu wa kilomita 10,970.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, wateja wa awali 153,821 waliunganishiwa umeme sawa na asilimia 62 ya lengo la kuwaunganishia wateja 250,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kazi ya kuunganishia umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya 13 za Busega, Buhigwe, Chemba, Itilima, Kakonko, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele, Momba, Nanyumbu, Nyasa na Uvinza zimekamilika na kufanya jumla ya Makao Makuu ya Wilaya zinazopata umeme kuititia *REA* kufikia 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu na hapo ndiyo pa kushika kalamu hapo!

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya mradi wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu yamekamilika na utekelezaji unaanza. Mradi huu ni wa miaka mitano kuanzia 2016/2017 hadi 2020/2021. Mradi unahusisha kuongeza wigo wa usambazaji umeme kwenye maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya umeme (*densification*); kufikisha umeme wa gridi kwenye vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme (*grid extension*); na miradi ya umeme ya nje ya gridi (*off-grid*) utokanao na nishati jadidifu, hasa umeme juu (*solar power*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizofikiwa kwa sasa ni pamoja na kusainiwa mikataba na kuanza utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa *densification* mwezi Desemba, 2016 na pia kukamilika taratibu za ununuzi na upatikanaji wa wakandarasi na kusambaza umeme kwenye vijiji vilivyo kwenye mkuza wa njia ya kusafirisha umeme wa kutoka Iringa hadi Shinyanga.

Aidha, uchambuzi wa maoni maombi 300 ya kusambaza umeme wa nishati jadidifu kwa vijiji vilivyo nje ya gridi ya Taifa umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na miradi hiyo ya REA, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mingine ya usambazaji nchini. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kuboresha mfumo wa huduma za umeme pamoja na njia ya usambazaji umeme kwenye Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro na pia katika Miji ya Ngara, Biharamulo na Mpanda na katika maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu itaendelea kusimamia kwa weledi na ufanisi miradi yote ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ili kufikia azma ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie sentensi hiyo. Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu itaendelea kusimamia kwa weledi na ufanisi miradi yote ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ili kufikia azma ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda. Neno nchi ya viwanda iko *bolded*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Serikali imeendelea kuendeleza rasilimali za mafuta na gesi asilia katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utafutaji wa mafuta na gesi asilia; kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2016/2017 utafiti wa mafuta na gesi asilia umeendelea kufanyika katika maeneo ya baharini na nchi kavu ambapo hadi kufikia sasa kiasi cha futi za ujazo *TCF* triliioni 57.25 za gesi asilia zimeshagundullika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza matumizi ya gesi asilia nchini, jumla ya viwanda 42 tayari vimeunganishwa na miundombinu ya gesi asilia. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imeendelea kutafuta wateja wapya na kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia. Majadiliano kati ya *TPDC*na *Dangote Cement Tanzania Limited* ya Mtwara yamekamilika kwa ajili ya kupata gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kiwanda cha *Goodwill Ceramic Tanzania* kilichopo Mkuranga kimeunganishwa tayari na kuanza kutumia gesi asilia. Majadiliano yanaendelea kati *TPDC*na viwanda vya *Bakhressa Food Factory*, *Knauf Gypsum* na *Lodhia Steel* vilivyopo Mkuranga Mkoani Pwani ili navyo kupatiwa gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na usimamizi wa uagizaji mafuta kwa pamoja kupitia wakala wake (*Petroleum Bulk Procurement Agency*). Pamoja na manufaa mengine, mfumo huu umesaidia kupunguza gharama za meli kusubiri kupakua mafuta (*demurrage costs*). Hivi sasa gharama hizo ni kati ya dola 1.6 mpaka 3.5 kwa

tani moja ya mafuta, tofauti na dola na 45 hadi 50 kwa tani moja iliyo kuwa ikitumika kabla ya mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichomekee, Tanzania tunaagiza takriban tani za mafuta milioni 2.5 zidisha na *demurrage* ya 50 tuliyokuwa tuna-*suffer*, leo tuna-*suffer demurrage* moja, utajua umuhimu wa mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kushuka kwa ghamra ya manunuzi (*premium*) kutoka wastani wa dola za Marekani 50 kwa tani, kabla ya utaratibu huu mpaka wastani wa takriban dola 20 kwa tani na uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini ni manufaa mengine ya mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Serikali itaanzisha mpango wa kuongeza upakuaji wa mafuta kwa kutumia Bandari ya Tanga yatakiyokuwa yanasantazwa Mikoa ya Kaskazini na pia kuanzisha Mfumo huu Bandari ya Mtwara kwa ajili ya mikoa ya kusini na na nchi jirani. Vilevile kuanzisha uingizaji wa bidhaa za *Liquefied Petroleum Gas* kwa kutumia mfumo wa uagizaji wa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2016/2017 taarifa ya tathmini ya athari za mazingira na kijamii imekamilika. Pamoja na taarifa hiyo, Mpango wa kuwapatia maeneo mbadala wananchi waishio katika eneo litakalojengwa mitambo ya *LNG* la Likong'o Mkoani Lindi (*resettlement action plan*) umekamilika. Vilevile, kazi za kuingiza michoro ya eneo la Mradi wa *LNG* kwenye ramani ya Mipango Miji imekamilika. Majadiliano yanaendelea kufikia makubaliano ya utekelezaji wa mradi huo ambao unataraji kuchukua muda wa takriban miaka nane hadi 10 kufikia uzalishaji kamili wa *LNG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kushiriki katika Miradi mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha mafuta kwa ajili ya manufaa zaidi kwa Taifa letu. Miradi hiyo ni ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi la

Afrika Mashariki kutoka Hoima Kabaale (Uganda) hadi Bandari ya Dar es Salaam (Tanzania) ambapo kazi zilizofanyika hadi mwezi Machi, 2017 ni pamoja na kusainiwa kwa Mkataba wa Makubaliano ya Awali (*MoU*); kufanya tathmini ya njia ya bomba (*survey*); tathmini ya mahitaji ya njia ya bomba (*infrastructure requirements*) na tathmini ya athari ya mazingira kijamii na kusainiwa kwa *Inter-Governmental Agreement* tarehe 26 Mei, 2017 Kampala Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwingine ni wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta safi (*White Petroleum Products*) kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia) ambao pia utahusisha ujenzi wa mabomba ya matoleo ya mafuta (*take-off points*) katika maeneo ya Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe. Mambo ya kusafirisha mafuta kwa malori utakwisha, watu wa Mikoa ya Kusini mtakuwa mnatumia bomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudzi za kupanua wigo wa vyanzo vya umeme nchini, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya nishati jadidifu ambayo ni pamoja na nishati ya jua, nishati ya upepo, miradi ya tungamotaka, umeme wa maporomoko madogo ya maji, usambazaji wa umeme kwa mfumo wa gridi ndogo na uendelezaji wa matumizi ya *biogas*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi (*Tanzania Geothermal Development Company Limited*) ambayo ni kampuni tanzu ya TANESCO, imekamilisha utafiti wa kina (*detail surface study*) wa uendelezaji nishati ya jotoardhi katika maeneo ya Ziwa Ngozi kule Mbeya. Utafiti umewezesha kuainisha sehemu tatu za kuchoronga visima vya majoribio katika eneo la Ziwa Ngozi ili kutathmini kiasi cha hifadhi ya rasilimali ya jotoardhi na uwezo wake wa kuzalisha umeme.

Vilevile Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha utafiti wa kina katika maeneo ya Mbaka-Kiejo, Mkoani Mbeya na Luhoi Mkoani Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa sekta ya madini katika mwaka 2016/2017 na mpango kwa mwaka 2017/2018; Serikali imeendelea kuchukua hatua na kuweka mipango mbalimbali ya kuendeleza utafutaji na ugunduzi wa gesi ya *Helium* ambayo ni adimu duniani. Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Kampuni ya *Helium One Limited* imeendelea kufanya utafiti wa gesi hiyo kupitia kampuni zake tanzu za *Gogota (TZ) Limited*, *Njozi (TZ) Limited* na *Stahamili (TZ) Limited* kwenye Mikoa ya Rukwa na Manyara. Utafiti uliofanyika umewezesha kugundulika kwa *Helium* ya wingi wa takriban futi za ujazo bilioni 54 kutokana na sampuli za mavujia (*gas seeps*) zilizochukuliwa katika maeneo matano yaliyopo Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za kuchoronga visima vya utafiti katika maeneo hayo zinatarajiwa kuanza mwaka 2018 ili kuhakikil kiasi halisi cha gesi ya *Helium* kilichopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka 4% mwaka 2015 kutoka asilimia 3.7 ya mwaka 2014 katika kipindi cha kuanzia Machi - Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara ilikusanya mrabaha wa jumla ya dola za Marekani milioni 56.77 sawa na shilingi bilioni 130.90 kutoka kwenye migodi mikubwa ya Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, *New Luika*, *North Mara*, *STAMIGOLD*, *Tanzanite One*, Mwadui, Ngaka na Dangote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kiasi cha mrabaha wa shilingi bilioni 4.23 kilikusanywa kutokana na mauzo ya dhahabu illyozalishwa kwa kuchenjua "*vat leaching*." Aidha, shilingi bilioni 4.45 ulikusanywa kutokana na uzalishaji wa madini ya ujenzi na viwandani. Vilevile kiasi cha shilingi milioni 14.52 kutokana na ada za leseni na vibali mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara ilikusanya mrabaha wa dola za Marekani milioni 2.40 sawa na shilingi bilioni 5.55 kutokana na mauzo ya Almasi na dola za Marekani 906,347 sawa na shilingi bilioni 2.09 kutokana na mauzo ya vito ghafi na vilivyokatwa. Katika kipindi hicho, Serikali pia

ilikusanya Kodi ya Mapato (*Corporate Tax*) ya jumla ya shilingi bilioni 79.26 kutoka kwa Kampuni ya Geita *Gold Mining Limited* na *North Mara Gold Mine Limited*.

Mheshimia Naibu Spika, katika kipindi hiki Kampuni za uchimbaji mkubwa wa madini zimeendelea kulipa ushuru wa huduma (*service levy*) kwa Halmashauri mbalimbali ambapo Jumla ya shilingi bilioni 11.27 zimelipwa. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Wizara itaendelea kuzipatia Halmashauri husika takwimu sahihi za mauzo ya madini ili kuwezesha ukusanyaji ushuru wa huduma kutokana na uchimbaji wa madini ndani ya Halmashauri zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya wakia milioni 1.05 za dhahabu, wakia 414,128 za fedha na ratili milioni 10.4 za shaba, zenye jumla ya thamani ya dola za Kimarekani bilioni 1.36 sawa na shilingi trilioni 3.14 zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka migodi ya *STAMIGOLD*, Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, *New Luika* na *North Mara*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa wawekezaji wakubwa. Naomba nirudie, Serikali inatambua umuhimu wa wawekezaji wakubwa wa nje na wa ndani katika uwekezaji kwenye sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali inadhamiria kushirikiana na wadau kupitia sera, sheria na mikataba ya uendelezaji wa sekta hii ili kuhakikisha uwekezaji katika sekta unaendelea na kushamiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na jitihada za kuendeleza uchimbaji mdogo wa ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo zaidi kwa ajili ya wachimbaji wadogo, kutenga fedha zaidi za ruzuku na kuimarisha shughuli za ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kipindi hiki Serikali kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini wa Benki ya Dunia Awamu ya Pili inaendelea na

hatua za uanzishwaji wa Vituo vyta Mfano saba vyta kuchenjua madini katika maeneo ya Buhemba (Mara), D-Reef na Kapanda (Mpanda), Itumbi (Chunya), Katente (Geita), Kyerwa (Kagera) na Maweni (Tanga).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Wizara itaendelea kutoa huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo nchini. Aidha, kwa kupitia *STAMICO* na *GST*, imepanga kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wachimbaji wadogo 4,000 katika Kanda za Kusini, Ziwa Nyasa, Kati na Kusini Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya maombi ya leseni 8,942 ya utafutaji na uchimbaji wa madini yalipokelewa na Wizara kwa njia ya mtandao. Ili kuhakikisha leseni zinazotolewa zinafanyiwa kazi, Wizara imeendelea kufuatilia wamiliki wa leseni na walibainika kutotekeleza masharti husika ya leseni hizo walifutiwa leseni zao. Katika kutekeleza azma hiyo, jumla ya leseni 2,153 zilifutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kutoa wito kwa wadau wa sekta ya madini kujisajili kwa njia ya mtandao ili kurahisisha huduma za utoaji leseni na kuongeza uwazi hivyo kupunguza malalamiko ya kuwepo kwa upendeleo katika utoaji wa Leseni za Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya migodi 1,115 ilikaguliwa na kuhakikisha kuwa salama, afya na utunzaji wake ulikuwa vizuri. Pia usalama na mazingira ya migodi unazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudhi hizo za Wizara katika ukaguzi wa migodi, ajali zimeendelea kutokea hususan kwenye migodi ya wachimbaji wadogo. Katika kipindi cha hiki jumla ya ajali 17 zilitokea katika migodi hiyo na kusababisha vifo vyta wachimbaji 30. Aidha, katika ajali hizo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya madini walifanikiwa kuokoa wachimbaji 42 wakiwa hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuongezeka kwa ajali katika migodi, Wizara yangu katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 itaimarisha ukaguzi wa Migodi hiyo nchi nzima na kuwa na taarifa za kila mwezi. Migodi yote ambayo itabainika kutokidhi vigezo vya kiusalama kwa mujibu ya Kanuni za Afya na Usalama Migodini za mwaka 2010 itafungwa mara moja hadi marekebisho stahiki ya kiusalama yatakapofanyika na kuridhiwa na Mkaguzi wa Migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha na kuwezesha Kampuni za Madini kuendelea na miradi mikubwa ya madini. Miradi hiyo ni pamoja na *graphite* (Kinywe) iliyopo Nachu, Namangale na Chilalo Wilayani Ruangwa; Chidya na Chiwata Wilayani Masasi na Epanko, Mahenge Wilayani Ulanga. Madini ya *graphite* yanatumika kwenye kutengeneza vilainishi (*lubricants*), betri na vifaa vya kwenye injini za magari. Uwekezaji katika miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali za kukamilisha tathmini ya athari za mazingira na ulipaji wa fidia. Aidha, Miradi ya *Rare Earth Elements (REE)* na *Niobium* iliyopo katika Wilaya ya Songwe ipo katika hatua za juu za utafiti na uanzishwaji wa migodi sawia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi wanaozunguka migodi kuhusu fursa zilizopo katika migodi inayowazunguka. Kwa hali ilivyo sasa, ushiriki wa Watanzania katika kutoa huduma na kuuza bidhaa kwenye Migodi umefikia takriban asilimia 50. Vilevile, Wizara inaendelea kuhamasisha migodi kutoa zabuni kwa Wananchi wanaozunguka migodi na Kampuni za Wakandarasi wa Kitanzania ili kutoa fursa kwa Watanzania kuuza huduma na bidhaa kwenye migodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza ushiriki wa Watanzania katika migodi mikubwa, Serikali imetunga sheria na kanuni za kuzitaka kampuni za madini zenyе leseni kubwa za uchimbaji kuandikisha asilimia 30 ya hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Natoa wito kwa wananchi kujiardaa ili Kampuni za madini zikisajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar

es Salaam, Watanzania wajitokeze kwa wingi kununua hisa na hivyo kushiriki kwenye umiliki wa rasilimali zao za madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara itaendelea kuchukua hatua za makusudi kuelimisha umma kuhusu manufaa na fursa zilizopo katika sekta ya madini na kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali, kujenga uwezo wa Watanzania kushiriki katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Wizara imefanikiwa kufanya minada miwili ya Madini ya Tanzanite Mkoa wa Arusha ambapo mnada wa kwanza ulifanyika mwezi Agosti, 2016 na mnada wa pili ulifanyika mwezi Machi, 2017. Katika mnada wa Kwanza madini yenye thamani ya dola za Marekani milioni 3.45 yaliuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya mrabaha wa thamani ya dola za Marekani 150,491 sawa na shilingi milioni 347.78.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mnada wa pili, madini yenye thamani ya dola za Marekani milioni 4.20 yaliuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya mrabaha wa dola za Marekani 210,114.36 sawa na shilingi milioni 485.57. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ilikusanya ushuru wa huduma kiasi cha shilingi milioni 27.99.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na faida nyingine, minada hii husaidia kupunguza utoroshaji wa madini nje ya nchi na kuitangaza Tanzania katika medani ya Kimataifa kuhusu fursa za madini zilizopo hapa nchini. Aidha, Wizara ilifanya Maonesho ya Kimataifa ya Vito na Usonara, Arusha kuanzia tarehe 3 hadi 5 Mei, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini umeanza ujenzi wa Kituo cha Mafunzo kwa wachimbaji wadogo cha Rwanagasa, Geita. Kituo hiki kinajengwa kwa ushirikiano baina ya Wizara, Mgodi wa Geita na Ushirika wa Wachimbaji Wadogo wa Rwanagasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli nyingine zilizofanyika ni kukamilisha utaratibu wa ununuzi kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi za Madini za Bariadi, Bukoba, Chunya, Kigoma, Mpanda, Musoma, Songea, Ofisi za *STAMICO* na Chuo cha Madini Dodoma. Aidha, ununuzi wa vifaa mbalimbali vyta kutoa huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo kupitia *STAMICO*, *GST* na Ofisi za Madini za Kanda umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara kupitia mradi wa *SMMRP* unatarajia kuanza ukarabati na upanunzi wa Ofisi za Madini za Bariadi, Bukoba, Chunya, Kigoma, Mpanda, Musoma, Songea, ofisi za *STAMICO* na Chuo cha Madini Dodoma. Lengo la ni kuboresha mazingira ya kazi ya ofisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walifanya utafiti wa tetemeko la ardhi lillotokea Mkoani Kagera tarehe 10 Septemba, 2016 na kuaandaa taarifa za utafiti. Pia wataalamu kutoka Wakala, Chuo cha Ardhi na Chuo cha na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walitoa elimu kwa Umma na kwa wahanga wa tetemeko hilo. Aidha, wakala uliendelea kukusanya takwimu kutoka vituo nane vyta kudumu vilivyoko nchini vyta kupimia matetemeko ya ardhi, kuchakata takwimu, kuchora ramani na kuhifadhiya kwenye kanzidata kisha kuzitolea taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 wakala utaendelea kuratibu majanga asilia ya kijiolojia ikiwemo pamoja na matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano, maporomoko ya ardhi ili kubaini maeneo yenye hatari ya kupata maporomoko ya ardhi na kutoa ushauri kwa wananchi waishio katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mwaka 2009 ilianzisha wakala maalum kwa ajili ya ukaguzi wa shughuli za uwekezaji katika sekta ya madini, kazi kubwa ikiwa ni pamoja na kukagua gharama za uwekezaji wa makampuni makubwa, mapato yatokanayo na uwekezaji huo, kodi pamoja na mrahaba. *TMAA* hufanya kazi hizi kwa kushirikiana na Ofisi za Madini za Kanda, *TRA* pamoja na Wizara ya Mambo

ya Ndani. Utendaji wa taasisi hii uliendelea kuonyesha mapungufu katika sekta kwa kubaini mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali. Pamoja na utendaji huo, wadau mbalimbali wakiwemo wananchi wa kawaida waliendelea kupaza sauti wakidai Taifa linaibiwa kuitia miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia maoni na ushauri wa wadau wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa kulinda maslahi ya Taifa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuweka wataalamu wa kukagua uzalishaji wa madini katika baadhi ya migodi mipakani, viwanja vya ndege na katika bandari. Kutokana na jitihada hizo, kwa mwaka wa 2016/2017 wakala uliweza kukamata madini jumla ya thamani ya dola za Kimarekani 119,906.45 sawa na shilingi milioni 277.10 katika viwanja vya ndege vya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine iliyochukuliwa na Serikali ni kuifanya marekebisho Sheria ya Madini Namba 18 ya mwaka 2010 kuitisha Sheria ya Uwazi na Uwajibakaji katika rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia, *TEITI Act* Na. 23 ya mwaka 2015 ili kuruhusu kuwekwa uwazi taarifa za ustawishaji, gharama za uwekezaji na uendeshaji pamoja na mapato yatokanayo na madini ili kuongeza uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 wakala ulifanya ukaguzi na kuwezesha Serikali kukusanya mrabaha wenye thamani ya shilingi bilioni 4.45 ikilinganishwa na jumla ya shilingi bilioni 6.27 zilizokusanywa kwa kipindi cha 2015/2016. Kiwango kidogo cha mrabaha uliopatikana, kushuka kwa mrabaha kwa mwaka 2016/2017 na vilio vya wananchi viliipelekea Serikali kuchua hatua mbalimbali ili kuhakikisha mapato ya Serikali yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka fedha 2017/2018, Serikali itaimarisha Wakala wa Ukaguzi wa Madini kwa kuzingatia maoni na ushauri wa wadau mbalimbali pamoja na ushauri wa Kamati za kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile maoni na ushauri Maalum iliyoundwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuchunguza mchanga uliomo katika makontena ya makinikia ya dhahabu utazingatiwa. Lengo la jitihada hizi ni kuhakikisha kwamba Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali za madini. (*Makof*)

Aidha, tuna matumaini makubwa kuwa maoni, ushauri na maelekezo yatakayotolewa na Kamati Maalum iliyoundwa na Mheshimiwa Rais kupitia mfumo wa kisera, kisheria na kimundo kuhusu uendeshaji wa shughuli za Wizara hii katika masuala ya rasilimali ya madini tutatekeleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *STAMICO* imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mradi wa kununua madini ya bati kutoka kwa wachimbaji wadogo walioko Kyerwa Mkoani Kagera. Hadi kufikia Machi, 2017 tani 18.08 za madini hayo ziliuzwa na kulipatia Taifa jumla ya shilingi 325.49 ambazo Serikali ilipata mrahaba wa shilingi milioni 13.02 na shilingi 976,471 zimelipwa katika Halmashauri kama ushuru.

Vile vile ili kukidhi mahitaji ya makaa ya mawe nchini, *STAMICO* imeaanza rasmi uchimbaji wa makaa hayo katika kilima cha Kabulo Kiwira kuanzia mwezi Aprili, 2017. Jumla ya tani 107,078 zinakadiriwa kuchimbwa kwa mwaka. Lengo la mradi huu ni kuviuzia viwanda makaa ya mawe kwa ajili ya utengenezaji wa saruji na marumaru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Madini Dodoma kimedahili jumla ya wanafunzi 527 katika fani za Jiolojia na Utafutaji Madini, Uhandisi Migodi, Uhandisi Uchenjuaji Madini, Sayansi za Mafuta Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini. Pia chuo kimeandaa mtaala mpya wa upimaji ardhi na migodi ambao umewasilishwa *NACTE* kwa ajili ya usajili.

Aidha, chuo kimefanya upanuzi na ukarabati wa ofisi na madarasa, ujenzi wa ukumbi wa mihadhara pamoja na viwanja vyatia michezo katika mwaka wa fedha 2017/2018

chuo kitaendelea kupanua wigo wake kwa kutoa mafunzo, kuanzisha programu mbalimbali za upimaji ardhi migodini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua mchango wa taasisi mbalimbali za Serikali na washirika wa maendeleo ambao wamekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudii za Serikali za kuleta maendeleo kupitia misaada yao mbalimbali kwenye Sekta za Nishati na Madini.

Kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani za dhati kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini, Benki ya Dunia, Benki ya Exim China, Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa Japan, Benki ya Maendeleo ya Kiarabu, Benki ya *Unicredit Austria*, *Climate Investment Fund, Economic Development Cooperation Fund, OPEC Fund for International Development*, Mfuko wa Uendelezaji Jotoardhi pamoja na Taasisi na Mashirika ya *AFD* (France), Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa *ICEIDA, CIDA, DfID, IDA*, Benki ya Dunia, *JICA, KfW* (Germany), *GIZ* (Germany), *NORAD* (Norway), *NDF* (nchi za Nordic), *SIDA* (Sweden), Umoja wa Ulaya, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) *The Netherlands (DRIVE)*, *USAID* na nchi za Brazil, Denmark, Finland, Iceland, Norway na Korea ya Kusini kwa kutakja baadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/2018 Serikali kupitia Wizara hii itaendeleza ushirikiano wa shirika hawa kwa maendeleo na mengine kwa ujumla. Hiyo ndiyo inataitwa *economic diplomacy*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani. Naomba nimalizie kwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Merdad Matogolo Chananja Kalemani, Mbunge wa Chato, Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa mchango wake katika kusimamia sekta hii. Nakiri wazi kuwa mchango wake umekuwa msaada mkubwa katika kuendeleza sekta hii. Naomba nichomekee kidogo, napenda kusema kwamba Mheshimiwa Kalemani amevivaa kikamilifu viatu vya mtangulizi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nitumie nafasi hii kuwashukuru Naibu Makatibu Wakuu Profesa James Epiphan Mdoe pamoja na Mhandisi Juliana Leonard Pallangyo, Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa michango yao na utendaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii ya kipekee kuwashukuru Wakuu wote wa Taasisi, Wenyeviti wa Bodi na Wajumbe wa Bodi za Taasisi pamoja na watumishi mbalimbali wa taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mchango wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii. Mtawaona nje, hata mvao wao inaonekana kwamba wanatoka kwenye nishati na madini. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kumshukuru tena, Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyojitoa kusimamia rasilimali za nchi hii na kulinda maslahi mapana ya wananchi wa Taifa letu. Nawashukuru wananchi kwa namna ya kipekee wanaojitokeza kumuunga mkono Mheshimiwa Rais na kumwombea kila anapochukua hatua ili kuwaleta maendeleo Watanzania. Hakika kiongozi wetu mkuu anastahili maombi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2017/2018 pamoja na kutumika katika kutekeleza shughuli mbalimbali, imelenga katika kutekeleza miradi mikubwa ya nishati ili kuchochea sekta za kiuchumi na hivyo kukuza uchumi wa Taifa letu na maendeleo ya Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia katika kipindi hiki itaendelea na utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Tano ya upatikanaji wa nishati ya uhakika ili kuwezesha kufikiwa kwa lengo la Taifa ya kuwa nchi ya viwanda. Katika kutekeleza azma hiyo, fedha za miradi ya maendeleo ambazo ni shilingi bilioni 756.76 sawa na asilimia 80.6 ya fedha zote za maendeleo zimeelekezwa katika kutekeleza miradi ya kimkakati ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupidisha Makadirio ya fedha jumla ya shilingi 998,337,759,500 kwa mwaka wa 2017/2018. Mchanganuo wa bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Shilingi 938,632,006,000 sawa na asilimia 94.1, bajeti yote ni kwa ajili ya kutekeza miradi ya maendeleo. Asilimia 94.1 ya bajeti hii ni kwa ajili ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 763,304,679,000, sawa na asilimia 81 ya fedha zote za maendeleo ni fedha za ndani na shilingi 175,327,327,000, sawa na asilimia 19 ni fedha za kutoka nje.

(ii) Shilingi 59,705,753,500 sawa na asilimia 5.9 ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo ya Wizara Katiya fedha hizo, shilingi 28,833,681,500 sawa na asilimia 48.3 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 30,872,072,000 sawa na asilimia 51.7 zitatumika kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya [www.mem.go.tz](http://www.mem.go.tz) vilevile hotuba hii ina vielelezo mbalimbali kama mlivyoviona kwa ajili ya ufanuzi wa masuala muhimu yanayohusu sekta ya nishati na madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuota hoja.  
(*Makofii*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

**HOTUBA YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KUHUSU  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA  
FEDHA 2017/2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1. *Mheshimiwa Spika*,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha mpango na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

**2. *Mheshimiwa Spika*,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema sisi Waheshimiwa Wabunge wote na hivyo kutuwezesha kuendelea na utekelezaji wa majukumu yetu ya kitaifa ndani na nje ya Bunge. Kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu, Bunge limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kikatiba likiwemo la kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**3. *Mheshimiwa Spika*,** nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati viongozi wetu wa kitaifa kwa jinsi wanavyojituma katika kutatua matatizo na changamoto mbalimbali za Taifa letu na hatimaye kuwaletea wananchi maendeleo. Viongozi hao wameendelea kutoa miongozo ambayo kila mara imekuwa ikilenga kuwaondolea wananchi kero mbalimbali katika maeneo yao. Dhamira hii imedhihirika wazi kwa jinsi Serikali ya Awamu ya Tano inavyoshughulikia masuala yenye maslahi ya kitaifa yakiwemo ya vita dhidi ya rushwa, madawa ya kulevyaa, ubadhirifu wa mali za Umma, malipo hewa pamoja na kurudisha uwajibikaji Serikalini.

**4. *Mheshimiwa Spika*,** kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake jinsi anavyochukua hatua za kusimamia na kulinda rasilimali za Taifa hasa madini.

**5. Mheshimiwa Spika**, naomba pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kazi yake nzuri anayoendelea kuifanya tangu alipoteuliwa. Aidha, nampongeza Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa jinsi anavyoendelea kusimamia kwa karibu shughuli za Serikali tangu Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani. Ni wazi kuwa Viongozi wetu hao wa kitaifa kwa kipindi kifupi walichokaa madarakani wamefanya kazi nzuri na kubwa kwa kutoa na kutekeleza miongozo makini ya kulisaidia Taifa letu. Tuwaombee wote kwa Mwenyezi Mungu ili waendelee na kasi hiyo ambayo imekuwa ni chachu ya mabadiliko katika nyanja mbalimbali na hatimaye nchi yetu iweze kupiga hatua za kimaendeleo kwa kasi kubwa zaidi.

**6. Mheshimiwa Spika**, nikupongeze wewe binafsi, Mheshimiwa Nailbu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge lako Tukufu pamoja na Watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge letu Tukufu kwa ufanisi mkubwa. Nitoe Shukrani za kipekee pia kwa Mhe. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mhe. Deogratias Francis Ngalawa (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Kwa kweli, nikiri kuwa Kamati hii imekuwa msaada mkubwa katika usimamizi na uendelezaji wa Sekta za Nishati na Madini nichini kutokana na maoni na ushauri wao wanaoutoa kwa Serikali kuititia Wizara yangu.

**7. Mheshimiwa Spika**, naomba kuungana pia na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya walioteuliwa hivi karibuni na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaeo ni: Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete; Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo; Mheshimiwa Anne Killango Malecela; na Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum kuititia CCM.

Pia, nampongeza Mheshimiwa Juma Ali Juma, Mbunge wa Jimbo la Dimani kwa heshima kubwa aliopewa na wananchi wa Jimbo la Dimani ili awawakilishi kwenye Bunge hili la kumi na moja (11). Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia CHADEMA. Niwapongeze pia Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika Mashariki na ni matarajio yetu kuwa Wabunge hao wenzetu watatuwakilisha kwa ufanisi na umakini mkubwa kwenye Bunge la Afrika Mashariki.

**8. *Mheshimiwa Spika*,** nikupe pole wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza mwenzetu tuliyeCAA naye humu kwa muda mrefu, marehemu Samwel Sitta aliyekuwa Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Urambo Magharibi, Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa (2005 – 2010) na Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Wote tunakiri kuwa Kiongozi huyo alikuwa mchapakazi, hodari na mwenye msimamo katika masuala yenyе tija kwa Taifa. Vilevile, nitoe pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuwapoteza Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani, Zanzibar; pamoja na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha, Mbunge wa Viti Maalum wa CHADEMA. Naungana na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia za marehemu. Pia, natoa pole nydingi kwa wazazi, walezi, ndugu na familia za wanafunzi wa Shule ya Msingi Lucky Vicent waliopoteza maisha katika ajali ya gari iliyotokea Wilayani Karatu hivi karibuni. Msiba ni suala gumu, lakini hatuna la kufanya zaidi ya kumwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amen.

**9. *Mheshimiwa Spika*,** baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kuwasilisha **Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 pamoja na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.**

**B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA 2016/17 PAMOJA NA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/18**

**10. *Mheshimiwa Spika*,** Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 katika Sekta ya Nishati ni pamoja na: kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme nchini; Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Sekta Ndogo ya Umeme (*Electricity Supply Industry Reform Strategy and Roadmap*); Kuendeleza Nishati Jadidifu (*Renewable Energies*) kama vile umeme juu, upepo, maporomoko madogo ya maji, jotoardhi na tungamotaka; na kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Nishati, hususan kwenye uzalishaji wa umeme na katika utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia.

**11. *Mheshimiwa Spika*,** pamoja na maeneo hayo ya Nishati, Wizara pia ilitoa kipaumbele katika Sekta ya Madini hususan katika: Kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali za madini kwa kuziwezesha Ofisi za Madini za Kanda, Ofisi za Afisa Madini Wakazi, Kitengo cha Leseni cha Wizara pamoja na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA); Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo na wa Kati wa madini; Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani wa madini; Kuendelea na utafutaji wa *graphite* na madini mengine yanayohitajika kwenye teknolojia ya kisasa (*Rare Earth Elements-REE*); na Kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa afya, usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa.

**12. *Mheshimiwa Spika*,** sambamba na maeneo hayo ya ki-Sekta, Wizara vilevile iliweka msisitizo katika maeneo mengine yakiwemo: kuwajengea uwezo Watumishi wa Wizara katika fani za Umeme, Mafuta, Gesi Asilia, Jiolojia, Jemolojia, Uhandisi Migodi na Uthaminishaji wa Vito na Almasi; kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano kati ya Wizara na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya Nishati na Madini; kuboresha mazingira ya Ofisi na vitendea kazi kwa Watumishi ili kuongeza ufanisi na ubora katika utoaji wa huduma zinazohusu Nishati na Madini; na kusimamia,

kufuatilia na kuboresha Sera, Sheria, Kanuni, Mipango na Miongozo mbalimbali ili kuboresha ufanisi na tija katika Sekta za Nishati na Madini.

**13. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara ya Nishati na Madini itaendelea kutekeleza maeneo ya vipaumbele mbalimbali yakiwemo: kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini; kuimarisha ufuutilaji na ukaguzi wa afya, usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali za Gesi Asilia na Madini; kusimamia uingizaji, utunzaji na usambazaji wa mafuta nchini; na kuwezesha uwekaji wa mtandao wa usambazaji wa Gesi Asilia viwandani na majumbani pamoja na uendelezaji wa Mradi wa Kusindika Gesi Asilia (*Liquefied Natural Gas - LNG*). Aidha, Wizara pia itatekeleza maeneo mengine mapya ambayo ni pamoja na: kuendelea na utekelezaji wa Mradi Mkubwa wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Kabaale (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Ujenzi wa Bomba la Mafuta Safi kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia); Kukamilisha mazungumzo kuhusu ujenzi na upatikanaji wa Gesi Asilia kwenye Viwanda vya Mbolea vinavyotarajwa kujengwa katika maeneo ya Kilwa Masoko (Lindi) na Mtwara; Kuendelea na ujenzi wa Mradi wa kuzalisha umeme wa Rusumo, **MW 80**; na Kuendelea na utekelezaji wa Agizo la Serikali la kuhamia Dodoma.

#### *Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka 2016/17*

**14. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara ya Nishati na Madini katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ilipanga kukusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 370.68** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 286.66** kwa Mwaka 2015/16. Mapato hayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo: Ada za kijiolojia; Mrabaha; Ada za Mwaka za Leseni; Mauzo ya Nyaraka za Zabuni; Mauzo ya Gesi Asilia; Tozo ya mauzo ya umeme; na Shughuli za utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia. Hadi kufikia mwishoni mwa Mwezi Machi, 2017 Wizara ilikuwa imekusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 266.21** sawa na **asilimia**

72 ya lengo lilokusudiwa. Wizara itaendelea na juhudzi za kukusanya ili kufikia lengo liliowekwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17.

**15. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara inatarajia kukusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 727.50** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 370.68** kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kutokana na vyanzo vyake vya mapato, sawa na ongezeko la **asilimia 96.3**. Ongezeko hilo la makisio ya makusanyo limetokana na kuongezeka kwa mchango wa mapato yatokanayo na mauzo ya Gesi Asilia ambayo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 yalikadiriwa **Shilingi bilioni 115.13** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 477.36** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Kuongezeka kwa mauzo ya Gesi Asilia kutatokana na kuanza kutumika kwa Gesi Asilia katika viwanda vipyta vikubwa. Viwanda hivyo ni pamoja na: GOODWILL, Bakhresa Food Products na Lodhia Group vilivyopo Mkuranga - Pwani; Dangote kilichopo Mtwara; pamoja na Coca - Cola na Bidco vilivyopo Kinondoni - Dar es Salaam.

***Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini Kwa Mwaka 2016/17***

**16. *Mheshimiwa Spika*,** Bajeti iliyopitishwa kwa ajili ya Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ni Jumla ya **Shilingi triliioni 1.122**. Bajeti hiyo inajumuisha Fedha za Miradi ya Maendeleo **Shilingi triliioni 1.056**, sawa na **asilimia 94** ya Bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo za Maendeleo, **Shilingi bilioni 724.84** sawa na **asilimia 68.6** ni fedha za Ndani na **Shilingi bilioni 331.51** sawa na **asilimia 31.4** ni fedha za Nje. Kwa upande wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida, Wizara na Taasisi zake ilitengewa Jumla ya **Shilingi bilioni 66.23**, sawa na **asilimia 6** ya Bajeti yote kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 38.87**, sawa na **asilimia 58.7** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C.) na **Shilingi bilioni 27.36**, sawa na **asilimia 41.3** ni Mishahara kwa ajili ya Idara, Vitengo na Taasisi zilizopo chini ya Wizara. **Fedha zilizopokelewa hadi Mwezi Mei, 2017**

**17. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 25 Mei, 2017 Wizara ilikuwa imepokea Jumla ya **Shilingi bilioni 591.39**, sawa na **asilimia 52.71** ya Bajeti yote iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ambayo ni **Shilingi trilioni 1.122**. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, **Shilingi bilioni 51.64** ni fedha za Matumizi ya Kawaida ambapo Matumizi Mengineyo (O.C.) ni **Shilingi bilioni 28.48** na Mishahara (P.E.) kwa Wizara na Taasisi zake ni **Shilingi bilioni 23.16**. Kiasi kilichopokelewa ni sawa na **asilimia 77.97** ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida zilizotengwa ambazo Jumla yake ni **Shilingi bilioni 66.23**.

**18. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho Jumla ya **Shilingi bilioni 654.06** ambazo ni fedha za Miradi ya Maendeleo zilipokelewa ambapo fedha za Ndani ni **Shilingi bilioni 522.96** na fedha za Nje ni **Shilingi bilioni 131.1**. Fedha hizo ni sawa na **asilimia 61.93** ya Bajeti yote ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ambayo ni **Shilingi trilioni 1.056**. Fedha hizo zilizopatikana zilielekezwa katika Miradi ya kupeleka umeme vijijini kuititia Wakala wa Nishati Vijijini (REA); Mradi wa *Kinyerezi I Extension (MW 185)*; ulipaji wa deni la Mradi wa *Kinyerezi I (MW 150)*; Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme ya Makambako – Songea (kV 220); malipo ya madeni ya TANESCO na Mradi wa Uendelezaji wa Rasilimali za Madini (SMMRP). Aidha, kwa upande wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) hadi kufikia tarehe 25 Mei, 2017 ulikuwa umepokea Jumla ya **Shilingi bilioni 448.87** sawa na **asilimia 76.39** ya Bajeti yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17.

*Ufanisi wa Wizara katika Masuala ya Manunuza*

**19. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia matumizi ya fedha za Umma kwa umakini mkubwa kwa kuhakikisha kuwa masuala ya ununuza yanafanyika kwa ufanisi mkubwa. Katika ukaguzi wa ununuza (*Procurement Audit*) uliofanywa na PPRA katika kipindi cha Mwaka 2015/16, Wizara ya Nishati na Madini imekuwa mionganoni mwa Wizara tatu bora kwa kupata **alama ya asilimia 88.85**. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kusimamia manunuza kwa ufanisi zaidi katika

kuhakikisha kuwa fedha za Umma zinatumika ipasavyo kwa maslahi ya maendeleo ya Taifa letu.

## **SEKTA YA NISHATI**

### **SERA, MIPANGO NA SHERIA KATIKA SEKTA YA NISHATI**

*Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Umeme (PSMP) na Matumizi ya Gesi Asilia (NGUMP)*

**20. Mheshimiwa Spika,** Serikali katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 imekamilisha mapitio ya Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Umeme (*Power System Master Plan - PSMP 2016 Update*) ambayo ilikamilika Mwezi Desemba, 2016. Mpango huo umebainisha utekelezaji wa Miradi ya uzalishaji na usafirishaji wa umeme katika kipindi kifupi (2016 – 2020), kati (2021 - 2025) na kirefu (2026 - 2040). Katika kipindi kifupi, kiasi cha **MW 4,193** zinahitajika, kipindi cha kati **MW 1,280** na kirefu **MW 14,646** zinahitajika kuongezwa ili kuweza kukidhi mahitaji ya umeme nchini.

**21. Mheshimiwa Spika,** Mpango huo wa PSMP umezingatia ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini, gharama nafuu ya uwekezaji na uchangiaji wa vyanzo mbalimbali vya nishati (*energy mix*) ambapo umeme utazalishwa kutokana na Gesi Asilia, maporomoko ya maji, makaa ya mawe, juu, upepo, jotoardhi na tungamotaka. Mapitio hayo yalifanyika kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo: Wizara na Taasisi za Serikali; Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA); na Sekta Binafsi.

**22. Mheshimiwa Spika,** sambamba na mapitio ya PSMP, Wizara pia imeandaa Rasimu ya Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia (*Natural Gas Utilization Master Plan - NGUMP*) chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) kwa kushirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali, Sekta Binafsi na Wataalam kutoka nchi za Japan pamoja na Trinidad and Tobago. Mpango huu unatoa mwongozo kuhusu matumizi bora ya Gesi Asilia, uboreshaji

wa miundombinu ya Gesi Asilia pamoja na kuweka misingi ya kuhakikisha Sekta zote za uchumi zinahusishwa. Mpango huu utatekelezwa kwa kipindi cha Miaka thelathini (30) kuanzia 2017 hadi 2046, ambapo Jumla ya Futi za Ujazo Triliioni 18.7 za Gesi Asilia zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya Soko la Ndani. Aidha, Gesi Asilia kwa ajili ya uzalishaji umeme ndio kipaumbele cha kwanza cha Mpango huu ambapo kiasi cha Gesi Asilia kilichotengwa ni Futi za Ujazo Triliioni 8.3, sawa na **asilimia 44.4** ya Gesi Asilia iliyotengwa kwa ajili ya Soko la Ndani.

*Kanuni za Maboresho na Ushindani katika Sekta Ndogo ya Umeme, Upangaji wa Bei ya Gesi Asilia na Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia*

**23. Mheshimiwa Spika,** Serikali imekamilisha Kanuni za Maboresho na Ushindani katika Sekta Ndogo ya Umeme za Mwaka 2016 (*The Electricity (Market Re- Organization and Promotion of Competition) Regulations, 2016*) na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali, Na. 229 la tarehe 21 Oktoba, 2016. Kanuni hizo, pamoja na mambo mengine, zinatoa mwongozo wa jinsi ya kuchochea ushindani kwenye shughuli za uzalishaji umeme na kuratibu shughuli hizo kupitia Kamati Maalumu (*Electricity Infrastructure Procurement Coordinator - EIPC*).

**24. Mheshimiwa Spika,** Mwezi Oktoba, 2016 Serikali ilikamilisha Kanuni za upangaji wa bei ya Gesi Asilia kwa ajili ya matumizi mbalimbali na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 285. Aidha, kwa kutumia Kanuni hizo ukokotoaji wa bei za Gesi Asilia kwa ajili ya viwanda vya kimkakati vinavyojumuisha Viwanda vya Mbolea na Saruji ulikamilika Mwezi Januari, 2017. Lengo la upangaji wa bei hizo ni kuhamasisha uwekezaji katika Viwanda vya Mbolea ili kufanikisha upatikanaji wa mbolea ya bei nafuu nchini mwetu.

**25. Mheshimiwa Spika,** kufuatia mafanikio yaliyopatikana katika utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Serikali imeona upo umuhimu wa kuhakikisha Watanzania wanashiriki katika Tasnia hiyo ipasavyo. Ili kufanikisha azma

hiyo, Serikali imeandaa Kanuni Mahsusii zitakazoongoza Kampuni za Mafuta na Gesi Asilia jinsi zitakavyoewa kuwashirikisha Watanzania katika Tasnia ya Mafuta na Gesi Asilia (*Local Content Regulations*). Kanuni husika zimeandaliwa kwa kushirikisha Wadau mbalimbali wakiwemo Taasisi za Umma, Kampuni za Mafuta na Gesi Asilia na Asasi za Kiraia. Kanuni hizo zimekamilika na zimetangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 197 la tarehe 5 Mei, 2017.

**26. Mheshimiwa Spika** katika kuhakikisha huduma za udhibiti wa Nishati zinaendelea kufanyika kwa uwazi, ubora na ufanisi kwa lengo la kukuza Uwekezaji na kuboresha Ustawi wa Kijamii na Kiuchumi kwa Jamii ya Watanzania Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) iliandaa Kanuni (*Rules*) mbalimbali. Kanuni hizo ni pamoja na: Kanuni za Uendelezaji na Usimamizi wa Miradi Midogo ya Umeme (*The Electricity (Development of Small Power Projects) Rules, 2016, GN No. 217 of 2016*); Kanuni za Tozo na Ada za Leseni za Umeme (*The Electricity (Licensing Fees) Rules, 2016, GN No. 287 of 2016*); Kanuni za Usimamizi wa Mifumo ya Umeme (*The Electricity (System Operation Services) Rules, 2016, GN No. 324 of 2016*); Kanuni za Usimamizi wa Soko la Biashara ya Umeme (*The Electricity (Market Operation Services) Rules, 2016, GN No. 325 of 2016*); Kanuni za kusimamia Uuzajj umeme (*The Electricity (Supply Services) Rules, 2017, GN No. 4 of 2017*); na Usimamizi wa Biashara ya Rejareja ya Petroli Vijijini na kwenye Miji Midogo (*The Petroleum (Retail Operations in Townships and Villages) Rules, 2017, GN No. 14 of 2017*).

## **SEKTA NDOGO YA UMEME**

### *Hali ya Upatikanaji wa Umeme Nchini*

**27. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Serikali imeendelea kuboresha Sekta Ndogo ya Umeme kwa kuimarisha hali ya uzalishaji, usafirishaji pamoja na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme nchini. Umeme uliozalishwa kwa Mwaka 2016 na kuingizwa katika Gridi ya Taifa uliongezekwa na kufikia **GWh 7,092** ukilinganisha na **GWh 6,227** zilizozalishwa Mwaka 2015 sawa na ongezeko la **asilimia**

**12.20.** Aidha, mahitaji ya juu ya umeme kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 yameongezeka hadi kufikia **MW 1,051.27** iliyofikiwa tarehe 14 Februari, 2017 ukilinganisha na **MW 1,026.02** katika Mwaka 2015/16. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 mitambo yetu ina uwezo wa kuzalisha umeme wa kiasi cha **MW 1,450**.

**28. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na jitihada za makusudi za kuongeza Idadi ya Wananchi wanaopata huduma ya umeme kwa lengo la kushamirisha shughuli za kiuchumi na kijamii. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 Idadi ya Wananchi waliofikiwa na huduma ya umeme (*overall electricity access level*) imefikia **asilimia 67.5** kulinganisha na **asilimia 40** iliyokuwa imefikiwa Mwezi Aprili, 2016. Aidha, Idadi ya Wananchi wanaopata huduma ya umeme mijini (*urban electricity access level*) imefikia **asilimia 97.3** ikilinganishwa na **asilimia 63.4** iliyofikiwa Mwaka 2014/15; wakati wanaopata huduma ya umeme vijijiini (*rural electricity access level*) imefikia **asilimia 49.5** ikilinganishwa na **asilimia 21** iliyofikiwa Mwaka 2014/15.

**29. Mheshimiwa Spika,** kutokana na uhakiki ambao ulifanywa na Shirika la Takwimu la Taifa (*National Bureau of Statistics-NBS*), hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 imebainika kuwa Idadi ya Wananchi waliouanganishiwa umeme (*overall electricity connection level*) imefikia **asilimia 32.8** ikilinganishwa na **asilimia 30** Mwaka 2015/16. Aidha, Idadi ya Wananchi waliouanganishiwa umeme mijini (*urban electricity connection level*) imefikia **asilimia 65.3** wakati waliouanganishiwa umeme vijijiini (*rural electricity connection level*) imefikia **asilimia 16.9**.

### **Kuongeza Uzalishaji wa Umeme**

#### **Mradi wa Kinyerezi II – MW 240**

**30. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mradi wa Kinyerezi II unaendelea vizuri. Gharama zote za utekelezaji wa Mradi huu zimeshalipwa. Kazi zifuatazo zimeshafanyika au zinaendelea kufanyika: Mkandarasi SUMITOMO kutoka

Japan anaendelea na ujenzi wa miundombinu na misingi (*foundations and concrete beams*) kwa ajili ya kusimika Mitambo sita (6); ujenzi wa Jengo la Ofisi umekamilika na kwa sasa linatumwiwa na Wataalam wa SUMITOMO, TOSHIBA na TANESCO; na utengenezaji wa mitambo (*manufacturing*) unaendelea nchini Japan, Korea Kusini na Singapore. Aidha, transfoma nne (4) kati ya nane (8) na Mitambo mitatu (3) kati ya sita (6) iliwasili nchini Mwezi Februari, 2017 ambapo kazi ya kufunga Mitambo imeanza Mwezi Aprili, 2017.

**31. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18 utengenezaji wa Mitambo ya Mradi wa Kinyerezi II viwandani utakamilishwa na kazi ya ufungaji wa Mitambo itaendelea. Aidha, Mtambo wa kwanza wa kuzalisha umeme wa **MW 30** unategemewa kukamilika ifikapo Mwezi Desemba, 2017 na Mradi mzima unatarajiwaa kukamilika Mwezi Desemba, 2018.

#### *Mradi wa Kinyerezi I Extension – MW 185*

**32. *Mheshimiwa Spika*,** kama tunavyofahamu Mradi wa Kinyerezi I **MW 150** ulikamilika na kuanza kuzalisha umeme rasmi Mwezi Machi, 2016. Baada ya Mradi huo kukamilika, Serikali kupitia TANESCO illingia Makubaliano na Kampuni ya Jacobsen Elektro AS ya Norway ili kupanua Mradi huo kwa kuongeza Mitambo mingine ya **MW 185** (Kinyerezi I Extension) na hivyo kufanya uwezo wa Kituo hicho kuwa na Jumla ya **MW 335**. Makubaliano hayo yalitokana na azma ya Serikali ya kuondoa upungufu wa nishati ya umeme kwa kutumia Gesi Asilia inayopatikana nchini mwetu.

**33. *Mheshimiwa Spika*,** kazi zilizofanyika kwa Mradi wa Kinyerezi I Extension ni kukamilisha malipo ya Mkandarasi wa Ufundi, Kampuni ya Citec kwa **asilimia 90** na Kampuni ya General Electricitya Marekani imekamilisha matengenezo ya Mitambo kwa **asilimia 100** na Mitambo ipo tayari kusafirishwa kuja nchini. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Mkandarasi ataendelea na kazi ya ufungaji wa Mitambo ambapo **Shilingi bilioni 60**, fedha za Ndani zimetengwa kwa

ajili ya kazi hiyo. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa Mwaka 2019.

#### *Mradi wa Mto Malagarasi - MW 45*

**34. *Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahusisha ujenzi wa Mtambo wa kuzalisha umeme wa **MW 45** kwa kutumia maji ya Mto Malagarasi uliopo Mkoani Kigoma na unatekelezwa na TANESCO. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeonesha nia ya kufadhili Mradi huu. Taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi wa Mradi zinaendelea ambapo kwa sasa uchambuzi wa zabuni unafanyika na unatarajiwa kukamilika Mwezi Mei, 2017. Gharama za utekelezaji wa Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 149.5**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 345.49** na unatarajiwa kukamilika Mwaka 2020. Katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Serikali imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 2.8** kwa ajili ya kuanza kugharamia utekelezaji wa Mradi huu.

#### *Mradi wa Kakono - MW 87*

**35. *Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahusu ujenzi wa Mtambo wa kuzalisha umeme wa **MW 87** kwa kutumia maji ya Mto Kagera uliopo Mkoani Kagera na unateke- lezwa na TANESCO. Serikali imewasilisha maombi ya Mkopo kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Mwezi Julai, 2016 kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu ambapo AfDB wameonesha nia ya kuufadhili. Mshauri Mwelekezi Kampuni ya *SP Studio Pietrangeli* ya Italia amepatikana kwa ajili ya usimamizi wa Mradi.

**36. *Mheshimiwa Spika***, Serikali inakamilisha taratibu za kubadilisha umiliki wa eneo la Mradi wa Kakono lenye ukubwa wa Hekta 1,100 kutoka kwa Wamiliki wa sasa (NARCO na Kagera Sugar) kwenda TANESCO. Maombi yamewasilishwa kwa Mamlaka husika za Wilaya za Misenyi na Karagwe ili kupima na kutambua mipaka ya eneo la Mradi. Gharama za ujenzi wa Mtambo na njia ya usafirishaji umeme ni **Dola za Marekani milioni 379.4**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 876.79** na Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo

Mwaka 2021. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi huo kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 ni **Shilingi bilioni 2.05** ambazo ni fedha za Nje.

#### *Mradi wa Rusumo - MW 80*

**37. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu wa Rusumo wa **MW 80**, Tanzania itapata **MW 26.6**. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Wakandarasi wa kujenga Kituo cha kufua umeme, *COCO Group Jingal Water (China) and Hydropower Construction Company (Canada)*, walisaini Mkataba tarehe 9 Novemba, 2016. Wakandarasi hao watahusika na kazi za "Civil and Hydro-mechanical". Pamoja nao watakuwepo *Andritz Hydro GmbH and Andritz Hydro PVT Ltd* kutoka nchi ya Austria watakaohusika na kazi za *Electro-mechanical*. Aidha, malipo ya awali kwa Wakandarasi kiasi cha **Dola za Marekani milioni 16.3** sawa na takriban **Shilingi bilioni 37.67** yamefanyika na utekelezaji wa Mradi unaendelea.

**38. Mheshimiwa Spika**, uzinduzi rasmi wa kuanza ujenzi (*Ground breaking ceremony*) wa Kituo cha kufua umeme cha Rusumo ulifanywa na Mawaziri wanaosimamia masuala ya Nishati wa nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi, pamoja na Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) tarehe 30 Machi, 2017. Gharama za ujenzi wa Mtambo wa kufua umeme ni **Dola za Marekani milioni 340** sawa na takriban **Shilingi bilioni 785.74**. Mchango wa Serikali ni **Dola za Marekani milioni 113** ambao ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB). Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, kiasi cha **Shilingi bilioni 2.8** kimetengwa kugharamia shughuli za ujenzi wa Kituo hicho na Mradi unatarajiwaa kukamilika Mwaka 2020.

#### *Mradi wa Somanga Fungu (Lindi) - MW 300*

**39. Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza kiwango cha uzalishaji wa umeme nchini, Serikali imepanga kuongeza Mitambo ya kuzalisha umeme ya **MW 300** kwa kutumia Gesi Asilia katika eneo la Somanga Fungu Wilaya ya Kilwa, Mkoani

Lindi. Upembuzi Yakinifu wa Mradi ulikamilika Mwezi Oktoba, 2016 kuititia ufadhili wa Benki ya Dunia. Hatua inayofuata ni kutangazwa kwa Mradi ili kupata Mtekelezaji (*EPC & Financing*) atakayeshirikiana na Serikali kutekeleza Mradi unaokadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 423**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 977.55** na unatarajiwa kukamilika Mwaka 2020.

*Mradi wa Somanga Fungu - MW 240.*

**40. Mheshimiwa Spika**, ili kuendelea kuongeza kiwango cha uzalishaji wa umeme nchini, Serikali kupitia TANESCO imepanga kutekeleza mradi wa **MW 240** kwa kutumia gesi asilia. Mradi huu utatekelezwa katika eneo la Somanga Fungu, Kilwa kwa utaratibu wa *EPC with financing* kupitia Kampuni ya Sumitomo ya Japan. Gharama za kutekeleza mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani Milioni 300** ambapo asilimia 85 itatolewa na Benki ya Japan (*Japan Bank for International Cooperation - JBIC*) na asilimia 15 ya fedha hizo itatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

**41. Mheshimiwa Spika**, kazi ya upembuzi yakinifu wa mradi huu inaendelea na inatarajiwa kukamilika baada ya miezi mitatu (3). Kazi yote ya ujenzi inatarajiwa kufanyika ndani ya miaka miwili (2) na mradi unatarajiwa kukamilika Mwaka 2020. Mradi huu utamillikiwa na Serikali.

*Mradi wa Kufua Umeme Mtwara - MW 300*

**42. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TANESCO ilianza majadiliano na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Ushirikiano wa Kimataifa (JICA) kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Gesi Asilia wa **MW 300**. Mradi huu utahusisha ujenzi wa Mitambo ya kufua umeme na njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa **KV 400** kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu.

**43. Mheshimiwa Spika**, Kazi zinazoendelea kwa sasa ni upembuzi yakinifu na baada ya hapo TANESCO

itafanya majadiliano ya kiufundi na kifedha. Utekelezaji wa mradi huo utaimarisha upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara pamoja na kuingiza Mikoa hiyo katika Gridi ya Taifa. Aidha, ujenzi huo utawezesha kuuza umeme wa ziada nchi za jirani ikiwemo Msumbiji. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwaka 2020 na utamiliikiwa na Serikali.

*Mradi wa Umeme wa Makaa ya Mawe Kiwira - MW 200*

**44. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia STAMICO imeanza majadiliano na Serikali ya Urusi ambayo imeonesha nia ya kufadhili utekelezaji wa Mradi wa Kiwira kwa ajili ya kuzalisha umeme wa **MW 200** kwa kutumia Makaa ya Mawe pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **KV 400** kutoka Kiwira hadi Kituo cha Mwakibete (Mbeya) na kuingizwa katika Gridi ya Taifa. Kazi zitakazofanyika Mwaka 2017/18 ni pamoja na kukamilisha majadiliano na Mwekezaji na kuendelea kuchimba makaa ya mawe. Gharama ya Mradi wote inakaridiwa kuwa **Dola za Marekani milioni 440.**

*Mradi ya Kinyerezi III - MW 600 na Kinyerezi IV - MW 330*

**45. Mheshimiwa Spika,** Miradi hii imepangwa kutekelezwa chini ya Mpango wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP). Aidha, Majadiliano ya utekelezaji wa Miradi yamechukua muda mrefu kutohana na sababu mbalimbali ikiwemo Wabia kuhitaji dhamana ya Serikali (*Government Guarantee*); Mwekezaji kutaka Serikali iingie Makubaliano ya moja kwa moja na Wakopeshaji (*Direct Agreement with Lenders*); Mfumo wa utekelezaji miradi kati ya *Build Own and Operate (BOO)* na *Build Own Operate and Transfer (BOOT)* kwa miradi ya IPP, na Bei ya umeme (*tariff*) zinazopendekezwa na Wawekezaji kuwa za juu kuliko bei elekezi zinazotolewa na EWURA.

**46. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kusisitiza kuwa Mfumo wa utekelezaji miradi utumike wa *Build Own and Operate (BOO)* au *EPC & Financing* ambapo hakutakuwa

na Government Guarantee, Capacity Charge wala Minimum Off - Take. Aidha, CAPEX (*Investment cost*) isiwe sehemu ya formula itakayotumika kupata bei ya umeme (*tariff*) na TANESCO italipia gharama za *energy component* (*variable Operation and Maintenance cost - O&M*).

*Miradi ya Uzalishaji Umeme ya Sekta Binafsi*

47. *Mheshimiwa Spika*, upande wa Miradi ya Uzalishaji Umeme inayotekelawa na Sekta Binafsi (IPP) ikiwemo Mradi wa Somanga Fungu **MW 320** wa Kilwa Energy; Mradi wa Mchuchuma **MW 600**; na Ngaka **MW 400** chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) bado ipo katika hatua mbalimbali za majadiliano.

*Upanuzi na Uboreshaji wa Njia za Usafirishaji wa Umeme*

*Mradi wa Msongo wa kilovolti 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga (Backbone Transmission Investment Project - BTIP)*

48. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi wa njia ya umeme wa Msongo wa kilovolti 400 na upanuzi wa Vituo vya kupozea umeme kutoka Iringa – Dodoma – Singida – Tabora - Shinyanga ulikamilika Mwezi Desemba, 2016 kwa **asilimia 100**. Kwa sasa umeme unasafirishwa kwa kutumia njia hiyo na kupelekea kuboresha upatikanaji wa umeme katika maeneo ya Mikoa hiyo na kwenye Gridi ya Taifa kwa ujumla. Uzinduzi rasmi wa Mradi huu utafanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*Mradi wa Msongo wa kilovolti 220 kutoka Makambako hadi Songea na Usambazaji wa Umeme Vijijini kwa Mikoa ya Njombe na Ruvuma*

49. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa kV 220 kutoka Makambako hadi Songea yenye urefu wa kilomita 250, ujenzi wa Vituo Vipyta vya kupozea umeme eneo la Madaba na

Songea, umeme wa Msongo wa KV 220/33 na upanuzi wa Kituo cha kupozea umeme cha Makambako. Kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme KV 220 Makambako – Songea, Mkandarasi amekamilisha manunuzi ya vifaa vya Mradi na usimikaji wa nguzo umeanza Mwezi Machi, 2017.

**50.** *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa ujenzi wa Vituo vitatu (3) vya kupoza umeme vyenye uwezo wa KV 220/33 katika maeneo ya Makambako, Madaba na Songea, Wakandarasi Kampuni za Shandong Taikai na Norino International za China zinaendelea kupima sampuli za udongo na kusawazisha maeneo ya kujenga Vituo hiyo na ujenzi utaanza Mwezi Mei, 2017. Aidha, kwa upande wa kazi ya usambazaji umeme, Mkandarasi Kampuni ya Isolux Ingenieria S.A ya Hispania inaendelea na kazi ya kusimika nguzo na kuvuta nyaya ambapo hadi kufikia Mwezi Aprili, 2017 amekamilisha umbali wa kilomita 365 kati ya 580, sawa na **asilimia 62.9** katika maeneo ya Mkoa wa Ruvuma. Kwa upande wa Makambako hadi Njombe usimikaji wa nguzo na kuvuta nyaya umefikia kilomita 118 kati ya kilomita 393, sawa na **asilimia 30**. Aidha, Kituo kidogo cha kupozea umeme cha Songea KV 33/11 kimekamilika kwa **asilimia 52**.

**51.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wakandarasi Shandong Taikai na Norino International za China wataendelea na kazi za kukamilisha ujenzi wa Vituo vya kupoza umeme na Kampuni ya Kalpataru Power Transmission Ltd ya India itaendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Makambako hadi Songea. Aidha, Kampuni ya Isolux ya Hispania itaendelea na ujenzi wa njia ya usambazaji umeme na kuunganisha vijiji vilivyopo kati ya Makambako hadi Songea kwenye Mkuza wa njia ya usafirishaji umeme. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Mradi umetengewa **Shilingi bilioni 3** fedha za Ndani ikiwa ni mchango wa Serikali na **Shilingi bilioni 8** ikiwa ni fedha za Nje kutoka Serikali ya Sweden kuititia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa (Sida). Utekelezaji wa Mradi huu unatarajiwaa kukamilika Mwezi Agosti, 2018.

*Mradi wa Njia ya Umeme ya Msongo wa kilovolti 400 wa Singida – Arusha – Namanga*

**52. Mheshimiwa Spika,** Serikali inatekeleza Miradi ya ushirikiano wa ki- Kanda ikiwemo Mradi wa njia ya kusafirisha umeme Singida - Arusha - Namanga KV 400. Kazi zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ni pamoja na: TANESCO kusaini Mkataba na Kampuni ya Kalpataru Power Transmission Ltd kutoka nchini India kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme kutoka Singida hadi Babati (km 150), Kampuni ya Bouygues Energy & Services ya Ufaransa kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme kutoka Babati hadi Arusha (km 150) na Kampuni ya Ubia kati ya Energoinvest ya Yugoslavia na EMC ya India kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme kutoka Arusha hadi Namanga (km 114); na kukamilika kwa tathmini ya athari za mazingira na mali za Wananchi watakaopisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme.

**53. Mheshimiwa Spika,** taratibu za kupata Mkandarasi wa ujenzi wa Kituo kipywa cha Arusha cha Msongo wa KV 400/220 na upanuzi wa Kituo cha Singida zimekamilika. TANESCO inatarajia kusaini Mkataba na Kampuni ya Ubia kati ya Energoinvest ya Yugoslavia na EMC ya India ambayo imeshinda zabuni Mwezi Aprili, 2017. Aidha uchambuzi wa zabuni za Wakandarasi wa usambazaji umeme vijiji umeanza. Garama za Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 258.82**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 598.13**. Fedha hizi zinatolewa na AfDB, JICA na Serikali ya Tanzania ambayo itachangia **Dola za Marekani milioni 43.89**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 101.43**.

**54. Mheshimiwa Spika,** kazi zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ni pamoja na kukamilisha taratibu za malipo ya fidia na kuanza kutekeleza Mradi kwa awamu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Serikali imetenga fedha za Ndani **Shilingi bilioni 48** kwa ajili ya ulipaji wa fidia. Aidha, utekelezaji wa Mradi utaanza baada ya ulipaji wa fidia kukamilika na Wakandarasi kulipwa malipo ya awali. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Desemba, 2019.

*Mradi wa North - West wa kilovolti 400 kutoka Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi*

55. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kazi ambazo zimefanyika ni pamoja na: kudurusu Upembuzi Yakinifu wa Mradi kutoka Msongo wa kV 220 na kuwa kV 400 kwa eneo la Mbeya hadi Nyakanazi lenye urefu wa kilomita 1,080; utafiti wa athari za mazingira kwa Awamu ya Pili kutoka Nyakanazi – Kigoma - Mpanda, kilomita 568 ambaao umekamilika Mwezi Februari, 2017; na kuanza Majadiliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Korea ya Kusini kupitia Shirika lake la Maendeleo (*EDCF*) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji wa Mradi. Hatua iliyofikiwa ni kwamba tayari Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imewasilisha maombi rasmi kwa Taasisi hizo ya **Dola za Marekani milioni 428** sawa na takriban **Shilingi bilioni 989.11**.

56. *Mheshimiwa Spika*, kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za kutekeleza sehemu ya Mradi huo kutoka Nyakanazi hadi Kigoma kwa ufadhili wa *EDCF* ya Korea Kusini ambayo imeonesha nia ya kutoa Mkopo wa masharti nafuu wa **Dola za Marekani milioni 50**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 115.55**; kukamilisha utafiti wa athari za mazingira kutoka Mpanda hadi Sumbawanga; na kulipa fidia Wananchi kutoka Nyakanazi hadi Kigoma ambapo **Shilingi bilioni 12.3** zimetengwa katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

*Mradi wa North - East wa kilovolti 400 kutoka Kinyerezi hadi Arusha kupitia Chalinze na Segera*

57. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu una lengo la kusafirisha umeme kutoka Kituo cha Kinyerezi, Dar es Salaam hadi Arusha kwa lengo la kukidhi mahitaji ya umeme kwenye Gridi ya Taifa hususan katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Gharama ya Mradi huu ni takriban **Dola za Marekani milioni 692.7**, sawa na takriban **Shilingi**

**trilioni 1.6** ambapo Benki ya Exim ya China itatoa Mkopo wa **asilimia 85** na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itatoa **asilimia 15** ya gharama za Mradi.

**58. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kazi zilizofanyika kwenye Mradi huu ni pamoja na: kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo na pande husika Mwezi Agosti, 2016; kusainiwa kwa Mkataba kati ya TANESCO na Mtaalamu Mshauri Kampuni ya TBEA kutoka China kwa ajili ya usimamizi wa Mradi Mwezi Januari, 2017; na kukamilika kwa tathmini ya mali kwa maeneo ya kujenga Vituo vya kupoza umeme vya Segera na Tanga pamoja na eneo la njia ya umeme kutoka Kinyerezi hadi Kiluvya, Dar es Salaam.

**59. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kazi zilizopangwa kufanyika kwenye Mradi huu ni kukamilisha tathmini ya mali za Wananchi watakaopisha sehemu ya Mradi, pamoja na kulipa fidia kwa Awamu ya Kwanza kutoka Kinyerezi hadi Chalinze. Serikali imetenga fedha za Ndani kiasi cha **Shilingi bilioni 19.80** kwa ajili ya kulipa fidia kwa Waathirika pamoja na mchango wa sehemu ya **asilimia 15** ya gharama ya Mradi.

*Mradi wa njia ya umeme ya Msongo wa kilovolti 400 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi*

**60. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka eneo la Somanga Fungu Mkoani Lindi hadi Kinyerezi Mkoani Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme eneo la Somanga Fungu. Njia hii itatumika kusafirisha umeme utakaozalishwa na Mitambo yenyewe uwezo wa kufua takriban **MW 620** inayotarajiwa kujengwa eneo la Somanga Fungu Kilwa Mkoani Lindi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 TANESCO imesaini Mkataba na Mtaalam Mshauri Kampuni ya Byucksan Power Ltd ya Korea Kusini ili kudurusu Upembuzi Yakinifu na kusimamia ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme; na kulipa fidia kwa Wananchi wanaopisha ujenzi wa njia hiyo. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 ulipaji wa fidia kwa mali za Waathirika wa Mradi ulikuwa umefanyika kwa Waathirika

2,305 kati ya 3,901 (sawa na **asilimia 59.1**) kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 46.29**.

*Mradi wa njia ya Umeme wa Msongo wa kilovolti 220 kutoka Kituo cha Kufua Umeme wa Maji cha Rusumo hadi Nyakanazi*

**61. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Rusumo wa **MW 80** unahusisha ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kutoka Rusumo, Mto Kagera hadi kwenye Gridi ya nchi za Burundi, Rwanda na Tanzania. Kwa upande wa Tanzania, Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Kituo cha kuzalisha umeme cha Rusumo hadi Nyakanazi yenye urefu wa kilomita 98 kwenye Msongo wa kV 220. Mradi huu utasaidia kuunganisha Mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa na Katavi kwenye Mfumo wa Gridi ya Taifa na kuipatia umeme mwingi zaidi na wa uhakika.

**62. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kazi zilitofanyika kwenye Mradi huu ni pamoja na: kusainiwa kwa Mkataba Mwezi Desemba, 2016 kati ya TANESCO na Mtaalam Mshauri, Kampuni za WSP Canada Inc. na GOPA International Energy Consultant GmbH ya Ujeruman kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mradi; upimaji wa njia na kufanya tathmini ya fidia ya mali za Wananchi watakaopisha eneo la Mradi. Aidha, Serikali imewasilisha taarifa ya Upembuzi Yakinifu Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Mwezi Februari, 2017 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme eneo la Benaco liliopo Wilayani Ngara, Mkoani Kagera.

**63. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kazi zitakazofanyika kwenye Mradi huu ni: kukamilisha ulipaji wa fidia kwa Waathirika wa Mradi na kuwapata Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na Kituo cha kupoza umeme cha Benaco Wilayani Ngara, Mkoani Kagera. Serikali imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 5.2** fedha za Ndani kwa ajili ya kulipa fidia.

*Mradi wa Njia ya umeme ya Msongo wa kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita*

**64. Mheshimiwa Spika,** Mradi utahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa Msongo wa KV 220 yenye urefu wa kilomita 55 pamoja na usambazaji umeme katika vijiji vinavyopitiwa na Mradi Wilayani Geita. Mradi huu unatekelezwa kwa Mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kiarabu (*Arab Bank for Economic Development in Africa - BADEA*), *OPEC Fund for International Development* (OFID) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi zilizofanyika kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ni kukamilisha uchambuzi wa zabuni za kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme Mwezi Februari, 2017 na tathmini ya mali za Wananchi watakaopisha eneo la Mradi.

**65. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kazi zitakazofanyika kwenye Mradi huu ni kulipa fidia kwa Wananchi watakaopisha eneo la Mradi na pia kuanza ujenzi. Fedha za Nje zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu ni **Shilingi bilioni 7** na fedha za Ndani ni **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kulipa fidia.

*Mradi wa Njia ya umeme ya Msongo wa kilovolti 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi*

**66. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa KV 220 yenye urefu wa kilomita 133, Kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na kusambaza umeme kwenye vijiji vinavyopitiwa na Mradi. Aidha, Mradi huu utagharimu takriban **Euro milioni 45** sawa na **Shilingi bilioni 95.67** kwa ufadhili wa KfW ya Ujerumani, AFD ya Ufaransa, Jumuiya ya Ulaya (EU) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

**67. Mheshimiwa Spika,** kazi zilizofanyika kwenye Mradi huu kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ni pamoja na: upimaji wa njia kuu ya usafirishaji umeme kutoka Geita hadi Nyakanazi; tathmini ya gharama ya fidia kwa mali za

Wananchi watakaoathirika; tathmini ya athari ya kijamii na mazingira; pamoja na usanifu wa Mradi.

**68. *Mheshimiwa Spika*,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kazi zitakazofanyika kwenye Mradi huu ni pamoja na kukamilisha ulipaji wa fidia kwa Wananchi watakaoathirika pamoja na kuanza utekelezaji wa Mradi. Fedha za Nje zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu ni Jumla ya **Shilingi bilioni 9.1** ambapo **Shilingi bilioni 1.6** ni fedha za Nje na fedha za Ndani ni **Shilingi bilioni 7.5** kwa ajili ya kulipa fidia.

*Miradi ya Usambazaji wa Umeme*

*Mradi wa kuboresha Mfumo wa usamba- zaji umeme katika Jiji la Dar es Salaam chini ya Ufadhilli wa JICA*

**69. *Mheshimiwa Spika*,** Mradi huu ulihusisha kazi zifuatazo: ukarabati wa Kituo cha llala kV 132/33/11; ujenzi wa Jengo Jipyala "Control Center" la llala; ufungaji wa njia ya pili ya usafirishaji umeme wa Msongo wa kV 132 kutoka Ubungo hadi llala; kupanua Kituo cha kupoza umeme cha Msasani kV 33/11; ujenzi wa Vituo Vipyala vinne (4) vya kupoza umeme wa kV 33/11 vya Jangwani Beach, Mwananyamala, Msasani na Muhimbili; ujenzi wa njia mpya za Msongo wa kV 33 kutoka Vituo vya kupoza umeme vya Makumbusho, City Centre na Tegeta kwenda Vituo Vipyala vya Mwananyamala, Muhimbili, Jangwani na Msasani.

**70. *Mheshimiwa Spika*,** utekelezaji wa Mradi huu ulifadhilliwa na Serikali ya Japan kuitia Shirika lake la Maendeleo la JICA kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 38**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 87.82** na utekelezaji wake umekamilika kwa **asilimia 100** Mwezi Machi, 2017. Mradi huu unasubiri kuzinduliwa rasmi na Viongozi wa Kitaifa.

***Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Manispaa ya Dodoma chini ya Ufadhilli wa JICA***

**71.** *Mheshimiwa Spika*, Serikali kuitia TANESCO ipo katika majadiliano na Serikali ya Japan kuitia Shirika lake la Ushirikiano la Kimataifa (JICA) katika utekelezaji wa Mradi wa kuboresha mfumo wa Usambazaji Umeme katika Manispaa ya Dodoma. Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa KV 132 zenyne urefu wa kilometra 135 kutoka Zuzu kwenda Msalato na Kikombo na ujenzi wa Vituo viwili (2) vya kupoza umeme vyenye uwezo wa MVA 90 kila kimoja katika maeneo ya Msalato na Kikombo. Kazi nyingine itakuwa ni ujenzi wa njia za kusambaza umeme za msongo wa KV 33 zenyne urefu wa kilometra 71 katika Manispaa ya Dodoma.

**72.** *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa Mradi huu utaimarisha upatikanaji wa umeme katika Manispaa ya Dodoma na vitongoji vyake na pia kukidhi mahitaji ya umeme yatakayoongezeka kutokanaa na Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi. Aidha, Mradi huu unatarajiwa kuanza Mwaka wa fedha 2018/19 na utagharimu **Dola za Marekani milioni 38** sawa na takriban **Shilingi bilioni 76**.

***Mradi wa TEDAP wa Kuboresha Njia za Usambazaji Umeme (Distribution) Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Kilimanjaro chini ya Ufadhilli wa Benki ya Dunia***

**73.** *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahusisha upanuzi na ujenzi wa Vituo Vipya 19 vya kupoza umeme wa Msongo wa KV 33/11 pamoja na ujenzi wa njia za usambazaji umeme kwa Msongo wa KV 33 na KV 11 zenyne urefu wa kilomita 107 na kilomita 34.01 sawia katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Kilimanjaro kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 43**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 99.37**. Fedha hizi zimetolewa na Benki ya Dunia kuitia Mradi wake wa TEDAP.

**74.** *Mheshimiwa Spika*, ujenzi wa Mradi huu upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo hadi kufikia Mwezi Aprili, 2017 **asilimia 85** ya kazi zote zilizopangwa

zilikamilika na matarajio ni kukamilisha Mradi huo ifikapo Mwezi Juni, 2017.

***Mradi wa uboreshaji wa huduma za umeme Jijini Dar es Salaam chini ya Ufadhilli wa Finland***

**75.** *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu ulihusisha uboreshaji wa miundombinu ya umeme katika Jiji la Dar es Salaam kwa kufanya yafuatayo: kujenga Kituo kipyta cha kupoza umeme cha Msongo wa KV 132/33; kufunga Kangavuke mbili (2) zenyе uwezo wa MVA 50 kila moja kwenye Kituo cha *City Centre*; kujenga njia ya umeme wa Msongo wa KV 132 chini ya ardhi kutoka Kituo cha llala hadi Kituo kipyta cha *City Centre*; kujenga njia ya mzunguko wa umeme (*ring circuit*) chini ya ardhi wa Msongo wa KV 33 kutoka Kituo cha kupoza umeme cha *City Centre* kwenda Sokoine – *Railway* – Kariakoo na kurudi tena *City Centre*; pamoja na kuanzisha Kituo cha kuongozea Mifumo ya Usambazaji umeme katika Msongo wa KV 33 na KV 11 (*Distribution SCADA*) katika eneo la Mikocheni.

**76.** *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu ulifadhiliwa na Serikali ya Finland kwa gharama ya **Euro milioni 21.8** na **Dola za Marekani milioni 1.5** sawa na takriban **Shilingi bilioni 3.47**. Kituo cha kuongozea Mifumo ya Usambazaji umeme katika Msongo wa KV 33 na KV 11 (*Distribution SCADA*) kilichopo Mikocheni **kilizinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)** tarehe 16 Novemba, 2016. Mradi huo ulikamilika Mwezi Februari, 2017.

***Mradi wa ORIO kwa Miji ya Ngara, Biharamulo na Mpanda***

**77.** *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahusisha ufungaji wa Mitambo ya kufua umeme yenye uwezo **MW 2.5** kwa kila Wilaya za Biharamulo, Mpanda na Ngara na kupanua njia za usambazaji umeme kwa lengo la kuyapatia maeneo husika umeme wa uhakika. Gharama ya Mradi ni **Euro milioni 33.5** sawa na **Shilingi bilioni 71.22** kupitia ufadhilli wa Serikali

ya Uholanzi iliyotoa **asilimia 50** na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotoa **asilimia 50**.

**78. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu umekamilika kwa Wilaya ya Bihamulo Mwezi Septemba, 2016 na Wilaya ya Ngara Mwezi Desemba, 2016. Mafunzo ya Wajasiriamali katika maeneo ya Mradi na mafunzo ya afya na usalama kazini kwa Wafanyakazi wa TANESCO katika Vituo hivi vya umeme vya Bihamulo, Mpanda na Ngara yamefanyika Mwezi Machi, 2017. Kazi inayoendelea kwa sasa ni ufungaji wa Mitambo ya kufua umeme na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika Wilaya ya Mpanda ambapo unatarajia kukamilika Mwezi Juni, 2017.

#### *Mradi wa TANESCO wa Urban Electrification*

**79. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unahusu usambazaji umeme kwa Wateja ambao hawajaunganishwana umeme maeneo ya mijini (*urban electrification programme*). Aidha, Mradi wa njia ya kusafirisha umeme ya Msongo wa kilovolti 132 kutoka Morogoro hadi Mtibwa umeingizwa kama sehemu ya utekelezaji wa Mradi huu. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeonesha nia ya kufadhili Mradi huu kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 222.62** sawa na takriban **Shilingi bilioni 514.47**.

**80. Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazofanyika kwenye Mradi huu kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 ni pamoja na: TANESCO kuboresha Upembuzi Yakinifu (*feasibility study*) ikihusisha Mradi wa Morogoro – Mtibwa wa KV 132; Serikali kusaini Mkataba wa Ufadhilli na AfDB; na baadae kuanza utekelezaji wa Mradi.

#### **Miradi ya Kusambaza Umeme Vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA)**

(i) **Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Pili (REA Turnkey Phase II)**

**81. Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa Wananchi wengi zaidi wanapata

huduma za umeme, Serikali ilitekeleza Mradi Kabambe wa Awamu ya Pili (*REA Turnkey Phase II*) wa Kusambaza Umeme Vijiji ni katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Wakala ulikamilisha kazi zifuatazo: ujenzi wa Vituo sita (6) vya kuongeza nguvu ya umeme kutoka Msongo wa KV 11 hadi 33 katika Miji ya Kasulu, Kibondo, Kigoma, Mbinga, Ngara na Tunduru; ujenzi wa njia za kusambaza umeme za Msongo wa KV 33 zenye urefu wa kilomita 17,740; ujenzi wa Vituo Vidogo vya kupoza na kusambaza umeme 4,100; na ujenzi wa njia ndogo ya usambazaji umeme zenye urefu wa kilomita 10,970. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2017, Wateja wa awali 153,821 sawa na **asilimia 62** walikuwa wameunganishiwa umeme kati ya Wateja 250,000 walipangwa kuunganishwa.

Aidha, kazi za kuunganisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya 13 za Busega, Buhlgwe, Chemba, Itlima, Kakonko, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele, Mombasa, Nanyumbu, Nyasa, na Uvinza zimekamilika na kufanya Jumla ya Makao Makuu ya Wilaya zilizopelekewa umeme kupitia Miradi ya REA kufikia 25. Gharama za Mradi wa huu ni **Shilingi biliioni 900.15** zote zikiwa ni fedha za Ndani.

**(ii) Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijiji ni Awamu ya Tatu (REA Turnkey Phase III)**

82. *Mheshimiwa Spika*, hadi Mwezi Agosti, 2016 Vijiji 4,395 vilikuwa vimefikiwa na umeme sawa na **asilimia 36** ya vijiji 12,268 vilivyopo Tanzania Bara. Lengo la Serikali ni kufikia Vijiji 7,873 vilivyosalia ifikapo Mwaka 2020/21. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 maandalizi ya Mradi wa Kusambaza Umeme Vijiji ni Awamu ya Tatu yamekamilika na utekelezaji umeanza. Mradi huu ni wa miaka mitano (5) kuanzia 2016/17 hadi 2020/21 na unalenga kufikisha huduma ya umeme kwenye vijiji vyote nchini ambavyo bado havijafikiwa na umeme. Mradi unahusisha: kuongeza wigo wa usambazaji umeme kwenye maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya umeme (*Densification*); kufikisha umeme wa Gridi kwenye vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme (*Grid extension*); na Miradi ya umeme ya nje ya Gridi (*off-grid*) utokanao na Nishati Jadidifu, hasa Umeme Jua (*Solar power*).

**83. Mheshimiwa Spika**, hatua zilizofikiwa katika maandalizi na utekelezaji ni pamoja na kukamilika kwa uandaaji wa orodha ya vijiji ambavyo havijapatiwa umeme; kusainiwa Mikataba na kuanza utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mradi wa *Densification* Mwezi Desemba, 2016 unaohusisha Mikoa ya Arusha, Iringa, Mara, Mbeya, Pwani na Tanga kwa ufadhilli wa Serikali ya Norway kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 28.62**. Aidha, taratibu za upatikanaji wa Wakandarasi wa kusambaza umeme kwenye vijiji vilivyo kwenye Mkusa wa njia ya kusafirisha umeme wa *Backborne Transmission Investment Project (BTIP)* kutoka Iringa hadi Shinyanga umekamilika na Mradi umeanza kutekelezwa Mwezi Januari, 2017. Vilevile, uchambuzi wa maombi 300 ya kusambaza umeme wa Nishati Jadidifu kwa vijiji vilivyo nje ya Gridi ya Taifa umekamilika na utekelezaji wake utaanza Mwezi Julai, 2017.

**84. Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaendelea na utekelezaji kwa kufikisha umeme katika vijiji 3,559 ambavyo tayari Wakandarasi walishaanza kazi. Aidha, Serikali kupitia REA itakamilisha taratibu za ununuzi wa Wakandarasi kwa ajili ya kufikisha umeme kwenye vijiji 4,314 vilivyosalia ambavyo vinajumuisha vijiji ambavyo vitapatiwa umeme wa nje ya Gridi (*off-grid*). Aidha, Serikali itaendelea na kusambaza umeme kwenye vijiji vilivyo pembezoni mwa Mkusa wa njia ya kusafirisha umeme wa *Backborne Transmission Investment Project (BTIP)* kutoka Iringa hadi Shinyanga.

**85. Mheshimiwa Spika**, Fedha zinazohitajika kutekeleza Mradi huu kwa Miaka Mitano ni takriban **Shilingi trilioni 7**. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 469.09** fedha za Ndani na **Shilingi bilioni 30** fedha za Nje.

(iii) *Mradi wa Mfano wa Kupunguza Gharama za Miundombinu ya Usambazaji Umeme Vijijini (Low Cost Design Standards for Rural Electrification)*

**86. Mheshimiwa Spika**, katika kupunguza gharama za ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme vijijini,

Serikali ilipata ruzuku kutoka Benki ya Dunia ya kufanya utafiti kuhusu gharama hizi na kutekeleza Mradi wa Mfano. Utafiti huo ulifanyika katika Wilaya za Kilombero na Mbozi ambapo ulibaini kuwa gharama zinaweza kupungua kwa kati ya **asilimia 30** hadi **40** iwapo Miradi itatekelezwa kwa kutumia teknolojia ya gharama nafuu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kwenye Mradi huu kazi ya ujenzi wa miundombinu iliendelea na hadi kufikia Mwezi Desemba, 2016 kazi zilikuwa zimekamilika kwa **asilimia 96** (Mbozi) na **asilimia 94** (Kilombero). Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2017.

**(iv) Utekelezaji wa Programu ya Awamu ya Pili ya Mradi wa Sustainable Solar Market Package (SSMP – II)**

**87. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Programu ya Awamu ya Pili ya **Mradi wa Sustainable Solar Market Package (SSMP – II)** unahusu ujenzi wa Mifumo ya Umeme Jua katika Wilaya nane (8) za Biharamulo, Bukombe, Chato, Kasulu, Kibondo, Namtumbo, Sikonge na Tunduru. Hadi kufikia Mwezi Desemba, 2016, Jumla ya Mifumo Midogo ya Umeme 4,620 yenye uwezo wa kWp 115 ilifungwa. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 18** sawa na **Shilingi bilioni 41.60** ambazo ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia.

**(v) Mradi wa Kuhamasisha Upelekaji na Matumizi ya Umeme Vijiini (Lighting Rural Tanzania) 2014**

**88. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulihusisha kusambaza umeme unaotokana na Mifumo ya Nishati Jadidifu (*renewable energies*) kwa kujenga Gridi Ndogo Ndogo zinazojitegemea kwenye maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa na maeneo ya Visiwani. Mradi huu ulitekelezwa na Waendelezaji 18 kwa ujumla katika maeneo mbalimbali nchini. Mradi huu unatekelezwa katika maeneo ya vijijiini katika Mikoa ya Arusha, Iringa, Kigoma, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma na Singida. Hadi kufikia Mwezi Desemba, 2016 Mradi ulikuwa umefikia **asilimia 72** na gharama za Mradi ni **Shilingi bilioni**

4. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### ***SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA***

#### ***Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia***

**89. *Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia umeendelea kufanyika katika maeneo ya baharini na nchi kavu. Aidha, kushuka kwa bei za Mafuta na Gesi Asilia katika Soko la Dunia, kumeathiri kasi ya shughuli za utafutaji Mafuta na Gesi Asilia nchini. Pamoja na changamoto hizo, Jumla ya visima vitatu (3) vilichorongwa. Visima viwili (Kitatange-1 na Bunju-1) vilichorongwa na Kampuni ya Shell/BG katika Vitalu namba 1 na 4 vilivyopo kwenye kina kirefu cha maji ya Bahari ya Hindi ambapo vyote havikuwa na mashapo ya Gesi Asilia kama iliyotarajiwu. Kisima cha tatu (Ntorya -2) kilichorogwa na Kampuni ya Ndovu Resources katika Kitalu cha Mtwara kuhakiki Gesi Asilia iliyogunduliwa katika Kisima cha Ntorya -1 na kazi ya kutathmini kiasi kilichopo inaendelea. Kwa sasa kiasi cha Gesi Asilia kilichogunduliwa nchini ni Jumla ya Futi za Ujazo (TCF) Trillioni 57.25 ambapo Gesi Asilia iliyogunduliwa Nchi Kavu ni TCF Trillioni 10.12 na kina kirefu cha Bahari ya Hindi TCF Trillioni 47.13. Hata hivyo, ugunduzi huu mpya uliofanywa katika Kisima cha Ntorya - 2 utaongeza kiasi cha Gesi Asilia iliyogunduliwa nchini baada ya tathmini kukamilika.

#### ***Matumizi ya Gesi Asilia Viwandani***

**90. *Mheshimiwa Spika***, Jumla ya Viwanda 42 tayari vimeunganishwa na miundombinu ya Gesi Asilia. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Serikali kupitia TPDC imeendelea kutafuta Wateja wapya na kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya kusambaza Gesi Asilia. Majadiliano kati ya TPDC na Dangote Cement Tanzania Limited – Mtwara yamekamilika na majadiliano yanaendelea kati yake na Bakhressa Food Factory, Knauf Gypsum na Lodhia Steel vilivyopo Mkuranga Mkoani Pwani. Aidha, Kiwanda cha

Goodwill Ceramic Tanzania Limited tayari kimeunganishwa na kuanza kutumia Gesi Asilia ambapo kitatumia Jumla ya Futi za Ujazo milioni saba kwa siku (7 mmscf).

**91. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali kupitia TPDC itakamilisha mazungumzo na Kiwanda cha kuzalisha Mbolea cha Kilwa Masoko ambacho TPDC ni Mbia pamoja na Kampuni ya *Ferrostaal Industry Project GmbH* ya Ujeruman na Wabia wake *Holdor Topsoe A/Sna Fauji Fertiliser Company Limited*. Kiwanda hiki hadi kukamilika kitagharimu kiasi cha **Dola za Marekani bilioni 1.92** sawa na takriban **Shilingi trilioni 4.44**. Mahitaji ya Gesi Asilia yanatarajiwa kuwa Futi za Ujazo milioni 104 kwa siku (104 mmscf) na kitazalisha mbolea aina ya amonia tani 2,200 kwa siku pamoja na aina ya urea tani 3,850 kwa siku.

**92. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, mawasiliano na Majadiliano kuhusu upatikanaji wa Gesi Asilia kwa Kiwanda cha kuzalisha Mbolea cha Mtwara chini ya Kampuni ya *Helm* ya Ujeruman na Wabia wake ambao ni Halmashauri za Mkoa wa Mtwara yanaendelea. Kiwanda hiki hadi kukamilika kitagharimu kiasi cha **Dola za Marekani bilioni 1.2** sawa na takriban **Shilingi trilioni 2.77**. Mahitaji ya Gesi Asilia yanatarajiwa kuwa Futi za Ujazo millioni 80 kwa siku (80 mmscf) na kitazalisha mbolea tani 3,700 kwa siku.

#### *Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (Bulk Procurement System)*

**93. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea na usimamizi wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja kupitia Wakala wake (*Petroleum Bulk Procurement Agency – PBPA*). Taratibu za uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja zimeainishwa katika Sheria ya Petroli (*The Petroleum Act, No. 21*) ya Mwaka 2015 pamoja na Kanuni za Uagizaji wa Bidhaa za Petroli kwa Pamoja - (*The Petroleum (Bulk Procurement) Regulations, 2017, GN No. 198 of 2017*). Mfumo huu unaweka utaratibu wa mafuta yote kuagizwa kwa pamoja kwa kutumia utaratibu maalum unaowekwa ili pia kupata manufaa ya kiuchumi (*economies of scale*) na mafuta yanayokidhi ubora. Aidha,

Mfumo huu umelenga kuhakikisha usalama wa upatikanaji wa mafuta (*security of supply of petroleum products*) nchini kwa wakati wote.

**94. *Mheshimiwa Spika*,** Mfumo wa zabuni ndio umekuwa unatumika katika kupata Kampuni zitakazoagiza na kuleta mafuta nchini. Kampuni za mafuta huwasilisha kwa Wakala kiasi cha mafuta ya petroli, dizeli, mafuta ya ndege na mafuta ya taa wanachohitaji kuuza kwa Mwezi mzima. Baada ya kupata kiasi cha mafuta kutoka kwa Kampuni hizo, Wakala huandaa nyaraka za zabuni na baadaye kutoa taarifa ya zabuni hiyo kwa Kampuni zote zilizoidhinishwa (*pre-qualified*) kushiriki katika zabuni za kuleta mafuta. Mafuta yanayotakiwa kutumika hapa nchini ni lazima yaagizwe kwa kutumia Mfumo huu (*mandatory for locally used fuel*), lakini mafuta yanayopitia hapa nchini (*transit*) si lazima kuagizwa kwa kuitia Mfumo huu (*it is optional*).

**95. *Mheshimiwa Spika*,** Mfumo huu umeleta mafanikio makubwa katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Taifa kwa ujumla. Baadhi ya mafanikio hayo ni kushuka kwa gharama ya manunuzi (*Premium*) kutoka wastani wa Dola za Marekani 50 kwa tani kabla ya utaratibu huu mpaka wastani wa takriban Dola za Marekani 20 kwa tani na uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini. Hii ni kutohana na ukweli kwamba zabuni za mafuta ya Mwezi hutolewa zaidi ya Mwezi mmoja kabla ya muda husika, pamoja na uhakika wa usahihi wa takwimu za mafuta yaliyoagizwa na kuingia hapa nchini. Kutohana na takwimu hizi vyombo mbalimbali vinaweza kupanga mipango yake kwa ufanisi zaidi ikiwemo Mapato ya Serikali yatokanayo na Kodi za mafuta na kiasi cha fedha zinazoweza kupatikana kwa Mwezi kutohana na mafuta kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini, Mfuko wa Barabara, n.k.

**96. *Mheshimiwa Spika*,** Mfumo huu pia umesaидia kupunguza gharama za meli kusubiri kupakua mafuta (*Demurrage costs*). Hivi sasa gharama hizo ni katika **Dola za Marekani 1.6** na **3.5** kwa tani moja ya uzito tofauti na **Dola**

**za Marekani 45** hadi **50** kwa tani moja ya uzito iliyokuwa kabla ya Mfumo huu kuanza kutumiwa. Kupungua kwa gharama hizi kunatokana na upangaji mzuri wa meli unaofanywa na PBPA na kuongezeka kwa sehemu za kupakulia mafuta. Jitihada za TPA kujenga sehemu ya SPM ambapo meli kubwa za dizeli zinaweza kupakua mafuta na vilevile kuanza kutumika kwa Bandari ya Tanga kumepunguza sana msongamano wa meli katika sehemu ya Kurasini *Oil Jet One (KOJ 1)*.

**97. *Mheshimiwa Spika***, vilevile, Mfumo huu umewezesha EWURA kupanga bei elekezi kwa kutumia takwimu sahihi za bei ya Mafuta katika Soko la Dunia na gharama za kusafirisha mafuta hadi hapa nchini. Aidha, Mfumo huu umepunguza gharama za meli kusubiri kabla ya kupakua mafuta (*demurrage*) na umewezesha kudhibiti ubora wa mafuta yanayoagizwa nchini.

**98. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Mwezi Januari hadi Desemba, 2016 Jumla ya **lita bilioni 4.97** za mafuta ziliingizwa nchini ambapo **lita bilioni 4.73** ziliingizwa kuititia Bandari ya Dar es Salaam na **lita milioni 237.85** ziliingizwa kuititia Bandari ya Tanga. Kati ya mafuta hayo, **lita bilioni 2.34** sawa na **asilimia 47.11** yalikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na **lita bilioni 2.65** sawa na **asilimia 52.89** yalikuwa kwa ajili ya Nchi Jirani.

**99. *Mheshimiwa Spika***, mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani yameongezeka kwa **asilimia 2.23** kutoka **lita bilioni 2.29** Mwaka 2015 hadi **lita bilioni 2.34** Mwaka 2016. Aidha, mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya Nchi Jirani (Burundi, DRC, Rwanda, Uganda na Zambia) yameongezeka kwa **asilimia 3.02** kutoka **lita bilioni 2.57** Mwaka 2015 hadi **lita bilioni 2.65** Mwaka 2016. Ongezeko hilo linatokana na kukua kwa mahitaji ya mafuta ndani ya nchi hizo pamoja na nchi jirani kuongeza uagizaji wa mafuta kuititia Bandari ya Dar es Salaam.

**100. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaaniszisha Mpango wa kuongeza upakuaji

wa mafuta kwa kutumia Bandari ya Tanga yatakayokuwa yanasantazwa Mikoa ya Kaskazini mwa nchi na pia kuanzisha Mfumo huu kwa Bandari ya Mtwara kwa kusambaza katika Mikoa ya Kusini mwa nchi na Nchi Jirani. Vilevile, kuanzisha uingizaji wa bidhaa za *Liquified Petroleum Gas (LPG)* kwa kutumia Mfumo kama huu ili kuweza kupata faida zinazopatikana kwa Mfumo wa uagizaji kwa pamoja.

**101. *Mheshimiwa Spika***, uagizaji wa mafuta kwa pamoja umeendana na uboreshaji wa viwango vya mafuta anayonunua mlaji wa mwisho katika kituo. Ili kudhibiti ubora wa mafuta, Serikali ilifanya uamuzi wa kupunguza tofauti katи ya bei ya Mafuta ya Taa na bei ya mafuta ya Petroli na Dizeli. Kuimarisha udhibiti wa ubora wa mafuta, vinasaba vimekuwa vikitumika kubaini uchanganyaji wa mafuta unaoathiri ubora. Hata hivyo, utaratibu wa matumizi ya vinasaba umekuwa ukilalamikiwa na baadhi ya wadau hali iliyosukuma Wizara yetu kuangalia kwa makini mfumo huu mwaka wa fedha ujao.

***Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG Project)***

**102. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 taarifa ya tathmini ya athari za mazingira na kijamii imekamilika. Pamoja na taarifa hiyo, Mpango wa kuwapatia maeneo mbadala Wananchi waishio katika eneo litakalojengwa Mitambo ya LNG la Likong'o Mkoani Lindi (*Resettlement Action Plan*) umekamilika. Vilevile, kazi za kuingiza Michoro ya eneo la Mradi wa LNG kwenye Ramanii ya Mipango Miji imekamilika. Aidha, utaratibu wa uvunaji Gesi Asilia kutoka kina kirefu cha maji ya Bahari ya Hindi hadi eneo la nchi kavu (*Concept selection*) kwa Kitalu Na.1 na Kitalu Na.2 umekamilika na kwa Kitalu Na.4 unatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

**103. *Mheshimiwa Spika***, Majadiliano ya kufikia Makubaliano ya utekelezaji wa Mradi (*Host Government Agreement - HGA*) katи ya Kikosi Kazi cha Wataalam wa Serikali (*Government Negotiation Team*) na Kampuni za Utafutaji Mafuta na Gesi Asilia (IOCs) yalianza rasmi Mwezi

Septemba, 2016. Mradi huu utachukua muda wa takribani Miaka nane (8) hadi kumi (10) kufikia uzalishaji na utagharimu takriban **Dola za Marekani bilioni 30**, sawa na takriban **Shilingi trilioni 69.33**. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 **Shilingi bilioni 13** zimetengwa kwa ajili ya malipo ya fidia, upatikanaji wa ardhi pamoja na shughuli nyingine za Mradi huu.

*Miradi ya Usafirishaji wa Mafuta na Gesi Asilia*

*Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Kabaale (Uganda) hadi Bandari ya Tanga (Tanzania)*

**104. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kushiriki kwa karibu katika matayarisho ya ujenzi wa Bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Kabaale (Uganda) hadi Tanga (Tanzania), kilomita 1,445. Kazi zilizofanyika hadi Mwezi Machi, 2017 ni pamoja na: kusainiwa kwa Mkataba wa Makubaliano ya Awali (*MoU*); kutolewa kwa Vivutio vya Kodi; kufanya tathmini ya njia ya Bomba (*survey*); tathmini ya mahitaji ya njia ya Bomba (*infrastructure requirements*); na Tathmini ya Athari ya Mazingira Kijamii (*Environmental and Social Impact Assesment*) na kusainiwa kwa *Inter-Governmental Agreement (IGA)* tarehe 26 Mei, 2017. Gharama za Mradi huu ni **Dola za Marekani bilioni 3.5** sawa na takriban **Shilingi trilioni 8.09**. Wadau Wakuu katika Mradi huu ni Kampuni ya TOTAL (Ufaransa), CNOOC (China) na TULLOW (Uingereza) pamoja na Serikali za Tanzania na Uganda.

**105. Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazotekelawa katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 ni pamoja na Mabunge ya nchi husika (Tanzania na Uganda) kuridhia Mkataba huo; kuanza Mazungumzo ya Mkataba baina ya Serikali husika na Kampuni ya Bomba (*Host Government Agreement - HGA*); kuanza Mazungumzo ya Mkataba wa Wanahisa (*Shareholders Agreement*); kuanza Mazungumzo ya Mkataba baina ya Mamlaka ya Bandari (TPA) na Kampuni ya Bomba; Mwekezaji kukamilisha usanifu wa Mradi (*Front End*

*Engineering Design - FEED), upimaji (survey) wa eneo la kujenga ghala katika Bandari ya Tanga; utafiti katika Mkusa wa Bomba na katika eneo la Bahari karibu na Bandari ya Tanga (*mateocean and geophysical technical studies*).*

***Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi (White Petroleum Products) kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia)***

**106. *Mheshimiwa Spika***, Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi (*White Petroleum Products*) kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia) unahusisha ujenzi wa Bomba lenye urefu wa takriban kilomita 1,710 litakalojengwa sambamba na Bomba la TAZAMA linalosafirisha Mafuta Ghafi (*Crude Oil*) kutoka Dar es Salaam hadi Ndola. Bomba Jipya litakuwa na uwezo wa kusafirisha tani millioni nne (4) za mafuta kwa Mwaka. Mradi huu pia utahusisha ujenzi wa Mabomba ya Matoleo ya mafuta (*take-off points*) katika maeneo ya Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe. Gharama za Mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani bilioni 1.5** sawa na **Shilingi trilioni 3.47.**

**107. *Mheshimiwa Spika***, Makubaliano ya kuanza ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi yalitokana na ziara ya Rais wa Jamhuri ya Zambia **Mhe. Edgar Chagwa Lungu**, alioifanya nchini Tanzania tarehe **29 Novemba, 2016** na kukutana na Mwenyeji wake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**.

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi huu ni kuunda Kamati Ndogo (*sub - committees*) chini ya Makatibu Wakuu wanaoshughulikia masuala ya Nishati zitakazojadili masuala ya Sheria (*Legal and Institutional framework*), Fedha (*Fiscal and Financing Options*) na Utaalam (*Technical Issues*); kuandaa Andiko la Mradi (*Project Concept Paper*); kutengeneza Hadidu za Rejea (*Terms of Reference*) kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu (*Feasibility Study*) utakaoonesha gharama za Mradi na namna bora ya kutekeleza Mradi.

Kazi nyingine inayoendelea ni kupitia Mikataba iliyopo ya Kisheria na ya Kifedha ya TAZAMA (*TAZAMA Convention, 1968, Article of Association of TAZAMA*).

**108. *Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa Bomba hili utafanywa kwa ushirikiano wa nchi mbili za Tanzania na Zambia na utaleta manufaa makubwa kwa nchi zote. Kwa upande wa Tanzania manufaa yatakayopatikana ni pamoja na uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini hususan Mikoa ya Dodoma, Iringa, Katavi, Mbeya, Morogoro, Njombe, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Songwe, Rukwa na Tabora; ufanisi, usalama na bei nafuu katika kusafirisha mafuta ikiwa ni pamoja na kupunguza matumizi ya malori ya mafuta ambayo yamekuwa yakiharibu miundombinu ya barabara. Utekelezaji wa Mradi huu unatarajiwa kuanza Mwaka 2018 na kukamilika Mwaka 2021.

*Miradi ya Usambazaji Gesi Asilia Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani*

**109. *Mheshimiwa Spika***, Mwezi Desemba, 2016 Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) lilitangaza zabuni ya kumpata Mshauri Mwelekezi ili kuhuisha taarifa ya Upembuzi Yakinifu na usanifu wa kina wa michoro ya Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia Mkoani Dar es Salaam. Utaratibu wa kukamilisha zoezi la kumpata Mshauri linatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mwezi Juni, 2017. Taarifa ya Mshauri itakayopatikana itatumika kushawishi Taasisi za Fedha zilizoonesha nia ya kufadhili Mradi huu zikiwemo, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Benki ya Exim ya China. Katika Mwaka wa Fedha 2017/18 Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya uhuishaji wa taarifa ya Upembuzi Yakinifu. Aidha, kwa upande wa Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara, Serikali kupitia TPDC imeendelea na juhudhi za kutafuta fedha za Mikopo ya riba nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa usambazaji Gesi Asilia kwa ajili ya matumizi ya viwandani, majumbani na Taasisi mbalimbali kwenye Mikoa hiyo.

**SEKTA NDOGO YA NISHATI JADIDIFU (i) Nishati ya Jua (Solar Energy)**

**110.** *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ilifanikisha kupatikana kwa **MW 1** katika maeneo ambayo yako nje ya Gridi ya Taifa kwenye Kisiwa Cha Bwisyia kilichopo Ziwa Viktoria na maeneo mengine katika Wilaya za Simanjiro Mkoani Manyara na Lumuli Mkoani Iringa. Aidha, kupitia Mfumo wa Usambazaji wa Umeme wa Jua Majumbani na kwenye Taasisi za Afya na Elimu (*Solar Home Systems*), kiasi cha **MW 2** kilipatikana katika maeneo mbalimbali nchini na kufanya upatikanaji wa umeme kwa kupitia Mfumo huu kufikia takriban **MW 9**.

**111.** *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itakamilisha uandaaji wa Ramani ya maeneo yenye fursa za uwekezaji wa uzalishaji wa umeme wa Jua ikijumuisha uainishaji wa miundombinu husika kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika Sekta Ndogo hii. Aidha, Serikali kupitia TANESCO itaanza kufanya Upembuzi Yakinifu katika Maeneo ya Kishapu na Visiwa vya Mafia kwa ajili ya uzalishaji umeme wa Jua kwa katи ya **MW 50** hadi **300**.

Serikali pia kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itahakikisha kuwa Visiwa zaidi vya Ziwa Victoria vikiwemo vya Bukerebe, Bulubi, Bushengele, Bwiro, Izinga, Kamasi, Kweru Kuu, Kweru Mto, Sizu na Zeru vinapatiwa umeme kupitia Gridi Ndogo za Umeme wa Jua. Aidha, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Wasambazaji wa vifaa na Mifumo ya Umeme Jua ili maeneo mengine yaliyo pembezoni yapate umeme kwa njia hii.

**(ii) Nishati ya Upepo (Wind Energy)**

**112.** *Mheshimiwa Spika*, uwekezaji katika Nishati ya Upepo kwa kiasi kikubwa unaathiriwa na upatikanaji wa ardhi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe na Halmashauri ya Mji wa Makambako ilifanya utatuzi wa

mgogoro wa ardhi kati ya Mwekezaji (Kampuni ya Sino-Tan) na Halmashauri husika. Kazi inayoendelea ni kupitia upya tathmini ya fidia kwa wananchi watakaopisha utekelezaji wa Miradi.

Aidha, Kampuni ya Windlab ya Afrika Kusini ilianza utafiti wa takwimu za Upepo ili kuwekeza katika eneo la Makambako. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itafanya tathmini ya kina na ufuatiliaji wa Miradi ya Umeme wa Upepo na kuwabaini Waendelezaji wanaohodhi maeneo kwa muda mrefu bila kuyaendeleza ili maeneo hayo yaweze kushindanishwa na kupewa Waendelezaji wenye uwezo wa kuyaendeleza. Kiasi cha **Shilingi bilioni 1.3** ambazo ni fedha za Nje kimetengwa kwa ajili ya uendelezaji wa Miradi ya Nishati ya Jua na Upepo.

*(iii) Miradi ya Tungamotaka (Bio- Energies)*

**113. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 uzalishaji wa umeme kwa kutumia Tungamotaka (*Biomass*) zitokanazo na mabaki ya miwa katika Viwanda vya Sukari, mazao ya misitu na mkonge umefikia **MW 38** ambapo **MW 10.5** zimeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na **MW 27.5** zinatumika kwa ajili ya shughuli za Viwanda husika. Viwanda hivyo ni Tanganyika Planting Company (TPC) cha Mkoani Kilimanjaro **MW 10**; Kilombero Sugar Company Limited cha Mkoani Morogoro **MW 9**; Mtibwa Sugar cha Mkoani Morogoro **MW 5**; Kagera Sugar cha Mkoani Kagera **MW 5**; Tanzania Wattle Company (TANWAT) cha Mkoani Iringa **MW 2.5**; Ngombeni Biomass Project cha Mafia **MW 1** na Mkonge Energy cha Mkoani Tanga **MW 1**. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara itaendelea na uhamasishaji wa Sekta Binafsi ili kuongeza uzalishaji wa umeme utokanao na Tungamotaka. Hatua hii itaongeza mchango wa Tungamotaka katika upatikanaji wa umeme nchini kwa takriban **MW 2** ambazo zitaongezwa kwenye Gridi ya Taifa na kiasi kingine zaidi kutumika kwa ajili ya Viwanda husika.

(iv) *Miradi ya Jotoardhi (Geothermal)*

**114. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi (*Tanzania Geothermal Development Company Limited - TGDC*), ambayo ni Kampuni Tanzu ya TANESCO, imekamilisha utafiti wa kina (*detail surface study*) wa uendelezaji Nishati ya Jotordhi katika maeneo ya Ziwa Ngozi (Mbeya) mnamo Mwezi Septemba, 2016, chini ya ufadhili wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) na Shirika la Maendeleo la Iceland (ICEIDA). Aidha, utafiti umeweza kuainisha sehemu tatu (3) za kuchoronga Visima vya Majaribio (*Slim Wells*) katika eneo la Ziwa Ngozi ili kutathmini kiasi cha hifadhi ya rasilimali ya Jotoardhi na uwezo wake wa kuzalisha umeme. Vilevile, Serikali kupitia Mshauri Mwelekezi ambaye ni Electro- consult ya nchini Italia chini ya ufadhili wa Serikali ya Iceland kupitia Shirika la Maendeleo la Iceland (ICEIDA) yupo katika hatua za mwisho za kukamilisha utafiti wa kina (*detail surface studies*) katika maeneo ya Mbaka-Kiejo, Mkoani Mbeya na Luhoi Mkoani Pwani.

**115. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Serikali kupitia TGDC imejipanga kutekeleza Mradi wa uchorongaji Visima Vitatu (3) vya utafiti katika eneo la Ziwa Ngozi. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 12** sawa na **Shilingi bilioni 27.73**. Mradi huu utafadhiliwa na Serikali kwa kushirikana na Mfuko wa Uendelezaji Jotoardhi (*Geothermal Risk Mitigation Facility - GRMF*) ulio chini ya Kamisheni ya Afrika (AUC). Serikali itagharamia kiasi cha **Dola za Marekani milioni 8.78** sawa na **Shilingi bilioni 20.29** na kiasi kilichobakia cha **Dola za Marekani milioni 3.33** sawa na **Shilingi bilioni 7.70** kitatolewa na GRMF kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

**116. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Serikali kupitia TGDC inategemea kufanya utafiti wa kina (*detail surface study*) katika eneo la Kisaki, Mkoani Morogoro kwa kushirikiana na GRMF. Gharama za Mradi huu ni kiasi cha **Dola za Marekani milioni 1.32** sawa na **Shilingi bilioni 3.05**. Serikali itachangia kiasi cha **Dola za**

**Marekani 165,210** sawa na **Shilingi milioni 381.80** na GRMF itachangia kiasi cha **Dola za Marekani milioni 1.16** sawa na **Shilingi bilioni 2.68**.

**117. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TGDC inaendelea kutathmini uendelezaji wa rasilimali ya Jotoardhi kwa ajili ya matumizi ya moja kwa moja (*direct heat uses*). Matumizi hayo ni pamoja na kutengeneza mabwawa ya kuogelea ya maji moto pamoja na uboreshaji wa sehemu hizo za asili ambazo huvutia utalii. Matumizi mengine ni pamoja na uzalishaji wa mazao ya kilimo cha maua na mboga mboga, ukaushaji wa nafaka, ufugaji wa samaki na shughuli za viwandani (*industrial processes*). Miongoni mwa sehemu ambazo zinaweza kuendelezwa kwa matumizi hayo ni Ibadakuli iliyoko Mkoani Shinyanga na Songwe katika Mkoa wa Songwe.

**118. Mheshimiwa Spika,** ili kuwa na uendelezaji endelevu wa Nishati ya Jotoardhi nchini, Serikali inaendelea na uandaaji wa Mpango Mkakati wa Uendelezaji wa Jotoardhi na Sheria ya kuendeleza Jotoardhi nchini. Mpango wa kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kazi hii utakamilika Mwezi Agosti, 2017. Utekelezaji wa kazi hizi unafadhiliwa na *Climate Investment Funds (CIF)* kupitia Mpango wa *Scaling Up Renewable Energy Programme(SREP)* kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa gharama ya **Dola za Marekani 450,000**, sawa na takriban **Shilingi milioni 1.04**.

*(v) Umeme wa Maporomoko Madogo ya Maji (Mini-Hydro)*

**119. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuhamasisha uendelezaji wa Miradi ya Maporomoko Madogo ya Maji ili kuhakikisha inatoa mchango katika kuwafikishia umeme Wananchi na hasa wa vijijini. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kiasi cha **MW 36.99** kutoka Maporomoko Madogo ya Maji kilizalishwa ambapo **MW 6.11** zimeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na kiasi cha **MW 30.88** kinatumika katika Gridi Ndogo Ndogo na Taasisi. Baadhi ya maeneo hayo yenye Maporomoko Madogo ya Maji ni Andoya

(Mbinga), Darakuta (Manyara), Ikondo (Njombe), Kiliflower (Arusha), Mwenga (Mufindi), Tulila (Songea) na Yovi (Kilosa).

**120. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaendelea kuhamasisha uendelezaji wa Miradi ya Maporomoko Madogo ya Maji ili kuhakikisha inatoa mchango wa upatikanaji wa umeme wa bei nafuu nchini.

**(vi) *Usambazaji Umeme kwa Mfumo wa Gridi Ndogo (Mini-Grids)***

**121. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Serikali ilifanya ukaguzi na uhakiki wa Mifumo ya Gridi Ndogo ili kubaini changamoto zinazowakabili Waendelezaji. Katika kutatua changamoto hizo, Serikali ilianda Viwango na Kanuni za usimamizi wa Gridi Ndogo zinazotoa Mwongozo wa uendeshaji wake hususan pale eneo husika linapofikiwa na Gridi ya Taifa. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaendelea kuweka mazingira bora ya uendelezaji wa Gridi Ndogo za Umeme ili kuwezesha Wananchi kupata umeme hasa maeneo ya Visiwa na yale yaliyo pembezoni. Aidha, kupitia REA III, Mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 50** ambazo ni fedha za Nje kutoka Serikali za Uingereza na Sweden ambapo Jumla ya **MW 26.9** zinatarajiwa kuzalishwa.

**(vii) *Uendelezaji wa Matumizi ya Bayogesi (Biogas)***

**122. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Serikali kwa kushirikiana na Kituo cha Usambazaji na Uendelezaji wa Teknolojia ya Kilimo Vijiji (Center for Agricultural Mechanization and Rural Technology - CAMAR TEC) imeweza ujenzi wa Mitambo 1,980 na kufanya Jumla ya idadi ya Mitambo iliyojengwa kufikia 15,980 tangu Programu ianzé Mwaka 2009. Wananchi 95,880 katika Mikoa yote ya Tanzania Bara walinufaika na programu hii kwa kuweza kumiliki Mitambo na kutumia Bayogesi kwa ajili ya kupikia na kuwashaa taa. Aidha, Makampuni Binafsi ya ujenzi wa Mitambo ya Bayogesi yapatayo 100 yalianzishwa na kutoa ajira kwa Watanzania takriban 1,000. Ili kuongeza

msukumo wa ujenzi wa Mitambo mingi ya Bayogesi nchini, Mwaka 2016 Serikali kupitia Mfuko wa Nishati Vijiji ilianza kutoa ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa Mitambo 10,000 nchini. Gharama ya Utekelezaji wa Progamu nzima hadi kufikia Mwaka 2019 ni **Dola za Marekani milioni 10.7** sawa na takriban **Shilingi bilioni 24.73**. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Jumla ya **Shilingi bilioni 1.5** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu.

**123. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaendelea kutoa ruzuku kupitia Mfuko wa Nishati Vijiji ili kuhamasisha Kampuni za uzalishaji mkonge, korosho pamoja na Halmashauri za Miji kutumia teknolojia ya Bayogesi katika uzalishaji wa umeme kwa lengo la kuongeza thamani ya mazao na utunzaji wa mazingira kwa kutumia Mabaki ya Mazao na Taka za Mijini. Kupitia Mpango huu, REA imetenga Jumla ya **Shilingi bilioni 50** kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ya Nishati Jadidifu ikiwemo teknolojia ya Bayogesi.

*(viii) Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Upatikanaji wa Nishati Endelevu kwa Wote (Sustainable Energy for All initiative - SE4ALL)*

**124. Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni moja ya nchi zinazotekeliza Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Nishati Endelevu unaojulikana kama *Sustainable Energy for All* (SE4ALL). Mpango huu una lengo la kuwapatia nishati bora watu wote Duniani ifikapo Mwaka 2030. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Wizara ilikamilisha maandalizi ya "Action Agenda" na "Investment Prospectus" ambazo ni Miongozo muhimu katika utekelezaji wa malengo ya SE4All. Aidha, Serikali kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ilianza maandalizi ya kuandaa utaratibu wa utekelezaji wa miongozo hii. Vilevile, kupitia ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Wizara ilikamilisha maandalizi ya Programu ya Miaka Mitano (5) ambayo itasaidia kuanza kwa utekelezaji wa Mpango wa SE4ALL.

**125. Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua mchango wa Tanzania katika jitihada zake za utekelezaji wa SE4ALL, Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Umoja wa Mataifa uliichagua Tanzania kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa SE4ALL kwa nchi za Afrika zinazoendelea uliofanyika tarehe 5 hadi 6 Desemba, 2016. Mkutano huo uliandaliwa kwa ushirikiano na Ofisi ya Umoja wa Mataifa (UN) inayoshughulikia nchi zinazoendelea (*Office of the High Representative for LCDS*) pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

**126. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali kwa kushirikiana na UNDP, AfDB na Wadau wengine wakiwemo Umoja wa Ulaya na Benki ya Dunia itaendelea na utekelezaji wa SE4ALL ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi iliyobainishwa katika Mpango wa Uwekezaji wa SE4ALL (*Investment Prospectus*) na uratibu wa shughuli za Programu hii.

**(ix) Mpango wa Matumizi Bora ya Nishati (Energy Efficiency)**

**127. Mheshimiwa Spika**, Matumizi Bora ya Nishati (*Energy Efficiency*) ni suala linalotakiwa kupewa kipaumbele ili kupunguza upotevu wa nishati kuanzia uzalishaji, usafirishaji, usambazaji hadi mtumiaji wa mwisho. Kutohana na juhudimbalimbali zilizofanywa na Serikali pamoja na TANESCO zikiwemo za kukarabati na kuwekeza katika njia za usafirishaji na usambazaji wa umeme, upotevu wa umeme umepungua kutoka **asimilia 21** ya Mwaka wa Fedha wa 2015/16 hadi **asilimia 17** kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaendelea na uwekezaji wa kuboresha njia za usafirishaji na usambazaji umeme ili kuhakikisha kwamba upotevu wa umeme unashuka hadi kufikia **asilimia 16**.

**128. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Watumiaji wa mwisho (*demand side*), katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Serikali kwa ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya (EU) imeandaa Mpango Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati ulioweka mipango na Miradi mbalimbali ya kuzuia upotevu

wa nishati katika nyumba za makazi, majengo ya biashara, viwanda na Taasisi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wakiwemo Umoja wa Ulaya (EU), Sida, NORAD na GIZ itaendelea kutekeleza Mradi huu.

**129. *Mheshimiwa Spika***, Gharama za Nishati hususan umeme zinachukua sehemu kubwa ya gharama za uzalishaji katika viwanda. Ili kuongeza ushindani wa viwanda vyetu ni muhimu kupunguza gharama za uendeshaji kwa kudhibiti upotevu wa nishati na matumizi yasiyo ya lazima. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) imeandaa Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati kwa Watumiaji Wakubwa (*Energy Efficiency Action Plan for Designated Consumers*) na itatekeleza Mpango huo kwa kushirikiana na GIZ katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Mradi huu unakadiriwa kugharimu kiasi cha **Euro milioni 10** sawa na **Shilingi bilioni 21.3** na utatekelezwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18 hadi 2020/21.

## **SEKTA YA MADINI**

### ***Utafutaji na Ugunduzi Nchini wa Gesi ya Helium***

**130. *Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuchukua hatua na kuweka mipango mbalimbali ya kuendeleza utafutaji na ugunduzi wa Gesi ya Helium ambayo ni adimu Duniani. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Kampuni ya Helium One Limited imeendelea kufanya utafiti wa Gesi hiyo kupitia Kampuni zake Tanzu za Gogota (TZ) Limited, Njozi (TZ) Limited na Stahamili (TZ) Limited zenye leseni za utafutaji katika maeneo mbalimbali ya Mikoa ya Rukwa na Manyara (Ziwa Eyasi na Balangida). Katika kutekeleza kazi hizo, Kampuni hiyo ilitoa Kandarasi kwa Vyuo Vikuu vya Oxford na Durham vya nchini Uingereza kufanya utafiti katika leseni zake zilizopo Ziwa Rukwa. Utafiti uliofanywa na Vyuo hivyo umewezesha kugundulika kwa Helium ya wingi wa takriban Futi za Ujazo bilioni 54 kutohana na sampuli za mavujia (*gas seeps*) zilizochukuliwa na

kufanyiwa uchunguzi katika maeneo matano (5) yaliyopo eneo la Ziwa Rukwa. Kiasi hicho kinakadirisha kuwa kikubwa zaidi ya mara sita (6) ya mahitaji ya Dunia kwa sasa.

**131. *Mheshimiwa Spika***, Kazi ya uchorongaji wa Visima vya Utafiti katika maeneo hayo zinatarajija kuanza Mwaka 2018. Kazi hiyo itawezesha kuhakiki kiasi halisi cha Gesi ya Helium kilichopo katika maeneo ilipogunduliwa. Aidha, uchimbaji wa Gesi ya Helium utaanza mara baada ya kukamilika kwa kazi ya utafiti wa kina, Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari za Mazingira na pia leseni ya uchimbaji wa Gesi hiyo kutolewa. Kwa sasa shughuli za kukusanya taarifa zaidi za kijolojia, kijofizikia, na *2D Seismic survey* zinaendelea ili zitumike kwa ajili ya uchorongaji wa Visima vya Utafiti (*Exploration wells*). Gesi ya Helium, pamoja na matumizi mengine hutumika kupooza mashine za *MRI Scanners* na vinu vya *nuclearna* pia hutumika katika *floating balloons*. Serikali imeunda Kikosi Kazi chake ambacho kitafanya kazi na Wataalam Wazoefu kutoka nchi zenye uzoefu mkubwa wa Gesi ya Helium.

#### *Ukusanyaji wa Mapato yatokanayo na Shughuli za Uchimbaji Madini Nchini*

**132. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara ilikusanya Mrabaha wa Jumla ya **Dola za Marekani milioni 56.77** sawa na takriban **Shilingi bilioni 131.20** kutoka kwenye Migodi Mikubwa ya Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, NewLuika, North Mara, STAMIGOLD, TanzaniteOne, Mwadui, Ngaka na Dangote. Pia, kiasi cha Mrabaha wa **Shilingi bilioni 4.23** kilikusanywa kutokana na mauzo ya dhahabu iliyozalishwa kwa kuchenjua marudio kwa teknolojia ya "vat leaching". Aidha, Mrabaha wa **Shilingi bilioni 4.45** ulikusanywa kutokana na uzalishaji wa madini ya ujenzi na viwandani kutoka kwa Wachimbaji Wadogo. Makusanyo hayo yametokana na kazi ya ukaguzi na uhakiki wa madini yaliyozalishwa katika Migodi hiyo inayofanyika kwa ushirikiano baina ya Ofisi za Madini za Kanda na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA).

Vilevile, Wizara imekusanya kiasi cha **Shilingi milioni 14.52** kutokana na ada za Leseni na Vibali mbalimbali.

**133. Mheshimiwa Spika**, vilevile katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara ilikusanya Mrabaha wa **Dola za Marekani milioni 2.40** sawa na **Shilingi bilioni 5.55** kutokana na mauzo ya Almasi na **Dola za Marekani 906,347** sawa na **Shilingi bilioni 2.09** kutokana na mauzo ya vito ghafi na viliwyokatwa mathalan *Tanzanite, Garnet, Moonstones, Ruby, Spinel, Tourmaline, Garnet, Sapphire, Amethyst, Tsavorite na Zircon*. Malipo haya yalitokana na kazi ya uthamini iliyofanywa na *Tanzania Diamond Sorting Unit- TANSORT*.

**134. Mheshimiwa Spika**, pamoja kupungua kwa shughuli za uwekezaji katika Sekta ya Madini katika miaka hilvi karibuni kulikotokana na kushuka kwa bei ya madini katika soko la dunia, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa umeongezeka kufikia Asilimia 4 Mwaka 2015 kutoka Asilimia 3.7 Mwaka 2014/15.

**135. Mheshimiwa Spika**, aidha, Ajira za moja kwa moja (*direct employment*) kwa Watanzania kwenye migodi mikubwa nchini imepungua kutoka 7,335 Mwaka 2015 na kufikia 6,207 mwaka 2016 ikiwa ni punguzo la Asilimia 15. Punguzo hilo limesababishwa na migodi kupunguza wafanyakazi hususan wa ajira za muda na mikataba kutokana na kushuka kwa bei ya dhahabu. Aidha, idadi ya wataalam toka nje ya nchi (*expatriates*) imepungua kutoka 333 mwaka 2015 na kuwa 294 mwaka 2016 ikiwa ni punguzo la Asilimia 12.

**136. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho hicho, Wizara kuitia TMAA ilifanya ukaguzi wa hesabu za Fedha za Migodi Mikubwa na ya kati kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kuiwezesha Serikali kukusanya Kodi ya Mapato (*Corporate Tax*) ya Jumla ya **Shilingi bilioni 79.26** kutoka kwa Kampuni za uchimbaji mkubwa wa dhahabu nchini. Kati ya malipo hayo, **Shilingi bilioni 45.76** zimelipwa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited na

**Shilingi bilioni 33.50** zimelipwa na Kampuni ya North Mara Gold Mine Limited. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara kuititia Wakala wa Ukaguzi wa Madini (TMAA) itaendelea kufanya ukaguzi ili kuhakikisha malipo stahiki, hususan Kodi ya Mapato (*Corporate Income Tax*) yanalipwa Serikalini.

**137. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali inalenga kukusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 194.4** katika Sekta ya Madini ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 215.96** zilizokadiriwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Kiasi hicho ni sawa na upungufu wa **asilimia 9.98**. Upungufu huo unatokana na kushuka kwa bei ya Dhahabu kwenye Soko la Dunia na kupungua kwa shughuli za utafutaji wa Madini nchini. Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa shughuli za madini ikiwa ni pamoja na kuweka mkazo katika ukusanyaji wa ada na Mrabaha kutoka kwa Wachimbajji wa aina (kada) zote na Wafanyabiashara wa madini nchini ili kufikia lengo la ukusanyaji maduhuli kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

#### *Ushuru wa Huduma (Service Levy)*

**138. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi 2017, Kampuni za uchimbaji mkubwa wa madini zimeendelea kulipa Ushuru wa Huduma (*Service Levy*) kwa Halmashauri mbalimbali ambapo Jumla ya **Shilingi bilioni 11.27** zimelipwa. Kati ya Fedha hizo, Mgodi wa Geita umelipa kiasi cha **Shilingi bilioni 3.92** kwa Halmashauri ya Mji wa Geita; Mgodi wa Bulyanhulu **Shilingi milioni 760.57** kwa Halmashauriya Wilayaya Msalala na **Shilingi milioni 374.61** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang’wale; Mgodi wa North Mara **Shilingi bilioni 3.10** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime; Mgodi wa Buzwagi **Shilingi bilioni 1.48** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama; Mgodi wa New Luika **Shilingi milioni 697.77** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya; na Mgodi wa STAMIGOLD **Shilingi milioni 167** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo. Mgodi wa TanzaniteOne umelipa **Shilingi milioni 66** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjirio; na Mgodi wa Williamson **Shilingi milioni 516.87** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mwadui. Aidha, Kampuni ya

Dangote Tanzania Limited imelipa **Shilingi milioni 187.92** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kuzipatia Halmashauri husika takwimu sahihi za mauzo ya madini ili kuwezesha ukusanyaji wa ushuru wa Hudumakutokakwa Kampuni zinazoendesha uchimbaji ndani ya Halmashauri zao.

*Uzalishaji na Mauzo ya Madini Nje ya Nchi*

**139. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Jumla ya wakia milioni 1.05 za Dhahabu, wakia 414,128 za Fedha na ratili milioni 10.4 za Shaba zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka Migodi Mikubwa ya STAMIGOLD, Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, New Luika na North Mara. Thamani ya Madini yaliyosafirishwa kwa kila Mgodi ni kama ifuatavyo: Mgodi wa STAMIGOLD **Dola za Marekani milioni 15.09**, Mgodi wa Bulyanhulu **Dola za Marekani milioni 245.60**, Mgodi wa Buzwagi **Dola za Marekani milioni 174.35**, Mgodi wa Geita **Dola za Marekani milioni 465.76**, Mgodi wa New Luika **Dola za Marekani milioni 76.15** na Mgodi wa North Mara **Dola za Marekani milioni 381.02** ambapo Jumla ya thamani ya madini hayo ni **Dola za Marekani bilioni 1.36** sawa na **Shilingi trilioni 3.14**.

**140. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho, Jumla ya karati 163,748 za Almasi na kilogram 2,872.79 za Tanzanite (*Grade A - I*) zilizalishwa na Migodi ya Mwadui na Tanzanite One, sawia. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini na kuwavutia Wawekezaji Wapya hususan kwenye madini ya *graphite* (kinywe), *lithium* na madini mengine yanayohitajika kwenye teknolojia ya kisasa (*Rare Earth Elements- REE*) ili kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika maendeleo makubwa ya uchumi wa Taifa letu.

**141. Mheshimiwa Spika,** Serikali inatambua umuhimu wa wawekezaji wakubwa wa nje na wa ndani katika uwekezaji kwenye Sekta ya Madini. Kwa Mwaka wa

Fedha 2017/18, Serikali inadhamiria kwa kushirikiana na wadau kupitia Sera, Sheria na mikataba ya uendelezaji wa sekta hii ili kuhakikisha uwekezaji katika sekta unaendelea na kushimiri.

*Kuendeleza Shughuli za Uchimbaji Mdogo wa Madini*

**142. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na jitihada za kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini nchini. Jitihada hizo ni pamoja na kutenga maeneo zaidi kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo, kutenga Fedha zaidi za ruzuku na kuimarisha Shughuli za Ugani.

**143. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara imetenga maeneo 11 kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo wa madini yaliyopo Msasa na Matabe Mkoani Geita, Biharamulo na Kyerwa Mkoani Kagera, Itigi Mkoani Singida, D-Reef, Ibindi na Kapanda Mkoani Katavi, Ngapa Mkoani Ruvuma, Nzega Mkoani Tabora na Kitowelo Mkoani Lindi. Maeneo hayo yana ukubwa wa takriban **Hekta 38,951.7**. Aidha, Wizara kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) inaendelea kufanya tathmini ya kina katika maeneo hayo ili kubaini uwepo wa mashapo ya madini zaidi kwa lengo la kuongeza tija kwa Wachimbaji Wadogo.

**144. *Mheshimiwa Spika***, katika kuwawezesha Wachimbaji Wadogo wa madini kupata vifaa, Serikali ilitenga kiasi cha **Shilingi bilioni 7.48** kwa ajili ya kutoa Ruzuku Awamu ya III kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (*Sustainable Management of Mineral Resources Project – SMMRP*) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Maombi ya Ruzuku Awamu ya III yaliyowasilishwa yamefanyiwa uchambuzi wa kina na taratibu kwa ajili ya kutolewa ruzuku hiyo zinakamilishwa. Hata hivyo, utoaji wa Ruzuku hiyo umechelewa kutohana na baadhi ya Wanufaika wa Ruzuku Awamu ya II kutumia fedha hizo kinyume na Makubaliano ya Mikataba baina yao na Serikali.

**145. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na tatizo hilo, Wizara imewaandikia barua Wanufaika wa Ruzuku kwa kuwajulisha mapungufu ya utumiaji wa Ruzuku hiyo ili wafanye marekebisho na kwa wale watakaoshindwa warudishe fedha. Utoaji wa Ruzuku Awamu ya III utaendelea baada ya kujiridhisha na utekelezaji wa zoezi hili.

**146. Mheshimiwa Spika**, natoa rai kwa Wanufaika wote wa Ruzuku kuhakikisha kuwa wanatumia fedha hizo kuendeleza Miradi ya uchimbaji na uchenjuaji madini kwa mujibu wa Mikataba yao. Wale wote watakaothibitika kutumia Fedha za Ruzuku vibaya hatua za kisheria zitaendelea kuchukuliwa dhidi yao.

**147. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (*SMMRP*) wa Benki ya Dunia Awamu ya II inaendelea na hatua za uanzishwaji wa Vituo vya Mfano saba (7) vya kuchenjulia madini katika maeneo ya Buhemba - Mara, D-Reef na Kapanda - Mpanda, Itumbi - Chunya, Katente - Geita, Kyerwa - Kagera na Maweni Mkoani Tanga. Uanzishwaji wa Vituo hivi utagharimu Jumla ya **Dola za Marekani milioni 8.4** sawa na **Shilingi bilioni 19.41**. Vituo hivyo vitatumiwa na Wachimbaji Wadogo kuchenjua madini na kujifunza namna bora na endelevu ya kuendesha Migodi yao kitaalam na kwa tija zaidi. Kazi iliyofanyika hadi sasa ni utafiti wa kina ambapo uchorongaji wa miamba umefanyika katika maeneo hayo ili kubaini uwepo wa mashapo ya kutosha ya madini husika. Kituo cha saba (7) kitakuwa eneo la Masakasa/Mkwenyule-Wilayani Kilwa ambacho ni Kituo cha uongezaji thamani madini ya chumvi. Tayari eneo la Kituo hiki limekaguliwa na linafaa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**148. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara imetoe mafunzo kwa Wachimbaji Wadogo 6,000 katika Kanda ya Kati, Kanda ya Kati Magharibi, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kusini, Kanda ya Kusini Magharibi, Kanda ya Mashariki, Kanda ya Ziwa Nyasa, Kanda ya Ziwa Viktoria Magharibi na Kanda ya Ziwa Viktoria Mashariki. Mafunzo hayo yalihu masuala ya

uchimbaji madini, uchenjuaji, afya na usalama Migodini, ujasiriamali na utunzaji wa mazingira na yalitekelezwa na Maafisa Madini wa Kanda na Mikoa. Zoezi hilo liliifanyika ikiwa ni sehemu ya kazi za kawaida za kupitia Bajeti za Ofisi za Kanda za Matumizi ya Kawaida.

**149. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara itaendelea kutoa Huduma za Ugani kwa Wachimbaji Wadogo nchini. Aidha, kwa kupitia STAMICO na GST, Wizara imepanga kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa Wachimbaji Wadogo 4,000 katika Kanda za Kusini, Ziwa Nyasa, Kati na Kusini Magharibi. Pia, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Mfano na kuendelea kufanya utafiti wa kina kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo. Shughuli hizo zimetengewa Jumla ya **Dola za Marekani milioni 5.6** sawa na takriban **Shilingi bilioni 12.94** na zitaghamariwa na Mradi wa SMMRP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia

*Uboreshaji wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini*

**150. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuboresha huduma za utoaji na usimamizi wa Leseni za madini kwa kuwezesha malipo ya ada za Leseni za madini kufanyika kwa njia ya Mtandao (*online payments*). Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Jumla ya maombi ya Leseni 8,942 ya utafutaji na uchimbaji wa madini yalipokelewa na Wizara kwa njia ya Mtandao (*Online Mining Cadastre Transactional Portal*). Kati ya hayo, maombi 585 ni ya utafutaji mkubwa, maombi 17 ni ya uchimbaji wa kati na maombi 8,340 ni ya uchimbaji mdogo. Baada ya uchambuzi wa maombi hayo, **Jumla ya Leseni 3,467** zilitolewa. Kati ya hizo, Leseni 296 ni za utafutaji mkubwa, 10 za uchimbaji wa kati na 3,161 za uchimbaji mdogo. Wizara itaendelea kusimamia kwa karibu utoaji wa Leseni ili kukuza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa.

**151. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa Leseni zinazotolewa zinafanyiwa kazi, Wizara iliendelea kufuatilia Wamiliki wa Leseni na waliobainika kutotekeleza masharti

husika ya Leseni hizo walifutiwa Leseni zao. Katika kutekeleza azma hiyo, **Jumla ya Leseni 2,153 zilifutwa**, kati ya hizo, Leseni 72 zilikuwa ni za utafutaji madini na 2,081 ni za uchimbaji mdogo wa madini. Aidha, hati za makosa (*default notices*) 243 zilitolewa kwa Wamiliki wa Leseni za utafutaji madini, 13 kwa Wamiliki wa Leseni za uchimbaji wa kati na 2,186 kwa Wamiliki wa Leseni za uchimbaji mdogo. **Naendelea kutoa wito kwa Wadau wa Sekta ya Madini kujisajili kwa njia ya Mtandao ili kurahisisha huduma za utoaji Leseni na kuongeza uwazi hivyo kupunguza malalamiko ya kuwepo kwa upendeleo katika utoaji wa Leseni za madini.**

**152. Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kuboresha Mfumo wa utoaji wa Leseni na kutoa mafunzo kwa Watendaji; kuhamasisha Wadau wa madini ambao hawajasajiliwa ili waweze kutumia Mfumo huu; kufanya ukaguzi wa Leseni; na kufuta Leseni ambazo hazifanyiwi kazi.

#### *Kuimarisha Usimamizi wa Migodi Nchini*

**153. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Jumla ya Migodi 1,115 ilikaguliwa ili kuhakikisha kuwa Kanuni za Usalama, Afya na Utunzaji wa Mazingira Migodini zinazingatiwa. Kati ya Migodi hiyo, Migodi Mikubwa minne (4), Migodi ya Kati 52 na Migodi Midogo 1,059 ilikaguliwa. Ukaguzi huo umesaidia kuimarisha hali ya Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira kwa Wachimbaji wa Migodi husika.

**154. Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudni za Wizara katika ukaguzi wa Migodi, ajali zinaendelea kutokea hususan, kwenye Migodi ya Wachimbaji Wadogo kutokeana na kutofuata Sheria na Kanuni za uchimbaji madini. Maeneo ambako ajali zimetokea kwa wingi ni maeneo yenye mifumuko ya madini (*mineral rush areas*) ambayo yanavamiwa na kuchimbwa bila leseni hususan kwenye maeneo ya hifadhi za misitu ambako Wizara ya Nishati na Madini haina uwezo wa kutoa leseni bila ridhaa ya Mamlaka husika. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Jumla

ya ajali 17 zilitokea katika Migodi hiyo na kusababisha vifo vya Wachimbaji 30. Aidha, katika ajali hizo, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta ya Madini walifanikiwa kuokoa Wachimbaji 42 wakiwa hai. **Wizara inatoa shukrani za dhati kwa Viongozi wa Serikali, Kampuni za Madini, Taasisi mbalimbali, Wachimbaji Wadogo na Wadau wote walioshiriki kwa namna moja ama nyngine kuokoa maisha ya wahanga wa ajali Migodini.**

**155. *Mheshimiwa Spika*,** kutokana na kuongezeka kwa ajali katika Migodi ya Wachimbaji Wadogo, Wizara katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 itaimarisha ukaguzi wa Migodi hiyo nchi nzima na kuwa na taarifa za kila Mwezi za Migodi yote inayofanya kazi. **Migodi yote ambayo itabainika kutokidhi vigezo vya kiusalama kwa mujibu ya Kanuni za Afya na Usalama Migodini za Mwaka 2010 itafungwa mara moja hadi marekebisho stahiki ya kiusalama yatakapofanyika na kuridhiwa na Mkaguzi wa Migodi.** Aidha, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Migodi kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi ili waweze kukagua Migodi kwa umakini zaidi na kupunguza matukio ya ajali.

**156. *Mheshimiwa Spika*,** katika kusimamia utunzaji wa mazingira Migodini, Kampuni ya ACACIA inayomiliki Migodi ya Buzwagi, Bulyanhulu na North Mara imeweka Hati Fungani (*Rehabilitation Bond*) ya kiasi cha **Dola za Marekani milioni 41.10** sawa na takriban **Shilingi bilioni 94.98** kwa ajili ya kurekebisha mazingira. Mkataba wa Makubaliano hayo umepitishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kusainiwa na pande zote mbili tarehe 14 Desemba, 2016. Aidha, Hati Fungani kwa ajili ya Kampuni ya Williamson Diamonds Limited inayomiliki Mgodi wa Almasi wa Mwadui inapitiwa na Wataalam wa Wizara na itawasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya ushauri wake kabla ya kusainiwa. Pia, Kampuni za Geita Gold Mining Limited, Shanta Mining Co. Limited (New Luika Gold Mine), STAMIGOLD Mine na Dangote Industries Tanzania Ltd zimewasilisha Mipango yao ya ufungaji Migodi yao kulingana na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kamati ya Kitaifa ya

Ufungaji wa Migodi imeshaanza kupitia Mipango hiyo. Wamiliki wa Mgodi wa TanzaniteOne wameelekezwa kutayarisha Mpango wa Ufungaji Mgodi huo na kuwasilisha Wizarani mapema iwezekanavyo. Migodi ya Kati na Mikubwa yote nchini inafuata utaratibu huo kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Pia, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa Wachimbaji Wadogo kuhusu kuandaa Mpango wa Utunzaji Mazingira (EPP) kwa kuzingatia Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

**157. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itakamilisha Mkataba baina yake na Kampuni ya Williamson Diamonds Limited kwa ajili ya kuweka Hati Fungani na kupitia na kukamilisha Mipango ya Ufungaji Migodi (*Mines Closure Plans*) kwa Migodi iliyobaki. Pia, Wizara kupitia *National Mine Closure Committee* itapitia na kukamilisha Mpango wa Ufungaji wa Hati Fungani kwa Migodi ya TanzaniteOne, Dangote, Geita Gold Mine, New Luika Gold Mine na STAMIGOLD.

#### *Usimamizi wa Masuala ya Baruti Nchini*

**158. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Jumla ya tani 31,092 za Baruti na Vipande 3,878,607 vya Fataki viliiingizwa nchini kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo uchimbaji wa madini, utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia na ujenzi wa miundombinu. Aidha, Wizara ilitoa vibali 135 vya kuingiza Baruti nchini, vibali 280 vya kulipulia Baruti na Leseni 31 za maghala ya kuhifadhia Baruti. Maghala hayo yana uwezo wa kuhifadhi Jumla ya tani 553 za Baruti (*fractured explosives*) na Vipande milioni 5.5 vya Viwashio (*detonators*).

**159. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa masuala ya Baruti nchini ikiwa ni pamoja na kutoa elimu na mafunzo ya matumizi bora na salama ya Baruti kwa Wachimbaji Wadogo wa madini na Wadau wengine kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali; kukagua maghala ya kuhifadhia Baruti; kusimamia matumizi sahihi ya

Baruti kulingana na Sheria zilizopo sambamba na kuwasilisha Bungeni Muswada Mpya wa Sheria ya Baruti ya Mwaka 2017 kwa kuwa Sheria iliyopo ina mapungufu ya udhibiti wa matumizi mabaya ya Baruti.

***Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini***

**160. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi 2017, Wizara ilitoa Jumla ya Leseni 40 za uchenjuaji wa marudio ya madini ya dhahabu. Aidha, ongezeko la leseni hizo limewezesha Serikali kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za uchenjuaji dhahabu ambapo Jumla ya Mrabaha wa **Shilingi bilioni 4.23** umekusanywa. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Kituo cha Jimolojia Tanzania (*Tanzania Gemological Centre – TGC*) kilichopo Arusha kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi (Mlezi 6) ya usanifu wa madini ya Vito (*lapidary*) ambapo wanafunzi 18 walidahiliwa Mwezi Machi, 2016 na kumaliza Septemba, 2016. Pia, wanafunzi wengine 18 walidahiliwa kuanzia Mwezi Oktoba, 2016 na wanatarajiwa kumaliza masomo yao mwishoni mwa Mwezi Mei, 2017 na hivyo kufanya Jumla ya Wahitimu wa Kituo hicho kufikia 65 tangu kuanzishwa kwa mafunzo hayo Mwezi Novemba, 2014. Mafunzo hayo yanaendelea kudhaminiwa na Mfuko wa Kuwaendeleza na Kuwajengea Uwezo Wanawake (*Arusha Gem Fair Women Foundation Fund*) ulioanzishwa kupitia Maonesho ya Vito ya Arusha.

**161. *Mheshimiwa Spika***, Wizara ilianzisha taratibu za usajili wa Kituo hicho kwenye Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundii (NACTE) katika Mwaka 2015/16. Hata hivyo, usajili wa Kituo hiki haujakamilika hadi sasa baada ya NACTE kusitisha kwa muda usajili wa vyuo nchini kwa lengo la kufanya uhakiki wa ubora wa vyuo vilivyopo. Mara NACTE watakapoanza tena zoezi la kusajili vyuo, Wizara itahakikisha kuwa usajili wa TGC unakamilishwa haraka. Usajili ukikamilika, Kituo kinakusudia kutoa mafunzo ya Diploma ya *Gem & Jewellery Technology* ambapo mhitimu katika Mwaka wa Kwanza atapata Cheti cha *Basic Technician Certificate in Gem & Jewellery Technology (NTA Level 4)*, Mwaka wa Pili *Technician*

*Certificate in Gem & Jewellery Technology (NTA Level 5) na Mwaka wa Tatu Ordinary Diploma in Gem & Jewellery Technology (NTA Level 6). Pia, Kituo kinatarajia kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa kozi mbalimbali za uongezaji thamani madini.*

**162. *Mheshimiwa Spika*,** katika juhudzi za kukijengea uwezo Kituo cha TGC, Wizara inawatumia Wakufunzi Waelekezi kutoka nje ya nchi na wakati huo huo inajenga uwezo wa Wakufunzi wa Kitanzania. Wizara imepeleka Watumishi watatu (3) katika nchi za Sri Lanka, India na Thailand kusomea fani za usonara (*Jewelly design & making*), ukataji na uchongajji (*lapidary*) na jimolojia (*gemology*). Wataalam hao wamehitimu mafunzo hayo na wameanza kazi kwenye Kituo cha TGC.

**163. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara imepanga kupeleka Watumishi wengine saba (7) kusomea fani mbalimbali za uongezaji thamani madini kupitia Mradi wa SMMRP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Jumla ya **Shilingi milioni 694.76** zinakadiriwa kutumika kwa ajili ya kugharamia mafunzo hayo. Aidha, ili kukiongezea ufanisi, Kituo kimepewa *sub-vote* itakayoanza kutumika Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

#### *Uchambuzi na Uthaminishaji wa Madini ya Vito*

**164. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara kupitia TANSOR T imeendelea kusimamia uthamini wa madini ya Almasi na Vito ambapo kiasi cha karati **174,700** za Almasi zenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 47.95** sawa na **Shilingi bilioni 110.81** zilithaminishwa na kusafirishwa nje ya nchi. Vilevile, Wizara ilifanya uthamini wa madini ya Vito ambapo ilithaminisha **tani 604.39** za madini ya mapambo (*Ornamental stones*), **gramu milioni 3.30** za vito ghafi na karati **177,339** za madini ya vito yaliyosanifiwa kwa thamani ya **Dola za Marekani milioni 23.46** sawa na **Shilingi bilioni 54.22**. Kutokana na shughuli hizo, Serikali imekusanya Mrabaha wa **Dola za Marekani milioni 3.31** sawa na **Shilingi bilioni 7.65**.

**165. *Mheshimiwa Spika*,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara itaendelea kusimamia kwa umakini zaidi shughuli ya uthaminishaji wa madini ya Almasina Vito vingine ili kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki. Aidha, Wizara itaanizisha na kusimamia masoko (magulio) ya ndani ya madini ya Vito kwa kushirikiana na Ofisi za Madini za Kanda na itatoa huduma za kijimolojia kwa Wachimbaji Wadogo na wa Kati.

**166. *Mheshimiwa Spika*,** uanzishwaji wa masoko (magulio) ya ndani ya madini ya Vito unalenga kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo kwa kuwapatia soko la uhakika na bei za ushindani karibu na maeneo ya Morogoro (Mkuyuni), Merelani, Tanga na Tunduru na kupata madini yenye ubora unaohitajika katika Maonesho ya Kimataifa ya Vito ya Arusha (*Arusha Gem Fair - AGF*) ambayo hufanyika mara moja au zaidi kwa mwaka.

#### *Miradi Mikubwa ya Madini*

**167. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara inaendelea kuhamasisha na kuwezesha Kampuni za madini katika uendelezaji wa Miradi Mikubwa ya madini. Miradi hiyo ni pamoja na Miradi ya *graphite* (kinywe) iliyopo Nachu, Namangale na Chilalo Wilayani Ruangwa; Chidya na Chiwata Wilayani Masasi na Epanko, Mahenge Wilayani Ulanga. Madini ya *graphite* yanatumika kwenye kutengeneza vilainishi (*lubricants*), betri na vifaa vya kwenye injini za magari. Uwekezaji katika Miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali za kukamilisha tathmini ya athari za mazingira na ulipaji wa fidia. Hata hivyo, Mradi wa Epanko umekumbwa na tatizo la baadhi ya Wananchi kukataa kupisha maeneo yao kwa ajili ya kuanzhishwa kwa Mradi huo. Wizara kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Morogoro inaendelea kutoa elimu kwa Wananchi juu ya umuhimu wa Mradi huo.

**168. *Mheshimiwa Spika*,** Miradi mingine ambayo ipo katika hatua ya uendelezaji ni pamoja na Mradi wa Urani ambaeo upo eneo la Mto Mkusu katika Wilaya ya Namtumbo. Mradi huo unaendelezwa na Kampuni ya Mantra Tanzania

Limited. Hata hivyo kutokana na kushuka kwa bei ya madini ya urani katika Soko la Dunia, Mradi huo umechelewa kuanza kwa kuwa uchimbaji ukifanyika sasa Serikali na Mwekezaji hawataweza kupata manufaa stahiki.

**169. *Mheshimiwa Spika***, Miradi ya *Rare Earth Elements (REE)* na *niobium* iliyopo katika Wilaya ya Songwe ipo katika hatua za juu za utafiti na uanzishwaji wa Mgodi, sawia. Kukamilika na kuanzishwa kwa uchimbaji wa madini katika Miradi hii kutasaidia nchi kupata Mapato kutoka kwenye madini mengine zaidi ya dhahabu ambayo Migodi yake mingi inaendelea kufungwa kutokana na kuisha kwa mashapo katika maeneo husika.

#### *Utatuzi wa Migogoro*

**170. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Wizara imeendelea na juhudzi za kutatua migogoro mbalimbali katika Sekta ya Madini. Katika kipindi hicho Wizara kupitia Kamati Maalum ya Wataalam wa Serikali imefanya uhakiki kwa Wananchi wa Kitongoji cha Nyamichele Kijiji cha Nyakunguru wanaozunguka eneo la Mgodi wa Dhahabu wa North Mara ambao walifiekewa mazao yao wakati wa zoezi la kufanya tathmini ya mali na ardhi Mwaka 2013. Jumla ya Wananchi 2,742 walifanyiwa uhakiki wa maeneo yao ili kupisha shughuli za Mgodi. Lengo la uhakiki huo lilikuwa ni kubaini Wamiliki halali wa maeneo hayo ili walipwe fidia ya mazao yaliyofyekwa pamoja na gharama za usumbufu.

**171. *Mheshimiwa Spika***, kati ya Wananchi 2,742 waliohakikiwa, Wananchi 1,586 wamebainika kutokuwa na kasoro za umiliki wa maeneo yao na Kamati ilipende- keza walipwe fidia ya mazao yao yaliyofyekwa pamoja na gharama za usumbufu. Wananchi wenyе umiliki wa maeneo (*parcels*) 1,016 wamebainika kuwa na kasoro mbalimbali za umiliki wa ardhi, Kamati ilipendekeza majina ya wamiliki wa maeneo hayo yachunguzwe na TAKUKURU na Vyombo vingine vya Dola ili haki itendeke.

**172. *Mheshimiwa Spika*,** pamoja na kutoa muda wa kutosha kwa ajili ya uhakiki huo, Wananchi wanaomiliki maeneo (*parcels*) 139 hawakujitokeza kwa ajili ya kuhakikiwa, hivyo Kamati ilipendekeza kuwa Wananchi hao wasilipwe chochote na kama wataona hawakutendewa haki wanaweza kudai haki hiyo kupitia Vyombo vya Sheria. Aidha, pamoja na malipo hayo, Wananchi wataendelea kumiliki maeneo yao kwa kuwa Mgodi umeazimia kuendeleza uchimbaji kwa njia ya chini kwa chini (*Underground Mining*).

**173. *Mheshimiwa Spika*,** Pamoja na kushughulikia malalamiko ya fidia za Wananchi wa Kijiji cha Nyakunguru, Kamati pia ilitoa maelekezo kwa Mgodi wa North Mara kuwalipa fidia stahiki na kuwahamisha Wananchi wote walio ndani ya eneo hai laMgodi (Mita 200) ili kupisha shughuli za Mgodi. Maeneo hayo ni yale yaliyomo katika Vijiji vya Matongo, Nyangoto, Nyabichune, Mjini Kat, Nyakunguru, Komarera na Kijiji cha Kewanja.

**174. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imefanikiwa kutatua mgogoro wa Wananchi wa eneo la Magambazi Wilayani Handeni waliokuwa wamevamia eneo la Leseni ya uchimbaji la Kampuni ya Canaco. Wananchi hao wameondolewa katika eneo hilo na Kampuni hiyo imekubali kutoa sehemu ya eneo ndani ya Leseni kwa ajili ya kuendesha shughuli za uchimbaji kwa Wananchi hao. Aidha, Wananchi wameelekezwa kuunda vikundi na kuvisajili kabla ya kupewa Leseni za uchimbaji. Hadi sasa vikundi saba (7) vimeundwa na kusajiliwa, kikundi kimoja kimeshapewa Leseni na kimeanza shughuli za uchimbaji na vikundi vingine sita (6) viko katika utaratibu wa kupatiwa Leseni za uchimbaji mdogo. Kampuni ya Canaco imeahidi kuvipatia baadhi ya vifaa vya uchimbaji vikundi vitakavyopatiwa Leseni katika maeneo hayo.

***Ushiriki wa Watanzania Katika Shughuli za Madini (Local Content)***

**175. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara inaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa Wananchi wanaozunguka

Migodi kuhusu fursa za kiuchumi zilizopo katika Migodi inayowazunguka. Kwa hali ilivyo sasa, ushiriki wa Watanzania katika kutoa huduma na kuza bidhaa kwenye Migodi umefikia takriban **asilimia 50**. Vilevile, Wizara inaendelea kuhamasisha Migodi kutoa zabuni kwa Wananchi wanaozunguka Migodi na Kampuni za Wakandarasi wa Kitanzania ili kutoa fursa kwa Watanzania kuza huduma na bidhaa kwenye Migodi hiyo.

**176. *Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kuhamasisha Wamiliki wa Viwanda kutumia malighafi za madini yanayopatikana hapa nchini ili kukuza Viwanda nya Ndani. Katika kutekeleza hilo, Wizara imeweka zuio kwa Viwanda nya Saruji kuingiza malighafi (Makaa ya Mawe na Madini ya Jasi) kutoka Nje ya Nchi. Ili kuhakikisha Wamiliki wa Viwanda nya Saruji wanapata malighafi zinazotakiwa na kwa muda muafaka, Serikali imewaelekeza kuingia Mikataba na Wachimbaji wa madini ya Jasi na Makaa ya Mawe.

**177. *Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza uwazi na ushiriki wa Watanzania katika Migodi Mikubwa, Serikali kupitia Gazeti la Serikali Na. 286 la tarehe 07 Oktoba, 2016, imetunga Kanuni za Usajili wa Hisa kwa Kampuni za Madini (*The Mining (Minimum Shareholding and Public Offering) Regulations, 2016*). Kanuni hizi zinazitaka Kampuni zenyenye Leseni kubwa za Uchimbaji wa Madini (*Special Mining Licence*) kuandikisha **asilimia 30** ya Hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (*Dar es Salaam Stock Exchange – DSE*). Kanuni zinazitaka Kampuni zilizopata leseni kabla ya kutangazwa kwa Kanuni kusajili **asilimia 30** ya Hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ndani ya kipindi cha miaka miwili tangu kutangazwa kwa Kanuni hizi. Aidha, Kampuni ambazo zitapata leseni baada ya kutangazwa kwa Kanuni hizi zinatakiwa kutekeleza masharti ya Kanuni hizi ndani ya mwaka mmoja kutoka tarehe ya kupewa Leseni.

**178. *Mheshimiwa Spika***, kupitia Gazeti la Serikali Na. 44 la tarehe 24 Februari, 2017 (*The Mining (Minimum Shareholding and Public Offering) (Amendment) Regulations*,

2016), Serikali imefanya Marekebisho ya Kanuni hizi kwa kuzitaka Kampuni ambazo zinamiliki Leseni za Uchimbaji Mkubwa zilizotolewa kabla ya kutangazwa kwa Kanuni hizi kutekeleza masharti ya Kanuni hizi ndani ya kipindi cha miezi sita (6) tangu tarehe ya kutangazwa kwa mabadiliko ya Kanuni hizo. Pia, Kampuni ambazo zitapata leseni baada ya kutangazwa kwa Kanuni hizi sasa zinatakiwa kusajili **asilimia 30** ya Hisa katika Soko la Hisa mara baada ya kuanza shughuli za uchimbaji.

**179. Mheshimiwa Spika**, kwa sasa kuna Jumla ya Kampuni 12 zinazomiliki Leseni 14 za uchimbaji mkubwa zinazohitajika kusajiliwa kwenye Soko la Hisa. Kampuni hizo ni Bulyanhulu Gold Mine Limited, Pangea Minerals Limited, Geita Gold Mining Limited, North Mara Gold Mine Limited (2), STAMIGOLD Company Limited, Williamson Diamonds Limited, Mantra Tanzania Limited, El-Hilal Minerals Limited, Kiwira Coal Mines Limited, Tanzania China International Mineral Resources Limited (2), Uranex Tanzania Limited na Dangote Industries Limited. Wizara imeagiza Kampuni hizo zisajili kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (*DSE*).

**180. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara itaendelea kuchukua hatua za makusudi kuelimisha umma kuhusu manufaa na fursa zilizopo katika Sekta ya Madini na kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali kujenga uwezo wa Watanzania kushiriki katika Sekta hiyo. Natoa wito kwa Wananchi kujandaa ili Kampuni za madini zikisajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, Watanzania wajitokeze kwa wingi kununua Hisa na hivyo kushiriki kwenye umiliki wa rasilimali zao za madini.

#### *Kuvutia Uwekezaji Katika Sekta ya Madini*

**181. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara imeendelea kuhamasisha na kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini kupitia Balozi za nchi mbalimbali zilizopo ndani ya nchi na Balozi zetu zilizopo nje ya nchi zikiwemo Afrika Kusini na Canada. Aidha, Wizara

imefanikiwa kushiriki kwenye Mkutano Mkubwa wa kuvutia wawekezaji Afrika unaojulikana kama *Mining Indaba* – Afrika ya Kusini ambapo Serikali imetoa taarifa mbalimbali kuhusu mazingira ya uwekezaji katika Sekta ya Madini. Pia, Wizara imeshiriki katika Mikutano ya *Kimberly Process Certificate System* (KPCS) katika Nchi ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na *International Conference on Great Lakes Region* (ICGLR) katika Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

**182. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara imefanikiwa kufanya Minada Miwili ya Madini ya Tanzanite Mkoani Arusha ambapo Mnada wa Kwanza ulifanyika Mwezi Agosti, 2016 na Mnada wa Pili ulifanyika Mwezi Machi, 2017. Katika Mnada wa Kwanza madini yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 3.45** yaliuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya Mrabaha wa thamani ya **Dola za Marekani 150,491** sawa na **Shilingi milioni 347.78**. Katika Mnada wa Pili madini yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 4.20** yaliuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya Mrabaha wa kiasi cha **Dola za Marekani 210,114.36** sawa na **Shilingi milioni 485.57**. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ilikusanya Ushuru wa Huduma kiasi cha **Shilingi milioni 27.99**.

**183. *Mheshimiwa Spika*,** lengo kuu la Minada hii ni kuwakutanisha moja kwa moja Wazalishaji wa Madini ya Tanzanite, Wafanyabiashara na wenyewe Viwanda vyta kuongeza thamani madini ili kuwezesha Wafanyabiashara kuza madini yao kwa bei ya ushindani na Serikali kukusanya Mapato stahiki. Aidha, Minada hii husaidia kupunguza utoroshaji wa madini nje ya nchi na kuitangaza Tanzania katika medani ya Kimataifa kuhusu fursa za madini yanayopatikana nchini. Pia, Wizara ilifanya Maonesho ya Kimataifa ya Vito na Usonara, Arusha kuanzia tarehe 03 hadi 05 Mei, 2017.

**184. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kushiriki katika Maonesho na Makongamano ya Kitaifa na Kimataifa ili

kutangaza fursa za uwekezaji katika Sekta ya Madini hapa nchini. Pia, kuandaa Maonesho ya Kimataifa na Minada ya Madini ya Vito itakayohusisha Wanunuzi wa Ndani na Nje.

Katika Minada ya madini ya Tanzanite Serikali itahakikisha Wauzaji wanajumuisha Tanzanite iliyokatwa ili kukuza Viwanda vya ndani vya kukata Madini ya Vito. **Natoa wito kwa Wadau wa madini ya Vito waendelee kushirikiana na Wizara ili kufanikisha Maonesho na Minada hiyo kwa lengo la kukuza Masoko ya Ndani na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini.**

***Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) wa Benki ya Dunia***

**185. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (*Sustainable Management of Mineral Resource Project – SMMRP*) Awamu ya II unaofadhiliwa na Benki ya Dunia umeanza ujenzi wa Kituo cha mafunzo kwa Wachimbaji Wadogo cha Rwamgasa - Geita. Kituo hiki kinajengwa kwa ushirikiano baina ya Wizara, Mgodi wa Geita na Ushirika wa Wachimbaji Wadogo wa Rwamgasa. Ujenzi wa Kituo hicho utagharimu kiasi cha **Dola za Marekani 500,000** sawa na **Shilingi bilioni 1.16** ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Julai, 2017.

**186. Mheshimiwa Spika,** shughuli nytingine za Mradi huu zilizofanyika ni pamoja na kukamilika kwa taratibu za ununuzi za kuwapata Washauri Waelekezi (*Consultants*) kwaajiliyakusanifunakusimamiaukarabatiwa Ofisi za Madini za Bariadi; Bukoba; Chunya; Kigoma; Mpanda; Musoma; Songea; Ofisi za STAMICO; na Chuo cha Madini Dodoma. Kwa sasa Mradi unaendelea na utaratibu wa kuwapata Wakandarasi ili ukarabati huo uanze. Aidha, Mradi umekamilisha ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kutoa Huduma za Ugani kwa Wachimbaji Wadogo kuititia STAMICO, GST na Ofisi za Madini za Kanda. Shughuli hizo zimegharimu takriban **Dola za Marekani milioni 5.68** sawa na **Shilingi bilioni 13.13** na zimefadhliliwa na Benki ya Dunia.

**187. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mradi wa SMMRP imewezesha GST na STAMICO kufanya utafiti wa kijiolojia katika maeneo yanayokusudiwa kuanzishwa Vituo Bora veya Mfano na maeneo mengine ya uchimbaji mdogo. Fedha zilizotumika kwa ajili ya kazi hii ni **Dola za Marekani milioni 3.7** sawa na **Shilingi bilioni 8.55** ambazo zimetolewa na Benki ya Dunia. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kupitia Mradi wa SMMRP, Wizara inatarajia kuanza ukarabati na upanuzi wa Ofisi za Madini za Bariadi; Bukoba; Chunya; Kigoma; Mpanda; Musoma; Songea; Ofisi za STAMICO; na Chuo cha Madini Dodoma. Lengo la ukarabati ni kuboresha mazingira ya kazi ya Ofisi hizo ikiwa ni pamoja na kuongeza vyumba vyaya mikutano na madarasa vitakavyotumika kufundishia Wachimbaji Wadogo (*Centres of Excellence*). Vilevile, Wizara itaanza ujenzi wa Vituo veya Mafunzo (*Demonstrating Centres*) vitatu (3) katika Awamu ya Kwanza kwenye maeneo ya Itumbi (Chunya), Katente (Bukombe) na Mkwanyule (Kilwa).

**Wakala wa Jiolojia Tanzania (Geological Survey of Tanzania - GST)**

**188. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Serikali kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) iliendelea kukusanya taarifa za Jiosayansi na kuchora Ramani kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. GST kwa kushirikiana na *Geological Survey of China* wamefanya na kukamilisha utafiti wa Jiomeria katika Mikoa ya Mbeya na Songwe ambao ulifadhiliwa na Serikali ya China.

Pia, GST kwa kushirikiana na *Geological Survey of Finland* na Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) imetengeneza Ramani za Jiomeria za nchi nzima (*Country Wide Multi-Element Geochemical Maps*) zinazoainisha wingi wa madini ya aina mbalimbali za metali (kama dhahabu, shaba, chuma, nikeli, bati n.k.) katika sehemu mbalimbali za nchi. Mradi huu umefadhiliwa na Serikali ya Finland kwa kiasi cha **Euro 750,000** sawa na takriban **Shilingi bilioni 1.59**.

**189. Mheshimiwa Spika**, Wakala unaendelea na kazi ya utafiti wa uchenjuaji ili kuongeza thamani ya madini ya Nikeli kwa Wachimbaji Wadogo wa Millima ya Mwahanza Haneti Dodoma. Wakala umekamilisha utafiti wa uchenjuaji wa madini ya Shaba katika Wilaya za Mpwapwa na Kilosa kwa lengo la kuongeza thamani ya madini ya Shaba. Pia, Wakala uliendelea kutoa Huduma za Maabara za uchunguzi na upimaji wa sampuli za Jiotekinolojia kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kwa Wateja mbalimbali wakiwemo Chuo Kikuu cha Dodoma na Mgodi wa Almasi wa Mwadui.

**190. Mheshimiwa Spika**, Wakala kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walifanya utafiti wa Tetemeko la Ardhi lililotokea Mkoani Kagera tarehe 10/9/2016 na kuandaa taarifa za utafiti. Pia, Wataalam kutoka Wakala, Chuo Kikuu cha Ardhi na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walitoa elimu kwa umma na kwa wahanga wa Tetemeko hilo. Aidha, Wakala uliendelea kukusanya takwimu kutoka Vituo nane (8) vya kudumu vilivyoko nchini vya kupimia Matetemeko ya Ardhi, kuchakata takwimu, kuchora Ramani na kuzihifadhi kwenye kanzidata (*database*) kisha kuzitolea taarifa.

**191. Mheshimiwa Spika**, Wakala kwa kushirikiana na *Geological Survey of Finland* (GTK), umechapisha Ramani za Jiolojia za *block* ya Nachingwea-Masasi/Tunduru na taarifa (*Explanatory Notes*) zake baada ya kupata matokeo kutoka Maabara za GST, SUA pamoja na GTK-Finland. Vilevile, Wakala umekusanya takwimu katika maeneo ya Wilaya za Kondoa na Singida unaolenga kupata vyanzo vya nishati ya Jotoardhi kwa ajili ya uzalishaji umeme na umefadhiliwa na USAID kwa thamani ya **Shilingi milioni 33.44**. Utafiti huu unafanyika chini ya Mradi wa “*Partnership for Enhanced Engagement in Research Project (PEERP)*”, unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani.

**192. Mheshimiwa Spika**, Wakala umeanzisha Mfumo wa kuza na kusambaza Ramani mbalimbali za Jiolojia na Jiofizikia, taarifa na takwimu kwa Wadau mbalimbali kwa

njia ya Mtando (data sales portal) na inaendelea kuimarisha na kuboresha Mfumo wa kuchakata, kutunza na kusambaza takwimu na taarifa za Jiosayansi kwa Wadau (*Geological and Mineral Information System – GMIS*).

**193. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wakala umepanga kuendeleza tafiti na kukusanya taarifa za Jiosayansi kwa ajili ya kuchora Ramani nne (4) za Jiolojia za Mfumo wa QDS kwa skeli ya 1:100,000 (QDSs 264, 275, 276 na 277) na Ramani nyingine mbili za Jioskemia za Mfumo wa QDS (QDS 264 na 275) kwenye maeneo yaliyopo katika Wilaya za Songea Vijijini, Ludewa na Madaba. Pia, Wakala umejipanga kufanya uhakiki maalum (*field checks*) wa Jiolojia, Jioskemia na kuboresha Ramani za QDS 49, 64 na 65 na kukusanya na kuhakiki taarifa za uwepo wa madini nchini na kuboresha kanzidata yake.

**194. *Mheshimiwa Spika*,** Wakala utaendelea kuratibu majanga asilia ya Kijiolojia ikiwa ni pamoja na Matetemeko ya Ardhi, Milipuko ya Volkano, Maporomoko ya Ardhi (uchunguzi wa Jiromofolojia) ili kubaini maeneo yenye hatari ya kupata Maporomoko ya Ardhi na kutoa ushauri kwa Wananchi waishio katika maeneo hayo. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa Wakala kwa kununua vifaa vya utafiti wa Kijiolojia na Maabara. Wakala wa Jiolojia ulichakata takwimu na taarifa mbalimbali za Matetemeko ya Ardhi zilizokusanywa kuanzia Mwaka 1900 kuhusu mahali yalipowahi kutokea pamoja na ukubwa wake katika Mji wa Dodoma. Hii itawezesha kuainisha maeneo yenye Mipasuko chini ya Ardhi ambayo yana uwezekano mkubwa wa kutokea Matetemeko. Ramani zinazoonesha taarifa hizi zinaweza kutumika katika upangaji bora wa Mji wa Dodoma, hivyo nachukua fursa hii kuwashauri Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na Wadau wengine kushirikiana na GST katika kupanga matumizi bora ya Ardhi.

#### *Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA)*

**195. *Mheshimiwa Spika*,** Mwaka 2009 Serikali ilianzisha Wakala maalum kwa ajili ya Ukaguzi wa Shughuli za

Uwekezaji katika Sekta ya Madini (TMAA). Kazi kubwa ikiwa ni pamoja na kukagua gharama za uwekezaji wa makampuni makubwa, mapato yatokanayo na uwekezaji huo, kodi pamoja na mrabaha unaolipwa Serikalini. TMAA hufanya kazi kwa kushirikiana na Ofisi za Madini za Kanda husika, TRA, pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani. Utendaji wa Taasisi hiyo uliendelea kuonesha mapungufu katika Sekta kwa kubaini mianya ya upotezaji wa mapato ya Serikali. Pamoja na utendaji huo, wadau mbalimbali wakiwemo Wananchi wa kawaida waliendelea kupaza sauti wakidai Taifa linaibiwa kuititia miradi ya madini.

**196. *Mheshimiwa Spika***, kufuatia maoni na ushauri wa wadau, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kulinda maslahi ya Taifa. Serikali imeandaa na kuwaongezea uwezo watendaji, imepanga watendaji wenye ujuzi katika maeneo ya migodini, mipakani, viwanja vya ndege na kwenye bandari zilizopo nchini. Kutokana na jitihada hizo, kwa Mwaka 2016/17, Wakala uliweza kukamata madini yenye jumla ya thamani ya **Dola za Marekani 119,906.45** sawa na **Shilingi milioni 277.10** katika viwanja vya ndege vya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Songwe.

**197. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Wakala ulifanya ukaguzi na kuwezesha Serikali kkusanya mrabaha wenye thamani ya **Shilingi bilioni 4.45** ikilinganishwa na jumla ya **Shilingi bilioni 6.27** zilizokusanywa kwa kipindi cha Mwaka 2015/16. Kupatikana kwa kiwango kidogo cha mrabaha, kushuka kwa mrabaha uliokusanywa kwa Mwaka 2016/17 na vilio vya wananchi kulipelekea Serikali kuchua hatua mbalimbali ili kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki na kukuza Pato la Taifa.

**198. *Mheshimiwa Spika***, kwa Mwaka wa Fedha 2017/18, Serikali itaimarisha Wakala wa Ukaguzi wa Madini (TMAA) kwa kuzingatia maoni na ushauri wa wadau mbalimbali. Ushauri uliotolewa na Kamati Maalum za Bunge pamoja na Kamati Maalum ya Wataalam iliyoundwa rasmi na Mheshimiwa Rais kuchunguza mchanga uliomo katika makontena ya makinikia ya dhahabu utazingatiwa. Lengo la jitihada hizi ni

kuhakikisha kwamba Taifa linanufaika kikamilifu kutokana na rasilimali za madini.

***Shirika la Madini la Taifa (State Mining Corporation – STAMICO)***

**199. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, STAMICO kupitia Kampuni yake Tanzu ya STAMIGOLD imezalisha Jumla ya wakia 12,092 za Dhahabu na wakia 1,659 za madini ya Fedha (*silver*) na kuingizia Kampuni **Shilingi bilioni 36.88**. Kampuni pia iilipa Serikalini Mrabaha wa **Shilingi bilioni 1.48**.

**200. Mheshimiwa Spika**, kupitia uchimbaji unaofanyika kwa ubia kati ya STAMICO na Kampuni ya TanzaniteOne Mining Limited (TML), Jumla ya kilo 2,872.79 za Tanzanite zilizalishwa na kuuzwa kwa kipindi cha Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 ambapo Jumla ya **Shilingi bilioni 16.93** zilipatikana na **Shilingi milioni 846.5** zililipwa Serikalini kama Mrabaha.

**201. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua hizo, STAMICO pia inaendelea kutekeleza Mradi wa ununuzi wa madini ya Bati kutoka kwa Wachimbaji Wadogo walioko Kyerwa Mkoani Kagera ambapo hadi kufikia Machi, 2017 tani 18.08 za madini hayo ziliuzwa na kulipatia Shirika Jumla ya **Shilingi milioni 325.49** ambazo zimevezesha ulipaji wa Mrabaha kwa Serikali wa kiasi cha **Shilingi milioni 13.02** na **Shilingi 976,471** zimelipwa kama ushuru wa Huduma kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Januari hadi Machi, 2017 Jumla ya kilo 1,205 za madini ghafi ya Bati zimenunuliwa kwa Jumla ya **Shilingi milioni 22.90**.

**202. Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mahitaji ya Makaa ya Mawe nchini, STAMICO imeanza rasmi uchimbaji wa Makaa hayo katika Kilima cha Kabulo - Kiwira kuanzia Mwezi Aprili, 2017 ambapo Jumla ya tani 107,078 zinakadiriwa kuchimbwa kwa Mwaka na Mradi huu utagharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 2.39**. Lengo la Mradi huu ni kuwauzia Makaa ya Mawe Viwanda vya Saruji na watumiaji wengine.

**203. Mheshimiwa Spika**, Shirika limefanikiwa kufanya kazi ya ukadiriaji na uthaminishaji wa mashapo ya madini yaliyopo kwenye Mradi wake wa dhahabu wa Buhemba ambapo kiasi cha wakia 441,772 za dhahabu (*indicated resources*) zimekadiriwa kuwepo katika mashapo hayo. Aidha, Mwezi Juni, 2017 kazi za ukadiriaji na uthamini wa mashapo zitafanyika katika mashimo ya Buhemba *Main* na Mwizi na kazi hizo zitakapokamilika zitawezesha ongezeko la mashapo yanayokadiriwa kufikia wakia 600,000. Mpango uliopo ni kutafuta Mwekezaji wa kuingia naye Ubia.

**204. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Shirika limeendelea kufanya tathmini za uwepo wa mashapo katika Leseni zake za madini inazozimiliki. Leseni zilizofanyiwa utafiti ni Leseni ya dhahabu iliyopo Busanda – Mkoani Geita na Madini ya *Rare Earth Elements - REE* iliyopo Sengeri Mkoani Songwe. Pia, Shirika limepata Leseni 20 za uchimbaji madini mdogo (PML) wa kokoto katika maeneo ya Chigongwe Dodoma na Ubena Zomozi Pwani ambazo zitawezesha uanzishaji wa Mradi wa kokoto katika maeneo hayo. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 jumla ya **Shilingi bilioni 2.64** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu.

**205. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, STAMICO imeendelea kutoa huduma za kitaalam kwa Wachimbaji Wadogo nchini. Jumla ya Wachimbaji Wadogo 15 wamefanyiwa utafiti wa Kijolojia katika maeneo ya Lwamgasa - Geita (Blue Reef), Bukandwe - Mbogwe, Nyampalahala – Bukombe (Paso Mine), Mpanga-Bahi, Mkalama na Mandawa-Rwanga (Mkalama Copper Gold Project), Kazikazi – Itigi, Kiteto, Wami - Pangani (Jiwe Project), Kerezia na Ng’anzo – Bukombe, Nsagali Gold Mine na Makangaga – Kilanjelanje - Kilwa (*Mishangu International*). Tafiti hizo zimewezesha Wachimbaji hao kupata taarifa za uwepo wa madini katika maeneo yao ambazo wanaweza kuzitumia kupata mikopo kutoka Taasisi za Fedha. Wachimbaji waliofaidika na taarifa hizo za utafiti na waliofanikiwa kupata mikopo kutoka Benki ya Uwekezaji

Nchini - *TIB* ni Nsagali Gold Mine na Makangaga- Kilanjelanje - Kilwa (*Mishangu International*).

**206.** *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 STAMICO kwa kushirikiana na GST chini ya Mradi wa SMMRP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia imefanya utafiti wa Kijiosayansi unaohusisha uchorongaji wa miamba na ukadiriaji wa mashapo ya madini katika maeneo yanayotarajwa kuanzisha Vituo vya Mfano vya uchenjuaji wa madini kwa Wachimbaji Wadogo katika maeneo ya Itumbi (Chunya), Katente (Bukombe) na Kapanda (Mpanda). Katika kipindi hiki Jumla ya mita 4,138 za *Reverse Circulation (RC)* na mita 5,201 za *Diamond Drilling (DD)* zilichorongwa kwenye maeneo hayo. Aidha, STAMICO itaendelea kuboresha taarifa zinazohusu Wachimbaji Wadogo pamoja na upatikanaji wa masoko ya madini nchini kupitia Tovuti ya Wachimbaji Wadogo ya STAMICO (*Small Scale Mining Portal - www.ssm-stamico.co.tz*) na Mfumo wa utoaji wa taarifa hizo kupitia simu za kiganjani.

**207.** *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Shirika litaendelea kufanya tafiti katika maeneo yake ya Busanda (Dhababu), Sengeri *Southern Extension (Rare Earth Elements)* na Mingoyo Lindi (*Graphite*) pamoja na kutoa Huduma za kibashara za ushauri wa kitaalam (*Consultancy*) katika Sekta ya Madini.

**208.** *Mheshimiwa Spika*, kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Shirika pia limepanga kuendelea kuchimba Makaa ya Mawe katika Leseni yake ya Kilima cha Kabulo – Kiwira ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 10** kimetengwa na Serikali kwa ajili ya kuendeleza Mradi huo. Aidha, Shirika linaendelea kukamilisha ukadiriaji wa mashapo ya dhababu pamoja na usanifu wa Mgodi katika Mradi wa Buhemba pamoja na kutafuta Mbia mwenye uwezo ili kuendeleza Mradi huo. Pia, Shirika litaendelea kusimamia Miradi yake ya STAMIGOLD pamoja na Miradi ya Ubia ikiwemo TanzaniteOne ili kuongeza ufanisi na Mapato ya Serikali.

**Asasi ya Uwazi Katika Rasilimali za Madini na Gesi Asilia  
(Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative – TEITI)**

**209. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai 2016 hadi Machi, 2017 TEITI imeandaa Mpango-Kazi (*Road Map*) wa kuanzisha Rejista ya Majina na taarifa za Watu Wanaomiliki Hisa katika Leseni na Mikataba ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia kama ilivyoahidiwa na Mhe. Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) alipomwakilisha Mheshimiwa Rais katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi kuhusu Kudhibiti Rushwa (*London, Anti-corruption Summit, 2016*) uliofanyika Nchini Uingereza, tarehe 12 Mei, 2016. Aidha, TEITI imefanya mapitio ya Sheria (*Legal Review Study*) kwa ajili ya maandalizi ya uanzishaji wa Rejista hiyo. Lengo ni kubaini kama kuna vipengele katika Sheria zilizopo vinyavokataza uwekaji wazi wa majina ya watu wanaomiliki hisa katika Leseni na Mikataba ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia, hasa Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2002 (*Companies Act, 2002*) kwa ajili ya kuvifanyia marekebisho.

**210. Mheshimiwa Spika**, maandalizi kwa ajili ya ukusanyaji wa Takwimu za Kodi zilizolipwa na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia katika Mwaka wa Fedha wa 2014/15 na 2015/16 yamekamilika. Maandalizi hayo yamezingatia maelekezo ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaliyotolewa Mwezi Oktoba, 2016 kwa kukusanya na kuweka wazi takwimu za misamaha ya kodi, matumizi ya mafuta na mishahara ya Wafanyakazi wa Kigeni. Ripoti zitatolewa kwa umma kuanzia Mwezi Juni, 2017.

**211. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza matakwa ya Sheria ya TEITI ya Mwaka 2015 Kifungu 16 (1)(a) kinachomtaka Waziri kuweka wazi Mikataba ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia, Mwezi Desemba, 2016 Wizara ilizitaarifu Kampuni zenye Mikataba ya Madini na Gesi Asilia (MDAs na PSAs) kwamba inakusudia kuweka wazi Mikataba hiyo. Kampuni hizo zinatakiwa kuifahamisha TEITI kwa mujibu wa Kifungu 27 (2) kama kuna sehemu ndani ya Mikataba hiyo ambayo kibashara ni muhimu kutowekwa wazi. Kati ya

Kampuni 24, Kampuni nne (4) za madini na 20 za Mafuta na Gesi Asilia, Kampuni mbili (2) zimewasilisha maombi TEITI ambayo hivi sasa yanafanyiwa kazi. Aidha, maandalizi yanafanyika ili kuweka wazi Mikataba ya Kampuni hizo kwenye Tovuti za Wizara.

**212. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 TEITI itakamilisha na kutoa kwa Umma Ripoti ya Malipo ya Kodi yanayofanywa na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwa Serikali kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Aidha, TEITI itaendelea kuelimisha Umma juu ya matumizi ya takwimu zinazotolewa katika Ripoti zake ili waweze kutumia takwimu hizo katika kuhoji uwajibikaji wa Serikali.

***Chuo cha Madini Dodoma (Mineral Resources Institute – MRI)***

**213. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Chuo kimedahili Jumla ya **wanafunzi 527** katika fani za Jiolojia na Utafutaji Madini; Uhandisi Migodi; Uhandisi Uchenjuaji Madini; Sayansi za Mafuta na Gesi Asilia; na Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini. Pia, Chuo kimeandaa Mtaala mpya wa Upimaji Ardhi na Migodi (*Curriculum for Land and Mine Surveying*) ambaoumewasilishwa NACTE kwa ajili ya usajili. Aidha, Chuo kimefanya upanuzi na ukarabati wa Ofisi na madarasa, ujenzi wa ukumbi wa mihadhara pamoja na viwanja vya michezo kupitia Mradi wa SMMRP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Pia, Wizara imetoa Jumla ya **Shilingi milioni 148.03** kwa ajili ya ufadhili kwa **vijana 71** wanaosoma fani mbalimbali za madini, Mafuta na Gesi Asilia katika Chuo hiki.

**214. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Chuo kitaendelea kupanua wigo wake wa kutoa mafunzo kwa kuanzisha programu mpya ya Upimaji Ardhi na Migodi. Pia, Chuo kimekusudia kuandaa Mtaala wa Wachimbaji Wadogo kwa ajili ya Watendaji wa kada ya kati watakaoweza kujiajiri kama Wachimbaji Wadogo wenye ujuzi au kufanya kazi moja kwa moja na Wachimbaji Wadogo

wengine kote nchini. Aidha, Chuo kitaendelea kuwajengea uwezo Watumishi wake na pia kuendelea kuimarisha miundombinu yake muhimu.

### C. AJIRA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

**215. *Mheshimiwa Spika*,** ili Watumishi wa Wizara waweze kufanya kazi kwa weledi na ufanisi zaidi ikilenga kuinua mchango wa Sekta za Nishati na Madini kwenye Pato la Taifa, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Wizara ilianaa Mpango wake wa mafunzo kwa kipindi husika. Kupitia Mpango huo, Wizara ilipanga kupeleka Watumishi 87 katika mafunzo ya muda mrefu na Watumishi 166 katika mafunzo ya muda mfupi. Mpango huo unaendelea kutekelezwa ambapo hadi kufikia mwishoni mwa Mwezi Machi, 2017, Watumishi 67 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi. Kati ya hao 2 wanasomea Shahada ya Uzamivu, 43 Shahada ya Uzamili, 16 shahada ya kwanza na 6 Stashahada. Aidha, katika kipindi hicho Wizara ilipeleka Watumishi 28 katika mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Mafunzo hayo yalitolewa katika fani mbalimbali zikiwemo: Uthaminishaji, Ukataji na Utafiti wa Vito; Uhandisi Migodi; Jiolojia; Fedha, Uhasibu na Usimamizi katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia; Usimamizi wa Mazingira; Uchumi na Sera za Umma; Sheria hususan katika Mafuta na Gesi Asilia; Petroli; na masuala ya Jiosayansi kwa ujumla. Pamoja na mafunzo haya kufanyika nchini, Watumishi walihudhuria mafunzo nje ya nchi zikiwemo: Australia, Brazil, China, India, Norway, Sri Lanka, Thailand na Uingereza. Mafunzo hayo ya muda mrefu na muda mfupi kwa ujumla yaligharimu Jumla ya **Shilingi bilioni 1.41** zikiwa ni fedha za Ndani na Nje zilizotengwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17.

**216. *Mheshimiwa Spika*,** pamoja na mafunzo hayo, Wizara pia iliendelea kushirikiana kwa karibu na Washirika wa Maendeleo ili kupata ufadhili wa masomo kwa Watanzania wanaokidhi vigezo katika nchi mbalimbali kwenye mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Watanzania 16 walipata ufadhili wa kusomeshwa nchini China Shahada ya Uzamili

na wawili (2) Shahada ya Uzamivu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia.

**217. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuendelea kuwapa Watumishi ujuzi mbalimbali kwa ajili ya kuinua utendaji wao, Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 imepanga kuwapeleka Jumla ya Watumishi 227 katika mafunzo ya fani mbalimbali zikiwemo: Usimamizi wa Rasilimali za Mafuta na Gesi Asilia; Sheria; Uchumi; Jiolojia; Jemolojia; pamoja na Fedha na Uhasibu katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia. Kati ya Watumishi hao, 77 watahudhuria mafunzo ya muda mrefu na Watumishi 150 mafunzo ya muda mfupi. Katika kipindi hiki Wizara imetenga Jumla ya **Shilingi milioni 679.73** kwa ajili ya kuwezesha mafunzo hayo.

**218. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuboresha ustawi na afya za Watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI walijitokeza, Wizara imeendelea kuwawezesha Watumishi 10 kwa kuwapa huduma ya lishe na dawa kwa kuzingatia Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa Mwaka 2006. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kutoa elimu mahali pa kazi ili kuzuia maambukizi mapya na kuwashudumia waathirika wa UKIMWI kadri watakavyojitokeza na Jumla ya **Shilingi milioni 12** zimetengwa kwa ajili hiyo. Sambamba na jitihada hizo, Wizara pia itaendelea kuhamasisha Watumishi kupima afya zao mara kwa mara ili kujua kama wana Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) kama vile magonjwa ya shinikizo la damu, kisukari na saratani ili waweze kuchukua hatua stahiki mapema. Aidha, Wizara itaendelea kuwashamasisha Watumishi juu ya umuhimu wa kufanya mazoezi ili kuimarisha afya zao kwa ajili ya kuendelea kulitumikia Taifa letu ipasavyo na kwa ufanisi zaidi.

**219. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuwapa motisha na kuongeza tija kwenye utendaji kazi kwa Watumishi wake, Wizara imeendelea kubuni njia mbalimbali ikiwemo ya kuwapandisha vyeo Watumishi wake. Katika kutekeleza dhana hii, kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara inatarajia kuwapandisha vyeo Jumla ya Watumishi 360

ambao wamepata sifa za kitaaluma na wenye utendaji mzuri wa kazi kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 1999.

#### **D. WIZARA YA NISHATI NA MADINI KUHAMIA DODOMA**

**220. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara ya Nishati na Madini inaunga mkono juhudzi za Serikali ya Awamu ya Tano ilioamua kwa dhati kutekeleza maamuzi ya Mwasisi wa Taifa letu, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya Mwaka 1973 ya kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi yetu ambapo pia maamuzi hayo yamesisitizwa kwenye Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020 katika Ibara ya 151 kuhusu kuhamishia Makao Makuu Dodoma. Katika kutekeleza Maamuzi hayo, Wizara imeanza kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa zoezi hilo ambalo linatekelezwa kwa awamu. Katika Awamu ya kwanza, tarehe 10 Februari, 2017 Wizara ilihamisha Watumishi 47. Awamu hii ilihusisha Watumishi wa ngazi mbalimbali wakiwemo Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Makamishna, Wakurugenzi na Maafisa. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kutekeleza Maamuzi hayo ambapo katika kipindi hicho Watumishi 107 wanatarajiwa kuhamishwa kuanzia Mwezi Agosti, 2017.

#### **E. UIMARISHAJI WA MAWASILIANO KATI YA WIZARA NA JAMII**

**221. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea na Mpango wake wa utoaji taarifa mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kuititia Kitengo chake cha Mawasiliano Serikalini. Katika Mpango huo, Wizara imeandaa na kuchapisha Matoleo ya Majarida 40 kuhusu habari za kila Wiki za Wizara na Taasisi zake. Majarida yamesambazwa kwa Wananchi, Balozi za Tanzania nje ya nchi, mitandao ya kijamii, makundi ya WhatsApp, Tovuti ya Wizara, vyombo vya habari na Maafisa Habari wa Taasisi mbalimbali. Kuititia Mpango huu zaidi ya wadau 7,500 wamepata taarifa hizo. Katika kipindi hiki pia, Wizara iliwhaharisha Wananchi na Wadau mbalimbali kuhusu masuala yanayoendelea katika Sekta za

Nishati na Madini kupitia vyombo mbalimbali nya habari vikiwemo radio, magazeti, tovuti na televisheni.

**222. *Mheshimiwa Spika***, Wizara pia imeendelea kutoa elimu kwa Wananchi katika maeneo mbalimbali kwa kutumia gari lake la matangazo ambalo kimsingi limekuwa chachu ya kuzitangaza shughuli muhimu zinazotekelawa na Wizara katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu yakiwemo ya uchimbaji mdogo wa madini. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendeleza juhudhi hizo kwa kutoa elimu kwa Wananchi wengi zaidi.

#### **F. USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**

**223. *Mheshimiwa Spika***, napenda kutambua michango ya Washirika wa Maendeleo ambao wamekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudhi za Serikali za kuleta maendeleo kwa kupitia misaada yao mbalimbali kwenye Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Sekta za Nishati na Madini. Kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa shukrani za dhati kwa: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini (DBSA), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Exim ya China, Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japan (JBIC), Benki ya Maendeleo ya Kiarabu (BADEA), Benki ya Unicredit Austria, *Climate Investment Fund* (CIF), *Economic Development Cooperation Fund* (EDCF), *OPEC Fund for International Development* (OFID), Mfuko wa Uendelezaji Jotoardhi (GRMF) pamoja na Taasisi na Mashirika ya: AFD (France), Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), ICEIDA (Iceland), CIDA (Canada), DfID (UK), IDA (Benki ya Dunia), JICA (Japan), KfW (Germany), GIZ (Germany), NORAD (Norway), NDF (Nchi za Nordic), Sida (Sweden), Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), *The Netherlands* (DRIVE) na USAID (United States of America); na nchi za Brazil, Denmark, Finland, Germany, Iceland, Norway na Korea ya Kusini. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini itaendeleza ushirikiano na Washirika hawa na wengine wa Maendeleo ili kuendeleza miradi mbalimbali.

## G. SHUKRANI

**224.** *Mheshimiwa Spika*, naomba nimalizie kwa kumshukuru kwa dhati Mhe. Dkt. Medard Matogolo Chananja Kalemani, Mbunge wa Chato, Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa ushirikiano anaonipatia katika kusimamia Sekta za Nishati na Madini. Nakiri wazi kuwa michango yake imekuwa msaada mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku ya Wizara na kitaifa kwa ujumla.

**225.** *Mheshimiwa Spika*, ni wazi kuwa mafanikio yote ya Wizara yanategemea ushirikiano wa Watendaji Wakuu na Wataalam mbalimbali. Hivyo, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Naibu Makatibu Wakuu Prof. James Epiphan Mdoe pamoja na Dkt. Mhandisi Juliana Leonard Pallangyo, Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na Watumishi wote wa Wizara. Watendaji hao wa Wizara wamekuwa makini katika kunipa ushauri na ufanuzi katika maeneo mbalimbali ya kiutendaji, hali ambayo imenisaidia katika kuiongoza Wizara kwa ufanisi na hatimaye kuleta mafanikio makubwa.

**226.** *Mheshimiwa Spika*, nichukue pia fursa ya kipekee kuwashukuru Wakuu wote wa Taasisi, Wenyeviti wa Bodi na Wajumbe wa Bodi za Taasisi pamoja na Watumishi mbalimbali wa Taasisi zilizo chini ya Wizara yetu kwa ushirikiano wao wanaonipatia katika kutekeleza majukumu tuliyopewa. Ni matumaini yangu kuwa ushirikiano huu utazidi kuendelezwa siku zijazo kwa lengo la kuinua mchango wa Sekta za Nishati na Madini katika Pato la Taifa.

**227.** *Mheshimiwa Spika*, kipekee napenda kumshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyojitoa kusimamia rasilimali za nchi hii kwa maslahi mapana ya wananchi na Taifa letu. Ninawashukuru wananchi wanaojitokeza kumuunga mkono Mheshiwa Rais na kumuombea kila anapochukua hatua ili kuwalettea maendeleo Watanzania. Hakika kiongozi wetu mkuu anastahili maombi.

## H. HITIMISHO

**228. Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 pamoja na kutumika katika kutekeleza shughuli mbalimbali, imelenga katika kutekeleza Miradi Mikubwa ya Nishati ili kuchochaea Sekta nyingine za kiuchumi na hivyo kukuza uchumi wa Taifa letu na maendeleo ya Watanzania kwa ujumla. Wizara pia katika kipindi hiki itaendelea kwa kasi na utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Tano ya upatikanaji wa Nishati ya uhakika ili kuwezesha kufikiwa kwa lengo la Tanzania kuwa Nchi ya Viwanda. Katika kutekeleza azma hiyo, sehemu kubwa ya Fedha za Miradi ya Maendeleo ambazo ni **Shilingi bilioni 756.76**, sawa na **asilimia 80.6** ya Fedha zote za Maendeleo zimeelekezwa katika kutekeleza Miradi ya kimkakati ya Nishati.

**229. Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Jumla ya **Shilingi 998,337,759,500** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:

(i) **Shilingi 938,632,006,000**, sawa na **asilimia 94** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 763,304,679,000**, sawana **asilimia 81** ya fedha zote za Maendeleo ni Fedha za Ndani na **Shilingi 175,327,327,000**, sawa na **asilimia 19** ni Fedha za Nje.

(ii) **Shilingi 59,705,753,500**, sawa na **asilimia 6** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwaajiliya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 28,833,681,500**, sawa na **asilimia 48.3** ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (*Other Charges – O.C.*) na **Shilingi 30,872,072,000**, sawa na **asilimia 51.7** zitatumika kulipa Mishahara ya Watumishi (*Personnel Emolument – P.E.*) wa Wizara na Taasisi zake.

**230. Mheshimiwa Spika**, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote

kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya [www. mem.go.tz](http://www.mem.go.tz). Vilevile, Hotuba hii ina vielelezo mbalimbali kwa ajili ya ufanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta za Nishati na Madini.

**231. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.**

**NAIBU SPIKA:** Tutaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. (*Makofi*)

**MHE. DOTO M. BITEKO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117 ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari mwaka 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio, mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya vikao kadhaa kwa lengo la kupokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kuchambua makadirio na mapato na matumizi kwa mwaka 2017/2018 sambamba na utekelezaji wa shughuli za Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilifanya mambo mambo yafuatayo; ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017; kupokea taarifa ya utekelezaji wa Bajeti pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017; uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inaonesha matokeo ya shughuli hizi pamoja na maoni na ushauri wa Kamati. Katika Mkoa wa Tanga Miradi ya Umeme Vijijiini (*REA*) katika Awamu ya Kwanza na Awamu ya Pili imetekelvezwa katika Wilaya nane za Mkoa huo. Miradi hiyo yenye ukubwa

wa Kv 33 imetekelvezwa na Wakandarasi wawili ambao ni *SDG International Service* na *Sengerema Engineering Group Ltd.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya vijiji 218 vya Mkoa wa Tanga vimenufaika na ukamilishaji wa miradi ya *REA* katika awamu ya pili. Ziara ya ukaguzi na utekelezaji wa miradi hiyo ilifanyika katika Kijiji cha Tongoni katika Wilaya ya Tanga Vijijini ambacho ni kijiji cha mfano mionganoni mwa vijiji vilivyopatiwa umeme wa *REA* Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi huu, Kamati yako ilibaini kuwepo na malengo ya mradi awamu ya pili hayakukamilika kwa asilimia 100. Miradi illenga kuvipatia umeme vijiji au kaya 138, hata hivyo ni kaya 90 peke yake ndizo zilizopatiwa umeme sawa na asilima 65.0.

Kwa upande mwingine Kamati ilibaini pia kuwa elimu kuhusu mradi wa umeme wa *densification* kwa wananchi haijaleleweka vizuri na pia miradi husika haijaanza rasmi katika vijiji vyote ambavyo vihavijaunganishwa na umeme katika awamu zilizotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Geita unanufaika na mradi wa umeme vijijini katika awamu ya pili ambapo zaidi ya vijiji 101 vilikuwa kwenye tathmini ya awali ya kuunganishiwa umeme. Mkandarasi anayeshughulika na uunganishaji wa umeme kwenye mkoa huu ni *Nakuroi Investment Company Limited*. Kamati ilifanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi hiyo katika vijiji vya Nyakato, Buzilayombo kama vijiji vya mfano mionganoni mwa vijiji vingi vinavyopatiwa umeme kwenye awamu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mahojiano na wananchi wa vijiji hivyo, Kamati ilibaini kuwa malengo ya mradi katika awamu ya pili ilikuwa ni kuzipatia kaya 165 umeme katika vijiji hivyo, lakini mpaka Kamati inakwenda kwenye vijiji hivyo kaya 127 ndizo zilikuwa zimeshapatiwa umeme. Hata hivyo, kati hizo kaya 130 ambazo ni sawa na asilimia 78.0 zilikuwa zimeshapata umeme. Katika kijiji cha

Buzilayambo kaya 32 sawa na asilimia 25 zilikuwa zimeshapatiwa umeme na katika kijiji cha Nyakato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kwamba changamoto kubwa katika miradi ya *REA* inayotekelizwa katika Mkoa wa Geita ni uunganishwaji mdogo wa wananchi katika huduma ya umeme na hivyo kutokufikiwa kwa malengo ya utekelezaji wa mradi huo katika maeneo hayo. Aidha, Kamati ilibaini kuwa mashine Humba iliyofungwa yenye uwezo wa Kv 200 ambayo ni kubwa ikilinganishwa na mahitaji ya eneo hilo ilifungwa kwenye kijiji hicho ilhali mahitaji ya umeme kwenye kijiji hicho siyo makubwa kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umeme wa Kinyerezi unatekelezwa na Shirika la Umeme la Tanzania (*TANESCO*) kwa lengo la kuzalisha Megawati 185 zaidi ya umeme katika mradi huu wa umeme wa gesi wa Kinyerezi *One* ambao tayari unazalisha Megawati 150; unakadiriwa kukamilika na dola za Kimarekani 188 zimeshalipwa na Serikali kwa asilimia 100 na unatarajwa kukamilika ifikapo Juni mwaka 2018. Kwa upande wa mwaka wa fedha 2016/2017 shilingi bilioni 110 zilitengwa na hadi wakati Kamati inakagua mradi huu, kiasi cha shilingi bilioni 88 sawa na asilimia 80 kilikuwa kimeshatolewa katika utekelezaji wa mradi huu. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa jitihada zake za kupeleka fedha kwenye mradi huu muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini changamoto kadhaa zilizokuwa zinakabili utekelezaji huu ikiwa ni pamoja na tozo mbalimbali zinazotozwa na *TANROADS* kutoka *TANROADS* na *VAT* zinazotokana na ukubwa na uzito wa mizigo usio wa kawaida wa mitambo inayotumika katika kutekeleza mradi huu. Tozo hizi zinachangia kuongezeka kwa gharama za miradi hivyo kuchelewesha utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto zinazoukabili mradi huu, bado dhamira ya dhati ya Serikali ya kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika nchi hii kinazidi kudhihirika, ambapo katika

mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya shilingi bilioni 90 kutoka katika vyanzo vya ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza na kukamiliisha mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati kupitia Bunge lako Tukufu linaitaka Serikali kupeleka fedha zote za miradi ya umeme zilizobaki yaani bakaa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ili kukamiliisha miradi hiyo muhimu kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania kupata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *Kinyerezi II* megawati 240, unatekelezwa vilevile na Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) kwa lengo la kuzalisha megawati 240 kwa mfumo wa kisasa zaidi unaoitwa *Combined Cycle Power Plant*. Gharama za mradi huo ni dola za Kimarekani 344 ambapo ni asilimia 85 ya gharama hizo italipwa na *Japan Export Trading Financing* na asilimia 15 pekee iliyobaki imelipwa na Serikali ya Tanzania mwezi Februari, 2016. Ujenzi wa mradi huu umeshaanza na unatekelezwa kwa kasi ambapo tayari misingi ya majengo imewekwa na baadhi ya mitambo kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, pamoja na ujenzi huo kuanza kwa kasi, bado kuna changamoto mbalimbali za tozo kama vile forodha kama vile *Custom Levies, Custom Processing Fees* pamoja na *Custom Duties* ambazo zinatakiwa kulipwa na *TANESCO*. Tozo hizi zimekuwa zikichangia ongezeko la gharama katika utekelezaji wa mradi huu na kufanya mradi huu kuto kutotelezwa kwa kasi inayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitaarifiwa kwamba maombi ya *TANESCO* kwenda kwa *TANROADS* ambayo yалиhusu kupatiwa msamaha wa kodi na tozo hizo zinazotokana na ukubwa wa uzito wa mitambo usio kuwa wa kawaida (*out of gouge heavy roads charges*) yalikataliwa. Aidha, ucheleweshaji wa malipo hayo unaweza kusababisha mitambo hiyo kuchelewa kufika eneo husika la mradi na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa mradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati vilevile ilitembelea mradi wa Bulyanhulu Geita Kv 220. Mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo kidogo cha kupoozea umeme cha Geita cha msongo wa Kilovoti 220 pamoja na usambazaji wa umeme katika vijiji 10 vilivyopo ndani ya eneo la utekelezaji ambapo gharama yote kwa ujumla ni dola za Kimarekani milioni 23 ambazo ni mkopo kutoka katika Benki ya *BADEA* na tayari gharama na fidia nyingine zote zimeshalipwa kwa wananchi wote waliopisha eneo la mradi huo kama inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kukamilika kwa ulipaji wa fidia wananchi waliopisha eneo la mradi bado mradi huu umeshindwa kuanza kutokana na kuchelewa kupatikana kwa Mhandisi Mshauri wa mradi. Mradi huu utakapoanza utasaidia kuongeza hali ya upatikanaji wa umeme wa uhakika katika Mkao wa Geita. Aidha, mradi huu utaunganisha wateja zaidi ya 1,500 ikiwemo Mgodi wa *GGM* ambao unahitaji MW zaidi ya 11 kwa ajili ya shughuli zake za mgodi na kusaidia migodi mingine ya wachimbaji wadogo wadogo iendeshwe vizuri kutokana na kupatikana kwa nishati ya umeme. Kamati inaishauri Serikali kutatua changamoto hizo haraka iwezekavyo ili mradi huo uwe wenyе tija kwa Mkao wa Geita na maeneo jirani na uweze kuwanufaisha wananchi pamoja na wawekezaji wanaohitaji umeme kwa ajili ya shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodi wa Dhahabu wa Buckleef wenyе leseni za uchimbaji mkubwa (*Special Mining Licence*) katika Mkao wa Geita unamilikiwa na mkataba wa ubia ulioingiwa mwaka 2011 kati ya Serikali ya Tanzania kupitia Shirika lake la *STAMICO*na Kampuni ya *TANZAM 2000*. Kupitia mkataba huo, *STAMICO* inamiliki asilimia 45 na *TANZAM* inamiliki asilimia 55 ya hisa.

Kwa mujibu wa mkataba huo (*Joint Venture Agreement*) *TANZAM* ina jukumu la kutafuta fedha za kuendesha mgodi huo wakati huo jukumu la *STAMICO* lilikuwa kuhamisha leseni zake 12 kwa kampuni hiyo. Hadi wakati wa ziara katika mgodi huu, Kamati ilibaini kwamba licha ya leseni zote za uchimbaji kukabidhiwa kwa mbia huyo,

hakuna kazi yoyote iliyokwisha kufanyika katika kuendeleza mgodi huo toka kampuni hiyo iingie mkataba na *STAMICO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kampuni kuripoti kuwa imekamilisha ufungaji wa mtambo mpya wa kuchenjulia dhahabu, Kamati inasikitishwa na kitendo cha mbia kutokuzingatia ushauri wa *STAMICO* kuhusu aina ya mtambo unaofaa kutumika katika eneo hilo, hatua ambayo imesababisha Serikali kupata hasara. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini inapoingia ubia katika sekta ya madini ili kuepuka wabia wa aina hii ambao hawazingatii ushauri wa mbia mwenza yaani *STAMICO*jambo linalosababisha hasara zisizo kuwa za msingi. Kamati haikuona jithada zozote za mbia huyo za kuendeleza mgodi huo kama walivyokubaliana kwenye mkabata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati imesikitishwa na usimamizi mbovu wa *STAMICO* katika mgodi huo licha ya kuwa na mashapo (*reverses*) yenye uhakika wa kuzalisha dhahabu yameishafanyiwa utafiti na kubainika. Hatua stahiki zinashauriwa kuchukuliwa ili kurekebisha kasoro hizo ambazo zimebainika kwa mbia huyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wachimbaji wa kati, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa migodi ya *Busolwa Mining* na *Nyarugusu Processing Plant*, iliyopo Mkoa wa Geita. Lengo la ziara ilikuwa ni kujifunza jinsi wachimbaji wa kati wanavyoendesha shughuli zao na kubainisha mchango walionao katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Busolwa Mining* ni mgodi unaomilikiwa na Mtanzania kwa asilimia 100 na Kamati ilijiona unavyoendesha shughuli zake kwa kutekeleza sheria na kanuni mbalimbali ikiwa ni pamoja na kulipa kodi zote stahiki za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mgodi huo uanze mwaka 2014, umeshalipa kodi ya thamani shilingi bilioni 120, mrabaha shilingi bilioni 562, kodi ya zuio kwa mwaka 2017 shilingi milioni 20 na *service levy* shilingi milioni 48.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa inayoukabili mgodi huu ni ufinyu wa eneo la kutupia mabaki yanayotokana na shughuli za mgodi (*TSF*). Hivyo ni mapendekezo ya Kamati kuwa maombi ya mgodi huo kupatiwa eneo lingine yashughulikiwe mapema ili kusaidia kuongeza uhai wa mgodi huo ambao umeajiri zaidi ya Watanzania 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madini ya vito ya Tanzanite, Kamati yako imeendelea kusikitishwa na jitihada ndogo zinazofanywa na Wizara ya Nishati na Madini kuokoa mapato yatokanayo na madini ya vito Tanzanite na Almasi nchini. Hata hivyo, hakuna mikakati madhubuti ya kuokoa rasimali hizi kutokana na usimamizi usioridhisha wa migodi hiyo. Pamoja na changamoto nyngi za mikataba baina ya *STAMICO* na *Tanzanite One* ambapo mgodi huo pekee ndio unaozalisha madini haya adimu duniani, Kampuni ya *Tanzanite One* amekuwa akitoa taarifa zisizokuwa sahihi kwa mbia mwenza yaani *STAMICO* toka alivyoanza kuzalisha Tanzanite hapa nchini. Kwa mfano, kuanzia Juni, 2013 hadi Machi, 2016, *STAMICO* ameripoti mauzo ya jumla ya dola za Kimarekani milioni 16.7 na *Tanzanite One* katika kipindi hicho hicho aliuza madini yenye thamani ya dola za Kimarekani Milioni 17.9 ambapo kuna tofauti ya dola milioni 1.3 hazikuripotiwa na kampuni hiyo na hivyo Serikali kukosa kodi yake. Hivyo, kutokana na tofauti hiyo *STAMICO* wamepoteza jumla ya dola za Kimarekani 182,855.19. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kampuni hiyo ya *Tanzanite One* imekuwa hailipi kodi ya mapato na tozo za għarama mbalimbali kwa *STAMICO* kama vile għarama ya uangalizi na usimamizi (*monitoring and evaluation unit cost*) ambapo jumla ya milioni 131.7 zinadaiwa na *STAMICO*. Pia kukosekana kwa akaunti ya pamoja katì ya wabia hawa, kunasababisha mambo mengi hasa ya kifedha kutokufahamika kwa mbia mwenzake yaani *STAMICO* kama inavyotakiwa na mkataba (*joint venture*). Kwa namna mkataba huo unavyoendeshwa kwa pande hizi mbili, umekuwa hauna manufaa kwa Serikali ya moja kwa moja, kwa kuwa kampuni hiyo imekuwa haitekelezi kwa kiasi

kikubwa matakwa ya mkataba huo pamoja na maagizo mbalimbali ya Serikali ambayo imekuwa ikipewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 3 Mei, 2017, Kamati yako ilihudhuria maonesho ya madini ya vito jijini Arusha na kujionea jinsi maonesho haya yanavyoweza kusaidia sekta hii ya madini ya vito hapa nchini. Pamoja na mafanikio ya kuanzisha mnada na maonesho hayo ya vito hapa nchini, bado changamoto ni nyngi zinazokabili sekta hii ya madini ya vito hasa madini ya Tanzanite. Changamoto kubwa ni utoroshaji wa madini haya nje ya nchi ambayo ndiyo inayoendelea kutuumiza kama Taifa kwa kuwa Tanzania ndiyo nchi pekee inayozalisha madini haya ya Tanzanite lakini Tanzania hiyo hiyo siyo muuzaji wa kwanza wa madini ya Tanzanite duniani. Hata hivyo, uanzishwaji wa maonesho haya kwa kiasi kikubwa bado haujaweza kusaidia kutatua changamoto zinazokabili sekta hii ya madini ya vito hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hasara kubwa tunayopata kama Taifa kwenye madini haya pekee nchini, Kamati inashauri Bunge lako Tukufu kwa mara nydingine tena kama tulivyokwishashauri siku za nyuma suala la mkataba baina ya *TM*L pamoja na *STAMICO* liweze kuangaliwa upya na kuangaliwa kwa namna bora zaidi litakayoweza kuleta tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madini ya dhahabu, sekta ya madini nchini inaendelea kukabiliwa na changamoto nyngi hasa katika suala la ukusanyaji wa kodi za Serikali. Sekta hii imechangia kwa asilimia nne katika Pato la Taifa mchango ambao bado ni kidogo sana ukilinganishwa na ongezeko la uzalishaji wa madini haya katika sekta hiyo. Kwa mfano, katika mwaka 2016 nchi yetu ilizalisha jumla ya wakia milioni 1.42 za madini ya dhahabu ikilinganishwa na wakia milioni 1.36 zilizozalishwa mwaka 2015. Ongezeko hilo la uzalishaji ambalo ni sawa na asilimia 4.4, lilitakiwa kwenda sambamba na ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya kodi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasikitishwa na ulipaji hafifu wa kodi za mapato unaofanywa na wawekezaji katika migodi mikubwa hapa nchini. Kwa mfano, mwaka 2016 ni migodi miwili peke yake ndio iliyolipa kodi ya mapato yaani *North Mara na Geita Gold Mine*. Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua madhubuti kufuatilia jambo hili ili migodi hii iweze kulipa kodi hizi kama inavyostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wawekezaji nchini hasa kwenye sekta ya madini wakidai Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT returns*) ambayo kiutaratibu inapaswa kulipwa baada ya migodi kukamilisha hesabu zao na kuwasilisha *TRA*, Serikali imekuwa hajjalipa hizo fedha kwa migodi hiyo kwa madai ya kuwa kuna changamoto kadhaa ambazo Serikali ilikuwa inazipitia ili kuhakiki madeni hayo. Kamati inaishauri Serikali kuhakiki haraka madeni haya na kuwalipa wawekezaji hawa ili kutokuathiri uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inamiliki mgodi mmoja tu kwa asilimia 100 ambao ni Mgodi wa *Stamigold* kuitia Shirika la *STAMICO*. Mgodi huu licha ya kuajiri Watanzania zaidi ya 700, bado kumekuwa na jitihada ndogo za Serikali katika kuusaidia mgodi huu katika masuala ya msingi ya kuuendeleza kama ifuatavyo:-

(i) Kutokuusaidia mgodi huu kupata fedha za kufanya utafiti katika leseni zinazozunguka eneo hili ili kuongeza uhai wa mgodi;

(ii) Mgodi haujasaidiwa kupata msamaha wa kodi ya mafuta na vipuli kama ilivyo kwa migodi mingine mikubwa;

(iii) Ukosefu wa *Mining Development Agreement* kwa muda mrefu unakwamisha mgodi huu kuijendesha kibiashara kama ilivyokuwa kwa migodi mingine; na

(iv) Mgodi huu unakabiliwa na deni kubwa kutoka kwa wazabuni mbalimbali wanaotoa huduma katika mgodi

huo. Kamati inaitaka na kuishauri Serikali kuingilia kati deni hili ili kuepusha shughuli za mgodi huo kusimama na kusababisha hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hairidhishwi na jitihada zilizofanywa na Wizara ya Nishati na Madini katika kuusaidia Mgodi huu wa *Stami Gold*. Changamoto hizi zikitatuliwa kikamilifu, zitaongeza uzalishaji wa mgodi huu na kuongeza uhai wa mgodi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwa sasa kutoka kwa wananchi wanaozunguka Mgodi wa *North Mara* katika maeneo ya Nyamichele katika vijiji vya Nyakunguru, Murwambe, Matongo na Nyamongo. Pamoja na tathimini ya ardhii kukamilika toka Aprili, 2013 na Kamati kutoka Wizara ya Nishati na Madini kukamilisha kazi yake ya tathimini na utatuzi wa changamoto hizi hasa za mauaji mpaka sasa wananchi bado hawajalipwa fidia zao.

Kamati inashangazwa na hatua ya malipo ya wananchi hao kucheleweshwa kwa takribani miaka minne sasa licha ya Serikali kuititia Wizara ya Nishati na Madini kuunda na kutuma Kamati za Uhakiki nne kati ya mwaka 2014 na 2017. Kamati inaishauri Serikali kuingilia kati suala hili ili wananchi hao ambao wameteseka kwa muda mrefu waweze kupata stahiki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli na kuunga mkono jitihada zake katika kuendelea kufuatilia kwa karibu sekta ya madini nchini ikiwa ni pamoja na kuunda Kamati Maalum ya Wataalamu iliyochunguza mchanga uliyoko katika makontena wa madini (makinikia) yaliyopo katika maeneo mbalimbali nchini. Kamati iliweza kubaini uwepo wa viwango vingi vya dhahabu, shaba, silva, salfa na chuma katika makinikia hayo yanayosafirishwa nje. Pia uchunguzi huo umeonesha kuwepo kwa madini ya kimkakati yaani *strategic metals* ambayo yalitajwa kwenye Kamati hiyo. Madini hayo kwa sasa

yanahitajika sana duniani na yana thamani kubwa sambamba na madini ya dhahabu ambayo taarifa zake zilikuwa hazitolewi na wawekezaji. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusubiri taarifa nyingine ya Kamati Maalum iliyoundwa na Mheshimiwa Rais itakayoendelea na uchunguzi ambao utabainisha masuala ya kiuchumi na kisheria ili sasa kama Taifa tuweze kunufaika na rasilimali za madini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekte ndogo ya gesi. Tangu kugundulika kwa gesi asilia mwaka 1974 katika eneo la Songo Songo mwaka 1982 katika eneo la Mnazi Bay pamoja na eneo la Bahari ya Kina kirefu mwaka 2010/12, uzalishaji wa gesi katika miradi iliyogundulika hapa nchini ulianza miaka ya 2004 hadi 2006. Kamati inaipongeza sana Serikali kupitia Shirika lake la *TPDC* kwa kuandaa Mpango Kabambe wa Matumizi na Usambazaji wa Gesi Asilia ya nchi mwaka 2016-2045 yaani *Natural Gas Utilization Master Plan*. Mpango huu utasidia kwa kiasi kikubwa kutoa dira ya matumizi bora ya gesi asilia kwa kuzingatia vipaumbele mbalimbali vilivyowekwa ili rasirimali hii iwafikie Watanzania walio wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo zinazofanywa na *TPDC*, bado *TPDC* inakabiliwa na madeni makubwa yaliyokwamisha shirika hili kuendelea kwa miradi yake. Madeni hayo yanababishwa na hatua ya Serikali kutenga fedha kidogo kwa miradi hiyo muhimu, hivyo kukwamisha shirika hili kutekeleza miradi hiyo. Tangu kugundulika kwa gesi hiyo hapa nchini, jumla ya viwanda 41 na taasisi mbili zimekwisha kuunganishwa katika mtandao wa matumizi ya gesi asilia.

Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuendeleza miradi hiyo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia. Miradi hiyo mikubwa inatarajia kukamilika ifikapo Juni, 2018 ambapo inatarajia kuongeza zaidi ya megawati 425 katika Gridi ya Taifa, hivyo kupunguza tatizo la umeme nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kutokana na ziara ya

ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa bajeti kwa Wizara ya Nishati na Madini haukuwa wa kuridhisha kwa kuwa fedha zilizotolewa hadi kufikia Machi, 2017 ni asilimia 36 peke yake. (*Makofii*)

(ii) Miradi mingi haikutekelezeka kama ilivyopangwa kwa kuwa fedha zilizotengwa hazikutolewa na kupelekwa kwa wakati kama ilivyotakiwa.

(i) Miradi mingi ya *REA* katika Awamu ya Pili haikukamilika kutokana na kasoro mbalimbali kama vile uainishaji wa maeneo bila kuzingatia vijiji na vitongoji ambavyo tayari vina wananchi wengi na ufungaji wa mashine humba nyingi kutokidhi mahitaji ya eneo husika. (*Makofii*)

(ii) Serikali iangalie upya namna bora ya kuwasaidia wachimbaji wa kati kwa kuwapatia maeneo ya kutosha kwa kuwa wameonesha nia ya dhati ya kuendeleza sekta ya madini.

(iii) Ruzuku iliyotolewa na Wizara ya Nishati na Madini kwa wachimbaji wadogo haikusimamiwa vizuri na hivyo kushindwa kuleta tija kwa waliokusudiwa.

(iv) Pamoja na Mipango mizuri ya *TPDC* katika kuendeleza sekta ya gesi nchini, ni lazima Serikali iwekeze fedha za kutosha katika miradi ya gesi ili kuharakisha azma ya nchi yetu kuingia katika uchumi wa viwanda.

(v) Serikali itenye fedha za kutosha na kuzipeleka kwa wakati kwenye miradi ya kimikakati kama vile Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira.

(vi) Uwekezaji katika sekta ya madini unahitaji kuangaliwa na kusimamiwa upya ili uweze kuleta faida kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa na utekelezaji wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati mwaka 2016/2017; Kamati ilifanya uchambuzi wa bajeti kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017; hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi bilioni 370.68 ikilinganishwa na shilingi bilioni 286.66 kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 239.38 sawa na asilimia 64.5 ya lengo. Makusanyo hayo yaliweza kufikia lengo kutokana usimamizi mzuri uliokuwa umewekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio ya mchango wa Idara ya Madini kwa mwaka fedha 2017/2018 yameshuka kwa asilimia 4.5 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, Makadirio ya mchango wa Idara ya Madini, yameongezeka kwa asilimia 4.5 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/2017. Ufanuzi zaidi umeoneshwa kwenye kielelezo kilichoambatishwa pamoja na hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Nishati na Madini iliidhnishiwa jumla ya shilingi triliuni 1.12 kwa ajili ya kutekeleza malengo yake. Hadi kufika tarehe 13 Machi Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 404, sawa na asilimia 36 kama nilivyoeleza hapo nyuma. Bajeti ya miradi ya maendeleo na yenewe ilikuwa imepangwiwa shilingi triliuni 1.1 sawa na asilimia 94 ya bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2017 shilingi bilioni 372 zilikuwa zimekwisha kupokelewa sawa na asilimia 35. Kwa upande wa fedha za Matumizi Mengine iliidhnishiwa shilingi bilioni 64.22 hadi kufikia Machi, 2017

Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 31.24 sawa na asilimia 47 ya fedha zilizoidhinishwa. Ni maoni ya Kamati kwamba fedha hizi ziweze kupelekwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa bajeti wa mwaka 2016/2017, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekozo kwa Wizara kwa kuzingatia matakwa ya Kikanuni. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa vizuri na Wizara ya Nishati na Madini na kufanyiwa kazi. Bado kuna tatizo la usimamizi usioridhisha katika miradi ya Umeme Vijiji katika maeneo mengi hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara ambazo zimefanywa na Kamati kuna maeneo mengi ambayo usimamizi haukuwa wa kuridhisha. Mfano, ufungaji wa mashine humba zillzokuwa chini ya kiwango katika maeneo mengi umesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya umeme iliyokwisha kutayarishwa katika maeneo mbalimbali. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya mkakati ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya kuendeleza miradi hiyo. Kamati inaiomba Serikali ione sasa umuhimu wa kuipatia miradi hiyo hasa Mradi wa Jotoardhi fedha za kutosha ili uweze kutekelezwa kwa sababu una *potential* kubwa ya kupatia umeme nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba hotuba yote iingie kwenye *Hansard*, sasa nitasoma maoni ya Kamati.

Baada ya Kamati kutekeleza majukumu ya Kikanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Wizara, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na makadirio ya matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kwa kuwa utekelezaji wa Miradi ya Umeme Vijiji katika awamu mbili zilizotangulia umekuwa na changamoto nyingi hasa katika Mikoa ya Tanga na Geita ambako Kamati

ilitembelea na kukagua; Kamati inashauri kuwa changamoto zilizobainika ikiwa ni pamoja na baadhi ya maeneo yaliyorukwa zipatiwe ufumbuzi haraka kabla ya kuendelea na Awamu ya Tatu ya REA. (*Makofj*)

(ii) Kamati inaishauri Serikali ikamilishe taratibu na changamoto zilizojitokeza katika kuchelewesha *VAT returns* kwa wawekezaji ili kutokuathiri uwekezaji nchini.

(iii) Pamoja na juhudhi mbalimbali zilizofanywa na Wizara katika usimamizi wa madini ya Tanzanite, Kamati inashauri Serikali iangalie upya mikataba hiyo ilioingiwa na STAMICO na wabia mwenzake kama ina tija kwa Taifa.

(iv) Ruzuku kwa wachimbaji wadogo iliyotolewa na Serikali kwa awamu zote mbili kwa kiasi kikubwa imeshindwa kutimiza malengo na kukosa usimamizi mzuri. Aldha, ni vema Serikali kuititia Wizara ya Nishati na Madini ikaangalia namna bora ya kusimamia fedha hizi ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo wachimbaji wadogo wadogo ili kufuatilia kwa karibu wachimbaji hao.

(v) Sekta ya uchimbaji wa kati imeendelea kukua kwa kiasi hapa nchini kwa kiwango cha kuridhisha. Hivyo ni vyema Serikali ikaangalia upya jinsi ya kuisaidia kupata baadhi ya misamaha ya kodi kama vile mafuta na vipuli ili kuwanufaisha wachimbaji hawa wa nchini.

(vi) Leseni zote ambazo zinakiuka Sheria ya Madini ikiwa ni pamoja na kushindwa kuendelezwa kwa muda mrefu zifutwe na kupewa wachimbaji wadogo wadogo na wa kati kwa kuwa wameonesha nia ya dhati ya kuendeleza sekta hiyo. (*Makofj*)

(vii) Pamoja na Serikali kuandaa Mpango Kambambe wa Matumizi ya Gesi Asilia nchini, ni vyema ukafanyika utafiti na upembuzi yakinifu kuhusu miradi yote mikubwa ya usambazaji wa gesi katika maeneo mbalimbali ili kuweza kujua kama ina manufaa ya kiuchumi kwa Taifa letu. Hatua

hii itasaidia kuepusha nchi yetu kuingia kwenye mikopo ambayo ni mzigo kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Spika pamoja na wewe binafsi, Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge letu. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu wenu mkubwa tuliowakabidhi.

Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu kwa Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati na Madini pamoja na watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Kaimu Katibu Mkuu, Profesa James Mdoe na Dkt. Juliana Pallangyo kwa ushirikiano wao wanaoendelea kutupatia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, naomba nimshukuru sana mtoa hoja Mheshimiwa Mwijage aliyesoma hotuba kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kwa kweli amesoma vizuri sana na ameeleza vizuri sana mambo yote yaliyokuwa kwenye hotuba ile.

Kwa namna ya pekee naomba vilevile niwashukuru sana wWajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa michango yao muhimu katika shughuli zote za Kamati katika kipindi hiki cha uchambuzi wa bajeti. Ni dhahiri kuwa bila weledi na ushirikiano walionipa Kamati hii isingweza kufikia hatua hii ya mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndugu Mwanahamisi Mkunda na Ndugu Felister Mgonja pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Kokuwaisa Gondo kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana wananchi wa Bukombe ambao wamenituma kuja kwenye Bunge hili kuwawakilisha na naomba niwatie moyo kwamba kazi walijonituma tunaifanya kwa nguvu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio na Mapato na Matumizi ya Fungu 58 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo ni shilingi 998,337,759,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini.

## **TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAONI YA KAMATIKUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

### **1.0      UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2017 /2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya vikao kadhaa kwa lengo la kupokea na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi, kwa Mwaka

wa Fedha 2017/2018. Sambamba na utekelezaji wa shughuli hiyo, Kamati pia ilifanya mambo yafuatayo:-

i) Ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

ii) Kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inaonesha matokeo ya shughuli hizo pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati.

## **2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelizwa chini ya Wizara ya Nishati na Madini, katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Geita. Lengo la ziara hizo lilikuwa ni kujionea utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishiwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na changamoto zillizo jito keza katika utekelezaji wake.

Aidha, Kamati ilikagua Miradi iliyotengewa fedha na ambayo haikutengewa fedha katika Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2016/2017 na miradi ambayo inatekelezwa katika Sekta ya Madini. Miradi iliyokaguliwa ni hii ifuatayo:-

i) Miradi ya Umeme Vijijini, Wilaya ya Tanga Vijijini;

ii) Miradi ya Umeme Vijijini, Wilaya ya Geita Vijijini;

iii) Mradi wa Umeme wa Gesi Kinyerezi I Extension (MW 185);

- iv) Mradi wa Umeme wa Gesi Kinyerezi II (MW 240);
- v) Ukarabati wa Kituo cha Kufua Umeme, Hale;
- vi) Mradi wa Umeme Bulyanhulu-Geita KV 220;
- vii) Mgodi wa Dhahabu wa Backleef;
- viii) Migodi ya Wachimbaji Wadogo waliopata Ruzuku ya Serikali; na
- ix) Migodi ya Wachimbaji wa Katil.

## **2.1 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

### **2.1.1 Miradi ya Sekta ya Nishati iliyokaguliwa na Kamati**

#### **2.1.1.1 Miradi ya REA katika Mkao wa Tanga**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkao wa Tanga miradi ya umeme vijiji (REA) katika awamu ya kwanza na awamu ya pili, imetekelezwa katika wilaya nane (8) za mkoa huo. Miradi hiyo yenye ukubwa wa **KV 33** imetekelezwa na wakandarasi wawili ambao ni *STEG International Services Ltd* na Sengerema *Engineering Group Ltd*. Jumla ya vijiji **218** vya mkoa wa Tanga vimenufaika na ukamilishwaji wa miradi ya REA katika awamu ya pili.

**Mheshimiwa Spika**, ziara ya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi hiyo ilifanyika katika Kijiji cha Tongoni, katika Wilaya ya Tanga Vijiji, ambacho ni kama kijiji cha mfano miongoni mwa vijiji vilivyopata umeme wa REA Awamu ya Pili.

Katika mradi huu Kamati yako ilibaini kuwa malengo ya mradi katika awamu ya pili, hayakukamilika kwa asilimia mia moja. Mradi ulilenga kuzipatia umeme kaya **138**, hata hivyo, ni kaya 90 tu kati ya hizo ndizo zimepata umeme, ambazo ni sawa na asilimia **65%** tu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, changamoto kubwa iliyobainika katika miradi ya REA katika Mkoa wa Tanga, ni pamoja na uunganishwaji mdogo wa Wananchi katika huduma hii ya nishati, Mashine Humba (Transformer) kuharibika mara kwa mara na kushindwa kukidhi mahitaji ya eneo husika.

Pia Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya vitongoji na vijiji havijaunganishwa na huduma ya umeme katika awamu mbili zilizokwisha kamilika. Kwa maoni ya Wananchi ambao Kamati ilipata fursa ya kuzungumza nao wallieleza Kamati kuwa, tafiti (survey) zilizofanyika mwaka 2015 katika maeneo ya mradi hazikuwa za kimkakati (*not strategic*) kwa kuwa mchoro wa mradi husika ulisababisha nguzo za umeme kuwekwa katika maeneo ambayo wananchi walio wengi hawanufaiki.

Kwa upande mwingine, Kamati ilibaini kuwa, elimu kuhusu mradi wa **densification** kwa wananchi haikueleweka vizuri na pia mradi husika haujaanza rasmi katika vijiji vyote ambavyo havikuunganishwa katika awamu zilizokwishakamilika.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, kufuatia ziara ya Kamati katika Kijiji cha Tongoni, mashine Humba iliyokuwa na tatizo imebadilishwa, na Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuchukua hatua mapema.

#### **2.1.1.2 Miradi ya REA katika Mkoa wa Geita**

**Mheshimiwa Spika**, Mkoa Geita umenufaika na Mradi wa Umeme Vijijini katika awamu ya pili, ambapo zaidi ya vijiji 101 vilivyokuwa kwenye tathmini ya awali vimeunganishwa. Mkandarasi aliyeshughulika na uunganishaji wa umeme katika Mkoa huu ni M/s Nakuroi Investment Co Ltd. Kamati ilifanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi hiyo katika vijiji vyta Nyakato na Buzilayombo, kama vijiji vyta mfano mionganoni mwa vijiji vilivyopata umeme wa REA awamu ya pili.

Katika mahojiano na wananchi wa vijiji hivyo, Kamati ilibaini kuwa malengo ya mradi katika awamu ya pili ilikuwa ni kuzipatia umeme kaya 165 katika kijiji cha Buzilayombo na kaya 127 katika kijiji cha Nyakato. Hata hivyo, kati ya hizo, ni kaya 130 sawa na **asilimia 78%** zilikuwa zimepata umeme katika kijiji cha Buzilayombo na kaya 32 sawa na **asilimia 25%** tu katika kijiji cha Nyakato.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kwamba, changamoto kubwa katika miradi ya REA inayotekelizwa katika Mkoa wa Geita ni uunganishwaji mdogo wa Wananchi katika huduma ya umeme na hivyo kutokufikiwa kwa malengo ya utekelezaji wa mradi huu katika maeneo hayo.

**Aidha**, Kamati ilibaini kuwa Mashine Humbaa iliyofungwa ina uwezo wa KV 200, ambao ni mkubwa ikillinganishwa na mahitaji ya eneo husika ambalo halina watumiaji wengi. Yapo maeneo mengine ambayo Kamati ilibaini kuwa yanahitaji Mashine Humbaa zenye uwezo mkubwa lakini zimefungiwa Mashine Humbaa zenye uwezo mdogo na hivyo kusababisha uharibikaji wa mara kwa mara.

#### **2.1.1.3 Mradi wa Umeme wa Gesi Kinyerezi I Extension (MW 185) na Mradi wa Umeme wa Gesi wa Kinyerezi II (MW 240)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa lengo la kuzalisha MW 185 zaidi za umeme katika Mradi wa Umeme wa Gesi Kinyerezi I ambao tayari unazalisha MW 150. Mradi unakadiriwa kugharimu dola za kimarekani milioni 188 ambazo zimelipwa na Serikali kwa asilimia mia moja (100%) na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2018.

Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, shilingi bilioni 110 zilitengwa na hadi wakati Kamati inakagua mradi huu, kiasi cha **shilingi bilioni 88** sawa na **asilimia 80%** kilikuwa kimeishatolewa katika utekelezaji wa mradi huo. Kamati inapongeza jithada za Serikali kwa kupeleka fedha mapema katika mradi huo muhimu.

Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini changamoto kadhaa zinazokabili utekelezaji wa mradi huu, ikiwa ni pamoja na tozo mbalimbali (*surcharges*) kutoka TANROADS na VAT zinazotokana na ukubwa na uzito usio wa kawaida wa mitambo inayotumika katika mradi huu (out of gauge heavy loads charges). Tozo hizo zinachangia kuongezeka kwa gharama za mradi na hivyo kuchelewesha utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika, Pamoja na changamoto zinazoukabili mradi huu, bado dhamira ya dhati ya Serikali ya kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini kinazidi kudhihirika ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya shilingi bilioni 90 kutoka vyanzo vya ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza na kukamilisha mradi huu.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati kupitia Bunge lako inaitaka Serikali kupeleka fedha zote za miradi ya umeme zilizobaki (Bakaa) kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 ili kukamilisha miradi hiyo muhimu kwa wakati kama ilivyokusudiwa.**

**Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kinyerezi II MW 240 unatekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa lengo la kuzalisha Megawati 240 kwa mfumo wa kisasa zaidi unaoitwa *Combined Cycle Power Plant*. Gharama ya mradi huu ni dola za kimarekani milioni 344 ambapo asilimia themanini na tano (85%) ya gharama hizo italipwa na **Japan Export Trading Financing** na asilimia kumi na tano (15%) iliyobaki tayari imelipwa na Serikali ya Tanzania mwezi Februari, 2016.**

Ujenzi wa Mradi huu umeishaanza na unatekelezwa kwa kasi, ambapo tayari misingi ya majengo imewekwa na baadhi ya mitambo kufungwa. Hata hivyo, pamoja na ujenzi huo kuanza kwa kasi, bado kuna changamoto mbalimbali za tozo kama vile forodha (*customs levies*), railway levies, custom processing fees pamoja na *custom duties*, ambazo zinatakiwa kulipwa na TANESCO. Tozo hizo zimekuwa

zikichangia ongezeko la gharama katika utekelezaji wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, maombi ya TANESCO kwa TANROADS, ambayo yalihusu kupatiwa msamaha wa kodi na tozo hizo zitokanazo na ukubwa na uzito wa mitambo usio wa kawaida (out of gauge heavy loads charges) yalikataliwa. Aidha, ucheleweshaji wa malipo hayo unaweza ukasababisha mitambo kuchelewa kufika eneo husika la mradi na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa mradi.

#### **2.1.1.4 Mradi wa Ukarabati wa Kituo cha Kufua Umememe Hale**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi katika Kituo cha Hale ambacho kilizinduliwa mwaka 1964. Kituo hiki ni moja ya vituo vitatu vinavyotumia nguvu ya maji kuzalisha umeme nchini, na kina mitambo miwili (2) yenye uwezo wa kuzalisha MW 10.5 kila mmoja. Mwaka 1986 mtambo mmoja ulipata hitilafu kwenye msuko wa Mashine Humba (*stator winding*)ha ulifanyiwa marekebisho makubwa, hata hivyo, mtambo huo uliharibika tena mwaka 2004.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeamua kufanya ukarabati mkubwa wa mitambo yote miwili kwa ufadhili wa Serikali ya Sweden, ambayo ilikubali kutoa Kroner Milioni 200 kupitia Shirika lake la misaada la SIDA. Asilimia 60 ya fedha hizo ni ufadhili na asilimia 40 ni Mkopo wa kibiashara. Makubaliano ya ufadhili wa mradi huu yalifanyika tarehe 11 Julai, 2013 baada ya upembizi yakinifu kukamilika, hata hivyo ukarabati wa mitambo hiyo bado haujaanza kwa kuwa bado hajapatikana mkandarasi atakaye tekeleza mradi huo.

Kamati inaona kwamba, kuchelewa kuanza kwa ukarabati wa Mitambo hiyo kunaendelea kupunguza zaidi Megawati 10 kwenye Gridi ya Taifa, hivyo Kamati inaishauri Wizara iharakishe taratibu hizo ili ukarabati uanzesha mapema kama ilivyokusudiwa.

### **2.1.1.5 Mradi wa Bulyanhulu- Geita KV 220**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea mradi huu ambao unahusisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita (msongo wa 220/33kv) pamoja na usambazaji wa umeme katika vijiji kumi (10) vilivyopo ndani ya eneo la utekelezaji wa mradi. Gharama za Mradi ni dola za kimarekani milioni 23 ambazo ni mkopo kutoka benki ya BADEA, na tayari gharama na fidia nyingine zote zimekwisha kukamilika na wananchi wote waliopisha eneo la mradi wameshalipwa fidia wanazostahili.

Pamoja na kukamilika kwa ulipaji fidia Wananchi waliopisha eneo la mradi, bado Mradi huu umeshindwa kuanza kwa wakati kutokana na kucheleva kupatikana kwa Mhandisi Mshauri wa Mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu utakapoanza utasaidia kuongeza hali ya upatikanaji wa umeme wa uhakika katika Mkoa wa Geita. Aidha, Mradi huu utaunganisha wateja zaidi ya 1500 ukiwemo Mgodi wa Geita Gold Mine (GGM) ambao unahitaji zaidi ya MW 11 kwa ajili ya shughuli za Mgodi, na kusaidia Migodi mingine ya Wachimbaji wadogo ambayo haiendeshwi vizuri kutokana na kukosekana kwa umeme wa uhakika.

Kamati inaishauri Serikali kutatua changamoto hizo haraka iwezekavyo ili Mradi huo wenyewe tija kwa Mkao wa Geita, uweze kuwanufaisha wananchi pamoja na wawekezaji wanaohitaji umeme mkubwa kwa ajili ya kuendesha shughuli zao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa kukamilisha mradi muhimu wa Rusumo Hydropower unaoziunganisha nchi tatu za Tanzania, Rwanda na Uganda, mradi huu umeongeza MW 26 kwenye Gridi ya Taifa. Mradi huu utasaidia upatikanaji wa umeme kwa mikoa ya Kagera na Kigoma na hivyo kupunguza matumizi ya umeme wa mafuta ambao ni ghali ukilinganisha na umeme wa maji.

## **2.1.2 Miradi ya Sekta ya Madini iliyokaguliwa na Kamati**

### **2.1.2.1 Mgodi wa Dhahabu wa Buckleef**

**Mheshimiwa Spika**, Mgodi wa Dhahabu wa Buckleef wenyewe leseni ya Uchimbaji Mkubwa(Special Mining License) SML Na. 04/92 uko katika Mkoa wa Geita na unamilikiwa kwa mkataba wa ubia ulioingiwa mwaka 2011 kati ya Serikali kupitia STAMICO na Kampuni ya TANZAM 2000.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia mkataba huo, STAMICO inamiliki **asilimia 45** na TANZAM 2000 inamiliki **asilimia 55** ya hisa. Kwa mujibu wa mkataba (Joint Venture Agreement) huo TANZAM 2000 ina jukumu la kutafuta fedha za kuendesha Mgodi (Operator) wakati jukumu la STAMICO lilikuwa kuhamishia Leseni zake 12 kwa Kampuni hiyo.

Hadi wakati wa ziara katika mgodi huu, Kamati ilibaini kwamba, licha ya Leseni zote za uchimbaji na utafiti kukabidhiwa kwa Kampuni hiyo, hakuna kazi ye yeyote iliyokwishafanyika katika kuendeleza Mgodi huo tangu Kampuni hiyo iingie Mkataba na STAMICO.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kampuni kuripoti kuwa imekamilisha ufungaji wa Mtambo mpya wa kuchenjulia dhahabu, Kamati inasikitishwa na kitendo cha mbia huyo kutozingatia ushauri wa STAMICO kuhusu aina ya Mtambo unaofaa kutumika katika eneo hilo, hatua ambayo inaisababishia Serikali hasara. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini inapoingia ubia katika Sekta ya madini ili kuepuka wabia wa aina hii ambao hawazingatii ushauri wa Mbia mwenza, (STAMICO) jambo linalosababisha hasara zisizo za msingi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuona jitihada zozote za Mbia huyo za kuendeleza Mgodi kama walivyokubaliana kwenye M kabata. Aidha, Kamati imesikitishwa na usimamizi mbovu wa STAMICO katika Mgodi huo licha ya kuwa na Mashapo (Reverse) yenyе uhakika wa kuzalisha Dhahabu na

kuliingizia Taifa mapato. Aidha, hatua stahiki zichukuliwe ili kurekebisha kasoro ambazo zimebainika katika ubia huo.

#### **2.1.2.2 Migodi ya Wachimbaji Wadogo waliopata Ruzuku ya Serikali-Geita (Blueleef Mining na Mgesu Mining)**

**Mheshimiwa Spika**, katika awamu zote mbili za malipo, jumla ya Shilingi Bilioni **8,071,000,000/=** zimetolewa na Serikali kwa kuratibiwa na Wizara ya Nishati na Madini, na jumla ya Wachimbaji Wadogo 115 wamenufaika kwa kupata ruzuku hizo katika mikoa mbalimbali. Katika awamu ya kwanza ya malipo, kiwango cha juu kwa kila mnufaika kilikuwa ni **Dola za Kimarekani 50,000** na awamu ya pili kiwango cha juu cha mnufaika kilikuwa ni **Dola za Marekani 100,000**. Kwa maoni ya Kamati, viwango hivyo vyta fedha ni vikubwa ikilinganishwa na usimamizi mdogo unaotolewa na Wizara ya Nishati na Madini.

Katika Mkao wa Geita jumla ya Wachimbaji Wadogo Wadogo Saba (7) wamenufaika na ruzuku ya Serikali, vikiwemo Vikundi vyta Wajasiriamali wanaoshughulika katika maeneo ya wachimbaji wadogo. Katika ziara ya ukaguzi wa Migodi ya wachimbaji wadogo waliopata ruzuku, Kamati iliridhishwa na utendaji wa wachimbaji wadogo watatu (3) tu katika Saba (7) waliopata ruzuku ambao wameendeleza shughuli zao za uchimbaji katika maeneo yao.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo kwa baadhi ya wanufaika, Kamati ilibaini changamoto kubwa ya usimamizi wa fedha usioridhisha kwa Wachimbaji Wadogo. Aidha, Wanufaika hao wa ruzuku kwa namna moja ama nyingine hawakutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa na Serikali.

Kwa kuwa, awamu zote mbili za utoaji wa ruzuku kwa Wachimbaji Wadogo kumekuwa na kasoro mbalimbali kwenye matumizi na usimamizi wa ruzuku hizo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini (evaluation) ya fedha hizo kabla haijaanza awamu nyingine ili kuhakiki na kutatua changamoto nyingi ambazo zipo kwa sasa.

### **2.1.2.3 Migodi ya Wachimbaji wa Kati**

#### **(Busolwa Mining na Nyarugusu Processing Plant)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa Migodi ya Busolwa Mining na Nyarugusu Processing Plant, iliyopo Mkoa wa Geita. Lengo la ziara lilikuwa ni kujifunza jinsi Wachimbaji wa Kati wanavyoendesha shughuli zao na kubaini mchango wao katika mapato ya Serikali.

Busolwa Mining ni Mgodi unaomilikiwa na Mtanzania, yaani mzawa kwa aslimia mia moja, na Kamati ilijionea jinsi unavyoendesha shughuli zake kwa kutekeleza Sheria na Kanuni mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kulipa kodi zote za Serikali. Tangu Mgodi huo uanze kazi mwaka 2014, umeshalipa kodi za thamani ya **shilingi bilioni 120, Mrabaha shilingi Bilioni 562**, kodi ya zuio kwa mwaka 2017 **shilingi Milioni 20 na Service Levy shilingi Milioni 48**.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa inayoukabili Mgodi huu ni ufinyu wa eneo hasa la kutupia mabaki yatokanayo na shughuli za Mgodi yaani (TSF). Hivyo ni mapendekezo ya Kamati kuwa, maombi ya Mgodi huo kupatiwa eneo lingine yashughulikiwe mapema ili kusaidia kuungeza uhai wa Mgodi huo ambao umeajiri zaidi ya Watanzania 300.

### **3.0 SEKTA YA MADINI**

#### **3.1 Madini ya Vito ya Tanzanite**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yako imeendelea kusikitishwa na jitihada ndogo zinazofanywa na Wizara ya Nishati na Madini za kuokoa mapato yatokanayo na Madini ya Vito yaani Tanzanite na Almasi nchini. Hata hivyo hakuna mikakati madhubuti ya kuokoa Rasimali hizi kutokana na usimamizi usioridhisha wa Migodi hiyo, pamoja na changamoto nyingi za Mikataba baina ya Stamico na Tanzanite One Mining Limited (TML), ambao ndiyo Mgodi pekee unaozalisha Madini haya Duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Tanzanite One Mining Limited (TML) amekuwa akitoa Taarifa za uongo kwa mbia mwenza yaani STAMICO toka alivyoanza uzalishaji wa Tanzanite hapa nchini, kwa mfano kuanzia Juni, 2013 hadi Machi, 2016 STAMICO ameripoti mauzo ya jumla ya **Dola za kimarekani Milioni 16,671,167** na TML katika kipindi hicho hicho aliuza Tanzanite yenyeye thamani ya **Dola za kimarekani Milioni 17,930,653** ambapo tofauti ya **Dola Milioni 1,259,483** hazikuripotiwa na Kampuni hiyo na hivyo hazikuripiwa kodi ya Serikali. Hivyo, kutokana na tofauti hiyo Stamico wamepoteza jumla ya **Dola za kimarekani 182,855.19**.

**Mheshimiwa Spika**, pia kampuni hii ya Tanzanite One Mining Limited (TML) imekuwa hailipu kodi ya Mapato na tozo/gharama mbalimbali kwa Stamico kama vile Gharama ya Uangalizi na usimamizi (*Monitoring and Evaluation Unit Cost*) ambapo jumla ya **shilingi milioni 131,695,626** zinadalwa na STAMICO, pia kukosekana kwa akaunti ya pamoja kati ya wabia hawa kuna sababisha mambo mengi hasa ya kifedha kutokufahamika kwa STAMICO kama inavyotakiwa na Mkataba (*Joint Venture*) huo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna Mkataba huo unavyoendeshwa kwa pande hizi mbili (*Joint Venture*) umekuwa hauna manufaa kwa upande wa Serikali, kwa kuwa Kampuni hiyo imekuwa haitekelezi kwa kiasi kikubwa matakwa ya Mkataba huo pamoja na maagizo mbalimbali ya Serikali inayokuwa ikipewa hasa wakati Kampuni hiyo ilipofukuza Wafanyakazi zaidi ya 201 bila kufuata Sheria na utaratibu za nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 3 Mei, 2017, Kamati yako ilihudhuria maonesho ya madini ya Vito jijini Arusha, na kujiona jinsi maonesho haya yanavyoweza kuisaidia sekta hii ya Madini ya Vito hapa nchini. Pamoja na mafanikio ya kuanzisha Mnada na Maonesho hayo ya Vito hapa nchini, bado kuna changamoto nyingi zinazoikabili Sekta hii ya Madini ya Vito hasa kwa madini ya Tanzanite.

Changamoto kubwa ni utoroshawaji wa madini hayo nje ya nchi. Changamoto hiyo ndiyo inayoendelea kuliumiza Taifa letu kwa kuwa ndiyo nchi pekee Duniani yenye neema hiyo, nakuifanya Tanzania kuwa siyo nchi ya kwanza kwa uuzaaji wa Madini hayo ya Vito duniani. Hata hivyo, uanzishwaji wa maonesho hayo kwa kiasi kikubwa bado haujaweza kusaidia kutatua changamoto zinazokabili sekta hii ya Madini ya vito hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hasara kubwa tunayopata kama Taifa kwenye Madini haya pekee nchini, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kwa mara nyingine tena lifuatilie kwa kina changamoto za Mkataba huo baina ya TML na STAMICO ili Bunge tuweze kuishauri Serikali namna bora ya kukabiliana na Mikataba isiyokuwa na maslahi kwa Taifa.

### **Madini ya Dhahabu**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Madini nchini imeendelea kukabiliwa na changamoto nyingi hasa katika suala la ukusanyaji wa Kodi za Serikali. Sekta hii imekuwa ikichangia asilimia 4% tu katika pato la Taifa, mchango ambao ni kidogo sana ikilinganishwa na ongezeko la uzalishaji katika Sekta hiyo.

Kwa mfano; katika mwaka 2016 nchi yetu ilizalisha jumla ya **Wakia milioni 1.42** za Madini ya Dhahabu ikilinganishwa na **Wakia milioni 1.36** zilizozalishwa katika mwaka 2015. Ongezeko hilo la uzalishaji ambalo ni sawa na **asilimia 4.4%**, lilitakiwa kwenda sambamba na ongezeko la ukusanyaji wa Kodi za Mapato nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasikitishwa na ulipaji hafifu wa kodi za Mapato unaofanywa na Wawekezaji katika Migodi mikubwa hapa nchini. Kwa mfano; Mwaka 2016 ni Migodi miwili tu nchini ndiyo iliyolipa Kodi ya Mapato ambayo ni **North Mara Gold Mine na Geita Gold Mine**. Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua madhubuti juu ya Wawekezaji ambao hawalipi kodi ili kuhakikisha Kodi zote muhimu zinalipwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa Wawekezaji nchini hasa kwenye sekta ya Madini, wakiidai Serikali Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT returns*) ambayo kiutaratibu inapaswa kulipwa baada ya Migodi kukamilisha hesabu zao na kuwasilisha TRA. Serikali hajjalipa fedha hizo kwa Migodi hiyo kwa madai ya kuwepo changamoto kadhaa ambazo Serikali ilikuwa inazifuatilia ili kujiridhisha kabla ya kuzilipa. Kamati inaishauri Serikali kutatua changamoto hizo ili Migodi hiyo iweze kulipwa fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inamiliki mgodi mmoja tu kwa asilimia mia ambao ni Mgodi wa Stamigold kupitia Shirika la STAMICO. Mgodi huu licha ya kuajiri Watananzania zaidi ya mia saba (700), bado kumekuwa na jitihada ndogo za Serikali katika kuusaidia Mgodi huo katika masuala ya msingi ya kuuendeleza kama vile;

1. Serikali kutousaidia Mgodi kupata fedha za kufanya utafiti katika leseni zinazozunguka eneo hili ili kuongeza uhai wa mgodi;

2. Mgodi haujasaidiwa kupata msamaha wa kodi ya mafuta na vipuli vya uendeshaji kama ilivyo kwa migodi mingine ya wawekezaji nchini;

3. Ukosefu wa Mining Development Agreement (MDA) kwa muda mrefu unaukwamisha Mgodi kujidesha kibashara kama ilivyo kwa Migodi mingine nchini;

4. Mgodi huu unakabiliwa na deni kubwa kutoka kwa Wazabuni mbalimbali wanaotoa huduma katika Mgodi huo. Kamati inaitaka Serikali kuingilia kati deni hilo ili kuepusha shughuli za Mgodi huo kusimama na kusababisha hasara kubwa.

Kamati hairidhishwi na jitihada zilizofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini katika kuusaidia Mgodi huo wa Stamigold. Changamoto hizo zikitatuliwa kikamilifu,

uzalishaji wa Madini ya Dhahabu unaweza kuongezeka katika Mgodi huo.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu sasa kutoka kwa Wananchi wanaozunguka Mgodi wa North Mara hasa maeneo ya **Nyamichele** katika vijiji vya **Nyakunguru, Murwambe, Matongo** na **Nyamongo**. Pamoja na tathimini ya ardhi kukamilika toka mwezi Aprili, 2013 na Kamati kutoka Wizara ya Nishati na Madini, kukamilisha kazi yake ya tathmini na utatuzi wa changamoto hasa zile za mauaji katika eneo hilo, mpaka sasa Wananchi hao bado hawajalipwa fidia zao.

Kamati inashangazwa na hatua ya malipo ya Wananchi hao kucheleweshwa kwa takribani miaka minne sasa, licha ya Serikali kuititia Wizara ya Nishati na Madini, kuunda na kutuma Kamati za Uhakiki nne (4) katil ya mwaka 2014 hadi 2017.

Kamati inaishauri Serikali kuingilia kati suala hili, ili Wananchi hao ambao wameteseka kwa muda mrefu sasa waweze kupata stahiki zao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Magufuli na kuunga mkono jitihada zake katika kuendelea kufuatilia kwa karibu zaidi Sekta hii ya Madini nchini, ikiwa ni pamoja na kuunda Kamati maalum ya Wataalamu iliyochunguza mchanga uliyo katika makontena ya mchanga wa madini (Makinikia)yaliyopo katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kamati hii iliweza kubaini uwepo wa viwango vingi vya madini ya dhahabu, shaba, silva, salfa, na chuma katika makinikia hayo yanayosafirishwa nje ya nchi.

Pia uchunguzi huo umeonesha kuwepo kwa madini ya kimkakati yaani (*Strategic metals*) ambayo nilridium, Rhodium, Ytterium, Beryllium, Tantalum na Lithium, madini haya kwa sasa yanahitajika sana Duniani na yana thamani kubwa sambamba na madini ya dhahabu ambayo Taarifa zake zilikuwa hazitolewi na wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, Kamati inaendelea kusubiri taarifa nyingine ya Kamati Maalum ya Waatalamu iliyoundwa na Mhe. Rais, inayoendelea na uchunguzi ambao utabainisha masuala ya Kiuchumi na Kisheria ili sasa kama Taifa tuweze kunufaika na Rasilimali zetu za Madini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa Kamati inakupongeza wewe binafsi kwa kuamua kufuatilia jambo hili kwa ukaribu, na kutoa uamuzi kuwa utaunda Kamati maalumu ya kufuatilia masuala ya Madini, ili Bunge lako tukufu nalo litekeleze kikamilifu jukumu lake la kikatiba la kuisimamia na kuishauri Serikali.

#### 4.0 SEKTA NDOGO YA GESI.

**Mheshimiwa Spika**, tangu kugundulika kwa Gesi Asili nchini mwaka 1974 katika eneo la Songo Songo, mwaka 1982 katika eneo la Mnazi Bay pamoja na eneo la Bahari ya Kina kirefu mwaka 2010/12, uzalishaji wa gesi katika miradi yote iliyogundulika hapa nchini ulianza miaka ya 2004 hadi 2006.

Kamati inaipongeza Serikali kupitia Shirika la TPDC kwa kuanda Mpango Kabambe wa Matumizi na Usambazaji wa Gesi Asilia nchini wa mwaka 2016-2045 (**Natural Gas Utilisation Master Plan**). Mpango huu utasaidia kwa kiasi kikubwa kutoa Dira ya Matumizi bora ya Gesi Asilia kwa kuzingatia vipaumbele mbalimbali viliviyowekwa ili Rasirimali hii iwafikie na kuwanufaisha Wananchi wengi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na **TPDC**, bado kuna changamoto kubwa ya Madeni yanayolikwamisha Shirika hili katika uendelezaji wa miradi yake. Madeni hayo yanasaababishwa na hatua ya Serikali kutenga fedha kidogo kwenye miradi hiyo muhimu na hivyo kukwamisha Shirika kutekeleza miradi hiyo kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, tangu kugundulika kwa Gesi hiyo hapa nchini, jumla ya Viwanda 41 na Taasisi 2 vimekwisha unganishwa katika mtandao wa matumizi ya Gesi Asilia.

Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendeleza miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi Asilia. Miradi hiyo mikubwa inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2018 ambapo inatarajiwa kuongeza zaidi ya Megawati 425 kwenye Gridi ya Taifa, na hivyo kupunguza tatizo la umeme nchini.

### **2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Bajeti kwa Wizara ya Nishati na Madini, haukuwa wa kuridhisha kwa kuwa fedha iliyotolewa hadi Machi, 2017 ni asilimia 36 tu;

(ii) Miradi mingi haikutekelezeka kama ilivyopangwa kwa kuwa fedha zilizotengwa hazikutolewa na kupelekwa kwa wakati kama ilivyotakiwa;

(iii) Miradi mingi ya REA katika Awamu ya Pili haikukamilika kutokana na kasoro mbalimbali kama vile uainishaji wa maeneo bila kuzingatia vijiji na vitongoji ambavyo tayari vina wananchi wengi, na ufungaji wa Mashine Humba nyingi kutokidhi mahitaji ya eneo husika;

(iv) Serikali iangalie upya namna bora ya kuwasaidia **Wachimbaji wa Kati** kwa kuwapatia maeneo ya kutosha kwa kuwa wameonesha nia ya dhati ya kuendeleza Sekta ya Madini;

(v) Ruzuku iliyotolewa na Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa Wachimbaji Wadogo Wadogo, haikusimamiwa vizuri na hivyo kushindwa kuleta tija kwa Wananchi waliookusudiwa;

(vi) Pamoja na Mipango mizuri ya TPDC katika kuendeleza Sekta ya Gesi nchini, ni lazima Serikali iwekeze fedha za kutosha katika miradi ya Gesi ili kuharakisha azma ya nchi yetu kuingia katika uchumi wa viwanda;

(vii) Serikali itenye fedha za kutosha na kuzipeleka kwa wakati kwenye miradi ya kimkakati kama vile Mgodi wa makaa ya Mawe wa Kiwira; na

(viii) Uwekezaji katika sekta ya madini unahitaji kuangaliwa upya hasa katika uwekezaji wa Migodi mikubwa.

### **3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni:- Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini wakati huo.

#### **3.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya Shilingi bilioni **370.68** ikillinganishwa na **Shilingi bilioni 286.66** kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa, hadi kufikia 28 Februari, 2017, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 239.38** sawa na **asilimia 64.5** ya lengo. Makusanyo hayo yanaweza kufikia lengo lilielowekwa kama Wizara itaongeza juhudii katika kipindi kilichobaki.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Makadirio ya mchango wa Idara ya Madini kwa mwaka fedha 2017/18 yameshuka kwa asilimia **4.5%** ikillinganishwa na mwaka wa fedha 2016/17. Aidha, Makadirio ya mchango wa Idara ya Nishati, yameongezeka kwa asilimia **4.5%** katika mwaka wa fedha 2017/18 ikillinganishwa na mwaka wa fedha 2016/17. Ufanuzi zaidi umeoneshwa kuitia Kielelezo Na. 01 cha Taarifa hii.

## Kielelezo Na. 01



Aidha Kamati ilielezwa sababu zilizosababisha kuongezeka kwa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kama ifuatavyo:-

- i) Usimamizi bora wa mapato kutoka vyanzo vya ndani;
- ii) Kuanzishwa kwa Minada ya Madini ya Vito nchini;
- iii) Kuongezeka kwa Mauzo ya Gesi Asilia kwa watumiaji wapya hasa baada ya viwanda vipyta zaidi ya 41 kuunganishwa kwenye mtandao wa matumizi ya Gesi;

### 3.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Nishati na Madini ilidhinishiwa jumla ya **Shilingi**

**triliioni 1.12** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia tarehe 13 Machi, 2017 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 404.12**, sawa na **asilimia 36** ya Bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

Bajeti ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge lako ilikuwa ni **Shilingi Triliioni 1.06**, sawa na **asilimia 94** ya bajeti yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/17. Hadi kufikia Machi, 2017 **Shilingi Bilioni 372.88** zilikuwa zimetolewa, sawa na **asilimia 35 tu** ya fedha za Maendeleo.

Kwa upande wa fedha za Matumizi Mengineyo (OC), fedha iliyoidhinishwa ilikuwa **Shilingi bilioni 66.22** na hadi kufikia Machi, 2017 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi Bilioni 31.24**, sawa na **asilimia 47%** ya fedha zilizoidhinishwa. Mwenendo huu wautolewaji wa fedha za matumizi mengineyo unakwamisha usimamizi bora wa fedha za miradi ya maendeleo, kwani Watendaji wanashindwa kusimamia miradi hiyo kwa kukosa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya fedha za maendeleo kutoka nje kwa mwaka wa fedha 2016/17 ilikuwa ni **Shilingi Bilioni 331.51**. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya **Shilingi Bilioni 38.57**, sawa na **asilimia 12%** tu zilipokelewa na kupelekwa katika miradi mitatu ambayo ni Miradi ya Umeme Vijijiini, Mradi wa Hale Hydropower na Mradi wa Makambako- Songea. Upatikanaji huu mdogo wa fedha za nje kwenye miradi ya Maendeleo, umekwamisha kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi mingi iliyotengewa kiasi kikubwa cha fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa kubaini namna utegemezi wa fedha za nje za maendeleo unavyoathiri utekelezaji wa miradi hiyo, na hivyo kuamua katika Bajeti ya Mwaka wa fedha 2017/18 kutenga fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani tu. Uamuzi huu utasaidia miradi mingi kutekelezwa bila kutegemea fedha za Wahisani ambao wamekuwa hawatekelezi kikamilifu ahadi zao.

Ufafanuzi zaidi kuhusu uwiano kati ya Bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizopatikana hadi Machi, 2017 ni kama unavyoonekana kupitia Kielelezo No.2 katika taarifa hii.

### Kielelezo Na. 2

BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2016/2017			FEDHA ILIYOPATIKANA HADI MACHI,2017	
UFAFANUZI	KIASI	ASILIMIA	KIASI	ASILIMIA
JUMLA KUU	Tri 1.12	100	Bil 404.12	36
FEDHA ZA MAENDELEO	Tri 1.06	94	Bil 372.88	35
MATUMIZI YA KAWAIDA	Bil 66.22	6	Bil 31.24	47

**CHANZO:** Taarifa ya Wizara ya Nishati na Madini Fungu 58 kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasikitishwa na utolewaji wa fedha za miradi ya maendeleo usioridhisha, hivyo kusababisha miradi mingi kushindwa kukamilika kama ilivyopangwa katika mwaka wa fedha 2016/17. Kamati inaona ni vyema kuwa na miradi michache ya kipaumbele ambayo itaweza kupelekewa fedha kuliko kuwa na miradi mingi ambayo haitawenza kutekelezwa kwa mwaka husika kwa kukosa fedha.

### 3.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka 2016/17, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Toleo la Januari, 2016 iliyoelezea majukumu ya Kamati ya kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa shughuli za Wizara katika Sekta za Madini na Nishati.

Napenda kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa, baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado haujafanyiwa kazi na Serikali kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika**, bado kuna tatizo la usimamizi usioridhisha katika miradi ya Umeme Vijijini, katika maeneo mengi hapa nchini. Katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilibaini changamoto mbalimbali katika maeneo mengi zilizoathiri utekelezaji wa miradi. Mfano; ufungaji wa Mashine Humba zilizochini ya kiwango katika maeneo mengi umesababisha kuharibika mara kwa mara na hivyo wananchi waliopata miradi ya umeme vijijini kutokupata faida ya Nishati hiyo hata baada ya kukamilika kwa miradi hiyo.

Fedha zilizotengwa kwa ajili ya baadhi ya miradi ya kimkakati ni kidogo sana ukililinganisha na mahitaji halisi ya fedha zinazohitajika katika kuendeleza miradi hiyo. Kamati haioni dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendeleza miradi hiyo, hasa ile ya Joto Ardhi ambayo utekelezaji wake haujaanza licha ya upembuzi yakinifu kukamilika muda mrefu uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu jitihada zinazofanywa na Serikali za kulipa madeni ya TANESCO, Kamati haioni mikakati ya dhati ya Serikali ya kumaliza madeni hayo kwa wakati. Aidha, mwenendo hafifu wa ulipaji wa madeni hayo unakwamisha kwa kiasi kikubwa shughuli za utendaji wa Shirika hilo.

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA (FUNGU 58) MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

##### **4.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/18, Kamati imebaini kuwa Wizara imekuwa ikisimamia na kutekeleza malengo hayo zaidi ya miaka mitano sasa. Hii

inatokana na umuhimu wake kwa kuzingatia majukumu yaliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini, Sura 299, The Ministers (Discharge of the Ministerial Functions) Act.

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka wa Fedha 2017/18 Wizara itatekeleza na kusimamia Malengo Makuu Matano (5) yafuatayo:-

- i) Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Nishati kwa Maendeleo endelevu ya Taifa;
- ii) Kuboresha uendelezaji na usimamizi endelevu wa rasilimali za madini kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi;
- iii) Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wadau katika Sekta za Nishati na Madini;
- iv) Kuboresha utoaji wa huduma kwa watumishi waathirika wa VVU na UKIMWI ili kupunguza maambukizi; na
- v) Kuondoa vitendo vya rushwa katika sekta ya Nishati na Madini.

**Mheshimiwa Spika**, malengo haya yakitekelezwa vizuri yatatimiza azma ya Wizara ya kuendeleza sekta inazoisimamia hasa Sekta ya Madini ambayo inatarajiwa kuongeza pato la Taifa, na Sekta ya Nishati inayotegemewa kutekeleza azma ya Taifa kufikia Uchumi wa Viwanda unaotarajiwa na Wananchi wetu.

#### **4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato**

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka wa Fedha 2017/18 Makisio ya makusanyo ya Maduhuli yanakadiriwa kuwa jumla ya **Shilingi bilioni 360.99** ikililinganishwa na **Shilingi bilioni 370.68** kwa mwaka wa fedha 2016/17. Kati ya makusanyo hayo **Shilingi bilioni 194.39** sawa na **asilimia 53.8** zitakusanywa na Idara ya Madini, **Shilingi bilioni 166.33** sawa na **asilimia 46.6%**

zitakusanywa na Idara ya Nishati na **Shilingi bilioni 266.40** sawa na **asilimia 0.1%** zitakusanywa na Idara na Vitengo vingine katika Wizara.

Makadirio ya makusanyo ya mapato yameshuka kwa **asilimia 2.6%** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo ya mwaka wa fedha 2016/17. Aidha Makusanyo ya maduhuli kwa Idara ya Madini yameshuka kwa **asilimia 9.98%** ikilinganishwa na makusanyo ya Mwaka wa fedha 2016/17.

**Kamati inataka kufahamu ni kwa sababu gani Makusanyo ya Maduhuli kwa Idara ya Madini yanatarajiwa kushuka ilhali kama nchi tunatamani Sekta ya Madini iendelee kutoa mchango mkubwa kwenye pato la Taifa.**

#### 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, makadirio ya matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni jumla ya **Shilingi Bilioni 998,337,759,500** ikilinganishwa na **Shilingi Trilioni 1,122,845,741,000** zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2016/2017. Bajeti hii ya Matumizi imepungua kwa **asilimia 11.1%**.

Kamati ilitaka ufanuzi ni kwanini Bajeti hii imeshuka kwa kiwango hicho, wakati nchi inatarajia kuendeleza miradi mikubwa ya Nishati ambayo inategemewa katika uchumi wa Viwanda. Wizara ilifanua kuwa Bajeti hii imeshuka kutokana na kupungua kwa fedha za nje hasa kwenye Miradi ya Maendeleo.

Kamati inaishauri Wizara kuacha kutegemea sana fedha za nje, kwa kuwa zimekuwa hazitolewi kwa wakati na hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka husika. Kwa mfano; Bajeti ya nje kwa mwaka wa fedha 2016/17 ilikuwa **Shilingi Bilioni 331.51**. Hadi kufikia Machi, 2017 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi Bilioni 38.57** sawa na **asilimia 12%** ya Bajeti yote iliyotegemewa katika miradi ya maendeleo.

Fedha za ndani kwa ajili ya REA zimepungua kutoka **Shilingi Bilioni 534,400,000,000** mwaka 2016/17 hadi **Shilingi Bilioni 469,090,426,000** kwa mwaka 2017/18, upungufu ambaao ni sawa na **asilimia 12.2%**. Aidha, bajeti hii itatoka kwenye tozo mbalimbali, ambapo tozo za mafuta ni **Shilingi 354,950,000,000** na tozo ya Umeme ni **Shilingi 41,514,000,000** na Bajeti ya Serikali ni **Shilingi 72,626,426,000**.

**Mheshimiwa Spika**, kupungua kwa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo pamoja na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Miradi ya maendeleo usioridhisha, kama ilivyoshuhudiwa kwa mwaka wa fedha 2016/17, kunaweza kusababisha miradi mingi ya kimkakati kushindwa kutekelezwa kama ilivyokusudiwa.

Aidha, bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni **Shilingi Bilioni 59,705,753,500**. Bajeti hii imepungua kwa **asilimia 10.2%** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17 ambayo ilikuwa **Shilingi Bilioni 66,481,072,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 28,833,681,500** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), ambazo pia zimepungua ikilinganishwa na **shilingi Bilioni 38,654,138,000** zilizotengwa mwaka 2016/17.

Kuendelea kupungua huku kwa bajeti ya Matumizi ya Kawaida kunaweza kupunguza ufanisi katika kusimamia Bajeti ya Miradi ya Maendeleo iliyotengwa kwa Watumishi kukosa fedha za kwenda kusimamia Wakandarasi wanaotekeleza miradi hasa ile ya Umeme Vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yako hairidhishwi na utekelezaji wa Bajeti ya Wizara inayoidhinishwa na Bunge lako tukufu, kutohana na kiasi cha fedha kinachotolewa kuwa kidogo. Kwa mfano; kwa upande wa bajeti ya maendeleo, fedha zinazoidhishwa na Bunge, na kiasi ambacho kimekuwa kikitolewa ni chini ya asilimia 50.

Mwenendo huo wa Bajeti hauwezi kuleta tija kwenye utekelezaji wa miradi inayokusudiwa katika kipindi husika. Ni vyema Serikali ikatenga Bajeti inayotekelzeza kwa

kuanisha miradi michache na kuhakikisha fedha za utekelezaji wake zinapelekwa kikamilifu.

## **5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara, kwa mwaka wa fedha 2016/17 na makadirio na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/18, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

5.1 Kwa kuwa, utekelezaji wa Miradi ya Umeme vijiji katika awamu mbili zilizokamilika ulikuwa na changamoto nyingi hasa katika Mikoa ya Tanga na Geita, ambako Kamati ilitembelea na kukagua; Kamati inashauri kuwa, changamoto zillizobainika ikiwa ni pamoja na baadhi ya maeneo kurukwa, zipatiwe ufumbuzi wa haraka kabla ya kuendelea kwa Mradi wa Umeme vijiji, Awamu ya Tatoo (REA III) .

5.2 Kamati inashauri Serikali ikamilishe taratibu za kumaliza changamoto zilizojitokeza na kuchelewesha malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT returns) kwa wawekezaji wa sekta ya Madini ili kuendelea kuboresha hali ya uwekezaji hapa nchini.

5.3 Pamoja na juhudhi mbalimbali zinazofanywa na Wizara katika usimamizi wa Madini ya Tanzanite, Kamati inashauri Serikali kuwa, iangalie upya Mikataba yote ilioingiwa na STAMICO na mbia mwenza kama ina tija kwa Taifa.

5.4 Ruzuku kwa Wachimbaji Wadogo iliyotolewa na Serikali katika awamu zote mbili kwa kiasi kikubwa imeshindwa kutimiza malengo kwa kukosa usimamizi mzuri. Aidha, ni vema Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ikaangalia namna bora ya kusimamia fedha hizi ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo Wachimbaji na kufuatilia kwa karibu shughuli za Wachimbaji hao.

5.5 Sekta ya Uchimbaji wa Kati imeendelea kukua kwa kiasi cha kuridhisha, hivyo ni vyema Serikali ikaangalia upya jinsi ya kuisaidia kupata baadhi ya misamaha ya kodi kwenye Mafuta na Vipuli vinavyotumika katika shughuli za uchimbaji nchini.

5.6 Leseni zote ambazo zinakiuka Sheria ya Madini ikiwa ni pamoja na kushindwa kuendelezwa kwa muda mrefu, zifutwe na kupewa Wachimbaji Wadogo na wa Kati, kwa kuwa wameonesha nia ya dhati ya kuendeleza Sekta hiyo nchini.

5.7 Pamoja na Serikali kuandaa Mpango Kambambe wa Matumizi ya Gesi Asilia nchini, ni vyema ukafanyika utafiti na upembuzi yakinifu kuhusu miradi yote mikubwa ya usambazaji wa Gesi katika maeneo mbalimbali, illi kuweza kujua kama ina manufaa ya kiuchumi (*Economic Value*)kwa Taifa. Hatua hii itasaidia kuepusha nchi kuijilingiza kwenye mikopo ambayo ni mzigo kwa Taifa.

## **6.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara, katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tullowakabidhi.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini, kwa Mhe. Prof. Sospeter Mhongo, (Mb) - aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Mhe. Dkt. Merdad Kalemani, (Mb)- Naibu Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Kaimu Katibu Mkuu, Prof. James Mdoe, kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

Kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa mchango wao adhimu katika shughuli za Kamati, katika

kipindi hiki cha uchambuzi wa Bajeti kwa Fungu 58. Ni dhahiri shahiri kuwa, bila weledi na ushirikiano walionipa, Kamati isingweza kufikia hatua hii ya mafaniko.

Kwa heshima kubwa naomba majina yao katika orodha ifuatayo yaingizwe kwenye Hansard:-

1. Mhe. Doto Mashaka Biteko, Mb	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Deogratius Ngalawa, Mb	-	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb	-	Mjumbe
4. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb	-	"
5. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb	-	"
6. Mhe. Zainabu Mussa Bakar, Mb	-	"
7. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb	-	"
8. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb	-	"
9. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb	-	"
10. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb	-	"
11. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	-	"
12. Mhe. Stella Ikupa Alex, Mb	-	"
13. Mhe. Joyce Bitta Sokombi, Mb	-	"
14. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb	-	"
15. Mhe. Mauled Said Abdalah Mtulia, Mb	-	"
16. Mhe. Desderius John Mipata, Mb	-	"
17. Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb	-	"
18. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb	-	"
19. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb	-	"
20. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb	-	"
21. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb	-	"
22. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb	-	"
23. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb	-	"
24. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb	-	"
25. Mhe. John Wegesa Heche, Mb	-	"
26. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb	-	"

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndg. Mwanahamisi Munkunda na Ndg. Felister Mgonja, pamoja na Msaidizi wa Kamati, ndg.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Kokuwaisa Gondo, kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

Naomba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 58** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambayo ni **Shilingi 998,337,759,500**.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Dotto Mashaka Biteko, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

01Juni, 2017

**NAIBU SPIKA:** Sasa tutamsikia Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Nishati na Madini. (*Makofii*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Hotuba hii imegawanyika katika sehemu 11 kuanzia (a)mpaka (k) na zimezungumzia kuhusu mchakato wa Katiba Mpya na mustakabali wa madini; mapitio ya utekelezaji wa bajeti; sekta ya nishati; sekta ya gesi; nishati jadidifu na teknolojia ya upepo na jua; sekta ya madini; utekelezaji wa Maazimio ya Bunge na mwenendo usioridhisha wa mpango wa uwazi na uwajibikaji katika tasnia ya uziduaji. Kwa sababu maeneo haya ni mengi na muda ni mfupi, naomba hotuba yote kwa ukamilifu wake iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna rekebisho katika ukurasa wa tano kwenye aya ya mwisho, maneno “asilimia 30 ya dhahabu inayozalishwa” yasomeke “asilimia 30 ya madini yanayozalishwa” kwa sababu dhahabu ni 5% na 25% ni fedha, shaba na madini mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niungane na wote wenye mapenzi mema katika kuomba ulinzi wa

Mwenyezi Mungu wakati wa kutimiza wajibu wa Kibunge kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuishauri na kuisimamia Serikali kwa Wizara ya Nishati na Madini juu ya bejeti ya mwaka 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, nitumie fursa hii kuwatakiwa waislamu wote mfungo mwema katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitambue mchango Mheshimiwa John Heche, Naibu Waziri Kivuli wa Wizara ya Nishati na Madini alioutoa katika maandalizi ya hotuba hii. Aidha, tuendelee kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aweze kupona na kurejea katika utekelezaji wa majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa familia ya marehemu Mzee Philemon Ndesamburo, wanachama wa CHADEMA kote nchini, wananchi wa Moshi Mjini na Kilimanjaro, Wabunge na Watanzania wote walioguswa na msiba huu. Marehemu atakumbukwa kwa mchango wake kama mmoja wa waasisi wa chama chetu, Mbunge mstaafu na mfanyabiashara mashuhuri, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa Katiba Mpya na mustakabali wa madini na gesi asilia. Novemba 4, 2016 Mheshimiwa Rais alipokuwa akizungumza na Watanzania kuititia vyombo vya habari lkulu jijini Dar es salaam, alinukuliwa akisema hakuwahi kuzungumzia Katiba Mpya wakati wa kampeni zake, kwa hiyo si kipaumbele chake na kwamba kipaumbele chake ni kuinyoosha nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali hii ya Awamu ya Tano ikitisema swala la Katiba Mpya sio kipaumbele chake, Watanzania walitoa mapendekezo ya kuwepo kwa vifungu kwenye Katiba Mpya vinavyohusika na madini, mafuta na gesi asilia ili kuondoa migogoro inayohusu rasilimali na kuwezesha mali ya nchi na wananchi kunufaika na maliasili ambazo Mwenyezi Mungu amelijalia Taifa letu. Mapendekezo

na matakwa ya wananchi kuhitaji Katiba Mpya kuwa na vifungu vinavyohusika na madini, mafuta na gesi asilia yalitokana na ukweli kwamba Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan Ibara ya 27 hajjaweka misingi bora ya umiliki, usimamizi na ushughulikiaji wa masuala ya rasilimali za nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu wa nchi nydingine kuhusu Katiba na mustakabali wa madini, mafuta na gesi asilia; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kutoa mifano michache juu ya uzoefu wa nchi nydingine ili kuionesha Serikali hii ni nini hasa kilitokea kwa wenzetu ambao pia walikuwa na tatizo kama la kwetu. Nchini Norway uchimbaji wa mafuta na gesi asilia ulianza mwaka 1971 na kwa sasa Norway ni mojawapo ya nchi zilizofanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kuboresha uchumi na maisha ya wananchi kutokana na sekta ya mafuta na gesi asilia. Mafanikio ya Norway yalipatikana baada ya kubadili sera zilizokuwa zinatoa upendeleo kwa makampuni binafsi na kuweka sera zilizokuwa zinatoa kipaumbele kwa maslahi ya nchi na wananchi. Pamaja na hayo Norway iliveka mafuta na gesi asilia katika Katiba yake Ibara ya 110 na msimamo huo ukafafanuliwa zaidi na Sheria ya Mafuta. Huu ni mfano wa Katiba na sheria kuwekwa kipaumbele na kutumika kama nyenzo ya kunyoosha nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya Bolivia ni mfano wa pili ambao Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuutoa kwa nia na malengo yaleyale. Nchi hii ni mionganoni mwa nchi ambazo zimejaliwa kuwa na utajiri mkubwa wa mafuta na gesi. Pamoja na utajiri huo, wananchi wa Bolivia kwa kipindi kirefu walikuwa na malalamiko kuwa mafuta na gesi asili haziwanufaishi. Bolivia ilifanya mabadiliko ya sera zake lakini tofauti na Norway, mabadiliko ya Bolivia yalisababishwa na malalamiko na vurugu za wananchi waliokuwa wanataka mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia miaka ya 2000, nchi ya Bolivia ilishuhudia vurugu na maandamano zilizosababishwa na kile kilichoitwa vita ya maji kutokana

na kupinga kubinafsishwa kwa maji na baadaye vurugu hizi zilihamia katika gesi asilia na mafuta.

Aidha, mwaka 2003 vurugu na maandamano makubwa dhidi ya sera mbovu zilisababisha aliyekuwa Rais wa Bolivia Gonzalo Sanchez de Lozada maarufu kama Goni kuijuzulu na kukimbilia Marekani. Hata hivyo, alirithiwa na Makamu wa Rais ambaye naye alilazimishwa kuijuzulu mwaka 2005 kwa maandamano kama mtangulizi wake. Mwaka 2006 Evo Morales alichaguliwa kuwa Rais wa nchi hiyo na aliongoza nchi hiyo kupata Katiba Mpya mwaka 2009 ambayo pamoja na mambo mengine ilihakikisha kuwa mafuta na gesi yananufaisha wananchi wa Bolivia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania pia inayo madini, mafuta na gesi asilia kama zilivyo nchi ambazo mifano yake imeelezwa, ikumbukwe kwamba mwaka 2013, Tanzania ilishuhudia vurugu na umwagaji wa damu kwa wananchi wasiokuwa na hatia Mkoani Mtwara zilizosababishwa na mgogoro wa gesi ambao kiini chake ni madai ya wananchi kutonufaika na rasilimali. Mchakato wa mabadiliko ya Katiba ulibeba matumaini ya Watanzania kwamba pamoja na mambo mengine nchi ingeweka misingi ya wananchi kunufaika na rasilimali ikiwemo madini, mafuta na gesi asilia. Hata hivyo, mchakato huo ulikwama na kupunguza matumaini kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii inayoongozwa na CCM inataka mpaka wananchi waanzishe migomo na maandamano ndiyo itambue kwamba Katiba Mpya ni kipaumbele cha wananchi katika masuala ya msingi ikiwemo rasilimali za nchi. Hivi ni lini Rais atatambua kwamba Katiba na sheria ndio zana muhimu za kunyoosha nchi?

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Nishati na Madini kuwa mstari wa mbele kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha mchakato wa mabadiliko ya Katiba unaendelezwa na masuala ya madini na mafuta yanapewa kipaumbele katika Katiba Mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa kufanya katika kipindi hiki ambacho Katiba Mpya haijapatikana. Kwa kuwa Tanzania tunakabiliwa na changamoto kubwa katika sekta za madini, mafuta na gesi asilia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapendekeza kwamba Serikali ilete mbele ya Bunge lako Tukufu marekebisho ya sheria ambayo yataweka misingi ifuatayo:-

- (i) Serikali isimamie shughuli za uvunaji wa madini katika mfululizo wake wote (*entire chain*) kuanzia kwenye uchimbaji ili kuhakikisha kuwa madini yanatoa mchango katika maendeleo ya kiuchumi ya Taifa.
- (ii) Kuwepo na utaratibu wa kutoa leseni kwa njia ya zabuni ya wazi badala ya utaratibu wa mikataba kati ya Serikali na mwekezaji. (*Makofi*)
- (iii) Serikali iwe na makampuni ya kutosha yanayoweza kuingia katika ubia na makampuni au taasisi zingine au mjumuiko wa makampuni katika shughuli za uvunaji wa madini, mafuta na gesi asili. Serikali pia imiliki hisa kutokana na thamani ya rasilimali za madini yetu. (*Makofi*)
- (iv) Ili kupunguza mianya ya rushwa na kuongeza uwajibikaji katika mikataba, iwepo sheria inayotaka Bunge kuridhia mikataba yote ya utafutaji na uvunaji wa madini, mafuta na gesi asilia. (*Makofi*)
- (v) Serikali ihakikishe kuwa kwa niaba ya wananchi, Tanzania inanufaika na uvunaji wa madini, mafuta na gesi asilia na usiwepo mkataba wowote unaokiuka misingi hii.
- (vi) Uvunaji wa madini, mafuta na gesi asilia uhakikishe unachangia kuboresha maisha ya jamii, ajira na kulinda mazingira, kuhakikisha pia maslahi ya Serikali kuu, Halmashauri za Wilaya, vijiji na waathirika wa uwekezaji mkubwa wananaufaika na miradi hiyo.
- (vii) Wananchi ambako uwekezaji unafanyika washirikishwe kuhusu maamuzi yote yanayohusu utafutaji na

uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia na Halmashauri zao zihusike katika umiliki kuititia hisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, makinikia ama mchanga wa dhahabu na hatma ya sekta ya madini nchini. Tarehe 24 Mei, 2017 Mheshimiwa Rais Dkt. John Magufuli alipokea Ripoti ya Kamati ya Kwanza ya Rais juu ya kusafirishwa nje kwa makinikia ya dhahabu ama shaba maarufu kama mchanga wa dhahabu. Aidha, wakati wa tukio la kukabidhi ripoti hiyo, Mwenyekiti wa Kamati tajwa Profesa Abdulkarim Mruma alieleza muhuktasari wa matokeo ya ripoti hiyo na Rais alitoa kauli mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema ikafahamika kwamba makinikia haya yanahu su migodi miwili ya Bulyankulu na Buzwagi chini ya kampuni moja ya Acacia. Makinikia haya yanahu su takribani 30% ya madini, 5% ikiwa dhahabu, 25% ikiwa shaba, fedha na madini mengine ambayo kwa sheria mbovu na mikataba mibovu ni mali ya mwekezaji huku stahili ya nchi ikiwa ni mrabaha wa 4% tu. Ripoti hiyo ya makinikia ama mchanga wa dhahabu haihusu mapato ya Taifa na maslahi ya nchi katika 70% ya dhahabu inayopatikana katika mgodi wa Bulyankulu na Buzwagi wala haihusu 100% ya dhahabu na madini mengine yanayopatikana katika migodi mingine nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais makini kabla ya kufikiria makinikia angefikiria kuhusu madini yanayochimbwa na kuchenjuliwa kwa ukamilifu hapa nchini lakini nchi haipati mapato yanayostahili. Hivyo, taarifa ya Kamati ya Profesa Mruma na kauli za Rais zimeingiza nchi na wananchi katika mjadala mdogo wa makinikia ama mchanga badala ya mjadala mkubwa wa madini na matatizo makubwa yaliyopo katika mfumo wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika muktadha huo, kabla ya kutoa maoni kuhusu makinikia ama mchanga wa dhahabu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa mwito kwa Bunge na wananchi kujadili matatizo makuu ya sekta ya madini katika Taifa letu. Matatizo makubwa katika sekta

ya madini katika nchi yetu yamesababishwa na sera na sheria mbovu zilizotungwa chini ya Serikali inayoongozwa na CCM na mikataba mibovu ilioingiwa katika awamu mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapojadili mathalani kukosa mapato kutoka Mgodi wa Bulyankulu ni vyema tukakumbuka kuwa katika kipindi cha mwisho cha Rais Ali Hassan Mwinyi makampuni ya kigeni yaliongezeka kuingia katika nchi yetu. Kati ya makampuni hayo ni pamoja na Sutton Resources ya Vancouver, Canada, iliyopatiwa leseni kwa ajili ya eneo la Bulyanhulu au Butobela mwaka 1994. Leseni hiyo ilitolewa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete alipokuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya Rais Benjamin Mkapa kuapishwa mwaka 1995 illandikwa *fax* baada ya Rais kuapishwa iliyokuwa na maneno “*our man has been sworn into office, now Bulyankulu file will move.*” Na kweli mwaka 1996 wachimbaji wadogo wadogo walihamishwa kwa nguvu na wengine wakidaiwa kufukiwa katika mashimo na Kampuni ya Sutton Resources wakakabidhiwa eneo hilo. Yaliyofanywa Bulyanhulu pia kwa namna nytingine yamefanyika katika maeneo mengine kwa nyakati tofauti ikiwemo Nyamongo, Mererani, Geita na Buzwagi na mengineyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuyawekea makampuni hayo mazingira halali ya kisheria ya kunyonya rasilimali za nchi mwaka 1997, Bunge la Jamhuri ya Muungano lilitengeneza matatizo makubwa kwa kutunga sheria mbili mbovu kwa siku moja chini ya hati ya dharura. Kati ya sheria hizo ni Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Sheria ya Fedha (*Financial Laws Miscellaneous Act*) ya mwaka 1997 ambayo ilifanya marekebisho makubwa katika sheria mbalimbali za kodi ambayo yalifuta kwa kiasi kikubwa kodi, tozo na ushuru mbalimbali kwa kampuni za madini. Matokeo ya sheria hii ni miaka mingi ya kukosa mapato ya kutosha katika madini. Sheria nytingine ni ile Sheria ya Uwekezaji Tanzania (*Tanzania Investment Act, 1997*) ambayo iliyapa

makampuni ya nje kinga za kisheria za mambo ambayo mengine yanalamikiwa kuhusu makampuni hayo mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu katika mfumo mzima wa madini katika nchi yetu ukataasisishwa mwaka 1998 kwa Bunge kutunga Sheria ya Madini (*Mining Act, 1998*). Sheria hii kimsingi iliweka bayana kwamba madini yanayopatikana na fedha za mauzo yake ni mali ya mwenye leseni. Sheria iliruhusu makinikia ama mchanga kusafirishwa nje ya nchi kwa ajili ya usafishaji. Nchi yetu kupitia sheria hii ilipaswa kulipwa mrabaha wa asilimia tatu, sheria ya mwaka 2010 ilichofanya ni kuongeza tu kiwango mpaka asilimia nne tu. (*Makofj*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine sheria zetu zinatoa wajibu kwa makampuni kulipa kodi ya mapato ya 30%. Hata hivyo, ni baada ya kupata mapato yenye kutozwa kodi (*taxable income*) yaani baada ya kupata faida. Sheria hizi mbovu zimeruhusu kwa muda mrefu makampuni ya madini kuondoa gharama zote za uzalishaji kabla ya kutangaza mapato ya kikodi. Makampuni hayo yametumia mianya hiyo na udhaifu wa taasisi za nchi yetu mathalani *TMA* na *TRA* kuweka gharama zisizostahili na hivyo kutangaza kupata hasara na kutolipa kodi au kutangaza kupata faida kidogo na kulipa kodi kiduchu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais makini alipaswa kabla ya kuzuia makinikia ama mchanga kudhibiti mianya kama hii ya upotevu mkubwa wa mapato katika madini. Mfumo huu wa kuepuka kodi ama *tax avoidance* na kupanga kodi ama *tax planning* ambao umeikosesha nchi mapato kwa muda mrefu umehalalishwa na sheria mbovu za nchi yetu. Rais makini alipaswa kuanza na sheria mbovu. (*Makofj*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kuwa na sera bomu na sheria mbovu ni mikataba mibovu ambapo kwa upande wa mikataba ya uendelezaji wa madini kati ya Serikali na makampuni makubwa *MDAs*, mikataba hiyo imeweeka misamaha ya kodi na kuachia pia mianya ya

uepukaji wa kodi. Mikataba hiyo mibovu imetoa misamaha ambayo mingine hata haipo katika sheria tajwa kwa mfano, Halmashauri zilizo na migodi ya madini makampuni yameruhusiwa kutoa kiwango cha jumla cha dola laki mbili kwa ajili ya tozo za huduma badala ya kati ya 0.14% na 0.3% ya mapato ya mwaka ya kampuni (*annual turn over*) ambayo yangetuwa malipo makubwa zaidi kwa Halmashauri zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nyakati mbalimbali, tumeomba mikataba hiyo iletwe Bungeni ili ijadiliwe na kupitiwa upya, hata hivyo Serikali hii inayoongozwa na CCM imekuwa ikigoma. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuileta mikataba hiyo Bungeni na kuwesheha majadiliano ya marekebisho (*renegotiation*) kati ya Serikali na wawekezaji ili nchi na wananchi waweze kunufaika ipasavyo na rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu amelljalia Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala haya hayakuzungumzwa na Mwenyezeki wa Kamati ya Makinikia Profesa Mruma wala Mheshimiwa Rais wakati akipokea ripoti ya mchanga. Badala yake ilitolewa taarifa yenyewe kuonesha kuwa katika makontena 267 yaliyopo bandari ya Dar es Salaam kiwango cha dhahabu katika makontena yote ambacho ni cha mwezi mmoja tu wa uzalishaji kimetajwa kuwa tani 7.8 au wakia 250,000. Kwa mahesabu rahisi tu ya kuzidisha kiwango hicho kwa kufanya makadirio ya mwaka na kujumlisha na uzalishaji mwingine wa migodi hiyo ya Bulyanhulu na Buzwagi tu kunaifanya Tanzania kuwa mzalishaji namba tatu wa dhahabu duniani. Hapa kuna mwelekeo wa udanganyifu wa kitakwimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taswira hasi imeanza kujengeka kimataifa ambapo tarehe 25 Mei, 2017 jarida la *Mining Journal* lilichapisha makala "*Trouble in Tanzania*" ambayo ilimalizia kwa mwito wa kufanyika kwa "*World Risk Survey*" ambayo takwimu za sasa nchi yetu inatarajiwa kuporomoka. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni taarifa kamili ya Kamati hiyo ikiwemo metholojia iliyotumika kutathmini sampuli ili ijadiliwe

na Bunge liweze kuazimia kufanya uchunguzi huru kuhusu jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa Serikali iliwahi kuunda Tume ambayo ilijulikana kama Tume ya Mheshimiwa Jaji Mark Bomani ambayo ilipewa kazi ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa sekta ya madini. Aidha, Tume hiyo iligusia kipengele cha uchenjuaji na usafishaji wa madini. Katika ukurasa wa 157 wa Taarifa ya Kamati ya Rais ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa sekta ya madini ya mwaka 2008 Kamati ilisema na ninanukuu; "Kamati imechambua hali halisi ya shughuli za uchenjuaji na usafishaji (*smelting and refinery*) wa madini hapa nchini na kuona kuwa shughuli hizi hazifanyiki katika kiwango cha kuridhisha. Aidha, hakuna miundombinu hasa umeme na reli ya kuwezesha kuanzishwa kwa shughuli hizo. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa mkakati wa kisera wa kuhamasisha uwekezaji katika uchenjuaji na usafishaji wa madini hapa nchini."

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo iliendelea kusema kuwa; "Kamati ilibaini kuwa kukosekana kwa shughuli hizi hapa nchini kunazifanya kampuni kama vile *Bulyanhulu Gold Mine Limited* kusafirisha mchanga (*copper concetrate*) kwenda Japan na China ili kuchenjuliwa. Hali hii isiporekebishwa, italazimisha mgodi wa *Kabanga Nickel* unaotarajiwa kuanzishwa kupeleka mchanga nje ya nchi kwa ajili ya kuchenjuliwa. Hii itaifanya Serikali kutokuwa na uhakika wa kiasi na aina ya madini yaliyomo katika mchanga huo na inaweza kuathiri mapato ya Serikali."

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati katika mapendekezo yake kwa Serikali kuhusu kipengele hiki, ilipendekeza; "Serikali iweke mikakati katika Sera ya Madini na kutunga au kurekebisha Sheria ya Madini ili kuingiza vipengele vitakavyowezesha uanzishwaji na uimarishwaji wa viwanda vyta uchenjuaji na usafishaji wa madini hapa nchini."

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Magufuli alikuwa Mjumbe wa Baraza la Mawiziri wakati taarifa hii inawasilishwa

kwa Rais Jakaya Kikwete. Aidha, Rais Magufuli alikuwa na muda toka alipoingia madarakani kuweza kushughulikia jambo hili katika hali yenye kuepusha migogoro isyo ya lazima. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa mwito kwa Bunge kuingilia kuishauri na kuisimamia Serikali kwa mustakabali mwema wa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2016/2017. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Nishati na Madini iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,122,583,517,000 na katи ya fedha hizo shilingi 1,056,354,669,000 zilikuwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Aidha, hadi kufikia tarehe 13 Machi, 2017 fedha zilizokuwa zimetolewa na Hazina kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni shilingi 372,877,980,724 tu sawa na asilimia 35 ya fedha zote za maendeleo zillotengwa kwa mwaka 2016/2017. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia takwimu zilizooneshwa hapo juu utabaini kwamba miradi ya maendeleo ilitekelezwa kwa kiwango cha asilimia 35 tu. Miradi iliyokwama ni pamoja na miradi ya umeme vijijini. Aidha, miradi hii inatekelezwa kwa kiwango hicho pamoja na sababu nyingine ni kutokana na Taifa kukosa fedha za wafadhili kwa miradi ya umeme ikiwemo miradi ambayo ingepata ufadhili wa *MCC*. Kwa maneno mengine, Watanzania wameshindwa kunufaika na miradi ya maendeleo kutoka kwa wafadhili kutokana na kukosekana kwa utawala bora, kuvurugwa kwa uchaguzi Zanzibar na uvunjifu wa haki za binadamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali hii iliwaaminisha Watanzania kuwa miradi itatekelezwa kwa ghamama za fedha za ndani katika kipindi cha bajeti cha mwaka wa fedha 2016/2017, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata majibu ya kina kuhusu sababu zilizopelekea Serikali kushindwa kutekeleza bajeti yake huku ikijinadi ndani ya Bunge hili Tukufu kwamba fedha za *MCC* hazina madhara na Taifa litatekeleza miradi kwa fedha zake.

Je, kwa mwendo huu ni lini Taifa litafikia malengo tuliojiwekea kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Bunge hili limekuwa likitoa Maazimio mbalimbali yanayohitaji utekelezaji wa Serikali lakini kwa bahati mbaya sana Bunge limekuwa halipatiwi mrejesho wa utekelezwaji wa Maazimio hayo. Tafsiri ya jambo hili ni dharau au ni kutokana na ukweli kwamba Bunge hili halina meno. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Kumi lilipitisha Maazimio baada ya Kamati ya *PAC* kuitia Taarifa ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na fedha za *capacity charge* ambazo *TANESCO* ilikuwa inatakiwa kuilipa *IPTL* lakini kukawepo na kesi ya kupinga kiwango hicho cha malipo na kulazimu fedha hizo kuwekwa Benki Kuu kwa kufungua akaunti ilioitwa *Tegeta Escrow Account*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 Novemba, 2014, Bunge lilipitisha Maazimio nane kuhusiana na uporwaji wa mabilioni ya fedha za Serikali zilizowekwa Benki Kuu. Azimio moja lililokuwa na uhusiano wa moja kwa moja na utendaji wa *TANESCO* ni Azimio namba saba, nanukuu; "Bunge linaazimia kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kununua mitambo ya kufua umeme ya *IPTL* na kuimilikisha kwa *TANESCO* kwa lengo la kuokoa fedha za Shirika hilo."

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Bunge halijapewa taarifa ya utekelezaji wa Azimio hilo na hadi sasa *TANESCO* bado inalipa kiasi cha shilingi bilioni 4.3 kila mwezi kwa *IPTL*. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ni kwa nini Serikali imeshindwa kutekeleza Azimio hilo na inaendelea kumlipa mtu aliyeinunua *IPTL* katika mazingira yenye ufisadi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Spika Anne Makinda aliunda Kamati Maalum ya Bunge kwenda kuzungumza na wananchi wa Mtwara kuhusu sakata la ujengwaji wa bomba la gesi asilia kutoka mkoani humo mpaka Dar es Salaam, kufuatia kuzuka kwa vurugu za tarehe 22 Mei 2013. Kamati hiyo ya

Mheshimiwa Spika Makinda ilikuwa chini ya Mbunge wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage ambaye leo amesoma hotuba kwa niaba ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ya Bunge ilitumia fedha za walipa kodi na ilifanya kazi hiyo na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Spika tarehe 20 Desemba, 2013. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Spika kuwezesha taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni ili mapendelekezo ya Kamati hiyo yajadiliwe na Bunge na kuwa maazimo rasmi ya Bunge kuweza kutekelezwa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, yamekuwepo pia maazimio mengine ya Bunge juu ya uchunguzi kuhusiana na mapato na ufisadi kwenye gesi asilia hususani juu ya Kampuni ya *Pan African Energy Tanzania (PAT)* ambayo nayo Serikali hajjawasilisha taarifa ya kuhitimisha utekelezaji mpaka hivi sasa. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwasilishwa Bungeni taarifa maalum juu ya utekelezaji wa Maazimio yote ya Bunge yanayohusu Wizara ya Nishati na Madini ambayo hayajatekelezwa mpaka hivi sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/ 2018; katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Nishati na Madini inakadiria kutumia jumla ya shilingi 998,337,759,500 ikilinganishwa na shilingi 1,122,583,517,000 zilizoidhinishwa na Bunge mwaka 2016/2017 sawa na upungufu wa asilimia 11. Sababu zinazotolewa na Serikali za kupungua kwa bajeti ni kupungua kwa makadirio ya fedha za nje kutoka shilingi 331,513,169,000 mwaka 2016/ 2017 hadi shilingi 175,327,327,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya kukosekana kwa fedha za nje...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga, una dakika moja, malizia.

**MHE. JOHN J. MNYIKA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kusisitiza kama ambavyo imekuwa ikifanya katika hotuba zilizowahi kutangulia kwamba, sehemu kubwa ya matatizo ya Wizara ya Nishati na Madini yamechangiwa na yanaendelea kuchangiwa na sababu za kibinadamu ikiwemo ukosefu wa utashi wa kisiasa huku masuala muhimu yakiachwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa bado linahitaji mabadiliko ya kimfumo ili kuwezesha hatua za haraka za kusimamia sera sahihi, uongozi makini na taasisi thabitii katika sekta ya nishati na madini pamoja na kuchukua hatua stahiki ili kuziwezesha sekta hizi za nishati na madini kuongeza pato la Taifa na kupelekea wananchi kuzifaidi rasilimali zao kuliko matamko hewa yanayolenga kupata umaarufu wa kisiasa, huku hatua zinazopaswa kuchukuliwa zikiachwa miaka nenda rudi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnyika.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WIZARA YA NISHATI NA MADINI MHESHIMIWA JOHN JOHN MNYIKA (MB), KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2016/2017 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/ 2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa chini ya 99(9) ya kanuni za Bunge,  
Toleo la Mwaka, 2016)*

#### **A. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote niungane na wenye mapenzi mema katika kuomba ulinzi wa mwenyezi Mungu wakati wa kutimiza wajibu wa kibunge kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuishauri na kusimamia Serikali kwa Wizara ya Nishati na Madini juu ya bajeti ya mwaka 2016/2017 na makadirio ya

mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, nitumie fursa hii kuwatakia waislamu wote mfungo mwema katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.

**Mheshimiwa Spika**, Nitambue mchango Mheshimiwa John Heche, Naibu Waziri Kivuli wa Wizara ya Nishati na Madini alioutoa katika maandalizi ya hotuba hii. Aidha tuendelee kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aweze kupona na kurejea katika utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa familia ya marehemu Mzee Philemon Ndesamburo, wanachama wa CHADEMA kote nchini, wananchi wa Moshi Mjini, wabunge na watanzania wote walioguswa na msiba huu. Marehemu atakumbukwa kwa mchango wake kama mmoja wa waasisi wa chama chetu, Mbunge wa Mstaafu na Mfanyablashara Mashuhuri. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema.

#### **B. MCHAKATO WA KATIBA MPYA NA MUSTAKABALI WA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA**

**Mheshimiwa Spika**, Novemba 4, 2016 Mheshimiwa Rais alipokuwa akizungumza na watanzania kupitia vyombo vya habari, ikulu jijini Dar es salaam alinukuliwa akisema hakuwahi kuzungumzia katiba mpya wakati wa kampeni zake, kwa hiyo siyo kipaumbele chake na kwamba anachotaka kwanza ni kunyoosha nchi.

**Mheshimiwa Spika**, wakati Serikali hii ya awamu ya tano ikisema swala la katiba mpya kama siyo kipaumbele chake, watanzania walitoa mapendelekezo ya kuwepo kwa vifungu kwenye katiba mpya vinavyohusika na madini, mafuta na gesi asilia ili kuondoa migogoro ambayo inayohusu rasilimali na kuwezesha nchi na wananchi kunufaika na maliasili ambazo Mwenyezi Mungu amelijalia taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, mapendelekezo na matakwa ya wananchi kuhitaji katiba mpya kuwa na vifungu vinavyohusika na madini, mafuta na gesi asilia, yalitokana

na ukweli kwamba katiba ya sasa ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania hususan ibara ya 27 hajjaweka misingi bora ya umilliki, usimamizi na ushughulikiaji wa masuala yanayohusu rasilimali za nchi.

**1. Uzoefu wa nchi nyingine kuhusu katiba na mustakabali wa madini, mafuta na gesi asilia**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kutoa mifano michache juu ya uzoefu wa nchi nyingine ili kuionesha Serikali ni nini hasa kilitokea kwa wenzetu, ambao nao pia walikuwa na tatizo kama la kwetu. Nchi ya Norway ilianza uchimbaji wa mafuta na gesi asilia mwaka 1971 na kwa sasa Norway ni mojawapo ya nchi zilizofanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kuboresha uchumi na maisha ya wananchi wake kutokana na sekta ya mafuta na gesi asilia. Mafanikio ya Norway yalipatikana baada ya kubadili sera zilizokuwa zinatoa upendeleo kwa makampuni binafsi na kuweka sera zilizokuwa zinatoa kipaumbele kwa maslahi ya nchi na wananchi. Pamaja na hayo, Norway iliweka mafuta na gesi asilia katika katiba yake, ibara ya 110b na msimamo huo ukafafanuliwa zaidi na sheria ya mafuta. Huu ni mfano wa katiba na sheria kuwekwa kipaumbele na kutumika kama nyenzo ya kunyoosha nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Nchi ya Bolivia ni mfano wa pili ambao Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia inapenda kuutoa kwa nia na malengo yaleyale. Nchi hiyo ni miongoni mwa nchi ambazo zimejaliwa kuwa na utajiri mkubwa wa mafuta na gesi. Pamoja na utajiri huo, wananchi wa Bolivia kwa kipindi kirefu walikuwa na malalamiko kuwa mafuta na gesi asilia haziwanufaishi. Bolivia ilifanya mabadiliko ya sera zake lakini tofauti na Norway, mabadiliko ya Bolivia yalisababishwa na malalamiko na vurugu za wananchi waliokuwa wanataka mabadiliko.

**Mheshimiwa Spika**, kuanzia miaka ya 2000, nchi ya Bolivia ilishuhudia vurugu na maandamano zilizosababishwa

na kile kilichoitwa vita vyatia maji kutokana na kupinga kubinafishwa kwa maji na baadaye vurugu hizo zilihamia katika gesi asilia na mafuta. Aidha mwaka 2003 vurugu na maandamano makubwa dhidi ya sera mbovu zilisababisha aliyekuwa Rais wa Bolivia Gonzalo Sanchez de Lozada "Goni" kuijuzulu na kukimbilia Marekani. Hata hivyo alirithiwa na makamu wa Rais ambaye pia alilazimishwa kuijuzulu mwaka 2005 kwa maandamano kama mtangulizi wake.

**Mheshimiwa Spika**, mwaka 2006 Evo Morales alichaguliwa kuwa Rais wa nchi hiyo na aliongoza nchi hiyo kupata katiba mpya mwaka 2009 ambayo pamoja na mambo mengine ilihakikisha kuwa mafuta na gesi asilia yananufaisha wananchi wa Bolivia.

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania pia inayo madini, mafuta na gesi asilia kama zilivyo nchi ambazo mifano yake imeelezwa hapo juu. Ikumbukwe kwamba mwaka 2013 Tanzania ilishuhudia vurugu na umwagaji wa damu kwa wananchi wasiokuwa na hatia mkoani Mtwara zilisababishwa na mgogoro wa gesi ambao kiini chake ni madai ya wananchi kutokunufaika na rasilimali. Mchakato wa mabadiliko ya katiba ulibeba matumaini ya watanzania kwamba pamoja na mambo mengine nchi ingeweka misingi ya wananchi kunufaika na rasilimali ikiwemo madini, mafuta na gesi asili. Hata hivyo mchakato huo ulikwama na kupunguza matumaini ya wananchi. Serikali hii inayoongozwa na CCM inataka mpaka wananchi waanzishe migomo na maandamano ndio itambue kwamba katiba mpya ni kipaumbele cha wananchi katika masuala mengi ikiwemo juu ya rasilimali za nchi? Hivi ni lini Rais atatambua kwamba katiba na sheria ni zana muhimu za kunyoosha nchi? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Nishati na Madini kuwa mstari wa mbele kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha mchakato wa mabadiliko ya katiba unaendelezwa na masuala ya madini, mafuta na gesi yanapewa kipaumbele katika katiba mpya.

## 2. Ushauri wa kufanya katika kipindi hiki ambacho katiba mpya hajapatiakana

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Tanzania tunakabiliwa na changamoto katika sekta ya madini, mafuta na gesi asilia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapendekeza kwamba, Serikali ilete mbele ya Bunge lako tukufu marekebisho ya sheria ambayo yataweka misingi ifuatayo;

- Serikali isimamie shughuli za uvunaji wa madini katika mfululizo wake wote (entire production chain) kuanzia kwenye uchimbaji ili kuhakikisha kuwa madini yanatoa mchango katika maendeleo ya kiuchumi ya Taifa.
- Kuwepo kwa utaratibu wa kutoa leseni kwa njia ya zabuni ya wazi badala ya utaratibu wa mikataba kati ya Serikali na mwekezaji.
- Serikali iwe na makampuni yake yanayoweza kuingia katika ubia na makampuni au taasisi zingine au mjumuiko wa kampuni katika shughuli za uvunaji wa madini, mafuta na gesi asili Tanzania. Serikali pia imiliki hisa kutokana na thamani ya rasilimali zetu.
- Ili kupunguza mianya ya rushwa na kuongezeka kwa uwajibikaji katika mikataba, iwepo sheria inayotaka bunge kuridhia mikataba yote utafutaji na uvunaji wa Madini, Mafuta na gesi asilia.
- Serikali ihakikishe kwa niaba ya wananchi, Tanzania inanufaika na uvunaji wa madini, mafuta na gesi asilia, na usiwepo mkataba wowote unaokiuka misingi hii.
- Uvunaji wa madini, mafuta na gesi asilia uhakikishe unachangia kuboresha maisha ya jamii, ajira na kulinda mazingira, kuhakikisha pia maslahi ya Serikali kuu, halmashauri za wilaya, vijiji na waathirika wa uwekezaji mkubwa wan'anufaika na miradi iliyopo.

- Wananchi ambako uwekezaji utafanyika washirikishwe kuhusu maamuzi ye yeyote yanayohusu utafutaji, na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia na halmashauri zao zihusike katika umiliki kuititia hisa.

### **3. Makinikia ama “Mchanga wa Dhahabu” na Hatma ya Sekta ya Madini Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 24 Mei 2017 Mheshimiwa Rais Dr John Magufuli alipokea ripoti ya Kamati ya Kwanza ya Rais juu ya kusafirishwa nje kwa makinikia ya dhahabu/shaba. (Maarufu kama “Mchanga wa Dhahabu”). Aidha, wakati wa tukio la kukabidhi ripoti hiyo Mwenyekiti wa Kamati tajwa Prof Abdulkarim Mruma alieleza muhuktasari wa matokeo ya ripoti hiyo na Rais alitoa kauli mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Ni vyema ikafahamika kwamba makinikia haya yanahu su migodi miwili ya Bulyankulu na Buzwagi chini ya kampuni moja ya Acacia. Makinikia haya yanahu su takribani asilimia 30 ya dhahabu inayozalishwa katika migodi hiyo ambayo kwa sheria mbovu na mikataba mbovu ni mali ya mwekezaji. Huku stahili ya nchi ikiwa mrabaha wa asilimia nne (4%) tu. Ripoti hiyo ya makinikia ama ‘mchanga wa dhahabu’ haihusu mapato ya taifa na maslahi ya nchi katika asilimia 70 ya dhahabu inayopatikana katika migodi ya Bulyankulu na Buzwagi wala haihusu asilimia 100 ya dhahabu na madini mengine yanayopatikana katika migodi mingine nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Rais makini kabla ya kufikiria makinikia angefikiria kuhusu madini yanayochimbwa na kuchenjuliwa kwa ukamilifu hapa nchini lakini nchi haipati mapato yanayostahili. Hivyo, taarifa ya kamati ya Prof Mruma na kauli za Rais zimeiiingiza nchi na wananchi katika mjadala mdogo wa makinikia ama mchanga badala ya mjadala mkubwa madini na matatizo makubwa yaliyopo katika mfumo wetu.

**Mheshimiwa Spika**, katika muktadha kabla ya kutoa maoni kuhusu makinikia ama mchanga Kambi Rasmi ya

Upinzani inatoa mwito kwa Bunge na wananchi kujadili matatizo makuu ya sekta ya madini katika taifa letu. Matatizo makubwa katika sekta ya madini katika nchi yetu yamesababishwa na sera na sheria mbovu zilizotungwa chini ya Serikali inayoongozwa na CCM na mikataba mibovu ilioingiwa katika awamu mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, tunapojadili mathalani kukosa mapato kutoka mgodi wa Bulyankulu ni vyema tukakumbuka kuwa katika kipindi cha mwisho cha Rais Ali Hassan Mwinyi makampuni ya kigeni yalionegezeka kuingia katika nchi yetu. Kati ya makampuni hayo ni pamoja Kampuni ya Sutton Resources ya Vancouver, Canada, iliyopatiwa leseni kwa ajili ya eneo la Bulyanhulu/Butobelwa mwaka 1994. Leseni hiyo ilitolewa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete alipokuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini. Mara baada ya Rais Benjamin Mkapa kuapishwa mwaka 1995 iliandikwa fax baada ya Rais kuapishwa iliyokuwa na maneno “**our man has been sworn into office, now Bulyankulu file will move**”. Na kweli Mwaka 1996, wachimbaji wadogo wadogo walihamishwa kwa nguvu huku mengine wakidaiwa kufukiwa katika mashimo na kampuni ya Sutton Resources wakakabidhiwa eneo hilo. Yaliyofanywa Bulyankulu yalifanywa pia kwa namna nyingine katika maeneo mengine kwa nyakati tofauti tofauti ikiwemo Nyamongo, Mererani, Geita na Buzwagi.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuyawekea makampuni hayo mazingira halali ya kisheria ya ‘kunyonya rasilimali nchi’ Mwaka 1997, Bunge la Jamhuri ya Muungano lilitengeneza matatizo kwa kutunga sheria mbili mbovu kwa siku moja chini ya hati ya dharura. Kati ya sheria hizo ni Sheria ya Marekebisho mbali mbali ya Sheria za Fedha (Financial Laws Miscellaneous Amendments Act, 1997) ambayo ilifanya marekebisho makubwa katika sheria mbali mbali za kodi ambayo yalifuta kwa kiasi kikubwa kodi, tozo na ushuru mbali mbali kwa makampuni ya madini. Matokeo ya sheria hii ni miaka mingi ya kukosa mapato ya kutosha katika madini. Sheria nyingine ni ile ya Uwekezaji Tanzania (Tanzania Investment Act, 1997) ambayo iliyapa makampuni ya nje kinga

za kisheria za mambo ambayo mengine yanalalamikiwa kuhusu makampuni hayo mpaka sasa.

**Mheshimiwa Spika**, udhaifu katika mfumo mzima wa madini katika nchi yetu ukataasisishwa mwaka 1998 kwa Bunge kutunga Sheria ya Madini (Mining Act, 1998). Sheria hii kimsingi iliweka bayana kwamba madini yanayopatikana na fedha za mauzo yake ni mali ya mwenye leseni. Sheria iliruhusu makinikia ama mchanga kusafirishwa nje ya nchi kwa ajili ya usafishaji. Nchi yetu kupitia Sheria hii ilipaswa kulipwa mrabaha wa asilimia 3, sheria ya mwaka 2010 imeongeza tu kiwango kuwa asilimia 4.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine sheria zetu zinatoa wajibu wa makampuni hayo kulipa kodi ya mapato ya asilimia 30, hata hivyo ni baada ya kupata 'mapato yenye kuweza kutozwa kodi' (taxable income); yaani baada ya kupata faida. Sheria hizo mbovu zimeyaruhusu kwa muda mrefu makampuni ya madini kuondoa gharama zote za uzalishaji kabla ya kutangaza mapato ya kikodi. Makampuni hayo yametumia mianya hiyo na udhaifu wa taasisi za nchi yetu mathalani TMAA na TRA kuweka gharama zisizostahili na hivyo kutangaza kupata hasara na kutolipa kodi au kutangaza faida ndogo na kulipa kodi kiduchu. Rais makini alipaswa kabla ya kuzuia makinikia ama mchanga kudhibiti mianya kama hii ya upotevu mkubwa wa mapato katika madini. Mfumo huu wa 'kuepuka kodi' (tax avoidance) na 'kupanga kodi' (tax planning) ambao umeikosesha nchi mapato kwa muda mrefu umehalalishwa na sheria mbovu za nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya kuwa na sera bomu na sheria mbovu ni mikataba mibovu ambapo kwa upande wa Mikataba ya Uendelezaji wa Madini (MDAs) kati ya Serikali na makampuni makubwa, mikataba hiyo imeweka misamaha ya kodi na kuachia pia mianya ya uepukaji wa kodi. Mikataba hiyo mibovu imetoa misamaha ambayo mingine hata haipo katika sheria tajwa kwa mfano kwa halmashauri zilizo na migodi ya madini makampuni yameruhusiwa kutoa kiwango cha ujumla cha dola laki mbili

kwa ajili ya tozo ya huduma badala ya asilimia kati ya 0.14 na 0.3 ya mapato ya mwaka ya kampuni (annual turn over) ambayo yangetuwa malipo makubwa zaidi. Kwa nyakati mbalimbali tumeomba mikataba iletwe Bungeni ili ijadiliwe na kupitiwa upya hata hivyo Serikali imekuwa ikigoma. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuileta mikataba hiyo Bungeni na kuwezesha majadiliano ya marekebisho (renegotiation) kati ya Serikali na wawekezaji ili nchi na wananchi waweze kunufaika ipasavyo na rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu amelijalia taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, masuala haya hayakuzungumzwa na MwenyeKITI wa ‘kamati ya makinikia’ wala Mheshimiwa Rais wakati akipokea ‘ripoti ya mchanga’. Badala yake ilitolewa taarifa yenye kuonyesha kuwa katika makontena 277 yaliyopo bandari ya Dar Es Salaam kiwango cha dhahabu katika makontena yote ambacho ni cha mwezi mmoja tu wa uzalishaji kimetajwa kuwa tani 7.8 (au wakia 250,000). Kwa mahesabu rahisi tu ya kuzidisha kiwango hicho kwa kufanya makadirio ya mwaka na kujumlisha na uzalishaji mwingine wa migodi hiyo miwili ya Bulyankulu na Buzwagi tu kunaifanya Tanzania kuwa mzalishaji namba tatu wa dhahabu duniani!.

**Mheshimiwa Spika**, hapa kuna mwelekeo wa udanganyifu wa kitakwimu. Taswira hasi imeanza kujengeka kimataifa ambapo tarehe 25 May 2017 jarida la Mining Journal lilichapisha makala “*Trouble in Tanzania*” ambayo ilimalizia kwa mwito wa kufanya kwa ‘World Risk Survey’. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni taarifa kamili ya kamati hiyo ikiwemo metholojia iliyotumika kutathmini sampuli ijadiliwe na Bunge liweze kuazimia uchunguzi huru uweze kufanya kia.

**Mheshimiwa Spika**, lkumbukwe kuwa Serikali iliwhahi kuunda tume ambayo ilijulikana kama, tume ya Mheshimiwa Jaji Mark Bomani, ambayo ilipewa kazi ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa sekta ya madini. Aidha tume hiyo iligusia kipengele cha uchenjuaji na usafishaji wa Madini. Katika ukurasa 157 wa taarifa ya kamati ya Rais ya kuishauri Serikali

kuhusu usimamizi wa sekta ya Madini ya mwaka 2008 kamati ilisema na nina nukuu "*Kamati imechambua hali halisi ya shughuli za uchenjuaji na usafishaji (smelting and refinery) wa madini hapa nchini...na kuona kuwa shughuli hizi hazifanyiki katika kiwango cha kuridhisha. Aidha hakuna miundombinu hasa umeme na reli ya kuwezesha kuanzishwa kwa shughuli hizo. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa mkakati wa kisera wa kuhamasisha uwekezaji katika uchenjuaji na usafishaji wa madini hapa nchini*"

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hiyo inaendelea kuwa "*kamati ilibaini kuwa kukosekana kwa shughuli hizi hapa nchini kunazifanya kampuni kama vile Bulyankulu Gold Mine Limited kusafirisha mchanga (Copper Concentrate) kwenda Japan na China ili kuchenjuliwa. Hali hii isiporekebishwa, italazimisha mgodi wa Kabanga Nickel unaotarajiwa kuanzishwa kupeleka mchanga nje ya nchi kwa ajili ya kuchenjuliwa. Hii itaifanya Serikali kutokuwa na uhakika wa kiasi na aina ya madini yaliyomo katika mchangano huo na inaweza kuathiri mapato ya Serikali*". Kamati katika mapendekezo yake kwa Serikali, kuhusu kipengele hiki, ilipendekeza "*Serikali iweke mikakati katika sera ya madini na kutunga au kurekebisha sheria ya madini ili kuingiza vipengele vitakavyowezesha uanzishwaji na uimarishwaji wa viwanda vya uchenjuaji na usafishaji wa madini hapa nchini*". Rais Magufuli alikuwa mjambe wa baraza la mawiziri wakati taarifa hii inawasilishwa kwa Rais Jakaya Kikwete. Aidha, Rais Magufuli alikuwa na muda toka alipoingia madarakani kuweza kushughulikia jambo hili katika hali yenye kuepusha migogoro isiyo ya lazima. Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa mwito kwa Bunge kuingilia kuishauri na kuisimamia Serikali kwa mustakabali mwema wa sekta ya madini nchini.

#### **C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Nishati na Madini ilidhinishiwa jumla ya shilingi **1,122,583,517,000** na katika fedha hizo, shilingi **1,056,354,669,000** zilikuwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha hadi kufikia

tarehe 13 Machi, 2017 fedha zilizokuwa zimetolewa na hazina kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni shilingi 372,877,980,724 tu sawa na 35% ya fedha zote za maendeleo zilizotengwa kwa mwaka 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, ukiangalia takwimu zilizooneshwa hapo utabaini kwamba, miradi ya maendeleo ilitekelezwa kwa 35% tu. Miradi iliyokwama ni pamoja na ya umeme vijiji. Aidha Miradi hii inatekelezwa kwa kiwango hicho pamoja na sababu nyingine ni kutokana na Taifa hili kukosa fedha za wafadhili kwenye miradi ya umeme ikiwemo miradi ambayo ingepata ufadhili wa MCC. Kwa maneno mengine watanzania wameshindwa kunufaika na miradi ya maendeleo kutoka kwa wafadhili kutokana na kukosekana kwa utawala bora, kuvurugwa kwa uchaguzi wa Zanzibar na uvijifu wa haki za Binadamu.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Serikali iliwaaminisha watanzania kuwa miradi itatekelezwa kwa gharama za fedha za ndani katika kipindi cha Bajeti cha mwaka wa fedha 2016/2017. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata majibu ya kina, kuhusu sababu zilizopelekea Serikali kushindwa kutekeleza bajeti yake, huku ikijinadi ndani ya Bunge hili tukufu kwamba fedha za MCC hazina madhara na Taifa litatekeleza miradi kwa fedha zake! Je, kwa mwendo huu ni lini Taifa litafikia malengo tulioyojiwekea kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa?

#### D. SEKTA YA NISHATI

##### 1. Shirika la umeme Tanzania – TANESCO

i. Usimamizi wa kampuni Binafsi za uzalishaji umeme na gharama za kuiuzia TANESCO

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la umeme Tanzania, TANESCO katika jitihada za kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa uhakika wa umeme nchini, shirika liliingia mikataba na makampuni binafsi yanayozalisha umeme kwa lengo la kuiuzia TANESCO. Aidha taarifa ambazo kambi Rasmi

ya Upinzani Bungeni inazo ni kwamba, TANESCO inanunua umeme kwa bei ya wastani wa shilingi 544.65 kwa kila "unit" na kuza kwa shilingi 279.35 na hivyo kulifanya shirika kupata hasara ya shilingi 265.3 kwa kila unit.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kusitishwa kwa mkataba na kampuni ya Symbion, TANESCO ilikuwa inalipa jumla ya dola za Marekani milioni 16.36 kama capacity charge kwa makampuni yanayozalisha umeme wa dharura. Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Bunge lako Tukufu inazo zinaonesha kwamba Kwa sasa, Shirika linatumia Dola za Marekani milioni 9.75 kwa mwezi kununua umeme kutoka Aggreko, Songas na IPTL na gherama za umeme zinazolipwa na TANESCO kwa mwezi ni Dola za Marekani milioni 9.75.

**Mheshimiwa Spika**, Bei za nishati ya umeme inayotozwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) zinadhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) kila robo mwaka baada ya mapitio ya gherama halisi za uzalishaji. Aidha kwa mujibu wa tarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kuwa mapitio ya kila robo mwaka ya bei ya nishati ya umeme hayahusishi madeni yaliyojitezea kabla ya kuanzishwa kwa utaratibu wa mapitio ya bei ya umeme ya robo mwaka. Hivyo, utaratibu huu Mheshimiwa Spika, hauwezeshi TANESCO kulipa madeni yote inayodaiwa.

**Mheshimiwa Spika**, bei ya umeme inayopitishwa na EWURA haionyeshi gherama halisi zilizotumiwa na TANESCO jambo linaloathiri uwezo wa TANESCO katika kulipa madeni yanayolikabili Shirika. Kambi Rasmi ya Bunge lako Tukufu inaishauri Serikali kupitia EWURA kuzipitia kwa umakini gherama za umeme ili kuhakikisha kuwa gherama zote za uzalishaji wa umeme zinahusisha, ili hatimaye, kusaidia upatikanaji wa faida baada ya uwekezaji wenyе lengo la kuboresha huduma na kuongeza matokeo chanya kwa TANESCO.

**Mheshimiwa Spika**, shughuli za TANESCO zinahusisha pia utekelezaji wa mikataba mbalimbali ikiwemo iliyoridhiwa

kipindi cha Serikali za awamu zilizotangulia. Miongoni mwa mikataba hiyo ni ile iliyopigiwa kelele na watanzania kuwa ina harufu ya ufsadi na baadhi ikidaiwa kutokuwa na maslahi kwa Taifa. Mikataba hii inayohusu ununuzi wa umeme ni ghali kwa unit kiasi cha kuipa wakati mgumu TANESCO kupata fedha za kujijendesha na wakati huo huo kuwauzia umeme watanzania kwa bei juu, hivyo inapaswa kupitiwa upya.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili tukufu pamoja na watanzania, ni lini TANESCO itapitia mikataba yote mibovu ya shirika hilo na ikibidi TANESCO kuachana na mikataba ile inayoongeza mzigo na gherama za uendeshajji wa shirika hilo?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Bunge lako Tukufu inaishauri Serikali mambo ya nyongeza yafuatayo:

i. Bei za umeme zinazopitishwa na EWURA zizingatie gherama halisi zinazotumiwa na TANESCO kuzalisha umeme au kununua toka kwa makampuni binafsi ya uzalishaji umeme kuliko hali ilivyo kwa sasa kwa kuwa shirika linaonekana kuendeshwa kwa kuficha ukweli kuliko uhalsia ambao hauwekwi wazi.

ii. Kwa kuwa miongoni mwa majukumu ya shirika hili ni pamoja na kufua na kuimarisha mitambo ya umeme ya shirika, kununua kutoka kwa wazalishaji binafsi na nchi za jirani, basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha manunuzi ya umeme toka kwenye makampuni binafsi ya uzalishaji umeme yanafanyika kwa **uwazi** na **ushindani** kama inavyotakiwa na sheria ya manunuzi ili kuiweesha TANESCO kununua umeme kwa bei nafuu.

iii. Ili kuhakikisha shirika linatimiza jukumu lake la kuwekeza kwenye miradi mipya ya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na kufanya tafiti za vyanzo mbalimbali vya nishati ya umeme kama vile nguvu za maji (hydropower), gesi asilia, makaa ya mawe (coal), jua na upepo; Serikali iliwezeshe

shirika la umeme nchini (TANESCO) ili iweze kuwekeza kwenye uzalishaji umeme wa bei nafuu hivyo kusaidia kuepukana na utaratibu wa kununua toka vyanzo vya gharama kubwa.

**ii. TANESCO kushindwa Kukusanya Madeni**

**Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni Mheshimiwa Rais alikaririwa akisema TANESCO wanapaswa kukusanya madeni wanayodai na akaenda mbali zaidi na kusema hata kama lkulu inadaiwa TANESCO ikate tu umeme. Aidha katika hali ya kawaida kauli hiyo ilitarajiwu iende sambamba na vitendo kwa Serikali pamoja na taasisi zake kulipa madeni ya shirika hilo kwa ukamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kuwa TANESCO inadai fedha nyingi ambazo hazijakusanya na hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 jumla ya deni la umeme kwa Serikali na taasisi zake zilifika Shilingi **bilioni 144.854**, sawa na asilimia 67.4 ya deni lote la umeme. Deni lilitlobaki kwa wateja binafsi ni Shilingi bilioni 70.063 sawa na asilimia 33. Ni wazi kuwa, kutokulipwa kwa madeni ya umeme na taasisi za umma na binafsi kunaathiri uwezo wa TANESCO kujidesha kwa ufanisi na kulipa madeni kwa wadaiwa wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wizara hii, kuliambia Taifa ni lini Serikali ilitoa maelekezo kwa taasisi zake kulipa madeni ya umeme kwa wakati na ni lini hasa deni hili la shilingi bilioni 144.8 litalipwa kwa TANESCO ili kauli ya Rais ionekene ni ya uhalisia na siyo matamko ya kufurahisha tu?

**iii. Wizara ya Nishati na Madini Kutolipa Deni la Kodi ya Pango kwa TANESCO**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaelewa kwamba Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini iliingia makubaliano na TANESCO ya kupanga jengo kwa muda wa miaka 10 kwa ajili ya matumizi ya ofisi kwenye jengo la TANESCO lilitlopo barabara ya Samora, jijini Dar es

Salaam. Aidha muda rasmi wa kuanza makubaliano hayo ilikuwa tarehe 1 Januari, 2013 kwa kodi ya Shilingi milioni 26.60 kwa mwezi. Hata hivyo, Kwa taarifa zilizopo Wizara hajjalipa kiasi chochote tangu mkataba uliposainiwa, kiasi ambacho hakijalipwa kimefikia Shilingi bilioni 1.12. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza ni lini Serikali itailipa Tanesco fedha hizo za pango?

**Mheshimiwa Spika**, Wizara imetenga fedha hizi kwenye fungu lipi kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kulipia deni la shilingi bilioni 1.12? Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, Serikali inapata wapi uthubutu wa kuiagiza TANESCO kuwakatia umeme wateja wake inaowadai wakati Wizara mama yake inadaiwa na TANESCO fedha nyingi kama hizo?

**iv. Miradi ya kuzalisha umeme kwa njia ya Maji na Jotoardhi**

**Mheshimiwa Spika**, miradi ya kufua umeme wa maji inakadirwa kuwa mionganoni mwa miradi ambayo umeme wake ni wa bei ya chini ikilinganishwa na uzalishaji wa umeme kwa kutumia mitambo inayozalisha umeme kwa kutumia nishati ya Mafuta. Pamoja na miradi ya kufua umeme ya Kakono- MW 87, mradi wa Malagarasi MW 45 na Mradi wa Rusumo – MW 80, lakini bado kuna miradi mingi ambayo Serikali halonyeshi jitihada zozote za kuikamilisha kwa wakati pamoja na kwamba miradi hiyo ilishatumia fedha za walipa kodi katika hatua za awali za utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Mpango wa pili wa Maendeleo wa Miaka mitano ni kwamba Serikali ilitarajiwa kuendeleza mradi wa kuzalisha 200MW wa Geothermal wa Ngozi- Mbeya. Takwimu zinaonesha kuwa ghamama za mradi huo ni shilingi bilioni 204.72 na kila mwaka hadi 2020/21 zilitakiwa kutengwa shilingi bilioni 40.94.

**Mheshimiwa Spika**, kama inavyojulikana kuwa mipango bila kuwa na bajeti ya utekelezaji ni sawa na hadithi tu. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze

Bunge, je kuna umuhimu kwa waheshimiwa wabunge kuendelea kurejea miradi ya umeme kama ilivyoorodheshwa kwenye kitabu cha Mpango wa awamu ya pili wa maendeleo ya miaka mitano huku Serikali ikiwa haitengi fedha kwa ajili ya utekelezaji?

**v. Ununuzi wa Transfoma kutoka nje ya Nchi**

**Mheshimiwa Spika**, TANESCO kwa kipindi kirefu wamekuwa wakinunua transfoma kutoka nje ya nchi wakati hapa nchini kuna kiwanda cha TANALEC kinachotengeneza transfoma hizo. Kwa mujibu wa Mkurungenzi wa kiwanda, Transfoma zao zina ubora wa Kimataifa na kwa sasa na wana matarajio ya kutengeneza Transforma ambazo hazitumii mafuta ili kuepukana na wizi wa mafuta kwenye Transforma wa mara kwa mara. Aidha aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Profesa Sospeter Muhongo alikaririwa akiliagiza Shirika la Umeme Tanzania TANESCO kuacha kununua Transfomer kutoka nje ya nchi na badala yake wanunue zinazotengenezwa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Katika ziara yake kwenye kiwanda cha utengenezaji transfoma cha TANALEC mkoani Arusha Waziri alionesha kushangazwa na kauli ya watendaji wa TANESCO kuwa transfoma zinazotumika nchini ni kutoka nje ya nchi. Aidha TANESCO kupitia kwa Meneja mauzo na masoko Kanda ya Kaskazini ilikiri kuwepo kwa changamoto hiyo na kwamba hali hiyo inasababishwa na sheria ya ununuzi kuwabana.

**Mheshimiwa Spika**, wakati TANESCO wakilalamikia sheria ya ununuzi kuwabana, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini alipotembelea kiwanda cha Kutengeneza Transforma cha TANALEC alipingana vikali na kauli ya watendaji wa TANESCO kuwa sheria ya manunuzi ndio inawakataza kununua Transforma hizo. Aidha Waziri aliagiza TANESCO kununua Transforma hizo ambazo wao wana hisa na kuhusu sheria za manunuzi kukataza kununua bidhaa zao wenywewe ni mbinu na rushwa zilizojaa katika zabuni za manunuzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu, inashangazwa na kitendo cha Serikali kwa kupitia Wizara ya Nishati na Madini kупингана na TANESCO kuhusu sheria ya manunuzi, wakati TANESCO wakisema kinachowafanya kununua transfoma kutoka nje ya nchi ni sheria ya ununuzi, Serikali kwa upande wao wanasesma hizo ni mbinu za rushwa zilizojaat katika zabuni za manunuzi. Kwa kuwa Serikali inakiri kuwepo kwa mbinu za rushwa katika zabuni za manunuzi, na kwa kuwa Serikali hii inasema ni Serikali ya viwanda lakini, Serikali yenye ikiwa hainunui bidhaa zinazotokana na viwanda vya ndani ya nchi; je ni lini Serikali itaacha maigizo haya na kuja na suluhihisho la tatizo hili kwa kuchukua hatua dhidi ya watendaji iliosema wanaendekeza mbinu hizo za rushwa?

## **2. Wakala wa nishati vijijiini- (REA)**

**Mheshimiwa Spika**, lengo la uanzishwaji wa REA liliikiwa ni kuwapatia wananchi waishio vijijiini nishati bora. Pamoja na umuhimu wa wakala huyu bado Serikali haijaonesha kwa vitendo kuwa ina nia ya kusaidia wakala huyu ili aweze kuimiza majukumu yake kikamilifu na hasa linapokuja suala la kuapatia fedha kama zinavyoombwa na zinavyopitishwa na Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kuwa Serikali imekuwa haitimizi wajibu wake wa kuipatia REA fedha kama zinavyotengwa na kuidhinishwa na Bunge hili, kwa mfano mwaka 2008/2009 zilipitishwa shilingi bilioni 20.00 lakini fedha zilizotolewa ni shilingi bilioni 12.06 sawa na 60%. Mwaka 2009/2010, fedha zilizopitishwa ni shilingi bilioni 39.55 na kiwango cha fedha zilizotolewa ni shilingi bilioni 22.14 sawa na 56%. Mwaka 2010/2011 kiasi cha fedha kilichotengwa ni shilingi bilioni 58.883 na kiasi cha fedha kilichotolewa ni shilingi bilioni 14.652 sawa na 25%, mwaka 2011/2012 kiasi kilichotengwa ni shilingi bilioni 71.044 na kiasi cha fedha kilichotolewa ni shilingi bilioni 56.748 sawa na 80%, mwaka 2012/2013 kiasi cha fedha kilichotengwa ni shilingi bilioni 53.158 na kiasi cha fedha kilichotolewa ni shilingi bilioni 6.757 sawa na 13%.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeamua kutoa takwimu hizo ili kuonesha kwamba tatizo la Serikali kutopeleka fedha kwa Wakala huyu pamoja na kwamba sasa fedha hizi zinatokana na fedha za wananchi kupitia ongezeko la shilingi 100 kwenye kila lita moja ya mafuta ya petroli kwa ajili ya nishati vijijini lakini bado fedha hazipelekwi kwenye miradi hiyo. Ni vyema sasa Serikali iwaambie watanzania sababu zinazosababisha kushindwa kupelekwa kwa fedha hizi kwa wakala huyu wakati wananchi wameshatoa fedha kwa ajili ya lengo hilo.

**Mheshimiwa Spika**, uzoefu kutoka kwenye awamu mbili zilizotangulia zinaonesha kwamba, Serikali imekuwa ikishindwa kupeleka fedha kwa ajili ya miradi ya REA kwa wakati na pale ambapo imekuwa ikipelekwa basi fedha hizo zimekuwa ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya mradi husika, hali inayosababisha miradi kushindwa kukamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, kucheleweshwa kupelekwa kwa fedha za miradi kunasababisha miradi pia kuchelewa kukamilika na kuchelewa kukamilika kwa miradi kwa wakati kunasababisha kuongezeka kwa gharama za miradi husika.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya wakala iliyotolewa Januari, 2017 takwimu zake zinaonyesha kuwa jumla ya miradi 13 inayoendelea kutekelezwa yenye thamani ya shilingi 1,210,050,878,902 kama mikataba yake ilivyosainiwa, hadi sasa fedha zilizotolewa na Serikali ni shilingi 1,019,957,110,048.20 na kiasi kilicho baki ni shilingi 190,093,768,854. Hiki ni kiasi kikubwa cha fedha, na ni miradi iliyoingiwa mikataba tu, lakini REA ina miradi mingi kwa kulingana na bajeti zilizopitishwa na Bunge pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, kitendo cha kuorodhesha miradi kumi na tatu tu inayoendelea kutekelezwa, maana yake ni kutaka kupimwa kwa kigezo kidogo na sehemu kubwa inayolingana na bajeti inayotengwa na miradi iliyopangwa

katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa isipimwe kwa kiwango cha fedha kilichotakiwa kutengwa.

i. **Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya umeme vijiji ni kwa awamu ya pili:**

**Mheshimiwa Spika**, kuna malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza kutokana na utekelezaji wa miradi ya umeme vijiji ni katika awamu ya pili ambayo Serikali imeeleza kuwa imekamilika. Baadhi ya mifano ya mapungufu kutoka maeneo mblimbali ni pamoja na mkoani Mara, mkandarasi kuweka transfoma zenye 50 kVA na ufungaji wake kutokamilika, badala ya transfoma yenye 100 kVA; Mkoani Morogoro kulikuwa na utekelezaji mdogo wa mradi ambapo ni 15.6% ya wateja wa umeme wa njia tatu waliunganishiwa umeme, huku kwa wateja wa njia moja waliounganishiwa umeme ni 29%. Aidha wakati utendaji wa mkandarasi huyu ukiwa hivi, mkandarasi inadaiwa alikuwa ameshalipwa karibia 69.6% ya fedha zote. Mapungufu mengine ni pamoja na kuongezwa kwa wigo kazi na mkandarasi bila idhini ya wakala wa umeme vijiji, transfoma 21 badala ya transfoma 10 ziliwekwa ambayo ni kinyume na mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, Huko Babati baadhi ya vijiji vilikosa umeme kutokana na TANESCO kushindwa kuidhinisha ombi la kutumika kwa nguzo zake za umeme; kasoro za kiufundi huko Arumeru; mgogoro wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro unaohusu ardhi inayodaiwa kuwa mali ya mamlaka ya viwanja vya ndege na hivyo kuathiri upatikanaji wa umeme kwa baadhi ya vijiji.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali, kutoa kauli juu ya hatua ilizochukua ili kurekebisha kasoro ambazo zilijitokeza katika utekelezaji wa REA awamu ya pili.

ii.      **Utekelezaji wa REA awamu ya Tatu**

**Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni wakala wa umeme vijijini REA umezindua mradi wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu, baada ya kukamilika kwa awamu mbili zilizotangulia, taarifa iliyotolewa kwa umma inaonesha kwamba mradi huu utajumuisha vijiji 7,873 katika mikoa yote na wilaya za Tanzania bara kwa utekelezaji wa kipindi cha miaka mitano.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na REA kuititia tovuti yake, wakala wa Nishati vijijini REA, ulikamilisha taratibu za zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kabambe wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu. REA kuititia taarifa hiyo uliwajulisha wakandarasi walioshinda kwamba hatua iliyokuwa inafuata ni kuwapatia barua za tuzo (Award Letters) na kusalni mikataba.

**Mheshimiwa Spika**, zabuni hizo zilihusu mradi wa REA awamu ya tatu, zinalenga kufikisha umeme wa gridi kwenye vijijini 3559 katika mikoa 25 ya Tanzania bara, kwa thamani ya zaidi ya Bilioni 900.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kwamba mradi huu unagharimu fedha nyingi za walipa kodi, takribani bilioni 900 lakini tayari kuna madhaifu mengi yameshajitokeza katika michakato ya dhabuni hizo. Taarifa ambazo kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imezipata kuhusu mapungufu katika mchakato wa zabuni za tenda ni pamoja na baadhi ya kampuni kupewa zabuni wakati hazijasajiliwa katika bodi ya usajili wa makandarasi; kampuni ambazo hazikusajiliwa na bodi ya wakandarasi lakini wakashirikiana na wabia ambaao ni wa madaraja ya chini na hawakustahili kupewa zabuni kubwa; baadhi ya makampuni yenyeye sifa sawa na makampuni yaliyopata zabuni kukosa zabuni hizo; baadhi ya makampuni kupewa zabuni wakati makampuni hayo hayana sifa za kupewa zabuni hizo na baadhi ya makampuni kupewa zabuni wakati makampuni hayo yalikosa sifa za uzoefu katika kazi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa zabuni zilizotangazwa makampuni yenyе sifa za moja kwa moja kwenye zabuni hizi ni makampuni yenyе sifa za daraja la kwanza. Makampuni yenyе sifa za daraja la kwanza hayana ukomo wa kiasi cha fedha zinazopaswa kulipwa kwenye kila kifungu. Daraja la pili kikomo cha fedha ni shilingi bilioni 2, daraja la tatu, shilingi bilioni 1.2, daraja la IV shilingi milioni 600, Daraja la V shilingi milioni 300 na Daraja la VI shilingi milioni 150.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepata zinaonesha kwamba, yapo makampuni yanayodaiwa kupatiwa zabuni katika mazingira yenyе utata na hivyo, Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu inaitaka Serikali kufanya uchunguzi juu ya makampuni hayo ili kuhakikisha fedha hizi za mradi wa REA III hazitumiki kwa makampuni yasiyo na uwezo wa kutekeleza miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Radi Service Limited ambayo iliingia ubia na kampuni za Njarita Contractor Ltd pamoja na kampuni ya Agwila Electrical Contractors Ltd, na walipata mafungu ya zabuni ya dola 991,971 za kimarekani na shilingi bilioni 7.393. Aidha wabia hao pia walishinda lot nyingine yenyе thamani ya dola milioni 3.787 na shilingi bilioni 25.61. Pamoja na ushindi wa kampuni hizi, zenyе ubia, taarifa za Bodi ya Usajili wa wakandarasi (CRB) zinaonesha kwamba, kampuni ya Radi ni ya daraja la II na III, kampuni ya Agwila kwa mujibu wa taarifa za CRB ni ya daraja la V, na kampuni ya Njarita Contractor, usajili wake ni wa daraja la V. Pale inapotokea kampuni zote wabia ikawa hakuna kampuni yenyе daraja la I, lakini zikawa zimeungana, zinaruhusiwa kuandika barua CRB ili zipatiwe kibali kabla ya kuomba zabuni. Kampuni zote hizi, pamoja na kuwa wabia hazikuwahi kuandika barua na kupewa kibali. Lakini pia pamoja na kwamba, kampuni hizi hazikusajiliwa kwa daraja la I, walipewa kazi ya mabillioni ya shilingi kwenye lots zote mbili zilizooneshwa hapo juu, kinyume na taratibu.

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni nyingine ya whitecity International Contractor Limited iliingia ubia na kampuni ya

Guangdong Jianneng Electric Power Engineering na kupewa zabuni ya lot yenye thamani ya dola milioni 2.9 za Marekani na shilingi bilioni 22. Wakati wabia hawa wakishinda zabuni hiyo, taarifa za Bodi ya Usajili wa Makandarasi zinaonesha kwamba, kampuni ya Whitecity International Contractor Limited imesajiliwa kwa kazi umeme daraja la IV, Majengo daraja la II, Civil daraja la IV na civil specialist daraja la II. Mbia mwenza, kampuni ya Guangdong Jianneng Electrical Power Engineering, kwa taarifa zilizopo hana usajili wowote kutoka bodi ya usajili wa makandarasi.

**Mheshimiwa Spika**, Zabuni nyingine yenye utata, ilitolewa kwa kampuni ya MF Electrical Engineering Limited ambayo iliingia ubia na kampuni ya GESAP Engineering Group Limited. Kampuni hizi kwenye lot ya kwanza wanalipwa dola milioni 5 pamoja na bilioni 23.748, lot ya pili walishinda zabuni yenye thamani ya dola milioni 3.852 za marekani na pia bilioni 19.899. Aidha taarifa kutoka bodi ya usajili wa makandarasi zinaonesha kwamba MF Electrical Engineering Limited usajili wake ni wa daraja la V, na kampuni ya GESAP Engineering Group Limited usajili wake kwenye maswala ya umeme ni wa daraja la II.

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Joe's Electrical Ltd iliingia ubia na kampuni ya AT & C Pty na L'S Solution Ltd, kampuni zote hizi hadi zinakabidhiwa barua za kusudio la kuwapa zabuni hazikuwa na usajili kutoka bodi ya usajili wa makandarasi, lakini pamoja na upungufu huo, REA waliweza kuwapatia lots mbili, lot ya kwanza ina thamani ya dola za kimarekani milioni 1.5 na shilingi bilioni 15.695 na huku lot ya pili ikiwa na thamani ya dola za kimarekani milioni 1.915 pamoja na shilingi bilioni 17.958. Ikumbukwe kwamba, ikiwa kampuni ya kigeni kama hii ya Joe's hata kama ina daraja la I, lakini akishakuwa na mbia mtanzania ambaye hana usajili, basi wanakosa sifa ya kupewa zabuni lakini, kama ambavyo inaonekana hapa, kampuni hii ilipewa zabuni ya ushindi wa lots mbili.

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Nipo Group Limited inausajili bodi ya usajili wa wakandarasi wa Daraja la V,

kampuni hii haina mbia lakini ilipewa zabuni yenyé thamani ya dola za kimarekani milioni 2.011 na kiasi kingine cha sh bilioni 15.545. Kampuni hii ilipewa zabuni hii ikiwa ni mara yake ya kwanza kufanya kazi za kiwango cha gridi na hivyo kama zilivyo kampuni nyingine pia uwezo wake unatiliwa mashaka.

**Mheshimiwa Spika**, ni vyema ikaeleweka kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi wazawa wala wageni kupewa zabuni za ujenzi, tunachotaka kuona ni taratibu zote zinazingatiwa. Hivyo, kutokana na uchunguzi huo makampuni yakayobainika kuwa yalipewa zabuni bila viwango ni vyema vigogo wote walio nyuma ya makampuni hayo wakajulikana na hatua zaidi zikachukuliwa.

**E. SEKTA YA GESI- NCHINI:**

**1. Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika**, Bomba la kusafirisha Gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam lilijengwa na Kampuni ya China Petroleum and Technology Development Company (CPTDC) kwa gharama ya takriban Dola za Kimarekani takriban bilioni 1.283 ambapo katì ya hiso, dola za Kimarekani bilioni 1.225 zilipatikana kama mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Exim ya China. Marejesho ya mkopo huo yalitegemea kupatikana kwenye mauzo ya gesi asilia baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa bomba na kuanza kutumika kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, kuna taarifa kwamba bomba la gesi lilijengwa kabla ya kutafuta wateja na kusainiana mkataba wa mauziano ya gesi asilia katì ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na wateja lengwa wa gesi asilia. Aidha mapungufu haya kwa vyovyote ile yanaathiri malipo ya mkopo kwa vile mauzo halisi ya gesi asilia yatakuwa chini ya kiwango cha makadirio ya awali cha futi za ujazo milioni 138.8 kwa siku (mmscf).

**Mheshimwa Spika**, taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepata zinaonyesha kwamba, kwa sasa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ndilo mteja mkuu wa gesi asilia; ambapo anatumia wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 kwa siku, sawa na asilimia sita (6%) tu ya ujazo wa bomba; ambapo, kiasi hicho ni pungufu futi za ujazo milioni 737.39 kwa siku ili kujaza bomba. Matumizi haya ni tofauti na makubaliano ya awali ambayo ilikua TANESCO liweze kutumia takribani futi za ujazo milioni 80 kwa siku kama ilivyokuwa kwenye makubaliano ya mkataba wa mauziano ya gesi asilia (GA).

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu inapenda kupata ufanuzi kutoka Serikali kuhusu jitihada ambazo Serikali imechukua ili kuhakikisha wateja zaidi wa gesi asilia wanapatikana ili mkopo uweze kulipwa kabla ya marekebisho ya ulipaji ambayo yataongeza gharama kubwa kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kwamba mkataba wa mauziano ya gesi asilia kati ya TPDC na TANESCO uko wazi kwamba TANESCO itatumia gesi asilia kwenye mitambo yake sita (6) ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi I, Kinyerezi II, Ubungo I, Ubungo II, Tegeta na Symbion kwa kima cha chini cha matumizi cha futi za ujazo milioni 80 kwa siku na futi za ujazo milioni 138.8 kwa siku kama kiwango cha juu. Hata hivyo, hadi sasa mtambo wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi I ndio pekee unaotumia gesi asilia kuzalisha umeme; na unatumia kiwango asilimia thelathini na nne (34%) ya kiasi cha gesi yote iliyolengwa kutumiwa na TANESCO.

**Mheshimiwa Spika**, Mitambo mingine mitano iliyokuwa imekadiriwa kutumia kiasi cha (66%) bado haijaanza kutumika; na haijulikani ni lini mitambo hiyo itaanza kutumia gesi asilia. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kwamba, TANESCO bado ina mikataba ya muda mrefu na wazalishaji wakubwa wa umeme ambao ni kampuni ya *Independent Power Tanzania Ltd (IPTL)* na *Songas*; ambapo mikataba yao inaisha mwaka 2022 kwa ule wa IPTL

na mwaka 2023 kwa Songas. Hii inaiongezea TPDC na TANESCO ugumu kwenye kutimiza vifungu walivyokubaliana kwenye mkataba wa mauziano gesi asilia (GA).

**Mheshimiwa Spika**, ni ushauri wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, mikataba ya makampuni yaliyotajwa hapo juu haina maslahi kwa taifa na hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazitaka TPDC, TANESCO na Wizara ya Nishati na Madini wajadiliane ni kwa namna gani mitambo ya uzalishaji umeme ya TANESCO itaweza kumalizika kwa haraka ili bomba la gesi litumike kwa ufanisi na kuweza kulipa mkopo wa bomba la gesi kutoka Benki ya Exim ya China kwa wakati.

Pia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliambila Bunge lako tukufu, Ni jitihada gani Serikali imefanya kutafuta wateja zaidi wa gesi asilia ili kuongeza mapato ya gesi na kuiwezesha TPDC kutimiza wajibu wa kulipa madeni?

## 2. TANESCO kudaiwa na TPDC Ankara za Mauzo kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 61.35

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kwamba mnamo tarehe 31 Oktoba 2013, TPDC na TANESCO walisainiana mkataba wa TPDC kuiuzia gesi asilia TANESCO. Katika mkataba huo pia, kulikuwa na makubaliano kwamba Serikali iweke dhamana benki kiasi kinachoweza kulipa mauzo ya gesi kwa miezi mitatu au zaidi kwa ajili ya TPDC huku dhamana hiyo ikitakiwa kuwapo hadi pale madeni yote ya TANESCO yanayohusiana na kuuziana gesi asilia yatakapolipwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sababu ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hajafahamu, Serikali haikuweka dhamana hiyo kinyume na makubaliano hayo. Aidha, hadi kufikia mwezi Desemba 2016, jumla ya deni la mauzo ya gesi asilia kiasi cha dola za kimarekani milioni 61.35, sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 133.4, kimelimbikizwa bila kulipwa na TANESCO.

**Mheshimiwa Spika**, hali ya TANESCO kuchelewa kuilipa TPDC, inasababisha TPDC kuchelewa kuyalipa makampuni yanazouza gesi. Na hivyo kuongeza hali ya sintofahamu kwenye ulipaji wa mkopo kutoka benki ya Exim ya China. Kuchelewa huku kwa malipo kunaweza kusababisha gharama zaidi za riba ambayo itatakiwa kulipwa na TPDC kwa wadai wake.

*Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni* inataka kufahamu nini mpango wa Serikali kupitia TPDC wa kuhakikisha inalipa madeni kutoka kwa wauzaji wa gesi na mkopo kutoka Benki ya Exim ya China ili kuepuka kulipa riba kubwa hapo baadaye.

### **3. Kuzuiliwa kuingia kwa Gesi ya Tanzania nchini Kenya**

**Mheshimiwa Spika**, Hivi karibuni, Serikali ya Kenya imepiga marufuku uingizwaji nchini humo wa gesi ya kupikia kutoka Tanzania. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati ya Kenya, Kenya ilipiga marufuku uingizwaji wa gesi kutoka Tanzania ndani ya siku saba kuanzia tarehe 24 Aprili, 2017. Uamuzi wa Kenya ni kinyume na misingi ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Tanzania na Kenya ni wanachama. Aidha kwa mujibu wa itifaki ya soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, bidhaa kutoka nchi wanachama zinaruhusiwa kusambaa ndani ya nchi wanachama wa Jumuiya hii.

**Mheshimiwa Spika**, Uamuzi wa Kenya kuzuia Gesi kutoka Tanzania ni uamuzi ambao kwa vyovyote vile unalenga kuvunja mkataba wa Jumuiya ya Afrika mashariki na kuwazuia watanzania wanaofanya bishara hii nchini Kenya, Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu, inaitaka Serikali kutoa ufanuzi ndani ya Bunge lako tukufu kuhusu

i. Hatua ambazo imechukua kwa kuhusisha Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuwanusuru watanzania wanaofanya biashara hii nchini

Kenya na kuhakikisha mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na pamoja na itifaki ya Masoko ya pamoja havivunjwi?

ii. Ikiwa Kenya inafanya hivyo kwa kulinda Bandari yao ya Mombasa, bidhaa zake za ndani pamoja na wafanya biashara wake, na kwa kuwa kwa kufanya hivyo Kenya imevunja mkataba na itifaki za soko la pamoja, je Serikali inachukua hatua gani za kisheria dhidi ya kitendo cha Kenya kuzuia bidhaa kutoka Tanzania na nini hatma ya bidhaa za Kenya zilizo kwenye soko la Tanzania?

**F. KIGUGUMIZI CHA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KURUHUSU UWEKEZAJI KATIKA UZALISHAJI WA UMEME KWA KUTUMIA NISHATI JADIDIFU (RENEWABLE ENERGY) KATIKA TEKNOLOJIA ZA UPEPO NA JUA (WIND & SOLAR ENERGY)**

**Mheshimiwa Spika**, kuna tatizo kubwa la uwekezaji katika uzalishaji wa nishati jadidifu kwa kutumia teknolojia ya jua na upepo, licha ya nchi yetu kuwa na rasilimali jua na upepo wa kutosha. Kutokana na uwepo wa rasilimali hizo, wapo wawekezaji ambao wameonyesha nia ya kutaka kuwekeza katika uzalishaji wa nishati hiyo, lakini Wizara ya Nishati na Madini imekuwa haitoi ushirikiano kwa wawekezaji hao, jambo ambalo linairudisha nyuma sekta ya nishati nchini.

**Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa umeme kwa kutumia teknolojia ya jua na upepo, unawenza kutoa mchango mkubwa wa umeme katika gridi ya taifa kwani tunazo rasilimali jua na upepo za kutosha kuliko hata majirani zetu. Nchi yetu inayo sera na sheria za kuendesha teknolojia hizi, lakini tunajuliza kwa nini Wizara inazuia sekta hii kuendelea?

**Mheshimiwa Spika, EWURA** wamefanya kazi iliyogharimu taifa ya kutengeneza kanuni za uzalishaji wa nishati jadidifu kwa wazalishaji wadogo (Small Power Producers – SPP Regulations) ambazo zilizokwisha kukamilika tangu July, 2016. Kanuni hizo zinaitwa "*the Second Generation Small Power Producers Regulations*" Regulation hizi

zimeainisha uzalishaji wa umeme katika teknolojia za upemo na juu katika makundi makuu matatu:

i. *Kiwango cha 0 - mpaka Mega Watt 1 (0 - 1MW)*

ii. *Kiwango cha kuanzia Mega Watt 1 - mpaka Megawatt 10 (1 - 10 MW)*

iii. *Kiwango cha kuanzia MegaWatt 10 na kuendelea.*

**Mheshimiwa Spika**, hizi kanuni za Second Generation Small Power Producers' ziliyofanyiwa kazi na **EWURA** zinaelekeza makundi yote matatu yaliyotajwa hapo juu kuzalisha umeme kwa kutumia teknolojia hizi na kuuza kwenye grid ya taifa kwa taratibu zilizoelekezwa kwenye sheria ya Umeme Sura 131 kama ifuatavyo:

**Kundi la 1: (0 - 1 MW)** litatumia "Feed-in Tarif inayopangwa na EWURA kwa kuzingatia ukokotoaji uliozingatia gharama za uzalishaji kwa teknolojia hizi ambazo ni chini kuliko teknolojia zingine zinazotumiwa na TANESCO kwa sasa isipokuwa teknolojia ya maji (hydro) ambayo imeathiriwa sana na hali ya "**tabianchi**"(climate change). Kwa kiasi kikubwa aina hii haina matatizo mengi kwa sababu inashughulikiwa na EWURA na TANESCO bila kulazimisha urasimu wa Wizara.

**Kundi la 2: (1 MW - 10 MW)** ambayo ndio inategemewa kuwa na mchango mkubwa katika kuongeza renewable energy kwenye grid ya taifa, sheria hii inaelekeza kufuata utaratibu wa "**Competetive bidding**"). Sheria hii itaipa Serikali/Tanesco kuchagua kwa kupitia zabuni za wazi, mwekezaji mwenye uwezo kiteknolojia, kifedha na mwenye kuahidi kuuza umeme kwenye gridi ya taifa kwa bei yenye maslahi kwa taifa kupitia SPPA (**Small Power Purchasing Agreement**).

**Mheshimiwa Spika**, Utaratibu huu ulishatangazwa na EWURA kwa wawekezaji wa teknolojia hizi wa ndani na nje kwa takribani Zaidi ya mwaka mzima sasa. Wawekezaji hawa hadi sasa wamekwisha kutumia gharama nydingi za kufanya maandalizi yaliyoelekezwa na EWURA kujiantaa kwa zabuni hizi; ikiwa ni pamoja na kufanya makubaliano ya Ardhi kubwa inayohitajika kwa miradi ya aina hii, na gharama nydingine nydingi zinazoambatana na uwekezaji wa miradi ya aina hii.

**Mheshimiwa Spika**, EWURA/na TANESCO wamekamilisha kazi yao na kukabidhi shughuli hii kwa Wizara ya Nishati na Madini ambayo kila wawekezaji wakiwafuata kuulizia kinachoendelea wanajibowi wasubiri. Hali hii inawakatisha tamaa wawekezaji wa teknolojia hizi, ambazo tunaamini zitaongeza umeme ulio rafiki kwa mazingira yetu kwenye gridi ya taifa, na umeme ulio na gharama nafuu ukillinganisha na wa kutumia mafuta. Miradi hii ndio inaweza kuwa **upgraded** kwa jinsi grid yetu ya taifa inavyokua na hatimae kufikia Megawatt 50 – 100 na kuendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangazwa na kitendo cha Serikali kuweka mkazo pekee kwenye miradi mikubwa ya upepo ya Singida na Makambako ambayo kiuhalisia haitakamilika hivi karibuni. Tafiti zinaonyesha kuwa hata wenzetu waliobobea katika teknolojia hizi walianza na miradi midogo midogo mingi ya 10 MW na ikawa **upgraded** taratibu hadi kufikia **giant wind farms and solar farms**.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Nishati na Madini iharakishe zabuni ya ushindani( **Competetive bidding process**) ya teknolojia hizi kama sheria ya EWURA inavyoelekeza ili kuwezesha kupatikana kwa teknolojia hizi tunazozihitaji kwa ukombozi wa wananchi wetu kwenye sekta hii ya umeme usioharibu mazingira.

**Kundi la 3:** Kwa mujibu wa sheria ya EWURA, EWURA haina udhibiti mkubwa. Mwekezaji ameachiwa uhuru wa kufanya majadiliano na TANESCO kuhusu **PPA (Power**

**Purchasing Agreement).**Lakini sheria inawataka wakashakubaliana wakasajili PPA hiyo EWURA. Uzoefu unaonyesha miradi hii itatuchukua nchi hii miaka minge kufanikiwa. Na mfano rahisi ni miradi mikubwa ya umeme wa upepo ya Singida na Makambako ambayo imegubikwa na migogoro mikubwa ya ardhi.

**Mheshimiwa Spia**, kwa kuzingatia taratibu za uzalishaji katika makundi yote matatu, wataalamu wengi wanashauri kuwa kipaumbele cha nishati jadidifu katika gridi yetu ya taifa kwa kutumia upepo na jua ni katika **Kundi la 2**, ambalo linaruhusu wawekezaji kuomba kufanya uzalishaji kwa kutumia zabuni za wazi – *competitive bidding*.

#### G. SEKTA YA MADINI

**Mheshimiwa Spika**, sekta ya madini inahusu utafutaji na uchimbaji wa madini. Nchi ya Tanzania imebarikiwa kuwa na utajiri mkubwa wa madini, lakini mchango wa sekta kwenye uchumi hauridhishi. Pamoja na maoni ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tumeyatoa kupitia hotuba hii kwenye kipengele kuhusu makinikia ama ‘mchanga wa dhahabu’ yapo masuala ya ziada ambayo ni vyema Wizara ya Nishati na Madini ikayatolea majibu kama ifuatavyo.

#### 1. Mapungufu katika Mikataba ya uchimbaji Madini

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi kirefu yamekuwepo malalamiko yanayohusu mikataba ya uchimbaji madini ambayo Serikali iliingia na wawekezaji wa makampuni ya uchimbaji wa madini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kwamba baadhi ya mikataba ya madini ilioingiwa kati ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania na makampuni ya madini ni pamoja na mikataba kati ya kampuni ya Geita Gold Mining (GGM) inayoendesha mgodi wa dhahabu wa Geita, na Kampuni ya ACACIA inayoendesha migodi ya Buzwagi, Bulyanhulu na Mara Kaskazini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kwamba, mikataba ya madini mingi ina vifungu visivyo linda maslahi ya umma, vifungu hivyo ni pamoja na vile vinavyoweka masharti yasiyoridhisha katika kuongeza mikataba, vifungu vinavyozuia mabadiliko ya sheria kuathiri mikataba husika, sera zisizoridhisha kwenye fedha za kigeni na forodha, motisha za kodi zilizozidi, kwenye taratibu za kihasibu katika kutambua na kukokotoa matumizi ya mitaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na mapungufu hayo yaliyoko kwenye mikataba ya uchimbaji wa madini, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali;

i. Kuacha kulalamika na badala yake itumie kifungu kinachoruhusu kurejewa kwa mikataba kinachopatikana kwenye mikataba mingi ya madini ili kurejea makubaliano yaliyoafikiwa na kuhakikisha kuwa Serikali inajiepusha na kutoa matamko ya potofu ambayo yanaenda kinyume na matakwa ya mikataba husika.

ii. Aidha ili kuhakikisha maslahi ya Taifa na maslahi hayaathiriki ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa Serikali iyaite makampuni ya wawekezaji kwenye madini na kujadiliana nayo jinsi ya kufanya marekebisho yanayohitajika.

iii. Serikali iboreshe usimamizi kwa makampuni binafsi yanayofanya kazi za kutafuta na kuvumbua miamba yenyé madini ili kuiwezesha Serikali kuwa na taarifa sahihi na za ziada zitakazoisaidia kwenye majadiliano na kufanya maamuzi.

## **2. Madhaifu ya sheria za kukusanya mapato kwenye sekta ya Madini**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi kirefu Taifa hili linakosa mapato yanayotokana na rasilimali za Taifa kutokana na sababu mbali mbali, ambazo mionganoni mwake ni sababu zinazotokana na madhaifu ya sheria zetu. Aidha mionganoni

mwa sheria ambazo zinachangia Taifa kukosa mapato kwenye sekta ya Madini ni pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Kwa mujibu wa sheria hii, kifungu cha 55(1) cha sheria hii, kinatoa mwanya kwa migodi ya uchimbaji wa madini kupewa marejesho ya Kodi ya VAT. Sheria hii, sawa na sheria za zamani kwa pamoja zinaruhusu tozo ya kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha sifuri kwa bidhaa zinazosafirishwa kuuzwa nje ya nchi.

**Mheshmiwa Spika**, Ni wazi kwamba soko kubwa la Madini liko nje ya nchi na kwa sababu hiyo madini yote yanayopatikana yanauzwa nje ya nchi. Hii inapelekea kodi inayotokana na manunuzi ya bidhaa za mtaji, mafuta na gharama nyingine yanayofanywa na makampuni ya migodi ndani ya nchi kuzidi ile inayotokana na mauzo (Output Tax). Hivyo, migodi hiyo kustahili marejesho ya kiasi kilichozidi kutokana na kifungu cha 83(2) cha sheria ya Kodi ya ongezeko la Thamani.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la Serikali kutoza kodi ya ongezekeo la thamani kwa kiwango cha sifuri kwenye bidhaa zote zinazosafirishwa kuuzwa nje ya nchi ilikuwa ni kukuza viwanda vya ndani. Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inazo zinaonesha kwamba migodi mikubwa minne (4) ya dhahabu Geita, Bulyanhulu, Mara Kaskazini, Pangea na mmoja wa Almasi wa Williamson kwa kipindi cha miaka minne mfululizo kuanzia Mwaka 2012 ilirejeshewa marejesho makubwa ya kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,144.

Mapungufu yanayoonekana ni kwa Sheria hiyo kutokuweka makundi ili kuonyesha ni bidhaa zipi zinazostahili motisha hiyo na hivyo kusababisha madini ambayo kwa namna yoyote lazima yauzwe nje ya nchi nayo pia kunufaika na motisha hiyo kama vile ambavyo bidhaa za kilimo na viwandani zinavyonufaika. Kambi Rasmi ya Bunge lako Tukufu inaitaka Serikali kutoa ufanuzi kuhusu;

i. Ni lini hasa Serikali italeta ndani ya Bunge lako tukufu Mabadiliko ya sheria ya Ongezeko la thamani VAT ili

kuondoa tozo ya kiwango cha sifuri kwenye mauzo ya madini na vito nje ya nchi kwa kuweka makundi yanaoonesha ni bidhaa zipi zinazostahili motisha ya tozo ya kiwango cha sifuri na kuziacha bidhaa za kilimo na Viwanda zikiendelea kunufaika?

ii. Kwa kuwa mabadiliko ya sheria hii, yataathiri mikataba iliyopo kati ya Serikali na makampuni ya Uchimbaji Je, Ni lini Serikali itaanzisha majadiliano na makampuni ya uchimbaji madini kuhusu matokeo ya mabadiliko hayo kwenye Mikataba yao (MDAs)?

### **3. Utofauti wa Kodi kwenye sekta ya Madini.**

**Mheshimiwa Spika**, Sote tunafahamu kwamba mikataba ya uchimbaji madini kati ya Serikali na makampuni ya uchimbaji katika migodi ya dhahabu ya Mara Kaskazini, Geita, Buzwagi na Bulyanhulu ilisainiwa kabla Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 haijatungwa, isipokuwa mkataba wa uchimbaji wa mgodi wa dhahabu wa Buzwagi uliosainiwa 2007. Kwa muktadha huo viwango vya tozo za kodi katika mikataba hiyo vilitokana na sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 1973 na havijabadilishwa kuendana na sheria mpya kutokana na kuwapo kwa kifungu kinachozua mabadiliko ya viwango vya tozo za kodi kwenye mikataba hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Ifuatayo hapa chini ni baadhi ya mifano inayotokana na baadhi ya maudhui ya mikataba hiyo;

i. Mikataba hiyo inaainisha viwango vya zuio la kodi katika ada ya usimamizi pamoja na huduma za kiufundi kati ya asilimia 3 mpaka 5. Hali hii ni tofauti na matakwa ya Sheria ya Kodi ya Mapato ambayo inataka viwango vya zuio la kodi katika ada ya usimamizi pamoja na huduma za kiufundi kuwa asilimia 15.

ii. Mikataba hiyo pia inataka ushuru wa halmashauri ulipwe kwa kiwango kisichozi Dola za Kimarekani 200,000 kwa mwaka. Takwa hili pia ni kinyume

na kifungu cha 6 (1) (u) cha sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 inayotaka ushuru wa ndani ulipwe kwa kiwango cha asilimia 0.3 ya mauzo ya mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mifano tajwa hapo juu ni *ushauri wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa Serikali inapaswa kujadiliana na makampuni ya uchimbaji madini kuititia kifungu cha utakaso wa mkataba kinachopatikana kwenye mikataba takribani yote ili kurekebisha viwango vya tozo za kodi kwa kuzingatia vigezo vya kiuchumi vinavyobadilika kufuatana na muda tangu kusainiwa kwa mikataba hiyo na hivyo kuliwezesha Taifa kupata mapato yanayostahili kulingana na rasilimali hii.*

#### **4. Misamaha ya tozo na Ushuru, sekta ya Madini.**

**Mheshimiwa Spika**, Misamaha kwenye tozo na ushuru wa mafuta ilitolewa kwa makampuni ya madini ili kuyapunguzia ghamraza za uzalishaji umeme kwa ajili ya kuendeshea mitambo. Kifungu cha 8 cha Sheria ya Tozo za Ushuru wa Mafuta na Barabara ya mwaka 1985 kinampa Waziri wa Fedha mamlaka ya kutoa msamaha wa tozo ya ushuru wa mafuta kwa kutangaza kwenye gazeti la Serikali. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kwamba Serikali, kuititia gazeti la Serikali Namba 190 lilichapishwa tarehe 15 Julai 2011, ilitoa msamaha wa tozo ya ushuru wa mafuta kwenye mafuta yanayoagizwa au kununuliwa na makampuni makubwa ya madini yanoyojihusisha na uchimbaji wa dhahabu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa toleo hilo, Serikali pia ilibatilisha matoleo yote yaliyowahi kutolewa awali kuhusu misamaha ya kodi; na tangazo hilo likaweka utaratibu wa kutumiwa na makampuni husika ili kuweza kupata msamaha huo. Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kwamba migodi mikubwa minne ya Geita Gold Mine, Bulyanhulu, Buzwagi na Mara Kaskazini inayojihusisha na uchimbaji wa dhahabu nchini imesamehewa tozo za ushuru wa ndani na mafuta kiasi cha shilingi bilioni 126.7 kwa mwaka 2015 na 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia ushauri iliota kwenye mgodi uliochini ya STAMICO kwamba, Serikali, kupitia Wizara ya Nishati na Madini na Shirika la Umeme Tanzania TANESCO, kuhakisha inapeleka umeme kwenye migodi mikubwa nchini ili kuiondolea Serikali sababu za kusamehe kodi kwenye mafuta. Kitendo cha kuipelekea migodi umeme, kitasaidia kuongeza mapato kwenye Serikali yatayotokana na kuuza umeme kwenye makampuni hayo.

#### **5. Misamaha ya kodi za Mafuta yanayonunuliwa nje kwa matumizi ya uchimbaji wa madini: 1URAYA Ta yaN**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 190 na 191 la mwaka 2011 na jedwali la tatu la sheria ya kodi ya ongezeko la thamani ya mwaka 1997 limetoa msamaha wa malipo ya ushuru wa bidhaa, ushuru wa mafuta, na kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta yanayoingia kwa lengo la kutumika katika migodi kwa ajili ya uchimbaji wa madini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa zinazoeleza kwamba mafuta yamekuwa yakisafirishwa kutoka bandari ya Dar es Salaam kuelekea kunakodaiwa kuwa ni kwenye migodi ya uchimbaji wa madini lakini hakuna uthibitisho unaoonesha kwamba mafuta hayo yalifika katika migodi ya Buzwagi na Bulyanhulu. Aidha Sehemu ya 2(g) ya jedwali la Tangazo la Serikali namba 190 na 191 la mwaka 2011 inasema kwamba tofauti yoyote inayosababishwa na kutokupokea mafuta yaliyotoka katika makampuni ya masoko ya mafuta, ukaguzi, matumizi ya mafuta kwa mtu mwagine zaidi ya makampuni ya migodi au matumizi yoyote yasiyokusudiwa yanatakiwa kutozwa kodi itakayokatwa kutoka kwenye akaunti ya escrow. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kufahamu hatua ambazo Serikali inachukua ili kuthibiti tabia hii ambayo inasababisha ukosefu wa mapato yanayotokana na kutolipiwa ushuru wa forodha.

**Mheshimiwa Spika**, kuna taarifa pia zinazohusu mapungufu yaliyojiteza katika uondoshaji wa mafuta ya

migodini kwa kutumia maghala yanayohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi. Ikumbukwe kwamba, Kifungu 74-75 cha Kanuni ya Ushuru wa Forodha Afrika Mashariki ya mwaka 2010 inahitaji mlipa kodi kupata leseni na kutimiza masharti yote yaliyoainishwa katika kifungu 74(1-4) na 75(1-2) ili kuweza kuendesha ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi. Zaidi ya hayo, kifungu 76 kinahitaji mmiliki leseni wa ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi kutekeleza dhamana kwa bidhaa zinazohifadhiwa katika ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi

**Mheshimiwa Spika**, taarifa zaidi zinasema kwamba lita 3,500,000 za mafuta ya petroli yaliyonunuliwa na kampuni ya mafuta ya Oryx na yaliondoshwa kupitia TANSAD yenye kumbukumbu namba TZSR-14-1171746 ya tarehe 10/12/2014. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka ufanuzi kuhusu maswala yafutayo:

i. Kama Serikali inaouhakika na ushahidi kwamba M/S Oryx Oil Company Limited ilikuwa na leseni ya kuendesha ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi;

ii. Serikali inasema nini kuhusu mizigo iliyookolewa chini ya usimamizi wa ghala linalohifadhi bidhaa zinazosubiri kulipiwa kodi bila dhamana kinyume na kifungu 76 cha Kanuni ya ushuru wa forodha Afrika Mashariki ya mwaka 2010;

iii. Serikali inao uhakika na ushahidi kama lita 49,046 za mafuta ya petrol zilihamishwa kwenda kampuni ya migodi (North Mara) na kampuni ya mafuta ya Oryx; na kama sivyo, inachukua hatua gani kwenye jambo hili.

iv. Kwa kuwa taarifa zinasema kwamba Oryx ndiye muingizaji wa mafuta; na siyo North Mara ambaye alifuzu kupata msamaha wa kodi, Serikali imechukua hatua gani dhidi ya Oryx?

**6. Kampuni ya STAMICO na mgodi kutopatiwa umeme na TANESCO.**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kuititia STAMICO, ilichukua mgodi wa dhahabu wa Tulawaka kutoka kampuni ya Afrikan Barrick Gold (ABG). Mkataba wa kuhamisha umiliki ulifikiwa tarehe 15 Novemba, 2013 na jina la mgodi likabadilika toka mgodi wa Tulawaka kwenda mgodi wa Biharamulo. Hata hivyo ili kuendesha mgodi, STAMICO iliunda kampuni mpya kwa jina la STAMIGOLD.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa taarifa zilizopo kuhusu ufanisi wa mgodi chini ya usimamizi wa kampuni ya STAMIGOLD ni kwamba, Wizara ya Nishati na Madini imechelewesha ruhusa ya Leseni Kubwa ya Uchimbaji Madini kwenda STAMIGOLD. Kwa mujibu wa Kifungu cha 9(2) cha Sheria ya Madini ya 2010 kunahitaji kuwepo kwa kibali cha maandishi kutoka Wizara ya Nishati na Madini kabla umilikishwaji wa leseni kubwa ya kuchimba madini haijaamishwa kutoka kwa kampuni moja kwenda nytingine. Taarifa zinaonesha kuwa baada ya STAMIGOLD kuchukua mgodi walihitaji pia kurithi mkataba uliokuwepo awali kati ya Afrikan Barrick Gold (ABG) na Serikali ili nao waweze kupata faida na motisha alizokuwa anapata muendeshaji wa awali.

**Mheshimiwa Spika**, kuchelewesha kutoa kibali cha kuhamisha leseni ni kuwanyima haki STAMIGOLD kutumia fursa kama vile misamaha ya kodi zinazopatikana kwenye mkataba waliorithi kutoka African Barrick Ltd kuna athari za kiutendaji kwa Kampuni hii ya Umma ukilinganisha na manufaa wanayopata makampuni binafsi kwa mfano msamaha wa kodi ya mafuta (Fuel levy & excise duty)

**7. Mgodi kutopatiwa umeme na TANESCO**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na hitaji la muda mrefu la mgodi kuunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa na au kupatiwa umeme kutoka shirika la umeme nchini TANESCO bila mafanikio. Aidha kwa sasa mgodi unatumia umeme unaozalishwa kwa kutumia majenereta. Taarifa ya

kila mwezi ya uendeshaji mgodi inaonyesha kuwa mahitaji ya umeme kwa mwezi mgodini ni takriban kilowati milioni 1.1 ambazo zinazalishwa na lita 300,000 za mafuta ya dizeli ambayo inagharimu takriban shilingi milioni 670. Kwa Uchambuzi uliofanywa na STAMIGOLD unaonyesha kuwa hizo kilowati zinazohitajika kama zikipatikana kutoka TANESCO, gharama zake ni takribani shilingi milioni 273.79 (gharama ikihusisha tozo zote zilizopo kwenye umeme kama VAT (18%) REA (3%) na EWURA (1%)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kutumia umeme wa TANESCO, STAMIGOLD itaokoa karibia nusu ya gharama inazoingia sasa kuzalisha umeme wa mafuta.

Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu inapenda kupata ufanuzi kutoka Serikalini kuhusu mgodi huu kama ifuatavyo:

i. Ni lini Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini itakamilisha mchakato wa kuipatia STAMIGOLD kibali cha kutumia mkataba wa kuchimba madini aliokuwa anautumia Afrikan Barrick Gold (ABG).

ii. Kwa kuwa mgodi huu ukiunganishwa kwenye gridi ya Taifa, kutasaidia kupungua kwa gharama hizi na kupelekeea mchango chanya kwenye faida ya kampuni na mapato kwa taifa. Je, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, itaunganisha lini mgodi wa STAMIGOLD kwenye gridi ya taifa ili kuupunguzia gharama za kuijendesha; na hivyo, kuuongezea fursa ya kupata faida kwa mgodi huu?

iii. Kwa kuwa migodi mingine mikubwa na ya kati inapata msamaha wa kodi ya mafuta (fuel levy & excise duty) Je, Serikali itatoa lini msamaha huo ili mgodi huu upate msamaha sawa na migodi mingine?

## **8. Mgodi wa MMG Gold Ltd**

**Mheshimiwa Spika,** kuna Mgodi unaoitwa MMG Gold Ltd, upo kwenye kijiji cha Seka, Jimbo la Musoma Vijijini kilometra zipatazo 42 kutoka Bunda mjini, ukiwa unaelekea

upande wa Ziwa Victoria. Kimsingi, mgodi upo karibu sana na Ziwa, hata maji ya kufanya shughuli zake wanavuta kutoka ziwani. MMG Gold Ltd ni Kampuni Tanzu ya Kampuni ya MUTUS LIBER INTERNATIONAL LTD (MLI) yenyeye makao yake makuu Dubai –Falme za Kiarabu na inafanya kazi zake nchini Ghana, Djibouti, Kenya, Madascar na Oman.

**Mheshimiwa Spika**, uendeshaji wa mgodi huo bado unaendeshwa kama vile ni mgodi wa wachimbaji wadogo wadogo, kwa maana kwamba watumishi/wafanyakazi wao hawapo kwenye mfumo wa hifadhi za jamii, hawakatwi kodi ya mshahara na hivyo Serikali kupoteza mapato yake. Na mbaya zaidi ni kwamba “Gold Pregnant Carbon” zinaenda kuchomwa Mwanza kinyemela na hivyo kutokuwemo kwenye mfumo rasmi wa ukaguzi wa Wakala wa Madini (TMAA).

**Mheshimiwa Spika**, Mgodi huu bado ni mpya na kama taasisi zetu za ukaguzi na uthibiti utashindwa kufanyakazi kama inavyotakiwa ni dhahiri kabisa, tutakuwa tunaambiwa kwamba mgodi unazalisha hasara na hivyo wanashindwa kulipa kodi ya makampuni. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kwamba yale yote yanayoendelea katika Mgodi yanafahamika na Wizara hivyo tunaitaka Serikali ilieleze Bunge hadi sasa utendaji wa mgodi huo ukoje na kodi ya wafanyakazi (PAYE) inalipwa kwa kiwango gani?

## **9. Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira:**

**Mheshimiwa Spika**, Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira kwa sasa unamilikiwa na Serikali kuititia STAMICO. Kabla ya mwaka 2005, mgodi huu ulikuwa chini ya usimamizi wa STAMICO. Lakini kufuatia sera ya ubinafsishaji ya Chama Cha Mapinduzi, mwaka 2005, 70% za umiliki wa mgodi huu zilihamishiwa kampuni iitwayo ‘Tan Power Resources Ltd’. Mwaka 2008 hisa zikachukuliwa na Serikali kuititia Msajili wa Hazina na umiliki wa mgodi huu ukarudishwa chini ya STAMICO mwaka 2014. Kwa taarifa ambazo kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kwamba Mgodi wa Makaa ya

Mawe Kiwira haujaanza tena kuchimba makaa ya mawe tokea ulipochukuliwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa mbalimbali zinaonesha kuwa mgodi wa Kiwira unakumbana na vikwazo vyta Kisheria, kwa mfano ipo changamoto inayohusu cheti cha hisa cha Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira (KCML) ambacho bado hakijahamishiwa STAMICO; na hivyo cheti hicho bado kinasomeka kwa jina la Tan power Resources Ltd. Kwa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kwamba, hali hii imesababishwa na kitendo cha Mamlaka ya Mapato Tanzania kutotoa hati ya kuthibitisha ulipaji wa kodi (tax clearance certificate) kwa kampuni ya Tan power Resources.

**Mheshimiwa Spika**, madhara ya kutobadilishwa kwa jina hilo, kulipelekea Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kwa mujibu wa kifungu 18(2)(b) cha Kanuni za Ukaguzi na Tathmini ya Athari za Mazingira (the Environmental Impact Assessment and Audit Regulations) 2005, kuikataa taarifa ya Tathmini ya Athari za Mazinigra ya STAMICO (Environmental Impact Assessment (EIA) report) kwa sababu hati ya hisa za kampuni hii ilikuwa bado inasomeka kwa jina Tan Power Resources Ltd.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kukosekana kwa hati ya umiliki yenye jina la STAMICO inakwamisha juhudzi za shirika kuendeleza mgodi na pia inawia vigumu shirika kuingia ubia na wawekezaji wengine, Je Serikali, kupitia ofisi ya Msajili wa Hazina na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), inafanya juhudzi gani kuhakikisha hati ya kutodaiwa inapatikana na hati hiyo ya hisa inatolewa kwa jina la STAMICO.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto za kiutendaji zinazoukabili mgodi wa makaa ya mawe ya Kiwira ni pamoja na ukweli kwamba toka mgodi huu uhamishwe STAMICO mwaka 2014, hakuna fedha za maendeleo zime wahii kupelekwa. Suala hili limesababisha kushindwa kuanza kuzalisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu inataka kufahamu ni lini Serikali itapeleka fedha katika mgodi huu kama ambavyo zimekuwa zkipangwa lakini hazipelekwi huko? Pia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka majibu kujuu ni lini Kiwira Italipa shirila la umeme TANESCO deni la muda mrefu la kiasi cha shilingi bilioni 1.8.?

#### 10. Mgodi wa Cata Mining Company

**Mheshimiwa Spika**, kuna kampuni ya uchimbaji madini inayoitwa CATA MINING COMPANY LTD yenye Mining License Na. 483/2013, inayofanya shughuli zake katika eneo la Kiabakari, Wilaya ya Musoma Vijiji. Kampuni hiyo iliyokuwa na leseni 16 za uchimbaji mdogo (Primary Mining License-PML) zilizokuwa zinamilikiwa na Ndugu MAHUZA MUMANGI NYAKIRANG'ANI.

**Mheshimiwa Spika**, wananchi wa vijiji vya Kiabakari na Nyamisisye wanalamika kuhusiana na uharibifu wa nyumba zao takriban mia saba (700) uliotokana na milipuko ya baruti za kupasua miamba na hivyo kupata hasara kubwa sana. Aidha, wananchi hao wanatuhumu pia kwamba sehemu ya uchimbaji huo unafanyika ndani ya Kambi ya Jeshi la Wananchi Tanzania. Kwa mujibu wa ramani ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani inayo nakala eneo la uchimbaji linaonekana kuwa ni kijiji cha Kyawazaru/Katario na Kitongoji cha Kyarano na si eneo la jeshi lilitoko kijiji cha Nyamisisye.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa kwamba Wizara ya Nishati na Madini ilishapewa malalamiko hayo lakini hajayapatia ufumbuzi unaostahili. Hivyo, Waziri atoe maelezo Bungeni ni kwanini ameshindwa kumaliza mgogoro huo mpaka sasa?

#### 11. Wachimbaji wadogo wadogo

**Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa changamoto zilizoko katika sekta hii ni pamoja na changamoto zinazowahu wachimbaji wadogo wadogo. Pamoja na maelezo ya Serikali kuhusu hatua ambazo Serikali imekuwa

ikichukua dhidi ya kundi hili lakini bado uchimbaji mdogo wa madini umekuwa ukiendelea kwa kutumia nyenzo na teknolojia duni ya uchimbaji na kukosa taarifa sahihi za mashapo katika maeneo wanayochimba. Pamoja na kutengwa kwa maeneo machache ya wachimbaji, kupewa leseni za uchimbaji lakini bado wachimbaji wadogo wadogo wanapewa maeneo ya kuchimba bila kuwa na uhakika wa uwepo wa madini kwenye eneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa wakipata mikopo kidogo kwa ajili ya kuendeshea shughuli za uchimbaji na kwa kuwa Serikali imekuwa ikiwatengea maeneo machache ya kufanya uchimbaji huo lakini baada ya muda wachimbaji wanalahazimika kuhama maeneo hayo kwa kile wanachodai maeneo hayo hayana madini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata maelezo ya Serikali ni lini sasa Serikali itasaidia kufanya utafiti wa awali kwenye maeneo ili wanapokuja kuwagawia wachimbaji wadogo wadogo hawa, uwepo uhakika kwa wachimbaji wadogo wadogo hao kupata madini kipindi wakipewa maeneo husika?

## **12.      Ukaguzi wa Mazingira Migodini**

**Mheshimiwa Spika**, uchafuzi wa mazingira migodini ni tatizo ambalo linaikumba migodi mingi iliyopo hapa nchini. Wakati swala la mazingira lipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Nishati na Madini pia inahusika na madhara ya mazingira yanayotokana na shughuli za uchimbaji wa madini kwa wachimbaji wadogo wadogo, wachimbaji wa kati pamoja na wachimbaji wakubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Nishati na Madini, kupitia Wakala wa Ukaguzi wa Madini (Tanzania Mineral Audit Agency) zilisaini hati za makubaliano na baraza la taifa la mazingira NEMC ili kuwawezesha TMAA kufanya ukaguzi wa uchafuzi wa mazingira migodini. Hata hivyo taarifa inaonesha kwamba mara nyingi migodi inapokuwa inafanya uchafuzi

wa mazingira hutozwa faini kulingana na uchafuzi ulifanywa na kutakiwa kumaliza tatizo hilo.

**Mheshimiwa Spika**, mgodi wa Tulawaka Gold Mines Project uliwalih kikutwa na tatizo la kutiririsha kemikali na mgodi huo ulipaswa kulipa faini ya shilingi milioni 25 na mgodi ulilipa faini hiyo, aidha tatizo siyo ulipaji wa faini hiyo ila tatizo linaonekana kuwepo kwenye kutokusitisha uchafuzi huo wa mazingira. Mgodi wa Kilimanjaro Mine Ltd ultiotzwa faini ya shilingi milioni 6 lakini zillipwa mil 2 pamoja na kwamba kiwanda kiliomba NEMC kuwapunguzia adhabu. Migodi ambayo imewahi kutembelewa na kubainika matatizo ya uchafuzi wa mazingira ni pamoja na Golden Pride Ltd ultiotzwa faini ya milioni 60 kutokana na kosa la kutiririsha uchafu wenyewe madhara, mgodi wa Bulyanhulu –kutiririsha uchafu hatarishi, mgodi wa North mara, Geita Gold Mines na mgodi wa Williamson Mines Ltd.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini-TMAA kwa kushirikiana na NEMC kuhakikisha inafanya ukaguzi kwa lengo la kuangalia ni kwa kiasi gani, matatizo yaliyopelekea migodi hiyo kutozwa faini yaliweza kuhitimishwa.

#### **H. UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge hili limekuwa likitoa maazimio mbalimbali yanayohitaji utekelezaji wa Serikali, lakini kwa bahati mbaya sana, Bunge limekuwa halipatiwi mrejesho wa utekelezwaji wa maazimio hayo. Tafsiri ya jambo hili ni dharau au ni kutokana na ukweli kwamba Bunge hili halina meno.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge la 10 lilipitisha maazimio baada ya Kamati ya PAC kupitia taarifa ya mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuhusiana na fedha za Capacity Charge ambazo TANESCO ilikuwa inatakiwa kuilipa IPTL lakini kukawepo na kesi ya kupinga kiwango hicho cha malipo na kulazimu fedha hizo ziwekwa Benki Kuu kwa kufungua akaunti iliyoitwa “Tegeta Escrow Account”.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 28 Novemba, 2014 Bunge lilipitisha maazimio nane (8) kuhusiana na uporwaji wa mabilioni ya fedha za Serikali zilizokuwa zimebekwa Benki Kuu. Lakini azimio moja liliwa na uhusiano wa moja kwa moja na utendaji wa TANESCO kwa kupunguza nguvu ya shirika nalo ni Azimio Namba 7- liliosema kwamba nanukuu "*Bunge linaazimia kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kununua mitambo ya kufua umeme ya IPTL na kuimilikisha kwa TANESCO kwa lengo la kuokoa fedha za Shirika hilo*".

**Mheshimiwa Spika**, hadi sasa Bunge halipewa taarifa ya utekelezaji wa azimio hilo na hadi sasa TANESCO bado inalipa kiasi cha shilingi bilioni 4.3 kila mwezi. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ni kwanini Serikali imeshindwa kutekeleza azimio hilo na kuendelea kumlipa mtu aliyeinunuua IPTL katika mazingira yenye ujisadi?

**Mheshimiwa Spika**, Spika Anne Makinda aliunda Kamati Maalumu ya Bunge kwenda kuzungumza na wananchi wa Mtwara kuhusu sakata la ujengwaji wa bomba la gesi asilia kutoka mkoani humo hadi Dar es Salaam, kufuatia kuzuka kwa vurugu tarehe 22 Mei 2013. Kamati hiyo ya Mheshimiwa Spika Makinda ilikuwa chini ya Mbunge wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage (CCM).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hii ya Bunge ilitumia fedha za walipa kodi na ilifanya kazi na kuiwakilisha kwa Mheshimiwa Spik tarehe 20 Desemba, 2013. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Spika kuwezesha taarifa hiyo kuwasilishwa Bungeni ili mapendekezo ya kamati hiyo yajadiliwe na Bunge na kuwa maazimo rasmi ya Bunge na kuweza kutekelezwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, aidha yamekuwepo pia maazimio mengine ya Bunge juu ya uchunguzi kuhusiana na mapato kwenye gesi asilia hususani juu ya Kampuni ya Pan African Energy Tanzania (PAT) ambayo nayo Serikali hajjawasilisha Bungeni taarifa ya kuhitimisha utekelezaji. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuwasilisha taarifa

maalum Bungeni juu ya utekelezaji wa maaazimio yote ya Bunge yanayohusu Wizara ya Nishati na Madini ambayo hayajatekelezwu mpaka sasa.

### **I. MWENENDO USIORIDHISHA WA MPANGO WA UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA TASNIA YA UZIDUAJI TANZANIA-TEITI**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uziduaji(EITI) ni wa kimataifa ulioanzishwa mwaka 2003 kwa utiwaji saini kanuni 12 za uwazi katika malipo na mapato ya sekta ya uziduaji ili kuongeza uwazi katika uendeshaji wa tasnia ya uziduaji. Mpango huu ni umoja wenye uwakilishi sawa baina ya Serikali, Makampuni na Asasi za kiraia.

**Mheshimiwa Spika**, Kimataifa, mpango huu unasimamiwa na Bodi ya Kimataifa yenye uwakilishi wa Serikali zinazotekeleza mpango huu, makampuni na asasi za kiraia zinazounga mkono uwazi na uwajibikaji katika tasnia ya uziduaji. Baada ya kusainiwa kwa kanuni hizo, mpango huu umeungwa mkono na asasi za kiraia, wawekezaji wakubwa karibia wote na mataifa 52 Tanzania ikiwemo. Tanzania ilijunga na mpango huu tarehe 16 mwezi wa pili mwaka 2009 kwa tamko la Rais.

**Mheshimiwa Spika**, toka Tanzania ianze kutekeleza mpango huu, wananchi wamepata fursa ya kupata baadhi ya taarifa za mapato yanayotokana na madini na gesi asilia, tofauti kati ya malipo yaliyofanywa na makapuni na mapato yaliyopokelewa na Serikali. Pia taarifa juu ya makampuni gani yanalipa kodi kwa kiasi gani na yapi hayalipi tozo na kodi mbalimbali stahiki zimetolewa.

**Mheshimiwa Spika**, hii imesaidia ukuaji wa mapato kutoka kwenye sekta ya uziduaji kwani uwazi na uwajibikaji umeongezeka kiasi. Tanzania imekwisha toa ripoti 6 za mlinganisho wa malipo na mapato ya tozo na kodi mbalimbali ambazo zilifichua upungufu wa takriban TZS 63,748,566,888.00 ambazo ni fedha za tozo na kodi zilizolipwa

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Serikalini kwa kipindi cha mwaka 2008 hadi 2014 kama ifuatavyo:

2008/9	23,738,542,000.00
2009/10	5,002,169,000.00
2010/11*	11,000,000,000
2011/12	2,148,537,891.00
2012/13	12,920,549,420.00
2013/14	8,938,768,577.00
Total	63,748,566,888.00

\* Ripoti ya tatu imeondolewa kwenye mitandao yote kwa shinikizo la makampuni

**Mheshimiwa Spika**, toka mpango huu uanze, fedha zilizoripotiwa kupotea zimekuwa zikipungua kila mwaka kama ilivyooneshwa hapo juu na mapato yaliyoripotiwa kupatikana yamekuwa yakipanda kama ifuatavyo; ripoti ya kwanza Bil. 128, ripoti ya pili Bil. 435, ripoti ya tatu takribani Bil.500, ripoti ya nne takribani Bil. 700, ripoti ya tano Bil. Takribani 900 na ripoti ya sita takribani Tril.1.2 fedha za kitanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2015 mpango huu ulipewa nguvu ya kisheria kwani baadhi ya Taasisi na makampuni yalikuwa hayatoi ushirikiano ipasavyo. Pamoja na mapungufu yaliyopo kwenye Sheria, sheria imeunda Kamati ya kutekeleza mpango huo iitwayo Kamati ya TEITI chini ya kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania Na. 23 ya 2015. Chini ya Sheria hii, Kamati hiyo inapaswa kuwa na Mwenyekiti anayeteuliwa na Rais wa Jamhuri ya

Muongano wa Tanzania na wajumbe wengine wasiopungua kumi na tano wakiwemo watano wanaoteuliwa na Waziri wa Nishati na Madini (Serikali), watano kutoka kampuni za uziduaji na watano kutoka asasi za kiraia zinazojihusisha na masuala ya utawala bora katika tasnia ya uziduaji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kanuni za kimataifa za mpango huu na kifungu cha 8 cha Sheria hii, Kamati ya TEITA inapaswa kuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu na wajumbe wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja tu. Kutowana na ukweli kuwa kamati hii ilianza kabla ya sheria kuanza, Kamati iliundwa mara ya kwanza mwaka 2009 na kumaliza muda wake mwaka 2012, uchaguzi na uteuzi wa wajumbe na mwenyekiti ulifanyika, japo baadhi ya wajumbe walirudi kwani kanuni ziliruhusu. Wajumbe hao wa mwaka 2012 walimaliza muda wao mnamo mwaka 2015 na uchaguzi na uteuzi wa wajumbe wengine ulifanyika mwaka 2016 kwa mujibu wa sharia ya TEITI. Mchakato huu uliingia doa kubwa la kisheria.

**Mheshimiwa Spika**, kinyume na matakwa ya Sheria, hususan kifungu cha 5(1) kinachompa mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumteua Mwenyekiti, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini Prof Sospeter Muhongo akiwa anafahamu hana mamlaka alimteua Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo nafasi ambayo haipo kisheria. Kaimu huyu ameendelea kuwepo na anaendesha shughuli za Kamati huku akiwa hana mamlaka kisheria na hivyo yote yanayofanyika chini yake ni batili licha ya fedha zinazoendelea kutumika kuyafanya hayo wakati wakitambua kuwa si halali mbele ya sheria.

**Mheshimiwa Spika**, tunafahamu kuwa Kamati ya Uteuzi ya Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI inayoundwa chini ya kifungu cha 6(1) iliitoa tangazo la wananchi kupeleka maombi ya kujaza nafasi hiyo ya Mwenyekiti. Kinachoibua maswali ni kuwa Kamati hii ya Uteuzi baada ya kufanya usaili na wananchi walioomba kujaza nafasi hiyo ilitoka na majibu kuwa wote walioomba hawana uwezo wa kujaza nafasi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa Kamati ya TEITI tulitarajia, Kamati ya uteuzi ingelirudia zoezi hilo mara moja au kutumia njia nyingine bora ili ipendekeze majina kwa Rais kwaajili ya uteuzi. Hadi leo, ni mwaka umekwisha pita na hakuna liilofanyika. Inashangaza zaidi hata Kamati ya TEITI iliyoko madarakani inayoongozwa na Kaimu Mwenyekiti ilipoomba kupata majina ya walioomba kujaza nafasi hiyo, mpaka leo hajawahi kupewa majina hayo ili ijiridhishe kuwa ni kweli hawana sifa, japo uchunguzi wa suala hili unaonesha kuwa CAG Mstaifu Utuoh ni mmojawapo wa watanzania walioomba kujaza nafasi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mazingira hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa ni dhahiri kuwa Serikali haina utashi wa dhati wa kushiriki mpango huu wa uwazi na uwajibikaji? Na hata kama hakuna utashi wa kisiasa, je ni halali kuvunja sheria halali illyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa makusudi?

**Mheshimiwa Spika**, ni muhimu pia ikafahamika kuwa katika kifungu cha 10(2) cha Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uziduaji ya Mwaka 2015, Kamati ya TEITI imepewa majukumu makubwa na muhimu, baadhi yakiwemo ni kufanya uchunguzi wa jambo lolote linalohusu uziduaji ikiwemo viwango vya uzalishaji wa makampuni ya uziduaji.

**Mheshimiwa Spika**, kama hiyo haitoshi, Waziri bila kuwa na mamlaka na kinyume cha sheria hususan kifungu cha 5(4) cha sheria hiyo Na. 23 ya 2015 hakutangaza mjumbe mmoja aliyechaguliwa kihalali na asasi za kiraia kama inavyotakiwa kisheria. Ifahamike kuwa, wajumbe watano toka asasi za kiraia wanapaswa kuchaguliwa na asasi za kiraia kwa utaratibu wao na kupelekwa kwa Waziri ili watangazwe kama walivyo na sio vinginevyo.

**Mheshimiwa Spika**, bila kuwa na mamlaka na huku akivunja sheria, Waziri aliacha kutangaza jina moja la mwakilishi wa asasi za kiraia kutoka kwenye majina matano yaliyowasilishwa kwake bila kutoa sababu zozote.

Tunafahamu kuwa yapo malalamiko ambayo yalipelekwa kwa Waziri juu ya mchakato wa kuwapata wawakilishi hao watano ila hata baada ya juhudzi za Waziri kueleweshwa juu ya kutokuwepo kwa uhalali wa malalamiko hayo kuliko fanywa na muungano wa asasi za kiraia zinazojishughulisha na masuala ya uziduaji uitwao HAKIRASILIMALI, bado Waziri hakulifanya kazi jambo hilo ambalo tarehe 30/05/2017 lilitamilisha mwaka. Pia ni vyema ikafahamika chini ya Sheria hiyo Namba 23 ya 2015, Waziri hana mamlaka kupokea rufaa za uteuzi wa wawakilishi wa asasi za kiraia wala wale wa kampuni za uziduaji.

**Mheshimiwa Spika**, ukiacha uvunjaji huo wa sheria ya uwazi, Sekretariat ya TEITI imekumbwa na kashfa ya kimataifa ya wizi wa kimtandao ambayo inalichafua jina la Taifa letu kitaifa na kimataifa. Sekretariat ya TEITI iliingia mkataba na asasi ya Ujerumani-Open Oil, ikiwapa kazi ya kutoa mafunzo juu ya uwazi wa mikataba ya sekta ya uziduaji. Katika makubaliano yao, TEITI ilipaswa kuilipa Open Oil baada ya kutoa mafunzo.

**Mheshimiwa Spika**, Open Oil walimaliza kazi yao na kudai malipo ambayo inasemekana yalilipwa kwa njia ya mtandao kutoka Benki Kuu ya Tanzania kwenda kwenye akaunti namba 26110562 iliyopo benki ya Llyods ya mjini London, Uingereza inayosemekana ni ya Open Oil UG baada ya mazungumzo na mwakilishi wa Open Oil. Hata hivyo, baada ya muda sio mrefu, OpenOil walidai malipo yao na kuambiwa kuwa yalishalipwa. Baada ya uchunguzi wa awali wa Serikali, iligundulika kuwa domain name ya Open Oil ilikuwa imedukuliwa na hivyo malipo hayakwenda kwa mlengwa Open Oil. Serikali ilianzisha uchunguzi wa udukuzi huo kuititia Interpol lakini uchunguzi huo haujakamilika mpaka sasa toka mwaka 2016 ulipoanza huku kukiwepo na taswira ya udanganyifu kwa upande wa taasisi za Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Uvunjwaji huu wa sheria katika uteuzi wa Kaimu Mwenyekiti na kutokutangaza Mjumbe wa tano aliyechaguliwa kihalali na asasi za kiraia na kutokufuatilia ipasavyo upotevu wa malipo ya Open Oil umelitia doa taifa

letu na Serikali ya Awamu ya Tano kitaifa na kimataifa kiasi kwamba, Tanzania iko mbioni kuondolewa kwenye utekelezaji wa Mpango huu wa Uwazi na Uwajibikaji wa Kimataifa.

Maswali ya msingi kwa Wizara ya Nishati na Madini ni kama ifuatavyo;

i. Je, Serikali inaelewa umuhimu wa kutatua matatizo haya mapema kwani ikichelewa Tanzania itaondolewa kwenye ushiriki wa mpango huu?

ii. Je, Serikali inaweza kulihakikishia Bunge hili kuwa bado inathamini uwazi na uwajibikaji na hivyo bado inaunga mkono mpango huu.

iii. Je, Serikali inaweza kulihakikishia Bunge hili ni lini itayatatua matatizo haya ikiwemo ni pamoja na kumtangaza mwakilishi wa tano wa asasi za kiraia, Rais kumteua mwenyekiti mahsus wa Kamati hii nyeti na kukamilisha uchunguzi wa malipo ya Open Oil na kuchukua hatua?

iv. Je, Wizara inamelezo gani kuhusu kuondolewa mtandaoni kwa taarifa ya tatu ya TEITI (2011/12)?

#### **J. MKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2017/ 2018**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Nishati na Madini inakadiria kutumia jumla ya shilingi 998,337,759,500 ikilinganishwa na shilingi 1,122,583,517,000 zilizoidhinishwa na Bunge mwaka 2016/2017, sawa na upungufu wa 11%. Sababu zinazotolewa na Serikali za kupungua kwa Bajeti ni kupungua kwa makadirio ya fedha za nje kutoka shilingi 331,513,169,000 mwaka 2016/ 2017 hadi shilingi 175,327,327,000.

**Mheshimiwa Spika**, madhara ya kukosekana kwa fedha za nje, yanaonekana kuendelea kuiathiri Bajeti ya

Serikali hii kwa kuwa, kwa mujibu wa makadirio ya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Nishati na Madini, Wizara imetenga kiasi cha shilingi **938,632,006,000** ikililinganishwa na shilingi **1,056,354,669,000** zilizotengwa mwaka 2016/17, sawa na upungufu wa 11.1%. Aidha wakati mwaka huu 2017/2018 bajeti ya Wizara hii ikipunguzwa asilimia 11.1%, bajeti ya 2016/2017 Wizara ya Nishati na madini ilipewa na hazina **404,120,668,889.00** sawa na 36% ya fedha zote za bajeti ya Wizara hii iliyopitishwa 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu inaona haya ni madhara ya Serikali kutopenda ushauri na kuona haipangiwi cha kufanya. Kwa muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka majibu kutoka Serikalini kuhusu mambo yafuatayo:

- i. Ni sababu zipi za msingi zinazopelekea kupungua kwa fedha za nje kwenye Bajeti ya Wizara.
- ii. Miongoni mwa vyanzo vya fedha kutoka chanzo cha nje kilikuwa ni fedha kutoka Millenium Challenge Corporation, na MCC ilisitisha msaada wake kwa Tanzania kutokana na kukosekana kwa utawala bora, kufutwa kwa uchaguzi wa Zanzibar na kuvunjwa kwa Haki za Binadamu, Je Serikali inachukua hatua gani za kuondoa sababu zilizopelekea wadau wa maendeleo kusitisha misaada yake kwa Tanzania likiwemo shirika la misaada la Marekani MCC

## K. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kusitiza kama ambavyo imekuwa ikifanya katika hotuba zilizowahi kutangulia kwamba, sehemu kubwa ya matatizo ya Wizara ya Nishati na Madini yamechangiwa na yanaendelea kuchangiwa na sababu za kibinadamu ikiwemo ukosefu wa utashi wa kisiasa huku maswala muhimu yakiachwa.

**Mheshimiwa Spika**, Taifa lilihitaji na bado linahitaji mabadiliko ya kimfumo ili kuwezesha hatua za haraka za kusimamia sera sahihi, uongozi makini na taasisi thabiti katika sekta nyeti za Nishati na Madini, pamoja na kuchukua hatua stahiki ili kuziwezesha sekta hizi za Nishati na Madini kuongeza pato la Taifa na kupelekeea wananchi kuzifaidi rasilimali zao, kuliko matamko hewa ambayo yanalenga kupata umaarufu wa kisiasa, huku hatua zinazopaswa kuchukuliwa zikiachwa miaka nenda miaka rudi.

**Mheshimiwa Spika**, nimalize kwa kuwashukuru wananchi wa jimbo la Kibamba na Wilaya mpya ya Ubungo kwa kukikataa Chama Cha Mapinduzi, nawashukuru kwa kunipatia ushirikiano wao katika kazi za kuwawakilisha kwenye vyombo vyaa maamuzi na kuhamasisha maendeleo jimboni kwetu. Kwa namna ya pekee Nitambue mchango wa Meya wetu wa Ubungo, Mheshimiwa Boniface Jacob pamoja na madiwani wote ambaa hufanya kazi kwa niaba yangu jimboni ninapokuwa kwenye majukumu mengine ya kitaifa. Nawashukuru Viongozi mbalimbali kwa ushirikiano wao, viongozi wa kidini na kiroho na wanafamilia ya Marehemu Mzee wetu John Michael Dalali kwa ushauri wao na kunipatia ujasiri wa kuendeleza uadilifu katika kusimamia ukweli, haki na ustawi wa jamii ya watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hao, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni naomba kuwasilisha!

.....  
John John Mnyika (Mb)  
Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani  
Wizara ya Nishati na Madini  
01/06/2017

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnyika.  
(Makof)

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji baada ya kusikia hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini,

hotuba ya Mwenyekiti na pia Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Tutaanza na wachangiaji walioko hapa mbele, kila chama kimeleta majina. Tutaanza na Mheshimiwa Najma Giga, atafuatiwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab ajiandae.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika mwezi huu wa Ramadhan tukiwa wazima na kutekeleza majukumu yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kabisa kwa kuunga mkono hotuba ambayo imetolewa na Wizara hii ya Nishati na Madini. Kwa kweli Serikali kwa upande wa Wizara hii imejitahidi. Vyovoyote tutakavyofanya na kusema hatuna budi kuishukuru Serikali kwa jitihada inazochukua katika suala la sekta hii ya nishati na madini hasa tukizingatia usimamizi imara uliopo katika Awamu hii ya Tano ya Serikali yetu chini ya uongozi makini kabisa wa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia sina budi kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa namna ambavyo amepokea wito wa uungwana kabisa na busara kulipokea deni ambalo *ZECO* inadalwa na *TANESCO* na kuahidi kulilipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile dawa ya deni ni kulipa, Mheshimiwa Rais amechukua hekima na busara kuweza kukubali na mpaka hivi sasa deni la shilingi bilioni 11.8 limeshalipwa ambapo shilingi bilioni 10 zimelipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na shilingi bilioni 1.8 zimelipwa kupitia *ZECO*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hatuna budi kuipongeza Serikali kupitia *TANESCO*, tusipoipongeza tutakuwa hatuna shukrani. Pamoja na upungufu yote ambayo *TANESCO* inayo lakini kazi inayofanywa lazima tuishukuru na kuithamini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwenye kitabu humu miradi mbalimbali imeshatekelezwa ikiwemo *Kinyerezi* / na II ambazo zinaendelea lakini pia tuna *REA*, usambazaji wa umeme vijijini, kazi inafanywa kubwa kwa mazingira magumu. Tukipita sisi wengine tunaona juu ya milima kuna nguzo huko, tunashangaa zimetandazwaje, chini ya mabonde huko tunakuta nguzo tunashangaa zimetandazwaje, lazima tuwe wenyewe kushukuru na lazima tuwapongeze. Naamini kwamba Serikali kuititia *TANESCO* itatatua changamoto hatua kwa hatua ili tuweze kwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utaelekea huko huko kwenye nishati ya umeme na hapa nitazungumzia mfumo uliopo baina ya Shirika la *TANESCO* na *ZECO*. Niseme wazi kwamba kutokana na mfumo uliokuwepo siku za nyuma na pengine huu uliopo sasa hivi, ndiyo umepelekea *ZECO* kuwa na deni kubwa kwa *TANESCO*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielezee yale ambayo yamepeleka mfumo huu kuonekana kama unaendelea kuipa deni *ZECO*. Kwanza ni tozo ya *KVA*. Hii nikzungumza wataalam wanaelewa, ni tozo ya watumiaji wakubwa wa umeme kwa mfano viwanda na kadhalika. *ZECO* tunachukua kilovoti 132 kwa bei ya shilingi 16,550 lakini watumiaji hawa wa kilovoti 33 amba wanachukua kwa Tanzania Bara wanatozwa shilingi 13,200 kwa *kilovott* moja. Kwa hiyo, utaona *difference* iliyopo ya mfumo katika uendeshaji na kuipelekea *ZECO* kuweza kulimbikiza deni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wawekezaji amba wana tamaa ya kuwekeza Zanzibar wanashindwa kuwekeza kwa ajili ya tozo hii, hivyo naomba sana Serikali ilizingatii. Kwa mfano, mwaka 2011 utaona pia mtiririko wa mabadiliko ya tozo unavyobadilika, naweza kutoa mfano mwaka 2011 *ZECO* iliongezwa tozo ya asilimia 81.1 wakati Tanzania Bara iliongezwa tozo ya asilimia 19.4 tu, ni *difference* kubwa sana. Kwa hiyo, naomba Serikali izingatie sana kuititia Shirika hili la Umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitoa mfano pia mwaka 2013 *TANESCO* na *ZECO* walikubaliana kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwamba sasa umefika wakati hizi *kilowatts per hour* Zanzibar ipunguziwe kwa asilimia 31. Matokeo yake, *TANESCO* iliendelea kuingiza hiyo asilimia 31 hatimaye deni hili likatajwa mwisho wake kuwa ni shilingi bilioni 121.9 ambayo *round figure* ni shilingi bilioni 122 wakati *ZECO* wanaendelea kuhesabu kwamba wameshatolewa punguzo la asilimia 31 na kulikubali deni hilo kuwa ni shilingi bilioni 65.5. Kwa hiyo, tunaweza kuona *difference* hizo na naomba sana Mheshimiwa Waziri husika na timu yake waweze kuangalia kwa upande huu wa *TANESCO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la *ZECO* kuwa *end user*, nikizungumza *end user* anakuwa kama mtumiaji wa kawaida wa Tanzania Bara. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu mtumiaji wa kawaida wa Tanzania Bara anapelekewa umeme kupitia miundombinu ya *TANESCO* lakini *ZECO* tunaletewa umeme kwa bei ambayo mtumiaji wa Tanzania Bara anapewa *with operational costs* za *ZECO*, miundombinu na gharama zote ni za *ZECO*. Kwa hiyo, tuangalie hali inavyokwenda tuone mfumo uko viperi, nia yangu ni kueleza mfumo huu tuweze kuusahihisha ili tuweze kwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutokana na hili tunasema kwamba *ZECO* na *TANESCO* ni mashirika ya Serikali, moja kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano na lingine kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *ZECO* yenyewe inakuwa na madeni ambayo inadai Taasisi za Serikali ikiwemo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Hussein Mwinyi, Wizara yake imeweza kupunguza shilingi milioni 400 deni ambalo tulikuwa tunawadai na sisi ndiyo tumeweza kurudisha *TANESCO*. Kwa hiyo, tuangalie haya mambo ili sisi tuweze kulipa deni na Serikali taasisi zake iweze kulipa. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Kwa hiyo, hilo ni moja ambalo nilipenda nizungumzie kwa upande huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna huduma nyingine za jamii ambazo zinaigusa jamii moja kwa moja. Kwa mfano, ZAWA ambayo inashughulika na masuala ya kusambaza maji Zanzibar, tunaidai zaidi ya shilingi bilioni 20. Tunashindwa kuwafungia umeme kwa sababu Watanzania wanaoishi Zanzibar watakosa maji. Kwa hiyo, inabidi shirika hili tuone mfumo gani ambao utaweza kuwa bora na mzuri ili tusije tukaingia kwenye migogoro ambayo mimi sipendi kuiita kero, nasema bado ni *challenge*, tuzirekebishe hizi *challenge* ili Watanzania wote wanaoishi Tanzania Bara na wale walioko Zanzibar ambao wote ni wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania waweze kunufaika na huduma hii bila matatizo yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili Shirika la *ZECO* linafanya kazi kubwa kuikusanya mapato *TANESCO*. Mbali na hayo madeni ambayo yametokana na hizo sababu nilizositaja, tunatumia umeme kuanzia shilingi milioni 400 hadi shilingi milioni 500 kwa mwezi na bahati nzuri kuanzia mwaka 2015 Desemba tunalipa *current bill* kwa maana kwamba ankara kamili ya kila mwezi. Kwa hiyo, ili kuweka sawa mambo haya, tuonekane na sisi *ZECO* kule kwamba tunaifanyia biashara *TANESCO* ambayo ni taasisi ya Jamhuri yetu ya Muungano Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mwingine, tumeweza kuikusanya shilingi bilioni 41.8 katika kipindi cha miezi tisa kuanzia 2016 hadi kufikia Machi, 2017. Kwa hiyo, sasa nachoshauri mbali na kuwekwa huyu Mtaalam Mwelekezi nitaomba ushauri wake ufuatwe ili twende sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kwamba sisi *ZECO* basi angalau tupewe fursa ya kuwa *agentwa TANESCO* ili tuweze kulipwa na kuweza kugharamia *operation cost* ili tusiweze kuleta migogoro katika Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, pamoja na kuunga mkono hotuba hii naomba sana ushauri huu uweze kuzingatiwa ili tuweze kuimarisha Muungano wetu. Ahsanteni sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu. Nadhani Serikali imesikia yale ambayo yataweza kujibowi hapa sawa yatajibowi hapa, yale ambayo hayatahusiana moja kwa moja na shughuli za Bunge hili, tafadhalii myashughulikie huko kwa namna ya ofisi ili Bunge lisije likajikuta linajadili mambo ambayo halina mamlaka nayo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Sixtus Mapunda atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri ambayo kwa kweli ukiitizama kwa kina inatoa matumaini ya Taifa letu kwenda kwenye nchi ya viwanda hasa ukizingatia msingi mkuu wa Taifa la viwanda unatokana na Wizara hii ya Nishati na Madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 kipindi cha kampeni, Rais wetu mpPENDWA wakati anajinadi alipofikia kuongelea suala la sekta ya madini alijipambanua pasipokuwa na kificho kwenye changamoto kubwa tano zinazoikabili Wizara ya Nishati na Madini au katika ujumla wake sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu mpPENDWA alizunguka nchi nzima akasema, toka tumeingia ubia na wabinafsishaji na hawa wenzetu, tukawapa migodi wakashirikiana na sisi tumepita kwenye changamoto kubwa zifuatazo:-

- (i) Kunyanyaswa kwa wachimbaji wadogo, sambamba na kulipwa fidia ndogo wawekezaji wanapotwa maeneo. (*Makof*)
- (ii) Sekta ya madini ina usimamizi mbovu unaopelekea Serikali kukosa mapato. (*Makof*)
- (iii) Sekta ya madini inakutana na changamoto ya kutoroshwa kwa madini kwa njia mbalimbali kunakoipotezea Serikali mapato. (*Makof*)
- (iv) Sekta ya madini inakutana na changamoto ya mikataba mibovu inayopunja Serikali mapato. (*Makof*)
- (v) Sekta ya madini inakutana na tatizo la matumizi mabaya ya misamaha ya kodi ambayo wawekezaji wamepewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais akamalizia kwa kusema mkinipa ridhaa ya kuongoza nchi hii, nitahakikisha haya mambo matano nakwenda kuyafanya kazi. Watanzania wakamuamini wakampatia Urais, akaingia ofisini toka siku kwanza kipindi cha hotuba yake hapa Bungeni akasema nchi yetu tajiri, nchi yetu ina rasilimali nyingi, tukizitumia rasilimali zetu vizuri nchi yetu itakuwa *donor country*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika aliyasema haya kwa sababu alikuwa anaijua Tanzania vizuri. Akajipa muda wa kutosha, akai-study hiyo sekta ya madini akaja kugundua kuna makinikia yanatoweka nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yote niliyoyasema yapo kwenye changamoto namba tatu niliyosema sekta ya madini inakutana na utoroshwaji wa madini, kwa namna yoyote ile iwe hoja ya kisheria, iwe hoja ya mahusiano, hoja ya kutoroshwa kwa madini yetu Watanzania Rais alikwishesemba na akafanya kazi. Leo hii namshangaa Mtanzania yeote yule anayehoji *modality* au namna Rais

alivyoitengeneza Tume ya kwenda kuyakamata na kuyachunguza yale makontena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu mmoja anaitwa Edmund Burke na baadaye Abraham Lincoln na Martin Luther the King waliwahi kusema, *evils will prevail if good people do nothing*. Changamoto zote za madini tunazoziona zitaendelea kuwepo kama watu wazuri hawatafanya kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, alichokifanya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ile *segment* ya watu wazuri wanapofanya jambo ambapo kuna uovu. Kinachonishangaza mnataka uovu tuutengenezee *modality?* Unavyokwenda kumkamata mwizi unataka umtaarifu mwizi kesho nitakuja kukukamata, ujiandae pamoja na mtu wa kukuwekea dhamana ili ukifika Mahakamani tukutoe, jamanil Hivi kweli sisi ni wazalendo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonikwaza zaidi sio hili...

**MBUNGE FULANI:** Sema baba.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonikwaza zaidi hii ajenda kwa muda mrefu *pioneers* walikuwa wale pale. *Pioneers* wa ajenda hii kwa muda mrefu walikuwa wale pale, tutawataja kwa majina ...

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo. (*Makofi*)

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, waliosema hizi changamoto tano wale kule, Mheshimiwa Mnyika umewahi kusema, Mheshimiwa Mwita Waitara umewahi kusema, Mheshimiwa Tundu Lissu amewahi kusema, hawa ndiyo waliosema hayo mambo matano. Tena wakasema mnakaa na hii mikataba ya nini si vunjeni, hawakusema wale. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Walisema.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilichowafanya leo wabadili gia angani ni nini? Hawa watu wana tatizo la uzalendo, niwaombe ndugu zangu tuwe wazalendo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu yejote anayeona shaka ambapo kuna *evils and good people they are doing something* halafu akawatilia mashaka, kwa kweli napata shida sana kuwaelewa. Nilichotarajia kutoka kwao, kwanza wangesema tunakushukuru Rais, tumejema kwa miaka mingi hakuna aliyewahi kutusikiliza wewe umetusikiliza halafu ndiyo twende yale mengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mnyika amekuja hapa ana hoja ya mikataba *it is true*, mikataba ni tatizo hakuna mtu anayepinga na Rais alishasema mikataba ni tatizo. Nilichotegemea waseme makinikia ndiyo *foundation* ya mjadala ya mikataba.

**MBUNGE FULANI:** Aaa wapi.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utakwenda kwenye kujadili mkataba ukiwa na *evidence* tunaibiwa kwa kiasi gani, ninyi wawekezaji rekebiseni hapa kwa sababu tumethibitisha pasipokuwa na shaka lolote mnatuibia. Sasa mnataka twende tujadili *terms* za mikataba hatuna kitu mikononi? (*Makofî*)

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sixtus kuna taarifa ya kupokea, endelea Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Sixtus kwamba Nzega kuna Kampuni ilikuwa inaitwa *Resolute* imeondoka na *ten billion* ya Halmashauri ya Nzega ya *service levy*, nilitaka nimuongezee tu madhara. Pia nilitaka nimuongezee kwamba ikimpendeza kwenye hotuba

amshauri Rais na Serikali *GGM*bado wanaendelea ku-process dhahabu kwa hiyo zikakaguliwe na zile ili tujue tunakoelekea. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sixtus Mapunda, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bashe, kwanza naipokea taarifa yako kwa mikono miwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna siku hapa niliwahi kusema *story ya jongoo* na mwana jongoo...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Katika misingi ileile ya habari ya jongoo na mwanajongoo, unapotaka kutatua tatizo la wizi wa watu....

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Endelea.

**NAIBU SPIKA:** Subiri uitwe Mheshimiwa Waitara.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Unapotaka kutatua matatizo katika sekta hii ya madini lazima uwe na sehemu ya kuanzia. Hivi mnataka tuanzie wapi kwenye hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sixtus taarifa nyingine, Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika taarifa inatolewa na mtu aliyepewa nafasi ya kuzungumza. Mheshimiwa Waitara mpe taarifa Mheshimiwa Mapunda.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Sixtus Mapunda kwamba ni kweli wapinzani walisema, tulisema na uliowatataja walisema na ni kweli kwamba mikataba hii yote na kama alivyosema *evils* nadhani ni wao wao ndiyo walitengeneza mikataba mibovu na sasa tunaendelea kusema kwamba hata mikataba hiyo pia hatuwezi kuiona leo hapa hata mpaka kesho. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa nyingine ni kwamba bado ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, nadhani unaelewa maana ya taarifa, sasa unachotoa hapo ni mchango ambapo jina lako umeshaomba chama chako kilete kwa hiyo utapewa nafasi ya kuchangia. Mpe taarifa katika anayozungumza yale ambayo hayapo sawa ama unamuongeza siyo unachangia. Hiyo siyo taarifa ni mchango, mpe taarifa. (*Makof!*)

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakuelewa na nakushukuru. Naomba nimpe taarifa kwamba yote yaliyofanywa wamefanya wao yaani Serikali na chama chake, waliotenda leo ni wao na yaliyopo na madhambi mengine ni wao.

**MBUNGE FULANI:** Wao wao.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo taarifa yangu. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sixtus Mapunda unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba unilindie muda wangu wameuchazea sana. Hii taarifa ngoja niipe maelezo mazuri ili iwe taarifa iliyokamilika kwa sababu haijakamilika. (*Makof!*)

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wowote wa kisheria kuna mhimili unaitwa mhimili wa Bunge ndio unaotunga sheria na mfumo wowote wa kuongoza nchi katika namna yoyote ile chimbuko lake ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Upungufu wowote unaoonekana ninyi mlikuwepo na sisi tulikuwepo.

**WABUNGE FULANI:** Aah.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Ajenda ya sheria zote zilizopitishwa humu ndani ninyi mlikuwepo sisi tulikuwepo.

**WABUNGE FULANI:** Aah.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *my concern is not about the past, my concern* ni sasa tunapoanza kupiga hatua. Tumeliona tatizo, tunatatua tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napata shida sana kuwaelewa watu wa aina kama ya akina Mheshimiwa Mwita. (*Makofi*)

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napata shida sana, kwanza naomba nilindie muda wangu, nina dakika zangu tatu zimekuwa *disturbed*...

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Naomba nipewe muda wangu nimalize vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba wote mkae amalizie mchango wake, Mheshimiwa Sixtus Mapunda dakika moja. (*Makofi*)

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kichekesho cha mwaka kama kile ambapo mtu

umeliona kosa, unalirekebisha halafu mtu anatokea anakuambia kwa nini ulikosea si uendawazimu huo? Yaani mimi napata shida kuelewa, kosa limetokea unalirekebisha, katika *process* ya kulitatua tatizo unasema eti kwa nini ulikosea, ni akili za chizi tu zenyе uwezo wa kufanya mambo kama haya. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mapunda, muda wako umekwisha.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab. (*Makofi*)

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii ambayo ni muhimu sana ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kitendo chake cha kuzuia yale makontena pale bandarini na nampongeza sana kwa kuunda ile Tume ya kuanza kuangalia kiini hasa cha utoroshaji wa madini hapa nchini. Ripoti ya Tume inhabidi Waheshimiwa Wabunge tuipongeze sana kwa sababu pale ndiyo mwanzo wa kuanzia, madini ya nchi hii yamekuwa yakitoroshwa kwa muda mrefu sana na kwa kiwango kikubwa. Tumeshuhudia baadhi ya migodi hapa nchini inatengeneza mpaka viwanja vyatia ndege ndani ya mgodi. Tumeshuhudia baadhi ya migodi hapa nchini inaweka kampuni za ulinzi kutoka nje kwenye migodi ya hapa nchini, maana yake ni nini hiyo? Maana yake ni utoroshaji kwamba wanatayarisha viwanja vyatia ndege, wanatayarisha ulinzi kutoka nje ili sisi tusiweze kuona na baadaye madini hayo yanaondoka kwa kiwango kikubwa. Sasa hii ripoti inadhirishwa kwamba tumeibowi muda mrefu sana.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Aah.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Balozi kuna taarifa, Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni Bunge na tunapenda tupate taarifa sahihi. Mchangiaji anasema hawa wageni wanatayarisha viwanja vya ndege bila utaratibu, hii nchi ina vyombo vya ulinzi na Usalama, taarifa hizi za kusema wanatayarisha bila utaratibu na hii ni nchi yetu ni kulipotosha Taifa. Naomba tuongee vitu ambavyo ni kweli na yeye mwenyewe amekuwa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa hiyo siyo taarifa, wewe unazijua Kanuni na unajua Kanuni gani utumie ili ulete hiyo hoja yako. Hiyo siyo taarifa ya kumpa Mheshimiwa Balozi, Mheshimiwa Balozi mallizia mchango wako. (*Makofî*)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** *Imprest, imprest* hizo.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana ...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** *Ana-retire imprest.*

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mimi mwenyewe nimeviona hivyo viwanja na nimeona hizo kampuni kwenye migodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa Waheshimiwa Wabunge lazima tushikamane, hii ni hoja ya Serikali, sasa hizi hoja za kupinga ambazo zinatolewa aidha, madini hayo ni mengi au siyo mengi lakini kuna dalili za utoroshaji jamani, lazima tushikamane. Sasa tunapotoa hoja hapa oo tutashtakiwa, ngoja twende tukashtakiwe, kwani tunaogopa kwenda *International court*, tunaogopa kwenda kwenye *arbitration*, twendeni tukashtakiwe na tutatoa *arguments*, tuna ushahidi ambao umeonekana na Kamati imedhihirisha. Waheshimiwa Wabunge hiki ni kipindi ambacho tunatakiwa tushikamane kwa sababu tutakopanikiwa kudhibiti madini

yetu maendeleo yatakuwa kwa kasi sana, kwa hiyo, nawaomba tushikamane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii sijaona Mheshimiwa Waziri akizungumzia suala la ujenzi wa Kiwanda cha Kusafisha Madini. Namuomba aipangue bajeti yake na ahakikishe kwamba anaweka huo msimamo wa kuweka hela za Kiwanda cha Kusafisha Madini. Wakati masuala haya yanaendelea kushughulikiwa ngoja tuanze mchakato wa kujenga kiwanda chetu hapa kama tukishindwa basi tuingie ubia na watu binafsi kwa maslahi yetu lakini lazima tuhakikishe kwamba kiwanda hicho tuna *ki-manage* sisi tusije kufanya makosa tena na kuibwa. Namshangaa ndugu yangu Mheshimiwa Lissu juzi wakati anaongea alipokuwa *ana-criticize* ya kuongelea *case* ya Bulyanhulu, naifahamu *case* hiyo nimeishughulikia na wakati huo Mheshimiwa Lissu alikuwa anatetea sana wachimbaji wadogo na namna makampuni makubwa ambavyo yanataka kuwadhulumu wachimbaji wadogo mali zao. Jana akawageuka tena anaponda mimi nimeshangaa sana. Kwa hiyo, nasema tushikamane ili tuondoe hili tatizo ili tuweze kupata hela nydingi za kuweza kuleta maendeleo hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie *REA III*, *REA* wamefanya kazi nzuri sana ila katika kipindi hiki hawakufanya kazi nzuri ukilinganisha na kipindi cha nyuma. Sasa sijui ni kwa sababu gani lakini mipango ambayo wameiweka kwenye *REA III* tunategemea waanze kutekeleza vizuri. Pale Muheza kwenye Jimbo langu Mheshimiwa Waziri unajua umenipa *REA III* vijiji 44, *list* ya mkandarasi ambayo umenikabidhi ina vijiji 37, nakuomba urudishe vile vijiji vyangu saba ili wananchi wa kule ambao wameanza kufunga nyaya waweze kupata umeme. Vijiji hivyo ni vya Kwakope, Kibaoni, Magoda, Mbambala, Kitopeni, Masimbani, Msowelo vyote hivyo wananchi wameshajitayarisha na wako tayari kwa ajili ya kufungiwa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kupongeza sana juhudhi ambazo zinafanyika kwa ajili ya bomba la mafuta la kutoka kule Hoima Uganda mpaka

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Tanga. Tunaamini hii ni chachu na wananchi wa Tanga wanategemea sana kwamba bomba hilo litawaletea maendeleo makubwa ya viwanda na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umemalizika kwa kipindi cha kwanza cha leo, nitataja majina machache tutakayoanza nayo mchana nao ni Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Jesca Kishoa, Mheshimiwa James Millya, Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mheshimiwa Yussuf Kaiza Makame na Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib. Hayo ndiyo majina tutakayoanza nayo lakini yapo majina zaidi ya hayo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilsitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2017/2018**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya hoja ya Wizara ya Nishati na Madini, tutaanza na Mheshimiwa Selemani Zedi atafuatiwa na

Mheshimiwa Hasna Mwilima na Mheshimiwa Almas Maige ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara muhimu sana, Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kwa dhati ya moyo wangu, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za dhati za kuzuia wizi kwenye rasilimali za nchi yetu na hasa rasilimali katika sekta ya madini. Jambo ambalo tunatakiwa wote tuwe *clear* ni kwamba hakuna anayepinga au anayekataa uwekezaji. Mheshimiwa Rais hapingi wala hakatai uwekezaji na siku zote Mheshimiwa Rais amekuwa akihlimiza wawekezaji wa ndani na wa nje waje kwa wingi kadri iwezekanavyo. Mheshimiwa Rais anachochukia ni wizi wa rasilimali zetu na ambao tukiuacha uendelee utaturudisha nyuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bashe asubuhi wakati anatoa taarifa kwa Mheshimiwa Sixtus aligusia kidogo, sisi Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ni wahanga wa kudhulumiwa na haya makampuni ambayo wakati mwingine hayafuati taratibu na sheria zinazotakiwa. *Resolute Tanzania Limited* wamechimba dhahabu pale Nzega tangu mwaka 1999 na sasa hivi wamesimamisha uchimbaji lakini navyoongea sasa hivi *Resolute* wameondoka na *service levy* zaidi ya shilingi bilioni kumi ya Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Mara zote tukifuatilia wanatoa visingizio vya kisheria, *by-laws* lakini kimsingi wanapaswa watulipe fedha hizi. Nina imani kubwa Serikali hii ya Awamu ya Tano itaingilia kati kutusaidia ili Halmashauri ya Wilaya ya Nzega tusiweze kudhulumiwa shilingi bilioni kumi zetu za *service levy* ambazo kimsingi ni haki yetu tulipaswa tupate kama sehemu ya ushuru wa huduma kutoka kwa Kampuni hii ya *Resolute*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kampuni hii imesimamisha uzaliashaji na haina mfanyakazi hata mmoja

lakini tunajua ma-directors wapo na tunajua director mmoja ni Mtanzania na wengine wa nje. Tunajua bado wapo wana issue zao zingine za kikodi na mambo mengine wanaendelea ku-sort out lakini kampuni ipo. Kwa hiyo, bado kuna uhalali wa sisi kuendelea kudai na wao kutulipa stahili yetu kama ambavyo inastahili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kushauri ni kwamba Mheshimiwa Rais ameonesha mfano kwenye eneo la madini lakini naomba jitihada hizo za Mheshimiwa Rais ziende sasa mpaka kwenye rasilimali ya gesi. Bahati nzuri gesi ambayo tumeigundua kwa kiwango kikubwa hatujaanza kuichimba nako huku kuna dalili kwamba tusipokuwa makini pia kuna uwezekano mkubwa wa wawekezaji kwa maeneo haya wakaendelea kutunyonya au kutudanganya na hatimaye tukajikuta kwamba hatupati stahili zetu kama ambavyo tunatakiwa. Kwa hiyo, jitihada hizi ziende hata kwenye eneo la gesi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie eneo la wachimbaji wadogo. Napongeza jitihada za Wizara, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kalemani tumekuwa tukiwasiliana lakini na watendaji wake wa madini, Ofisi ya Tabora na ya Kanda nipongeze kwa jitihada ambazo sasa hivi wanazifanya katika kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogowadogo maeneo ya Nzega na yanayozunguka wanapata leseni na shughuli zao zinarasimishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Nzega kuna maeneo mengi tu ambayo leseni zilizokwu zinamiliikiwa na hii Kampuni ya Resolute ambayo imeondoka na kimsingi walisha-surrender leseni zao. Wananchi wengi ambaao sasa wameamua kuondokana na umaskini kwa kufanya shughuli hizi za uchimbaji mdogo mdogo wamekuwa wakiomba leseni ili waweze kuchimba kihalali lakini kutokana na mfumo wa kuomba leseni, mfumo bado unaonesha leseni hizi zinamiliikiwa na hawa Resolute, kwa hiyo wananchi kila wakiomba mfumo unawakatalia lakini maeneo hayo yako wazi, Resolute walishaondoka hawafanyi chochote. Kwa hiyo, naomba Wizara ifanye utaratibu ili

maeneo haya sasa ndani ya mfumo yafunguliwe ili wananchi na vikundi ambavyo vimejihamasisha, vimeji-*organize*, wameamua kuondokana na umaskini kwa kuanzisha ajira katika shughuli za uchimbaji mdogomdogo mfumo uweze kuwakubaliana kuomba leseni hizi na kuweza kupata hatimaye wafanye shughuli zao kihalali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya yamezunguka eneo liliokuwa la Mgodi wa Resolute lakini hata maeneo ya Mwangoye ambayo yako ndani ya Jimbo la Bukene pia yanakabiliwa na tatizo hili. Nina imani kubwa sana na Naibu Waziri, Mheshimiwa Kalemani na wafanyakazi wa Ofisi ya Madini Tabora na Kanda, nina uhakika jambo hili liko ndani ya uwezo wao na watalifanya kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni bomba la kutoa mafuta Uganda mpaka Tanga. Jimbo langu la Bukene na Wilaya ya Nzega ni moja ya maeneo ambayo yatanufaika na kupitiwa na bomba hili. Juzi Jumatatu nilikuwa Jimboni na kuna Kampuni ya GSB ambayo ndiyo wamepewa kazi ya kufanya tathmini ya mazingira na athari za kijamii, walituita pale ili kutu-*sensitize* kuhusu bomba hili. Niseme kwamba wananchi wa Jimbo la Bukene na Wilaya ya Nzega wako tayari, wanalisubiri bomba kwa mikono miwili na habari njema tulizopata ni kwamba maeneo yote ambayo bomba litapita kutakuwa na fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ushauri wangu ni kwamba yule mkandarasi mkuu wa bomba ahakikishe kazi zile ndogo ndogo ana-*subcontract* kwa makampuni ya wazawa ili na wenyewe waweze kufaidi. Pia kazi za vibarua zisizohitaji utaalamu wa juu basi wapewe vibarua ambaa wanatoka katika maeneo ya vijiji husika ambapo bomba litapita. Nimeambiwa kwangu pale katika Kata ya Igusule ndipo kutakuwa na kituo kikubwa ambacho kutakuwa na wafanyakazi zaidi ya 1,000. Kwa hiyo, sisi tunalichukulia hili kama ni fursa ya ajira, kupata uzoefu na kuinua hali ya maisha ya wananchi wetu wa Jimbo la Bukene. Kwa hiyo, wananchi wa Igusule, Mwamala, Kasela, Mwangoe na Lusu wako tayari wanalisubiri bomba hili kwa mikono miwili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu umeme wa REA Awamu ya Tatu. Nichukue fursa kwa dhati kabisa niipongeze Wizara na hasa Naibu Waziri Mheshimiwa Kalemani ambaye alikuja Jimboni kwangu na kuhamasisha umaliziasi wa umeme wa REA Awamu ya Pili. Sasa hivi maeneo yote ambayo umeme umeweza kufanikiwa kumetokea mabadiliko makubwa kabisa kwa hali za maisha na hali za kiuchumi za wananchi. Kwa hiyo, Jimbo langu la Bukene ni mfano wa namna ambavyo nishati ya umeme inaweza kubadilisha maisha ya mahali fulani. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi, muda wako umeisha.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja na nawapongeza sana watendaji wote wa Wizara hii, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasna Mwilima atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Peter Msigwa ajandae.

**MHE. HASNA S. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kigoma Kusini nishukuru kwa kunapata nafasi ya kuchangia Wizara hii nyeti, Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze sana kwanza kwa kumpongeza Waziri aliyewasilisha makadario ya bajeti ya Wizara hii kwa kushirikiana na Mheshimiwa Naibu Waziri. Natambua kwamba uwezo wanao na wanaweza kufanya kazi vizuri katika Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuzungumzia suala la Jimboni kwangu, naomba nimpongeze sana Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, kwa hatua nzuri aliyochukua ya kuunda Tume. Leo tumesikia hapa taarifa ya upande wa

pili unaonesha masikitiko kwamba Rais ameanza kwa kazi ndogo walitaka aanze na mikataba lakini tarehe 29/03/2017 sote tunatambua kwamba Mheshimiwa Rais aliunda Tume na ikafanya kazi yake chini ya Profesa Mruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wote ni mashahidi, Mheshimiwa Rais alitumia uwazi, akaitoa ile taarifa kwa uwazi kwenye vyombo vyahabari, wananchi walioko vijijini, wanaotumia redio waliskia, wenyewe kuona luninga waliona na akasoma taarifa. Kwa mfano kwenye yale makontena 277 kwa taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Rais wetu ilionyesha kwamba Watanzania kuititia hayo makontena 277 tunapoteza takribani bilioni 676. Halafu leo tunasema hii ni kitu kidogo wakati pesa hizi zinazopotea tungezipeleka kwenye majimbo yetu, Serikali ingeelekeza kwenye kujenga hospitali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kwenye makontena hayo wakati Mheshimiwa Rais anatoa taarifa imeonekana pia tuna upotevu wa *copper* na *sulphur*. Kwa mfano, nilikuwa naangalia kwenye taarifa ya *copper* inaonesha kwamba kwenye kila kontena tuna tani 20 za *copper* zinazopotea. Ukijumlisha yale makontena yote 277 unapata tani 1440.4 zenye thamani ya jumla ya shillingi bilioni 17.9. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonishangaza sisi wote tunafahamu wakati sisi wageni hatujaingia Bungeni siku za nyuma tulikuwa tukiangalia Bunge tunawasikia wapinzani wanaisema Serikali ya Chama cha Mapinduzi inakumbatia mafisadi na wanaisema Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaachia rasilimali za nchi zinaabiwa. Leo Mheshimiwa Rais amewasikia kwamba wapinzani walikuwa na vidonda sasa anajaribu kuona ni jinsi gani anaponyesha vile vidonda walivyokuwa navyo siku za nyuma. Raha ya donda, ukiwa na kidonda chochote lazima kipate dawa, iwe ni dawa ya kizungu, iwe ni dawa ya kienyeji lakini lazima kipate dawa. Mheshimiwa Rais analeta dawa kwa kuanza na haya makontena 277 lakini tunasema kwamba angeanza na mikataba, angeanza na mikataba wapinzani hao hao

wangesema Rais kakurupuka, anaanzaje na mikataba kabla ya kufanya uchunguzi. Sasa ameanzia makontena ndugu zangu ili kubaini hivi kweli huu mchanga unapopelekwa nje tunaibiwa au hatuibiwi? Kamati imetueleza kuwa tunaibiwa na Mheshimiwa Rais ametuambia anajiandaa kutoa taarifa ya pili kwa nini jamani tusimpe muda tukaisikiliza na ile taarifa ya pili ili tuweze kuona inatuletea nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka siku za nyuma wakati wa makelele ya ujisadi, tunaibiwa rasilimali zetu, Baba Askofu, Mwadhadama Kadinali Pengo wa Jimbo la Dar es Salaam Katoliki aliwahi kuhoji, hivi hawa wanaopiga kelele kwamba Watanzania wanaibiwa rasilimali zao zinotoroshwa, wanaongea kwa uchungu wa dhati au wanaongea kwa sababu wamekosa fursa na wao ya kuiba? Mimi nilifikiri kwenye suala hili tusimame kama Watanzania, tusimame kama nchi, tuache itikadi zetu, tumpe moyo Rais. Kama hatumpi moyo atafikia wapi kuwaza kuichambua na mikataba, kutoa fursa ili Bunge nalo tuletewe hiyo mikataba tuipitie na tumsaidie Rais kubadilisha yale ambayo tunaona ni upungufu?

Kwa hiyo, naomba sana tuwe na subira ndugu zangu, mambo mazuri hayahitaji haraka. Tume imetoa taarifa ya kwanza tusubiri taarifa ya pili na nina imani Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni mtu makini na atatupa taarifa ya pili na kwa taarifa zilizoko huko nje ni kwamba Watanzania wamefurahi sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ile Rais anatoa taarifa kaka yangu Mheshimiwa Tundu Lissu hapa alihojija na waandishi wa habari akasema wao kama Upinzani wamekuwa wanapiga kelele siku nyangi sana lakini Serikali haichukui hatua, leo Serikali inachukua hatua tunasema nini sasa, si tuipongeze? Halafu jamani ndugu zangu tujenge utamaduni wa kupongeza au kukosoa Serikali pale ambapo inapostahili, sio kila kitu tupinge. Hata nyumbani kwako inawezekana kabisa ukirudi mke unamnunia lakini siku akikupikia chakula kizuri si ni lazima umsfie, umwambie kwamba leo mke wangu umenipikia chakula kizuri ili kesho

apate nafasi ya kwenda kununua zaidi na aweze kukupikia zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumpongeza Rais na hiyo jitihada aliyofanya, naomba sasa niende kwenye Jimbo langu. Jimbo langu lina vijiji 61 tuna umeme kwenye vijiji kumi tu.

**MBUNGE FULANI:** Eheee.

**MHE. HASNA S. MWILIMA:** Kwenye *REA* Awamu ya Pili tulipata vijiji kumi vya Kandaga, Mlela, Kazuramimba, Kalenge, Uvinza na Mwamila lakini kwenye Awamu hii ya Tatu ya *REA* pia tumepangiwa vijiji kama 11. Rai yangu, naomba Waziri ambaye amewasilisha hapa waweze kushirikiana na Naibu Waziri na Mkurugenzi wa *REA* Tanzania Ndugu Msofe waone ni jinsi gani wanatusaidia wananchi wa Uvinza illi basi tuweze kuongezewa vijiji. Ni jambo la aibu kuona tangu uhuru vijiji 61 tuna umeme kwenye vijiji kumi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawapongeza kwanza wametufikiria kwa mara ya kwanza tunapata umeme mpaka Kijiji cha Malagarasi kwenye Kata ya Mganza. Najua huu ni mwanzo mwema ndio hatua sasa ya kupeleka umeme kwenye Tarafa yangu ya Nguruka. Kwa maana utoke pale Malagarasi uende Mlyabibi, Bweru mpaka Nguruka. Nina imani kwa sababu Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu itayapokea haya na kuyafanyia kazi. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasna, muda wako umekwisha.

**MHE. HASNA S. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Anafuata Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Peter Msigwa ajiandae.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niongee au nichangie katika Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuwapongeza sana Wizara hii ya Nishati na Madini na niwakumbushe wananchi na Wabunge wenzangu humu jinsi gani tulikuwa miaka mitatu, mitano, sita iliopita wakati ambapo tulikuwa na mgawo, siku mbili au siku tatu hakuna umeme na hatukulalamika; leo mgawo umekuwa historia hakuna mtu anayepongeza? Si tuwapongeze hawa wenzetu kwamba, wamefanya kazi kubwa sana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, nyuma ya mafanikio yote haya yupo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ambaye amekuwa anatoa mlongozo ya kulipa hela chungu nzima kwa mfano Kinyerezi *Phase II* ilisimama kwa sababu haikuwa na hela. Hela nyingi zimeingizwa pale ili mradi ule uanze, haya ni mafanikio makubwa sana. Vile vile iko miradi ya Rusumo huko, miradi mingine ya gesi inayoleta umeme ambao tunautumia majumbani na viwandani; haya ni mafanikio ambayo Wizara hii inatakiwa ipongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, niseme ukweli kwamba mwenzangu, rafiki yangu Mheshimiwa Profesa Muhongo amepata ajali ya kisiasa na amemwacha hapa Mheshimiwa *Engineer Merdad*. Bado Wizara hii imewasilishwa vizuri na mwenzangu Mheshimiwa Mwijage hapa leo, tumefurahi kwa yote aliyoyasema na kama alivyosema yeye Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Merdad ameziba pengo, amevaa viatu vya Mheshimiwa Profesa Muhongo. Naipongeza Wizara hii kwa mambo hayo makubwa iliyoyafanya, lakini hasa kusimamia miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongea kwangu leo nitaongelea pia, suala la *REA* ambao ni mradi mkubwa unaoendelea, lakini vile vile ningependa nichukue nafasi hii

kuongelea mambo ambayo yametokea hivi karibuni ingawa yameongelewa pia, lakini suala la makinikia haliwezi kuitwa bila kusemewa kwa undani na kwa ukweli wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunapenda ku-*quote* au kunukuu maneno katika lugha nyingine, mimi ningependa kunukuu leo maneno kutoka lugha yetu ya Kinyamwezi na maneno hayo ni kwamba, "*Mradi Kuyile*" yaani mradi tunakwenda, "*Nabhagemanyile*" nilikuwa najua na kudharau yani "*Kubyeda*".

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo fulani akifanya kiongozi wa nje ya nchi, hasa kutoka kwa wakubwa hawa, kama *container* hili moja lingekamatwa kule Malaysia au Singapore au Marekani, basi watu hapo wangeandika na kusifia sana. Tumekamata makontena 277 watu wanaona *business as usual, mradi kuyile*, mradi tunakwenda, haiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, madini haya yaliyokuwemo katika mchanga huu wa makinikia umetia hasara sawasawa na bajeti ya nchi hii kwa miaka mitano. Si chini ya miaka mitano, makontena haya kwa miaka 17, tungeweza kupata mali iliyotoka mle ndani tungeweza kuendesha nchi hii kwa miaka mitano, bajeti ya nchi nzima. Sasa Mheshimiwa Rais amefanya juhudui kubwa sana, ametimiza wajibu wake wa kukamata makontena haya, lakini bado naona tayari kunakuwa na watu ambao wameanza kudharau suala hili, jambo hili si sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna juhudui kubwa sana ya waliokamatwa sasa kujaribu kufunika jambo hili na kuna watu wanasema tutashitakiwa, mimi nashindwa kuelewa! Umuuibie mtu na ushahidi upo halafu ukamshatki! Sielewi kama kutakuwa na sheria, au sijui watatumia njia gani ya kutushitaki sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napata tabu sana ninapoona wenzetu wanaanza kuongelea, kwamba ni tatizo la mikataba, kwa hiyo mikataba hii ingeanza kwanza

kuchanganuliwa kabla ya kushughulikia makontena. Hata hivyo, ijulikane kwamba ili uuchambue upya mkataba lazima mkataba uwe na makosa, sasa makosa yameonekana, kumbe katika mkataba huu watu wanaiba, sasa huu wizi ndio ushahidi wa kuweza kuchambua mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani kwamba, sisi wote humu ndani ya Bunge hili tunao wajibu wa kutetea maslahi ya watu waliotuleta humu ndani, nao ni wananchi, ili wananchi hawa wasiibiwe, lakini vile vile wananchi hawa wasidhulumiwe na wananchi hawa wajione wako salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilinukuu maneno ya Kinyamwezi, lakini sasa ninukuu maneno ya Kiyunani, *"Delegatus Non Protest Delegae"*; mtu aliyepewa jukumu, wajibu wa dhamana hana haki ya kumkabidhi mtu mwingine tena wajibu huo aliokabidhiwa. Wajibu wetu sote humu ndani ni kuungana kwa pamoja kutetea wananchi waliotuleta humu ndani; leo inakuwaje sisi Wabunge tunaanza kubadilika na kutetea mambo ambayo hayana ukweli ndani yake? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameunda Tume ya Wataalam, wamechambua mchanga ule na kutoa majibu; je, hatuaminiani? Wabunge humu ndani wanaanza kuongelea kwamba, inawezekana ule mchanga ni hadithi ambayo wanaicheza ngoma ya walioibiwa. Ukweli ni kwamba kuhusu mchanga ule tufuate maelekezo na taarifa iliyotolewa na wataalam wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye miradi ya REA. Pamoja na mafanikio makubwa katika awamu ya kwanza na ya pili ya REA kumekuwa na udhaifu mdogo mdogo uliotokana na utendaji, hasa uwajibikaji wa watu fulani katika mradi ule, wameruka vijiji fulani. Kwa mfano jimboni kwangu vijiji vikubwa ambavyo vina shule, vina zahanati, vina vituo vya afya vimerukwa! Bahati nzuri nilimwona Mheshimiwa Muhongo kabla hajaacha kuwa Waziri na tukakutana pia na mkandarasi huyu, nina imani

tulioongea yatakuwa sahihi kwamba, watafanya *variance* ya mabadiliko kidogo ya mkataba kwa aslimia 15 ambapo Vijiji vya Majengo, Ikongolo, Kanyenye, Nzubuka na Kituo cha Upuge vitapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa anithibitishie kwamba, walioniambia viongozi wa *REA* kwamba, maeneo haya yatapata umeme, yapate umeme. Maana itakuwa jambo la ajabu bahati nzuri au mbaya katika vijiji hivyo ndiko mimi natoka, sasa watu wamekuwa wanasema ahaa, Mbunge huyu mnaona hafai, hata umeme kwake hakuna! Hayumo kwenye *REA Phase Two* na *Phase Three*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo litaleta matatizo makubwa sana ya kisiasa, nawaombeni sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha awe ameongea na watu wa *REA* ili waingize Vijiji vya Upuge kwenye kituo kimoja cha afya kiko pekee, Vijiji vya Majengo, Kanyenye, Ikongolo, Nzubuka na Kiwembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengine katika Wizara hii ambayo ni mazuri sana, lakini mambo madogomadogo haya yanaipaka matope Wizara na ionekane kama haifanyi kazi. La sivyo, Wizara hii imefanya kazi kubwa sana kutafuta gesi, kusimamia upatikanaji wa gesi, kusimamia uunganishaji wa bomba kutoka Uganda kuja Tanga, kusimamia mambo mengi, gesi kutoka kule Mtwara kuja Dar-es-Salaam na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema sana, naomba niwaachie na wenzangu. Naunga mkono hoja moja kwa moja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kuchangia Wizara ya Nishati na Madini. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti ya Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo amechukua hatua za makusudi kuweza kutetea na kuangalia changamoto mbalimbali zinazogusa wachimbaji wadogo wa madini Tanzania. Mwanzoni kulikuwa na unyanyasaji mkubwa sana wa wachimbaji wa madini, lakini tumemwona Mheshimiwa Rais akiwa ikulu akiona wachimbaji wakinyanyaswa anatoa maagizo na maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitumie fursa hii kwa niaba ya Wachimbaji wadogo wa Tanzania kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuhusiana na suala la ile Tume iliyochunguza mchanga unaosafirishwa nje ya nchi. Mimi binafsi natoka sehemu ambako madini yako kwa wingi ya dhahabu. Kweli, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa hatua aliyochukua, kwa kweli, imetupa moyo sisi pamoja na wananchi kwani ilikuwa ni kero kubwa sana, hasa kwa sisi ambao tunatokea maeneo haya ya wawekezaji wakubwa wa dhahabu. Wananchi walikuwa kila wakati wakiuliza, inakuwaje mchanga unasafirishwa, walisema sisi hatuoni hata faida yoyote ya kuwa karibu na wawekezaji hawa wakubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa hatua ambayo Mheshimiwa Rais ameichukua mimi binafsi nimefarijika na wananchi wamefurahi sana; na tunamwambia Mheshimiwa Rais aendelee na kasi hii na mikataba iangaliwe upya ili kuona jinsi ambavyo wananchi tunaweza kunufaika zaidi kutokana na madini ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongozi hizo, binafsi napenda kuzungumzia kwenye madini. Jimbo la Busanda ni jumbo ambalo limebarikiwa na Mwenyezi Mungu, siku zote huwa nasimama hapa nasema tunayo madini ya kutosha. Nilipokuwa nikiangalia bajeti ya Mheshimiwa Waziri sijaona chochote kuhusiana na Jimbo la Busanda kwa kweli, japokuwa ndiko ambako madini mengi yanatokea, hasa wachimbaji wadogo wako wengi sana kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Mheshimiwa Waziri atakapo-*wind up* aniambie maeneo ya Nyarugusu, hajazungumzia maeneo ya Rwamgasa, pamoja na Mgusu na sehemu mbalimbali za wachimbaji. Naomba azungumzie atakapo-*wind up* kwa sababu kwenye bajeti sijaona chochote kuhusiana na maeneo hayo niliyoyataja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna eneo la *STAMICO* ambalo limekuwa ni kilio cha muda mrefu sana kwa wananchi wa Nyarugusu na Mheshimiwa Waziri mwaka uliopita alisema kwenye bajeti kwamba analishughulikia na atawezza kulitafutia ufumbuzi suala hili, lakini mpaka sasa hata kwenye bajeti sijona akizungumzia hata kidogo. Kwa hiyo, naomba atakapo-*wind up* aniambie na wananchi waweze kusikia kwa sababu wanasililiza na hata hivyo wako kwenye *TVwanaangalia* ili kuona kwamba, je, suala hili limeweza kushughulikiwa? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili na aweze kulifuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo pale Rwamgasa mwaka 2015, paliteuliwa kuwa sehemu maalum kwa ajili ya uanzishwaji wa eneo la uchenjuaji wa dhahabu wa mfano. Hata hivyo nimesikitika kwamba kwenye Kitabu cha Bajeti, ukurasa wa 103, kati ya vituo saba vya mfano vya kuchenjua dhahabu Rwamgasa haijatajwa tena; sasa napenda kuuliza, je, imeondolewa kwenye huo utaratibu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015, Benki ya Dunia ilikuja kuzindua rasmi mradi huo pale Rwamgasa na hata leo hakuna chochote kinachoendelea na wananchi

wanaendelea kuulizia juu ya suala hili. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, wawaeleze wananchi wa Rwamgasa kuhusiana na suala hili, kwa sababu Serikali ni kwa muda mrefu imeteua Rwamgasa kuwa Kituo Maalum kwa ajili ya uchenjuaji wa dhahabu lakini leo hii Rwamgasa haipo kwenye bajeti kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile maeneo ya *Buckreef* ni maeneo ambapo Serikali pamoja na *TANZAM*wamefanya uwekezaji, lakini sisi wananchi hatuoni faida yoyote kutokana na huo mgodi. Kwa nini Serikali isiangalie upya mkataba huo ili ikiwezekana wapewe wananchi maeneo hayo waweze kuchimba na kunufaika na rasilimali za Taifa zilizopo katika nchi ya Tanzania? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile *TANZAM* wamechukua eneo Rwamgasa, wakulima wamenyang'anywa maeneo na mpaka sasa hawajapewa fidia yoyote. Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie, kwa sababu maeneo hayo wananchi hawaruhusiwi kulima wala kufanya kazi yoyote pale, lakini hawajapewa fidia yoyote. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wazungumzie suala hili, ili wananchi waweze kujua hatma yao kuhusiana na suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi napenda kuishauri Serikali kwamba Mkataba huu wa *Buckreef* na *TANZAM*uangaliwe upya na ikiwezekana eneo hili wapewe wananchi ili waendelee kuchimba dhahabu na kuweka mchango wao kwenye pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa upande wa umeme; nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali japokuwa tunaona Serikali inaendelea kupeleka umeme hasa katika Miiji mbalimbali. Kwa mfano Katoro mpaka sasa hivi wanasantaza kwa kasi umeme, lakini bado jitihada zinahitajika zaidi kwa sababu wananchi wanahitaji umeme. Kati ya Kata zangu 22 ni kata 10 tu ndizo zilizofikiwa. Kwa hiyo, niombe Serikali iwekeze nguvu zaidi, ikiwezekana *REA*

iongezewe fedha zaidi ili wananchi hasa walio wengi walioko vijiji ni waendelee kupata umeme wa uhakika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niangalie kwa habari ya mafuta. Kuna vinasaba ambavyo vimekuwa vikilipiwa dola 14 kwa lita 1,000. Hivi vinasaba kwa nchi ya Tanzania kwa kweli, vinaongeza gharama ya mafuta. Naiomba Serikali iondoe hii gharama, ifute kabisa vinasaba hivi kwa sababu sasa hivi bei ya mafuta ya dizeli na bei ya mafuta ya petroli na mafuta ya taa karibu zinalingana, kwa hiyo uchakachuaji haupo tena umepungua kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kwa kuwa, katika nchi nyngine za Afrika Mashariki kama Kenya vinasaba hivi gharama yake ni dola tatu mpaka nne, lakini sisi ni dola 14, kwa nini inakuwa hivyo sisi katika nchi ya Tanzania? Ndio maana sasa mafuta yanakuwa na bei ya juu zaidi kuliko nchi nyngine wakati sisi tuna bandari hapa hapa Tanzania. Kwa nini bei ya mafuta iwe juu ukilinganisha na nchi nyngine wakati sisi tumebarikiwa pia kuwa na bandari katika nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa nichukue nafasi hii kuiomba sasa Serikali iangalie kiundani habari ya wachimbaji wadogo wadogo ambao nimewazungumzia kwa miaka mingi, iangalie namna ya kutatua changamoto zao sasa, kwa sababu imekuwa ni kipindi kirefu wananchi wanahangaika, wanalia, wanahitaji kupewa maeneo ya uchimbaji. Hatuwezi kufikia uchumi wa kati bila ya kuwawezesha hawa wachimbaji wadogo wa madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo wakati ule ambapo Mheshimiwa Profesa Muhongo alikuwa Waziri alikuja Geita akatoa maelekezo kwamba ziangaliwe zile leseni ambazo hazifanyi kazi waweze kupewa wananchi. Mkoa wa Geita tu tuna zaidi ya leseni 1,700 ambazo ni za utafiti pamoja na wachimbaji wadogo wadogo na wa kati. Hata hivyo, kati ya leseni hizo zinazofanya kazi ni leseni 30 tu,

kwa hiyo leseni nyingi hazifanyi kazi. Nitumie fursa hii kuiomba Wizara iangalie namna ya kuwapatia wananchi leseni hizi ambazo hazifanyi kazi, hasa vikundi vyta wachimbaji wadogo ambao wanafanya shughuli mbalimbali za uchimbaji. Kwa hiyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bukwimba, muda wako umekwisha.

**MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Peter Msigwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa na Mheshimiwa Ole-Millya ajiandae.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siwapongezi Wizara hii kwa sababu kwanza wanatimiza majukumu yao na pesa wanazotumia ni kodi ya wananchi. Ila ninachowea kusema Jimbo langu limekaa vizuri kwenye miundombinu ya maji na umeme tuko vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kinachofanyika humu ndani ya Bunge ni sawa na baba ambaye anaenda sebuleni anajisaidia halafu watoto na mama wanamchachamalia kwamba atoe uchafu aliojisaidia sebuleni, halafu anapoutoa anasema mnishangilie nimefanya kazi kubwa. Hiki ndio kinachofanyika na nyie Wabunge wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana, Bunge la Kumi...

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa naomba ukae; Kuhusu Utaratibu, Kanuni?

### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hiyo hiyo!

Mheshimiwa Naibu Spika...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mzungumzaji anayeongea anatumia lugha ya kuudhi humu ndani na hali yeye ni Mchungaji. Amejisaidia yeye?

**MBUNGE FULANI:** Unatumia Kanuni gani?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa, endelea na uchangiaji. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la 10 wakati wa saga la *Escrow* tulikaa katika Bunge hili mpaka saa sita za usiku na Waheshimiwa Wabunge wote tulikubaliana kuhakikisha Mheshimiwa Profesa Muhongo na watu wengine waondolewe. Pamoja na Mheshimiwa Kigwangalla wote mnajua kwenye kumbukumbu alisema hajawahi kuona Profesa muongo kama Mheshimiwa Muhongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wa CCM na sisi hapa kwa wingi wetu wote mkapiga makofi mkashangilia Mheshimiwa Profesa Muhongo aondoke na kwa sababu,

Mheshimiwa JK alikuwa anaheshimu maamuzi ya Bunge, Mheshimiwa Profesa Muhongo na wenzake waliondoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, alivyokuja Mheshimiwa Magufuli, alivyoanza kuteuwa Baraza la Mawaziri hakujali kwamba Bunge liliona nini, lilifanya nini, akasema hapa kazi, mnamuonea wivu, namchagua Mheshimiwa Muhongo; mkapiga makofi mkasema jembeee! Huko ng'ambo huko, kwa sababu ya wingi wenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi baada ya huu mchanga amemtumbua, tena mnashangilia mnasema jembee! Ninyi, ninyi! Hebu tufike mahali tuone wajibu wetu wa Bunge ni nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, amezungumza Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye walau katika Bunge hili ana historia ya migodi na jinsi ambavyo watu wameonewa, amefungwa mpaka ndani na mikataba iliyowekwa. Kweli, amekuwa akitetea na hajaacha kutetea wachimbaji wadogo, lakini leo tunaanza kujitoa ufahamu! Wataalam wanasema...

### **MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** ...when you are lost speed is useless; ukipotea spidi haina maana! Ukipotea unarudi unasoma ramani...

### **T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa taarifa kwamba maisha siyo *static*, hayasimami, ni *dynamic*, ndiyo maana hata Lowassa allitwa fisadi mkubwa lakini baadaye akageuka kuwa... (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Mukasa taarifa anayopewa mchangiaji inapaswa kuwa wewe unamwongeza yale aliyochangia, kama hayako sawasawa unarekebisha, ndiyo taarifa. Mheshimiwa Msigwa endelea kumalizia mchango wako.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *this is just a joke*, tunazungumza Bunge hatuzungumzi mambo ya Lowassa hapa. Tunazungumza Bunge na wajibu wa Bunge, na tunaowazungumzia humu ndani ni wale waliopewa madaraka ya kuongoza nchi hii. Leo mnajitoa ufahamu mnashangilia Magufuli utadhania ni Columbus anagundua kisiwa cha Australia huko bara la Australia. Anachokifanya Magufuli si kitu cha kwanza. Subirini ...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE WALEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwongozo

## M W O N G O Z O

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa naomba ukae, kuhusu utaratibu. Mheshimiwa Msigwa uwe na utulivu umepewa nafasi ya kuchangia, mimi ndiye ninayeamua kwa hiyo usitake kujibizana na mimi, ni kama nilivyokupa nafasi ndivyo ninavyompa mtu mwengine, kwa hiyo usitake kujibizana saa hizi. Mheshimiwa *Chief whip*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE WALEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Msigwa anaolewa ni Mbunge mzoefu na anajua utaratibu wa kikanuni. Sasa ninachotaka kusema, taratibu zinazotumika humu ndani katika kuchangia, kanuni ya 64 ukiangalia kanuni ya (g) kwanza inasema mchangiaji yejote lazima atumie lugha ambayo ni ya staha, haidhalilishi watu wengine na si lugha ya kuudhi.

Mheshimiwa Naibu Spikia, vile vile katika kuwa na staha unapomtaja Rais wa nchi hii ni lazima useme

Mheshimiwa Rais na umtaje jina lake. Hata hivyo sidhani hata kwa utamaduni wetu tu Mbunge anaweza akasimama hapa akasema Magufuli! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamheshimu Mchungaji Msigwa lazima atumie lugha ya staha. Mheshimiwa Rais wa nchi hii anaitwa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa hiyo naomba sana Wabunge wazingatie kanuni ya 64 halafu Mbunge aseme kwa kujenga hoja zake, lakini akizingatia utaratibu wa Kikanuni. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ameomba utaratibu na anataja kanuni ya 64(1) kifungu cha (g) kinasema;

*"bila ya kuadhiri masharti ya ibara ya 100 ya katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadilano katika Bunge, Mbunge hatatumia lugha ya kuhudhi au inayodhalilisha watu wengine."*

Waheshimiwa Wabunge hii kanuni ya 64 fasili (1) ina maeneo mengi tu ambayo yamekatazwa Bungeni, na ukiisoma utagundua haya ni mambo yasiyoruhusiwa, yametakwa mambo mengi hapa. Naomba tutumie muda wetu vizuri kwa kuchangia kwa kufuata masharti ya kanuni hii, yale mambo yasiyoruhusiwa tujiepushe nayo maana kila wakati tutakuwa tukipotezeana muda katika mambo ambayo tuna uwezo wa kutumia vinywa vyetu sisi kama viongozi kwa kuzungumza na kufikisha hoja inavyotakiwa. Mheshimiwa Msigwa naomba uzingatie masharti ya kanuni ya 64.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unitunzie muda wangu. Ninachokisema alichokifanya Mtukufu Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli si kipyaa, maana mnashangilia hapa utadhania ni Columbus amugundua Bara la Australia. Tume ya akina Maige hapa wapo akina Zito. Haya mambo waliyazungumza. Alipoingia Ikulu tulitegemea angeona mafaili, kitu gani kifanyike kuhusiana na matatizo ya tasnia hii na kwenye

Baraza la Mawaziri naye alikuwepo. Sasa hapa mnabeba ngoma mnashangilia kama tumevumbua bara lingine wakati ni mambo yenu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ninyi CCM ni waungwana mngewaomba radhi Watanzania, kwamba tumechafua sebule. Sebule tumeiweka katika hali mbaya ya hewa tunawaomba radhi tumewakosea. Sasa mnazunguka hapa kwa mlango wa nyuma kama vile sisi wote ni watoto. Eti tumpongeze Mheshimiwa Rais, hii nchi ni ya wote. Siku zote mnasema hapa ndiyo!, iweje nchi ya wote hapa kwenye mambo yasiyokuwa na maana? Tunajitoa ufahamu, ndiyo. Tume ya akina Maige hawa walienda walizunguka nchi nyingi duniani na walilipwa hela nyingi sana Tume...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa umetoka kukumbushwa yule ni Mheshimiwa Mbunge kwa hiyo anaitwa Mheshimiwa Maige tafadhalii, hizi kanuni tuisipungukie tumetunga wenyewe. Wewe unaitwa Mheshimiwa mwite na ye ye Mheshimiwa ili tusiwe tunarudia rudia haya mambo . Ahsante sana.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA...** na wenzake walizunguka dunia mzima, sasa leo mnakuja hapa tumpongeza Mheshimiwa Rais na nataka niwaambie Watanzania, hizi lugha tunazozungumza hapa kuhusu *investors* unajua kuna mtu mwingine anadhani *investorshawa* wa madini wana-*invest* kama kibanda chako unachouza mkaa huko nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi hapa mnazungumza kwa sababu hamjaenda kwenye migodi mkaona *heavy investments* walizoziweka kule ndani. Kwa hiyo si kitu cha dakika moja; unadhani kwamba unaweza ukawaambia toka leo ingia leo? *It is a heavy*, ni hela nyingi. Muwaulize wenzenu waliotangulia tulifanya nini kwenye *Dowans* tulivyojaribu kutaka kuwapeleka mahakamani. Mnasimama tu hapa mnasema tuwapeleke mahakamani, sawa tutaenda

lakini hiki tunachochenza nacho hapa si kitu kidogo; na kuwapoteza *investors* si kitu kidogo. Hakuna mtu wa upinzani anayetaka tulbiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunachozungumza ni juu ya *method* iliyyotumika na namna ya kufanya haya mambo. Tumezungumza miaka mingi tangu wakati wa Mheshimiwa Rais Ally Hassan Mwinyi; kwamba watu wanaingia vibaya mkabisha na ndiyo tabia yenu. Tulivyokuja na suala la Katiba, likiwa linatoka kwetu mkalivamia mkashindwa kulimaliza; tulipokuja na suala elimu bure mkashindwa kulimaliza; tuliwaambia haya madini nayo mnakosea, narudia, narudia tena, *When you are lost speed is useless; ukipotea huongezi accelerator*, hukanyagi mafuta bali unasoma ramani na ramani pekee ambayo mngechukua ni ile ya Tume ya Bomani, soma anasema nini, ndicho ambacho tungetakiwa kukifanya ndugu zangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawatukana wavezekaji kama vile *invaders* kama vile wametuvamia. Hawa watu tukiwaambia kesho tu wanaondoka. Leo tunawaambia wezi hii mikataba tumefanya wenyewe, Sheria tumetunga wenyewe, leo tunawaita wezi eti tumekamata makontena mia saba, kwani yameanza kusafiri leo? Vyombo vyaa usalama havikuwepo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokisema sisi kama Watanzania mbinu mnayotumia si sahihi. Njia mnayotumia si sahihi kwa sababu inatuingiza chaka zaidi. Niwaombe kama Bunge, tunachotakiwa kufanya hapa ni kuiomba Serikali *i-engage*, tuingie kwenye majadiliano badala ya kufikia kwenda mahakamani. Kwa sababu nawa- *guarantee*, *kama wakitupeleka Mahakamani we are going to lose big time, whether you like or not.* Cha msingi Bunge tungetoa ushauri badala ya kuwafukuza *investor* na kuwatuna. Ma-*investors* wale wanaweka *heavy money...*

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

**WABUNGE FULANI:** Mmehongwa hela,

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kama tumehongwa hela nyie

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuwe na utulivu.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** ... Mikataba mliingia wenyewe na mmeifanya hii nchi ya *trial and error* halafu leo...

**MBUNGE FULANI:** Sumaye alikuwepo.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Leo mnasema eti tuwe wazalendo. Katika Bunge liloisha kuna mikataba mingi Sheria nyingi zimetungwa kwa hati ya dharura na hizi Sheria nyingi tumekuwa tukizipinga...

**MBUNGE FULANI:** Morena.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA...** tukijaribu kuwashauri lakini huwa hamsikii. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge hebu tuache kujitoa ufahamu. Wengi wenu hapa mnapiga kelele hata hiyo Sheria ya Madini hamjasoma, hamjui hata hiyo migodi, mmekuwa washangiliaji tu kama Mheshimiwa Tundu Lissu anavyosema... (Kelele)

**MBUNGE FULANI:** Dolla dolla dollaa

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA** ...mmekuwa washangiliaji hamjasoma hata Sheria unakuja hapa hufanyi *research* huwezi kuuliza maswali, wewe walichosema tu unashangilia shangilia tu hapa, hili ni Bunge la aina gani? Hebu tuache kujitoa ufahamu turudi kwenye nafasi, tuache kujitoa ufahamu; na wengi wenu mnapiga kelele tu kwenye majimbo yenu hakuna lami, maji, umeme mnatetea mambo ya ovyo tu. Tunachozungumza hapa tunazungumza mustabali wa Taifa letu siyo ushabiki. Siyo ushabiki wa kupiga piga makofi hujaletwa kupiga piga makofi hapa. Kasome Sheria za madini chimba visima hakikisha unatetea maslahi ya nchi yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hii dozi inatosha nitarudi kidogo kwenye ufahamu.

**MBUNGE FULANI:** Morena! Morena!

**MBUNGE FULANI:** Dolla! Dolla hizo!

**MBUNGE FULANI:** Msigwa Morena hiyo!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, twende kwa utulivu. Mheshimiwa Msigwa yeye ameshasema jimbo lake halina shida yoyote, sasa Mbunge mwingine mwenye shida zako ukisahau kutaja mambo ya jimbo utakuwa hatarini. Mheshimiwa Jesca Kishoa, atafuatiwa na Mheshimiwa atafuatiwa na Mheshimiwa James Millya Mheshimiwa Maulid Said Abdallah Mtulia ajiandae.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nitazungumzia suala zima la gesi na baadaye nitajielekeza kwenye suala la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu katika taifa letu wananchi wa Tanzania wemekuwa na matumaini makubwa sana kuhusiana na suala la gesi ya Mtwara. Matumaini haya yametokana na sababu nyingi mbalimbali ikiwa ni pamoja na sababu ya miradi miwili mikubwa. Mradi namba moja ni mradi wa bomba la gesi kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam ambalo limechukua takriban shilingi trilioni 2.5 katika utekelezaji wake na mradi wa pili ni mradi wa *LNG* (*Liquefied Natural Gase*) ambayo kama ingekuwa imetekelezeka kwa sasa ingekuwa imetumia Dola za Kimarekani bilioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sana Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikitumia akili ndogo sana kupanga mipango na kutekeleza miradi mikubwa na mambo makubwa. Bomba la gesi la Mtwara kwenda Dar es Salaam limetumia pesa nyingi sana, lakini kwenye ripoti ya *CAG* anaonesha bomba hili la gesi lina uwezo

wa kufanya kazi kwa asilimia sita tu. Tafsiri yake ni kwamba hata hilo deni ambalo tumelikopa China la trillioni 2.5 hatuwezi kulilipa kwa sababu bomba hili halfanyi kazi vizuri; matokeo yake tutaanza kuchukua fedha kutoka kwenye madawa; tutaanza kuwabana wafanyabiashara kwa ajili ya kulipa deni hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo lingine ambalo ni kubwa sana. Naomba Mheshimiwa Waziri husika atakapokuja kuhitimisha atoe majibu ni ni kwa nini wanakuwa wana *poor project plan* ambayo inapelekea miradi mikubwa kama hii inashindwa kutekelezeka kwa ufanisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *LNG (Liquefied Natural Gas)* haijawahi kutokea katika Taifa hili kuwa na mradi mkubwa kama huu. Huu ni mradi wa kihistoria, lakini cha kushangaza mradi huu umeshindwa kutekelezaka kwa sababu Serikali mmeshindwa *ku-deal na investors*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwenye meza yangu nina taarifa kutoka kwenye jarida kubwa kabisa la kimataifa la *Reuters* la Uingereza ambalo nimem-quote meneja *wa Statoil* anaeleza kwamba mradi huu umeshindwa kutekelezaka kwa sababu ya kusuasua kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kama utahitaji taarifa hii naomba umtume mhudumu aje aichukue *copy yako nimekutolea*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha aseme tatizo ni nini? Nimesikia kwenye hotuba asubuhi anasema kwamba majadiliano bado yanaendelea. Wawekezaji wanalamakika, tatizo ni nini? Ni hivi, hawa *investors* ambao anawapiga danadana wamehamisha mradi huu wa *LNG* wameupeleka Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu kupelekwa Msumbiji tafsiri yake ni kwamba kufikia mwaka 2021 ambapo mradi huu unakwenda kutekelezaka maana yake ni kwamba Msumbiji watateka soko la gesi katika Afrika Mashariki pamoa na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri labda sijui ni kutofahamu, mimi nashindwa kuelewa! Unapozungumzia uwekezaji wa takriban dola za Kimarekani bilioni 60, bilioni 30 unakuwa unazungumzia uchumi wa Uganda. Uchumi wa Uganda ni takriban dola la Kimarekani bilioni 60. Unapozungumzia *investment* ya dola za Kimarekani bilioni 30 unazungumzia robo tatu ya uchumi wa Tanzania ambao ni dola za Kimarekani bilioni 45. Unapokuwa unazunguzia uwekezaji wa takriban dola bilioni 30 unakuwa unazungumzia mara kumi ya uchumi wa Rwanda. Uwekezaji huu ni mkubwa sana. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atupe sababu kwa nini mradi huu unashindwa kutekelezeka kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la umeme. Taifa hilli lina vyanzo vingi vya umeme. Tuna maporomoko ya mito, tuna upepo, kwa mfano mimi mkoawangu wa Singida kuna upepo wa kumwaga. Pia tuna makaa ya mawe ukienda kule Liganga na Mchuchuma takriban tani milioni 480 zimejaa kule, lakini bado umeme ni wa kusucasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia mpango wa miaka mitano uliotolewa na Waziri wa mwaka 2016 - 2021 ukurasa wa 12 unaonyesha kwamba mwaka 2011 Serikali ilidhamiria kuongeza *megawatt* kutoka 900 mpaka 2,700 kufikia mwaka 2011, lakini cha kusikitisha mpaka inafika mwaka 2016 *megawatt* zilizoongezeka 1,246 na kwa bahati mbaya sana nimemsikia na Mheshimiwa Waziri asubuhi kwenye hotuba yake na nimepitia kumbe zimeshuka tena mwaka huu zimekuwa *Megawatt* 1,051.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kama kuna Waziri yeoyote hapa asimame aniambie kama kuna nchi yoyote imewahi kufanya mapinduzi ya viwanda kwa *megawatt* 2,000. Mnampa Mheshimiwa Rais mizuka ya uchumi wa viwanda na wakati mmeshindwa na mnajua haiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mnapowaita wawekezaji waje kuweze katika taifa letu na wakati umeme uliopo ni wa kukatika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa naona kuna Waziri amesimama. Naibu Waziri Mheshimiwa Stella Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa sababu alitaka kujua kama kuna Waziri anaweza akampa taarifa nataka nimwambie kwamba viwanda vinatumia umeme kwa *capacity* tofauti tofauti, si viwanda vyote lazima vitumie *megawatt* 2000. Hata sasa hivi tulivyo kuna viwanda tena vikubwa vinatumia *KVA* 500 tu. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kishoa, unaikubali taarifa hiyo?

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanzaje kupokea *taarifa tena ya kijinga namna hii?* (*Makof/ Kicheko*) (**Maneno Haya Si Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na unilindie muda wangu...

**MBUNGE FULANI:** Acha kutukana bwana.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, yaani katika taifa letu ikitokea mvua hata ya saa moja tu, umeme unakatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnapowaita wawekezaji waje kuwekeza na wakati umeme wenu ni wa kukatika na kuwaka, mnataka kuwaharibia mitambo yao? (*Makof*)

## **T A A R I F A**

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa kuna taarifa nyingine, Mheshimiwa Deo Sanga

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 68(7). Kwa mzungumzaji anayezungumza sasa hivi; ni lazima tuwe na nidhamu na kauli ndani ya Bunge. Afute kauli yake ya kumwambia Mheshimiwa Mbunge mwenzake na ni Waziri mjinga, lazima tukubaliane hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa ilikuwa atoe taarifa lakini anakuomba ufute hayo maneno ya kumuita Mheshimiwa Naibu Waziri mjinga.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamwita Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ni mjinga, nilichosema ni kwamba taarifa aliyotoa ndio ya namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika ...

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Kishoa kwa sababu hiyo taarifa kuna aliyeitoa, naomba ili tuweze kwenda vizuri wewe ondoa hilo neno la “taarifa ya kijinga”, sema tu huikubali taarifa tusonge mbele.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa, kwa kulinda muda wangu naomba niondoe maneno haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Serikali inayojipambanua kwamba ni Serikali ya viwanda kuna mambo ambayo yalipaswa kupewa kipaumbele. Mimi binafsi nimeunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais za kununua ndege pamoja na kujenga reli ya *standard gauge*, lakini katika Serikali inayojipambanua kwamba yenyewe ni ya viwanda hii haikuwa kipaumbele. Kipaumbele namba moja kilipaswa kuwa ni umeme, kilimo na mambo mengine

lakini kukimbilia kufanya mengine ndiyo maana mambo yanakuwa hayaendi. Niwashauri Waheshimiwa Mawaziri wamsaidie Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye skendo (*scandal*) kubwa sana ambayo nimewahi kuzungumza humu ndani na leo nairudia na nitairudia kwa ufupi tu. Nataka njue kauli ya mwisho ya Serikali kuhusiana na *capital gain tax* ambayo haijalipwa kwenye *transfer of shares* kutoka kampuni ya BG kwenda kanuni ya Shell. Hii nchi si shamba la bibi, hii nchi ina wananchi na hii nchi ni ya wananchi. Nataka kauli ya mwisho kutoka Serikalini, hizi fedha ambazo mpaka dakika hii hazijalipwa. Tatizo ni nini? Akina nani walihusika? Ni nani alivunja sheria hii na amechukuliwa hatua gani? Mheshimiwa Waziri na Naibu wake naomba majibu hapa kesho atakapohitimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Jesca Kishoa. Mheshimiwa James Milly atafuatiwa na Mheshimiwa Maulid Mtulia na Mheshimiwa Yussuf Kaiza Makame ajiandae.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza nianze kuwapongeza rika langu, ndugu zangu wote, ma-korianga popote walipo nchini kwa kufikia hatua ya muhimu ya maisha yao, tunakwenda kukabidhi madaraka. Hata hivyo, niwatakie heri wenzetu wale wa Kimnyak, Irkimayana kwa namna ambavyo wanapokea madaraka kutoka kwetu kwa mila za kimasaii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimshukuru kipekee Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kufika jimboni kwangu na kuniahidi jambo moja, kwamba VAT ya asilimia 18 inayotozwa kwa mnunuzi wa *tanzanite* kwenye soko huria itaondolewa. Nina imani kwamba Waziri anapokuja kuhitimisha hii VAT ataiongelea. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nisikitike pia kuhusu ruzuku, hamjatoa kwa wachimbaji wadogo wadogo wa

Mererani hususani akinamama ambao na wenyewe wana wawakilishi wao kila mahali wanajaribu kujipambanua katika suala la kiuchumi lakini wamefanya *application* na Wizara yenu hajatoa hata ruzuku moja kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niingie kwenye suala la *tanzanite*. Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ambayo na wewe unaifahamu imeweka bayana kwamba madini ya vito yatachimbwa na wazawa lakini leseni yoyote itakayotoka haitazidi *square* kilometra moja. Kwenye *application* iliyo fanyika 2013 *application* ya leseni HQP26116 ya *Tanzanite One* iliombwa Wizara kutoa leseni ya madini, wao wenyewe wamempa *square* kilometra 7.6 kinyume na sheria. Kuna majadiliano makubwa ya kisheria kati ya Wizara yako na watumishi, wengine wakikataa lakini kulikuwepo na shinikizo mwaka 2013 na ushahidi huo upo naomba niulete acheni kufisidi nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu mmemwelewa Mheshimiwa Tundu Lissu vibaya. Ninyi mnafahamu kesi ya *Dowans* tumepoteza kama nchi na kesi ya *Richmond* tumepoteza kama nchi. Mheshimiwa Rais, Wabunge wa Upinzani hawakatai kwamba kuna madudu nchi hii kuhusu mikataba lakini nendeni kwa *style* ambayo nchi haitapata hasara kwa baadaye. Eleweni hivyo Wabunge wenzangu wa CCM. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu *Tanzanite One* ilipewa leseni kinyume na masharti ya sheria na aliye hiusika katika hilo, aliyesaini leseni hiyo ni ndugu *Engineer Ally Samaje* na anajulikana yupo, naomba Serikali ifuatilie. Walichokifanya ndugu zangu, kwa sababu sheria ya 2010 inaruhusu ye yeyote anayechimba *mable na graphite* aruhusiwe kupewa takribani *square* kilometra 10; wakasema kwenye leseni yao hiyo wana-*apply mable na graphite* na si *tanzanite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ukienda kwenye *documentation* zote Kampuni ya *Tanzanite One* haijawahi hata siku moja kusafirisha nje *mable na graphite*. Ujanja huu ulitumika na ninyi mnatakiwa mwelewe nchi yetu

inavyoibiwa. Mtu anaomba leseni ya kitu kingine lakini anachimba kitu kingine, ipo kwenye *documentation*. Anaomba leseni ya *mable* na *graphite* lakini anakwenda kuchimba *tanzanite*. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nchi yetu inamalizwa; tusiposimama kama wananchi wanaopenda nchi hii, tutaimala nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, kampuni iliyoingia mkataba na Serikali 2013/2014 inaitwa *Sky Associate*, sasa huyo *Sky Associate* ni nani? Ni kampuni iliyoasajiliwa mahali panaitwa *Virgin Island* ambayo inafanya kazi zake Hong Kong. Kampuni hii haipo Tanzania na hajjasajiliwa Tanzania. Mheshimiwa Ngonyani anafahamu kwa sababu taarifa aliyotoa kwa umma wakati yupo Wizarani pale; Mheshimiwa Ngonyani aliwaambia watu kwamba ndugu Faisal Juma Shabash ambaye ni Mtanzania anamilliki asilimia 25, alisema Hussein Gonga anamilliki asilimia 35, Ridhiwan Urah, si huyu Ridhiwan anamilliki asilimia 40. Hakuna popote, si *T/C*, sio kwenye usajili wetu wa makampuni Tanzania, watu hawa wanaonekana. Hii kampuni ni ya kitapeli na Serikali inawalinda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu lingine, hawa jamaa wanafanya minada. Kampuni hii ya *Tanzanite One* imeuzwa kwenda *Sky Associate* kwa dola milioni tano ya kulipana kwa mafungu. Minada miwili waliyofanya Agosti na Februari wameuza takribani dola millioni saba...

**MHE.HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, taarifa.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa tarifa ndugu yangu James Millya, kwamba kwa kuwa yeye katika maelezo yake anakiri *Tanzanite One* mchezo unaoendelea ni wizi. Ningewombwa katika hotuba

yake tu atumie fursa hii vile vile kumwomba Mheshimiwa Rais atoe *Executive Order* mgodi ule usimamishe uzalishaji na utaratibu wa kisheria ufuatwe. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Ole Millya, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa mikono miwili, nimwombe Mheshimiwa Rais atumie mamlaka yake leo asimamishe uzalishaji wa kampuni hiyo, lakini na Mheshimiwa Ngonyani pia ashughulikiwe. Pia niombe *STAMICO* inayohusika kufisadi nchi yetu, wewe tulia... (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Halafu *declare interest.*

## T A R I F A

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani, taarifa

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, msemajii anayesema sasa hivi analipotosha Bunge. Kampuni ya *Sky Associate* si ya Tanzania, Kampuni ya *Sky Associate* ni kama alivyosema ni ya *Virgin Islands*. Pili Kampuni ya *Sky Associates* haikuwahi kununua hisa za kampuni ya Tanzania, Kampuni ya *Sky Associates* ilinunua hisa za kampuni ya Uingereza kwenye soko la hisa la Uingereza ambalo Tanzania hatuna *control* nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ambayo ilikuwa inamiliki hisa hizo ambazo zilinunuliwa na *Sky Associate* ni kampuni ya *Richland Resources*. Kampuni ya *Richland Resources* ndiyo iliyo kuwa inamiliki kwa asilimia 100 kupitia kampuni ya South Africa, Kampuni ya Mererani *Mining Limited*. Kwa hiyo, namwomba sana...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** ... ni vizuri akaangalia jinsi kampuni hizi zilivyoingia nchini na jinsi *transaction* hiyo ilivyofanyika badala ya kulipoteza Bunge hapa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Ole Millya unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niombe tu kwa heshima kwamba sipokei taarifa hiyo, lakini kwa sababu nimeomba Tume ya Rais iundwe na haya yote anayoyasema yataonekana kwa sababu kwa kawaida na yeye atahojiwa; haya yote atakuja kuyaeleza kwamba, je, kampuni hii ni ya Kitanzania au sio ya Kitanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naongea kitu kimoja, akanushe mtu yejote hisa hizo zimeuzwa kwa dola milioni tano tu, lakini kwa masoko ya Agosti 2016 na Februari watu hawa wameuza madini kwa milioni saba, tayari *almost* bilioni 16 na *capital gain* hawalipi, ndugu zangu nchi yetu inaibiwa sana. Hata hivyo, Kampuni ya *Tanzanite One Limited* imekuwa ikitoa taarifa za uongo kwa mbia mwenza, yaani *STAMICO* tangu alivyoanza uzalishaji wa *tanzanite* hapa nchini. Kwa mfano, kuanzia Julai 13 hadi Julai 16, *STAMICO* ameripoti mauzo ya jumla ya dola za kimarekani milioni 16 wakati kiukweli ni milioni 17, tayari kuna dola *almost* kati ya milioni moja mpaka laki kadhaa zinaibiwa, ndiyo maana tunasema watu hawa wanaiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hilo halitoshi, minada inayoandaliwa yote, nilimwandikia barua Kamishna Msaidizi wa Madini pale Arusha, ndugu Ali Adam, tarehe 20 mwezi wa pili 2017, kwamba ninaomba uniambie tenda ya kwanza na tenda ya pili waliyouziwa madini yetu kwenye tenda ni akina nani? Alichonijibu *officially*, tarehe 24 Februari, ipo kwenye *documentation* na barua imegongwa; wameuziwa *Gemoro Company Limited*, kampuni ya India, *Viber Global*

*Limited* Kampuni ya India, Kala Jewels Kampuni ya India, Shree Narayan Gems ya India, hiyo ni tenda ya kwanza. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, tenda ya pili ameuziwa **Arwi International** ya India, Shree Narayanya India na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge watu hawa wote wana mahusiano ya karibu na kampuni ambayo imesajiliwa Virgin Island inayofanya kazi zake Hong Kong. Waheshimiwa Wabunge nchi yetu inaibiwa, ni muda muafaka madini haya ya *tanzanite* wengi wenu hamyafahamu, ni madini ambayo yangeweza kubadilisha maisha ya watu wa Simanjiro lakini yangeweza kubadilisha maisha ya watanzania wengi. Ninaomba kwa ukubwa wetu tuingilie jambo hili. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika ...

*(Hapa kengele illila kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James muda wako umeisha, zilishagonga zote mbili, hawa hapa ndio watunza muda, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Maulid Said Mtulia atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Kaiza Makame ambaye atachangia kwa dakika tano na Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib atakayechangia pia kwa dakika tano.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwiningi wa rehema kwa kunijalia kuwa na afya njema na kupata fursa hii ya kuchangia katika mjadala huu muhimu sana. Pili, nitoe mkono wa Baraka na kuwatakia *Ramadhan Mubarak Waislam* wote na hasa wa Jimbo la Kinondoni na Tanzania kwa ujumla. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili la Ramadhan vile vile niseme kwamba katika kupeana mkono wa baraka, ndugu zetu, kwa taarifa nilizonazo Zanzibar na hasa Pemba

kuna uhaba mkubwa wa nafaka, kwa maana ya viazi mbatata pamoja na mihogo. Mheshimiwa Mwijage kwa sababu ni Waziri wa Biashara anasikia hili achukue fursa kuwashakikishia wafanya biashara wetu wa bara wanajitahidi kupeleka vyakula haraka iwezekanavyo ili kupunguza ugumu huu na Ramadhan iwe nyepesi kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mwijage kwa usomaji mzuri wa taarifa ya bajeti na niombé mzee wa uchumi wa diplomasia kama wakati mwingine akiwa anamu-opt anaweza akafanya mambo yakawa mepesi sana, ameisoma vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati yangu, Mheshimiwa Dotto Biteko, kiongozi kijana, kamati yake iko makini na amesoma ripoti nzuri sana ambayo hata wachangiaji imewasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nizungumze, mimi mbunge wa Mjini na sina tatizo sana na REA I, II na III lakini mimi nina tatizo kubwa sana la bei ya umeme, tuna tatizo umeme ni bei juu sana. Bei juu ya umeme inatokana na gharama ya uzalishaji ambayo TANESCO wanaipata bila kusahau gharama za usambazaji. Hata hivyo, tuna umeme wa maji ambao gharama yake ni shilingi 36 tofauti na umeme wa gesi ambao ni shilingi 147na umeme wa mafuta tunaambiwa shilingi 368.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Wizara ya Fedha, Waziri Kivuli alisema kwamba umeme unanunuliwa kwa shilingi 500 na TANESCO wanaauza kwa shilingi 280.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia gharama hizi za uzalishaji kama tungetumia umeme wa maji na umeme wa gesi, gharama zetu za umeme zingeshuka kwa chini ya asilimia 50 ya sasa. Umeme wetu unakwenda juu sana, ni kwa sababu ya haya makampuni yanayozalisha umeme kwa njia ya dharura tulioingia mikataba, umeme wa mafuta, ni makampuni ambayo yananyonya sana nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna makampuni haya yanajulikana *Songas*, *Dowans*, *Pan African*; ni makampuni ambayo yanazalisha umeme kwa gharama kubwa na leo nimepata nafasi ya kuwauliza watendaji wetu, je, tukiacha kutumia umeme wa mafuta tukitumia umeme wa maji na gesi na njia nyingine hatuwezi ku-survive? Wanasema tunaweza, lakini tuna kikwazo kikubwa cha mikataba, mikataba tulioingia na makampuni ya uzalishaji umeme ni ya ajabu sana, ni mikataba ambayo mimi nashindwa, mikataba gani tunaingia, wataalam wetu wanaingiaje kwenye mikataba ambayo haina *room* ya kutoka? Hii ni ndoa ya aina gani? Au ndiyo ile ndoa wanayosema ya Kikatoliki?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunatamani na tunafikiria wataalam wetu wanapoingia kwenye mikataba waweke na mlango wa dharura wa kutoka, lakini leo mikataba yetu hii ukiingia, ukitoka, unapelekwa mahakamani. Nina habari kwamba *Dowans* wamesimamishiwa mkataba na wako mbio wanakwenda mahakamani na kuna hatari tukalipishwa pesa nyingi. Sasa kwa utaratibu huu nafikiri tatizo liko kwa watendaji na wataalam wetu. Inakuwaje mikataba tukiingia hatuwezi kutoka? Nafikiri hili jambo si sawa na kwa kweli umeme umekuwa ghali lakini sababu kubwa ni huu umeme wa mafuta ambao hatuwezi kujitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo *Songas* tungeweza kuachana nao, hatuwezi kwa sababu ya mikataba. Leo *Dowans* mnataka tuachane nao, hatuwezi kwa sababu ya mikataba. Leo *Pan African* tunataka kuachana nao hatuwezi kwa sababu ya mikataba. Hivi hii ni mikataba gani ambayo hawa wataalam wanaingiaje mikataba ambayo hatuna *room* ya kutoka? Napata taabu sana mimi hapa na kwa kweli kwa utaratibu huu nchi hii tutakuwa tunasokota kamba nyuma inaungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* ina deni kubwa linalofikia kiasi cha bilioni 800, inadaiwa. Kama *TANESCO* inadaiwa zaidi ya bilioni mia nane, lazima umeme upande na ili ushuke lazima tutoke kwenye mikataba hii. Kwa hiyo

Mheshimiwa Waziri aje kutueleza ni namna gani tutatoka kwenye hii mikataba ya kinyonyaji, mikataba ambayo inapandisha bei ya umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nimuunge mkono dada yangu, Mheshimiwa Najma leo amezungumza jambo zuri sana kuhusu Zanzibar. *TANESCO* inawa-treat ile Kampuni ya Umeme Zanzibar kana kwamba ni mtumiaji wa kawaida, wanamuuzia umeme kana kwamba wanamuuzza *Mr. Juma*, *Mr. Ali*, hawazingatii kwamba yule naye anakwenda kufanya biashara. Wanamtozea mpaka Kodi ya *VAT* wakati na yeye alipaswa atengeneze aweze kuiza aweke na kodi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono, ni vizuri wakapewa huo *u-agency*, au kama itashindikana wao wana uwezo wa kununua umeme wenyewe, wanunue kutoka katika makampuni yanayozalisha umeme wafanye *transfer* kwenda kwao Zanzibar ili na wao liwe ni shirika ambalo linaweza kujinunulia umeme kwa watengenezaji umeme na badala yake lisiwe shirika ambalo linapitisha umeme halafu linatozwa bei ya mtumiaji wa kawaida, hii siyo *fair*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka nilizungumze, tulikuwa katika bajeti ya maji, wachangiaji wengi hapa walivyochangia walionesha kwamba ili bajeti yetu ya maji ipate pesa nyangi tuongeze tozo kwenye mafuta, shilingi hamsini na mimi nilisema kuongeza tozo ya shilingi hamsini kwenye mafuta tafsiri yake hatumsaidii mwananchi wa kawaida, kwa sababu yeye atakwenda kuilipia hii kwenye upatikanaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikapendekeza kwamba, tuna hawa jamaa zetu wa *EWURA*, wao wanasi mamia vinasaba na juzi tu hapa kulikuwa na mchakato wa kumpata mzabuni wa vinasaba. Tenda imefanywa, makampuni yamejitokeza, makampuni matatu yaka-*qualify* kwa kutumia vigezo walivyoviweka *EWURA* na Makampuni yaliyo-*qualify* ilikuwa ni *SICPA*, *SGS* na kampuni nyingine ambayo jina lake sikulipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya makampuni ukiangalia tenda waliyoweka hii kampuni ambayo inaonekana imeshinda tenda bei yake ni kubwa. Nilipendekeza hapa, ni vizuri sasa watu wa *EWURA* wakaisaidia nchi kutafuta mkandarasi ambaye ame-tender kwa gharama ya chini ili... (*Makofi*)

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ajenda tatu tu za kuzungumza, ajenda ya kwanza ni huu mchanga wa dhahabu ambao kila mmoja anauzungumza. Ajenda ya pili ni ile sheria ambayo ilipitishwa na Bunge hili mwaka 2015 inayohusu mafuta na gesi na ajenda ya tatu ni hili deni la *ZECO* kwa *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mchanga; hapa hatuhitaji kunyoosheana vidole tena kama Bunge, hatuhitaji kunyoosheana vidole, hatuhitaji kuonesheana mchanga ulichukuliwa vipi au dhahabu iliibiwa vipi. Kinachohitajika sasa ni kuwa wamoja, hatuhitaji tena kukaa tofauti, kinachotakiwa tumeona kwamba tunaibiwa ni lazima Bunge liwe kitu kimoja, hatuhitaji kitu kingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu Mheshimiwa Profesa Muhongo kabeba wizi wote au uhanga wa miaka au nusu karne, miaka 50 tumekuwa tukiibiwa mhanga leo katolewa Mheshimiwa Profesa Sospeter

Muhongo, kaondoka. Mbuzi wa kafara kashaondoka na tulishajua nini tulichoibwa, tujitahidi tukae pamoja kwa ajili ya Taifa na manufaa ya watoto wetu wanaofuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri kwa Serikali; kwangu mimi na muono wangu, hii ni sehemu nzuri kabisa ya kuanzia. Haiwezekani unakuwa unaibiwa baadaye ukasema kwanza usizue mali iliyoibiwa utafute namna ulivyotayarisha kuibiwa. Kwanza ukamate mali, baadaye u..., haya, ila mkubali makofi haya myakubali kwamba ninyi ndio mliotuingiza katika wizi wa miaka 50 na hili mpige makofi. Kama mlivyoleta ndege, mkubali kwamba ninyi CCM au Serikali ya CCM ndio mliotupeleka kwenye wizi huu wa miaka 50; na mkisimama mjisifu na mkubali udhaifu wenu, hilo ni moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, nashauri mikataba, sheria na zile sera zote tuzilete Bungeni na zile zinazotakiwa kwenda kwenye mamlaka ya utendaji zifanyiwe marekebisho ili mambo haya yasijitokeze tena. Hata hivyo, tujenge *refinery* zetu wenyewe, kwa nini tunashindwa? Wameamua kuhamia Dodoma bila bajeti wameweza, kwa nini wanashindwa kujenga viwanda vya kuchakatia dhahabu yetu hapa? Kwa nini wanashindwa hili? Wamewalipa wafanyakazi wa Wizara ya Fedha milioni 10, 15, 20 wengine kuhamia Dodoma, wanashindwa ku-*maintain* hii mali yetu tuliyonayo? Hii ni *natural resources*, ikiondoka hakuna tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nashauri, kwa nchi za wenzetu wenyewe maono ya mbali wanajenga, kwa sababu hizi zikiondoka hazirudi tena, baada ya miaka 50, 55 hatuna tena hiki kitu. Kwa hiyo, tusije tukawaonesha wenzetu historia ya mashimo, tuwaoneshe kwamba tulikuwa na dhahabu, tulikuwa na *tanzanite*, tulikuwa na *whatever*, kwa hiyo hivi vyote vinatakiwa vifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie pia Sheria ya Gesi; Waheshimiwa Wabunge, Sheria ile ya Mafuta waliiingiza

mkenge Zanzibar na lazima wakubali na walivunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 102(1), Ibara ya 105(2), Ibara ya 106(3), zote walizivunja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Makame. Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Phillipo Mulugo.

**MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi. Niseme mapema tu kwamba leo nina saumu, kwa hiyo ule wasiwasi na mashaka kwamba kila atakayesimama hapa ataangusha nondo, mimi nina saumu, kwa hiyo nitazungumza kwa upole kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba nampongeza sana Mheshimiwa gwiji wa siasa, waliokuwa hawamfahamu Maalim Seif niwaambie kwamba yule ni gwiji wa siasa, pale chuo kikuu tena rekodi yake mpaka leo haijavunjwa, alifanya *Degree ya Political Science* pamoja na *International Relations*. Sasa wakati tunakuja Bungeni; nataka niwaondoe wasiwasi; alituita sisi akatufunda vizuri akatuambia kwamba mnakwenda huko lakini tunataka muwe Wabunge wastaarabu. Serikali inapofanya vizuri ipongezeni na inapofanya vibaya isemeni, ikosoeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi tulipokuwa katika kikao cha UKAWA, Mheshimiwa Mbewe akarudia maneno hayo hayo. Kwa hiyo niwaambie kwamba sisi Wapinzani tutasifu pale ambapo litafanyika jambo zuri, pale ambapo mtavurunda, msitegemee sisi tutawasifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri wameapa, tena kiapo cha Kikatiba kabisa cha kumshauri Mheshimiwa Rais, naomba hiyo kazi waifanye kwa ufanisi mkubwa. Wao kama *Cabinet* wana *collective responsibility*, wanatakiwa

wayaendee mambo ya kitaifa kwa pamoja, wanatakiwa wamshauri Mheshimiwa Rais kwa pamoja na kwa hekima. Isitokee wanakaa na Mheshimiwa Rais muda wote mpaka anaondoka madarakani halafu mmoja anakuja kusema kwamba mtu anatumia muda mwingi zaidi kwenda safari za nje kuliko kwenda kumsalimia mama yake. Hivi huu muda wote waliokuwa pamoja kama aliona kwamba hilo la kwenda safari za nje ni baya zaidi kuliko kwenda kumsalimia mama yake kwa nini hakusema mapema? Hilo ni la pili (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, niwape pole wananchi wa Tanzania hasa Tanzania Bara ambao Serikali, niseme kwa nia safi kabisa, walitegemea kuwaondolea matatizo mengi likiwemo la kukosa umeme katika maeneo yao. Kwa sababu nchi hii kabla ya Mradi wa *REA* ilikuwa imekatika mapande; pande la mijini pamoja na vijijini, huduma ya umeme ilikuwa iko mijini tu lakini vijijini kote kulikuwa giza tupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la kuanzisha Mradi huu wa *REA* ni suala zuri sana, lakini nalo limekumbwa na matatizo na moja katika matatizo hayo ni pale wakubwa wetu wanapotuambia kwamba wataulinda Muungano huu kwa gharama zote. Wananchi wa vijijini walikuwa wanategemea mradi wa *REA*, na mradi wa *REA* ulikuwa unategemea msaada mkubwa wa *MCC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huu msaada wa *MCC* umekosekana kwa sababu demokrasia hakuna, demokrasia haiheshimiwi, anayeingia kwenye uchaguzi akashinda siye anayepewa. Kwa hiyo, hili limewakwaza sana Watanzania Bara kwa ajili ya kupata umeme huu wa *MCC*, hilo ni la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Khatib, ahsante sana. Mheshimiwa Phillipo Mulogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Mheshimiwa Joseph Musukuma ajiandae. (*Makof*)

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua zote alizozichukua kuhusu masuala ya mchanga. Nakubaliana naye kabisa kwa asilimia 100 na tunasubiria hiyo Kamati nyingine ambayo inashughulika na masuala ya kiuchumi na sheria tuje tuone na yenye we itasema nini, halafu baada ya hapo twende mbele. Hata hivyo, kwa hatua mpaka hivi sasa tunavyosema nakubali kwa asilimia 100 kwamba Mheshimiwa Rais ni mzalendo sana katika nchi hii na anavaa kabisa uzalendo katika nchi hii kwa ajili ya kulitumikia Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nirudi kwenye masuala ya Jimbo langu la Songwe. Daima nikiwa nachangia hapa huwa nasema miaka yote, kwamba; sasa sijui nitumie neno Serikali kwa ujumla ama niseme tu Wizara hii; Wizara ya Nishati na Madini Jimbo la Songwe naona kama vile inapendelea. Mheshimiwa Mwijage utakumbuka ulipokuwa Naibu Waziri wa Wizara hii alifika jimboni kwangu, Kata ya Kanga na aliniahidi kunipa umeme na hivi nimwambie Kata ya Kanga umeme unawake kwa *initiatives* zako. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Jimbo la Songwe lina kata 18 na hivi ninavyosema kata sita angalau zina umeme na kata 12 hazina umeme. Hata hivyo, Waheshimiwa Mawaziri hawa wanashahau kwamba tulikuwa Mkao wa Mbeya zamani, sasa tuko Mkao wa Songwe. Kule kwa Mheshimiwa Mwambalaswa vijiji vingi vina umeme, kule Mbozi vijiji vingi vina umeme, kule Momba kwa Mheshimiwa Silinde vijiji vingi vina umeme, kasoro Jimbo la Songwe, kuna nini? Mheshimiwa Dkt. Kalemani, nimekwenda mara nydingi

sana ofisini kwake, nimekwenda kwenye dawati lake kumlalamikia, kwa nini Jimbo la Songwe hawatuletei umeme? Tumekosa nini mbele za Mungu?

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita nilichangia hapa kwenye Wizara ya Elimu, nikasema kwamba wenzetu kule, sisi wilaya mpya hatuna chochote, hatuna majengo ya wilaya, hatuna nyumba za watumishi, hatuna barabara ya lami, hatuna *VETA*, hatuna maji makao makuu ya wilaya, yaani kila kitu hatuna, hata umeme vijijini hatuna, yaani hata umeme tu tukose? Kwa kweli kesho nitakuwa mkali sana kwenye kushika shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijawahi kuwa mkali kwenye hilo, lakini kesho, Mheshimiwa Mwjjage, nitashika shilingi yake, kwa sababu yeye ameshawahidi kufika kwenye Jimbo langu, anawafahamu wananchi wangu na tulimpa na ng'ombe na mbuzi siku ile Mheshimiwa Mwjjage, tukamweka akawa Mtemi kwa sababu alifanya jambo zuri sana na alichangia na maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo Kata za Gua, Udinge, Kapalala, Mbangala, Manda, Namkukwe na Mpona na vijiji zaidi ya 30, hatuna umeme. Nimekwenda pale *REA* Makao Makuu kulalamika lakini mpaka leo umeme hakuna, kuna nini Songwe na ni mkoa mpya na ni wilaya mpya? Jamani naomba na sisi watufikirie tuweze kula keki ya Taifa na sisi, wanatunyanyasa mno, hatuna chochote, nalalamika kila siku hapa. Mwenzenu sina barabara, nimesema hapa, sina chochote, basi hata umeme wa *REA*. Naomba, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, nimemlalamikia sana kila siku nikija anasema atanipa mkandarasi, siwaoni hao wakandarasi wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu wamemweka kule Mbeya anayesimamia masuala ya nishati ya umeme Mkoa wa Songwe, hapatikani na Mheshimiwa Naibu Waziri, nimemlalamikia huyo mtu kwa nini wasimuwjibishe. Hataki kushirikiana na Wabunge wa Songwe masuala ya umeme

na anamfahamu na nilimpa na namba zake za simu, *please*, naombeni umeme. Safari hii na mimi sasa nitakuwa mkali, nimkuwa mpole mno, nitakuwa mkali sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Shanta Gold Mining* ambao kule kwetu wanajiita *New Luika Gold Mining*; kwa kweli watu wa madini hawa; ndiyo maana nimempongeza na Mheshimiwa Rais; watu hawa ni waongo sana. Mwaka wa jana amekuja Mheshimiwa Profesa Muhongo kwenye jimbo langu, tumekwenda kwenye Kijiji cha Saza, tumekubaliana na Mheshimiwa Dkt. Kalemani anajua, watu wa Kijiji cha Saza wamelalamika, kuna eneo la wachimbaji wadogo wadogo lakini watu wa *Shanta* wameliingilia eneo lile mpaka kwenye nyumba za wananchi, makaburi, miembe, miti, kila kitu kimekwenda *Shanta*, kwa nini.

Mheshimiwa Nailbu Spika, baada ya kumlalamikia Mheshimiwa Profesa Muhongo, wamekuja na Mheshimiwa Kandoro aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya mwaka jana wamefika pale, tumekaa vikao siku sita, tumehekumu kesi na watu wa *Shanta* wakashindwa mbele ya wanakijiji, mbele ya mkutano wa hadhara na *TBC* walionesha na mimi nilikuwepo pale. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri alitoa *ruling* pale pale, kwamba eneo hili tuwape wananchi, lakini mpaka leo sina barua inayowaonesha wananchi kwamba wamepata lile eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Kalemani na ye ye nakumbuka nilimwambia, naomba kesho aniambie, baada ya Waziri kutamka kwamba lile eneo ni la wananchi na wamuulize Mheshimiwa Profesa Muhongo popote huko alipo aseme baada ya pale nini kilichoendelea, nakwenda ofisini kila siku anasema subiri. Hawa watu wa *Shanta* wana nini? Wametoa nini huko?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya, juzi nilikuwa Jimboni, nimeuliza swali jana hapa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, nasema hivi; hawa watu wa *Shanta* hawa tena wamefunga tayari mto. Mto unatoka Rwika unakwenda Mbangala mpaka Maleza wamefunga kwa ajili ya wananchi wasipate maji,

kwa nini wanatuonea hivi jamani? Vijana wa Mbangala mpaka wakataka kufanya fujo lakini Polisi wakawaweka ndani, tunawaonea wananchi bure. Hawa watu wa madini ni waongo sana na mimi ndio maana sielewani nao kwa sababu ya hiyo toka mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu nilipomwambia Mheshimiwa Profesa Muhongo amekuja pale sasa na hilo eneo tumewanyang'anya, basi leo ni chuki ya Mbunge na wananchi hatuelewani kule Songwe. Naomba tafadhali sana, maji yafunguliwe la sivyo mimi nitakwenda jimboni kuwachukua watu wa Saza na kuwachukua watu wa Mbangala tukashirikiane tuchukue majembe na shoka tukatoboe lile bwawa ili na mimi mje mnipige, mnifunge, haiwezekani kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba wameweka na kijji lakini ni mikataba feki; na wamesema wao wenye kwamba; mikataba tumeweka, hamuwezi kutufanya chochote kwa sababu sisi Serikali inatulinda. Tafadhali sana Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, nawaomba suala hili walitamkie kesho watu wa *Ashanti* watoboe lile bwawa na wananchi wangu waweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo wala siwezi kuchangia mambo mengi sana, naomba tupate...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzunguzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILIP A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Lakini usiende kuwakusanya hao wananchi tafadhali, kwa sababu ni kosa Kisheria.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea hawa Wabunge waliosalia kwa muda tulionao watachangia dakika tano tano. Mheshimiwa Costantine Kanyasu atafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia ajiandae

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ujasiri mkubwa na hasa kwa sababu mimi na Mheshimiwa Rais mwenyewe tunatoka kwenye mkoa ambao hawa wachimbaji wa dhahabu kwa kweli wanatuachia mashimo matupu na watu wanaendelea kuwa maskini. Kwa hiyo, hizi jitihada za Mheshimiwa Rais tunaziunga mkono, tunampongeza sana na wananchi wa Mkoa wa Geita kimsingi ambao wameshuhudia miaka 19 dhahabu inachimbwa lakini Makao Makuu ya Mji wa Geita hakuna barabara, Makao Makuu ya Mji wa Geita hakuna maji, hospitalini hakuna wodi, shule watoto wanakaa chini kilometra moja kutoka kwenye mgodi pale watu ni maskini sana; wanaona juhudhi hizi za Mheshimiwa Rais zinatakiwa kuungwa mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nawashangaa sana wenzangu hawa ambao wanapinga kwa sababu kama walivyosema wenzangu huko nyuma, walikuwa kila siku wanalalamika wanasema kwamba nchi hii inaibiwa...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** ...lakini nataka kusema kwamba Mheshimiwa Rais aendele...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** ...na ikiwezekana na aangalie pia katika maeneo mengine ambapo Mheshimiwa Rais aangalie machimbo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika bahati mbaya muda wetu umekwisha sana, kwa hiyo, hakutakuwa na taarifa isipokuwa kuhusu utaratibu. Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza nataka nimkumbushe Mheshimiwa Mnyika katika ukurasa wake wa saba amezungumzia kwamba Serikali iliingia mkataba wa *loyalty* wa *four percent*. Hii ni *four percent* siyo ya *force declaration*. Unapofanya *force declaration*, *four percent* yejote haina maana yoyote ile kwa sababu unazungumzia *four percent* ya *valuegani*? Hawa watu wanafanya *four percent* ya uongo halafu wanakuja kuwatetea hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine la pili; nilikuwa namshangaa sana Mheshimiwa Mnyika kwenye ukurasa wake wa tisa anasema kwamba taswira ya Tanzania kwenye jarida moja huko la *Mining journal/inasema trouble in Tanzania* kwa sababu Rais ameanza kufuatilia wizi, *so what? Trouble, yes* kuna wizi unagundulika, unataka Rais asigundue wizi? Lazima ili hii...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** ...lazima Mheshimiwa Rais afuatilie kwa sababu unaposema *trouble in Tanzania*, kama kuna wizi umegundulika lazima Rais afuatilie sasa mimi nakushangaa unapo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Mnyika utaratibu kikanuni.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mse maji anayezungumza hasemi ukweli. Yeye anazungumzia...

**WABUNGE FULANI:** Kanuni!!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mnataka Kanuni?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hivi unaniuliza mimi kuhusu Kanuni? Kanuni ya 63 na Kanuni ya 64 sawa sawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika zungumza na Kiti muda wetu umekwisha kama nilivyokwambia ulivyo simama mwanzo, kwa hiyo zungumza na kitili tusipoteze muda.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, msemaji anazungumzia mgodi wa Geita, mgodi wa *GGM*. Mgodi wa *GGM* hausafirishi makinikia ya dhahabu nje ya nchi. Kwa hiyo, wizi anaousema kwamba Rais ameufuatilia hauhusu kabisa yaani anasema uongo hauhusu kabisa mgodi wa *GGM* na ndiyo maana sisi wengine tunasema mgodi wa *GGM*...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika umesema mwenyewe kwamba kanuni unazifahamu vizuri. Kanuni inayohusu yeye kuzungumza uongo wewe unajua unapaswa kulileta kwangu ili mimi niamue namna gani. Sasa hicho unachosema hapo huoneshi namna gani yeye anavyodanganya na ni Kanuni gani nitajie ili mimi sasa niweze kutoa *rulling* kwenye huo utaratibu unaouomba, sekunde moja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Nimekwisha kwambia ni Kanuni ya 63 na 64 juu ya kusema uongo Bungeni. Kanuni ya 63...

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Mnyika . Naomba ukae, kaa chini nimeshasimama, kaa. Naomba uzime hiyo *microphone* yako Mheshimiwa Mnyika.

Waheshimiwa Wabunge, nilishawahi kusema hapa narudia tena; ukitumia kanuni ya 63 kwamba mtu anazungumza uongo maana yake wewe uoneshe kwanza; wewe ndiyo unayetakiwa kuonesha namna anavyozungumza uongo. Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, mimi niko hapa wala sijasinzia kama Wabunge

wengine, Mheshimiwa alipokuwa anachangia ametaja Mkao wa Geita hajataja neno uchimbaji wa madini kwenye mgodi wa Geita *Gold Mine* hajataja kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mnyika naomba utulie; nitampa nafasi Mheshimiwa Kanyasu aendelee na mchango wake kwa sababu hayo maneno Mheshimiwa Mnyika unayosema amezungumza uongo Mheshimiwa Kanyasu hajasema, kasema Mkao wa Geita na ameendelea na mchango wake hajautaja mgodi wa Geita. Mheshimiwa Kanyasu malizia mchango wako.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ungenipa nafasi ya kueleza uongo.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ulichosema ni sahihi na namshangaa sana ndugu yangu hapa mimi nazungumzia *issue* katika *general/yake* yeye anajaribu kwenda katika eneo dogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sababu ya muda, kuna mzungumzaji pia mmoja amezungumzia kwamba uzalishaji wa umeme umepungua, nilitaka aende kwenye ukurasa wa 21 ataona mahitaji ya umeme ndiyo yaliyoongezeka kutoka *megawats* 1,026 kwenda *megawats* 1,051, lakini uzalishaji wetu ni *megawats* 1,450.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuishukuru sana Wizara hii. Geita tulikuwa tuna matatizo makubwa sana ya umeme, unakatika kila siku; hivi ninavyozungumza sasa hivi umeme wa Geita haukatiki, umeme wa Geita uko imara na ninachowaomba tu sasa hivi ni kuhakikisha sasa umeme huu kama ahadi ambavyo ilikuwa kwamba vijiji ambavyo vilikuwa havijapata umeme wa *REA* vinapata. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kusema hapa ni kwamba pamoja na umeme wa Geita

kutokatika, lipo tatizo ambalo nilimwambia Mheshmiwa Naibu Waziri kwamba *TANESCO* hawana vifaa. Kwa hiyo watu wanapoomba umeme wanachukua muda mrefu sana kupata *connection* ya umeme; hivyo nadhani pamoja na juhudzi za *REA TANESCO* wakae upya wafikirie namna ambavyo wanaweza kuongeza mtaji. Kama *TANESCO* wameshindwa kuwa na vifaa vya kutosha kwenye *store*, ni vizuri wakaruhusu *vendors* wengine wakawa na vitu hivi kwenye maduka na wao wa-*control quality* kuliko ilivyo sasa, mteja ameomba umeme leo anafungiwa mwezi wa 10 kwa sababu wewe huna *meter*, kwa sababu wewe huna waya wakati soko hili ni soko huria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ushauri wangu. Nakushukuru sana kunipa nafasi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, dakika tano ni kidogo, ningemwomba dada yangu Hawa Ghasia akaniachia sijui kama atakubali.

**WABUNGE FULANI:** Amekubali.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Amekubali, kwa hiyo dakika 10, nakushukuru sana dada yangu (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa ujasiri aliouonesha kwenye makinikia hayo yaliyoshikwa huko bandarini. Pia nimpongeze kwa ujasiri na kwa bahati mbaya leo Profesa Muhongo hayupo hapa, nilitaka nimkaribishe darasa la saba huwa tunakaa huku ili tuwe tunamfundisha hali halisi ya Watanzania tunayoina kule majimboni, tukaachana na ule u-profesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi humu wanaopiga kelele wamekaa na wawekezaji na wengine

hata dhahabu hawaijui. Wanasema hatujaisoma Sheria ya Madini lakini ye ye hajawahi hata kuona madini, anamiliki nyanya, kwa hiyo hivi vitu bora akakaa ili tuzungumze watu tulio na uchungu. Iringa na dhahabu wapi na wapi? Huyu mtu anamiliki nyanya, kuku na mbwa halafu anakuja kuanza kujadili vitu nya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie rafiki yangu msomi kabisa tuachane suala la mchanga; anifafanulie na aelewé wizi ambaó uko kwenye migodi hii mikubwa. Ukienda kwenye uhalisia...

### **MBUNGE FULANI:** Taarifa

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** ...kwenye hii migodi ya *North Mara* ukienda Buzwagi, ukienda Kahama *Mining* kote kuliko na migodi hii kuna kanembo kadogo kameandikwa *ACACIA*; na *ACACIA* ana hisa asilimia 21 kila mgodi na ameziua kule Uingereza amepata Dola bilioni 275 na Serikali yetu *TRA* wakaenda kudai kodi, akawaambia mimi sina file kwenu, tumeshinda kesi amekata rufaa. Sasa alichokiuza kule Uingereza ameza nini? si ameza *North Mara* ya *Mara*, ameza *ACACIA*, ameza Buzwagi ya Kahama, ameza Kakola? Sasa hawa watu wana kesi nyingi na ndiyo maana Mheshimiwa Rais amesema tuwachunguze. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kingine, suala hili siyo la Bunge, ni Mbunge gani aliyeendumu kama tunaibiwa ule mchanga pale? Ni Mheshimiwa Rais na jitihada zake, acheni akamilishe Tume atuletee humu ndani. Tunaacha kushughulika na mambo ambayo tumelipwa posho kuzunguka kama Kamati tukayaibua sisi wenyewe, mtu kaibua mwenyewe, hajakamilisha uchunguzi wake, ninyi mnaanza kusema anafukuza wawekezaji, anawafukuza wapi? Hii ni mifano tu, hili Bunge siyo lile mlilozoea kwamba mnakaa kule nyie wenyewe midomo, mnapewa hela kuja kutupigisha makofi, mtazirudisha *time* hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wenzangu hawa upinzani wengine humu ndani mnapiga makofi bure wenzenu wamekula hela Morena pale mnataka tuwataje? Acheni watu wafanye uchunguzi...

**MBUNGE FULANI:** Taja

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** .....tufike mahali Rais atoe mwelekeo. Rais ndiyo ameshika makontena wala hayakushikwa na Tundu Lissu. Nawashangaa Wanasheria mimi siyo Mwanasheria huyu ndiyo Rais. Dira ya Wanasheria wetu inayoongozwa na Rais Tundu Lissu ndiyo hiyo ya kupingana na sisi tunaibiwa? Naomba sana hawa vijana watulie Mheshimiwa Rais afanye kazi, kile ni kichwa acha kishike na mtashikwa na mengine zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli huu mchanga wanavyosema wenzetu kwamba ukipelekwa kule *Japan* wao wanatoa madini ya aina tatu; wanatoa dhahabu, *copperna silver*. Sasa uchunguzi tu wala hatuhitaji Maprofesa waliohangainka na wanaoendelea kupiga maneno humu ndani, watupeleke kule *Japan* wakatuoneshe ule mchanga baada ya kutoa yale madini matatu ule mchanga una madini 32 ule unaobaki una nini? Kama una mali tuuze basi kule *Japan* hata kama wameyafyatua matofali si tutavunja tu hivi, tunapima, tunapata yale madini yetu? Tunapiga hesabu kubwa ambazo hawa hawaelewii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natokea kwenye hiyo migodi mikubwa, nataka niwaambie ambao hawaijui hata dhahabu. Tunanunua mfuko mmoja wakati hawajaanza kusafirisha na bunduki, vijana walikuwa wanazunguka na wale madereva ukiuziwa kamfuko kamoja karambo ka-Azam kale Sh.800,000 unapata Sh.16,000,000 na tulikuwa tunaiba kweli na watu wamepata hela. Sasa kama hakuna dhahabu kwa nini wanasantikiza na Mapolisi mbele na nyuma na makontena yale yanalindwa hata yakiwa bandarini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie Watanzania wajue na kama ingekuwa Mheshimiwa Rais

anaweza kupokea ushauri wangu; hawa wanaobwabwaja huku tukawaruhusu wakafanye mikutano kule Kanda ya Ziwa, hamtarudi ninyi, hamjui shida tulizonazo. Tumeibowi va kutosha, tumuache Mheshimiwa Rais afanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Ole Milya kwa sababu ye ye anajua maana ya *Tanzanite*, anajua tunavyohaingaika, ameunga mkono, achana na hao watu, mtu wa Dar es Salaam na dhahabu wapi na wapi? Mnyika anamiliiki mtambo wa kujengea nyumba, hakuna kitu, hawa wanatusumbua...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Watuache, tumemwamini Mheshimiwa Rais afanye kazi

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Muhongo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Waitara kuhusu utaratibu kanuni?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru natumia Kanuni ya 68(7) lakini pia isomwe pamoja na Kanuni ya...

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya 68(7) inahusu Mwongozo, umeomba Kuhusu Utaratibu, taja Kanuni.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Kanuni ya 64(1)(a)

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kaa chini!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, 64(1) (a).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika wewe ambaye unazijua sana Kanuni, Mbunge mwenzio ametajwa jina anazungumza kuhusu utaratibu na wewe unasimama kuhusu utaratibu, sasa unampa utaratibu yule ama yule? Sasa kama unataka kumwambia yeze kakosea Kanuni subiri nimalizane naye mimi kwa sababu yeze anazungumza na mimi. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Kanuni ya 68(1) isomwe sambamba na Kanuni ya 64(1) (a) kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba Mheshimiwa Musukuma amesema hapa kwamba kuna watu wamepokea fedha kule Morena na wanapiga kelele inaangukia kwenye Kanuni ya 64(1) (a) hayo maneno aliyoyasema kama ni ukweli athibitishe na kama si kweli ayafute maana hizo ni tuhuma. Anachafua Bunge hili kwamba kuna watu wamepokea rushwa kuja kubadilisha maneno humu ndani.

**MBUNGE FULANI:** Ataje majina! Taja!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Waitara amesimama kuhusu utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1) akisema kwamba kanuni ya 64(1) (a) ndiyo anayotumia, kwamba:-

*"Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli"*

Kanuni ya 64(a) inamtaka Mheshimiwa huyu kwa sababu maana yake ni kwamba hizi taarifa hazina ukweli, Mheshimiwa Waitara ungetupeleka kwenye Kanuni ya 63 inayohusu kutosema uongo Bungeni. Baada ya kutupeleka Kanuni ya 63 ungetimiza masharti yaliyoko hapo ili sasa Kiti kiweze kutoa maamuzi. Kwa sababu hiyo Kanuni uliyoisoma, kwamba Mbunge hatasema uongo Bungeni, Kanuni ya 63 inataka wewe kwanza ndiye uanze.

Nayasema haya kila wakati wewe ndiyo uoneshe yeye anadanganya vipi ili Kiti kitoe maamuzi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge Kanuni hizi tunavyozisoma tuzisome zote kwa pamoja.

Baada ya kusema hayo, tutamalizia na Mheshimiwa Musukuma muda wetu unakwisha watu wanakwenda kufuturu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waitara asifikiri mimi ni mwoga wa kupokea taarifa, kwa vile umefafanua nilikuwa *right* tu kuwataja, lakini nitawavumilia. Nimwambie tu kwamba, kwa vile yeye ameona nimesema uongo, anaweza akasimama yeye akatuambia kule *African dream* aliyelipa posho ni nani kwenye kile kikao kilichofanyika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaotoka kwenye machimbo tunaiomba Wizara ya Nishati na Madini, maeneo mengi yamemilikiwa na watu wanakaa Dar es Salaam wala hawayachimbi. Sisi tunapata shida kila mwaka kuomba Wabunge wa Geita na Mungu katupa neema hii. Mheshimiwa Waziri alikuja akatuambia mwezi wa Saba na wa Tisa kuna maeneo yanarudishwa kwa wananchi tunayasubiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nataka niwaambie wako wawekezaji wazawa wadogo tu wamewekeza zaidi ya bilioni 30 migodi kama ya *GGM* kwa nini Serikali na Wizara yake isiwakuze watu kama hawa? Uko mgodi wa Busolwa *Mining*, uko mgodi huko Bunda, kwa nini tusijaribu kuwakuza hawa tukaachana na hawa Wazungu wababaishaji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Geita siku moja ilikuja ile *helicopter* kuchukua dhahabu. Ilipofika pale wakazidishia tofauti na mkataba ulivyo, akakataa kurusha *helicopter*, lakini *TMAA* hawa walikuwa wamegonga dhahabu iende kwa kiwango kile kile. Kwa hiyo, hawa wanaopiga kelele hawaelewi jamani nchi inaibiwa wajaribu kuja kututembelea

wenzenu tunaachiwa mahandaki. Naliomba Bunge tumuachie Rais kazi hii aimalize, potelea mbali hata kama tunashtakiwa kwani Sheria ni *ruler* au ni *glass* kwamba ikidondoka itavunjika? Tukishtakiwa...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** ...Kwani Tundu Lissu asiposhtakiwa ana kazi gani? Wanasheria wetu watafanya kazi tuiachie Serikali na tumuachie Rais, sisi kama Bunge tumuunge mkono.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** ...na mimi binafsi sijawahi kuona Rais wa ajabu kama Tundu Lissu, huyu ndiyo wa kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais hajawahi kuzuia *helicopter*, makinikia hayana uhusiano kabisa na ile *helicopter*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hamnyanyaswi, kasomeni tu hizi Kanuni, halafu msipende sana kuropoka humu ndani, wananchi wanajua ninyi ni viongozi wakubwa sana ndiyo maana mnaitwa Waheshimiwa. Msipende kuropoka na usipende kusema kitu ambacho huna uhakika nacho, kwa hiyo someni hizi Kanuni vizuri ili twende vizuri humu ndani maana tuko wengi sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tumefika mwisho wa michango yetu ya leo. Kuna majina ya Wabunge wa CCM.

Mheshimiwa Kubenea; Waheshimiwa Wabunge Kanuni hizi zinataka kwanza; Kiti kikisimama wewe unanyamaza kimya ndiyo Kanuni zetu tulizojitungia hilo ni

moja. La pili; usizungumze wakati mtu aliyeitwa Spika na Kanuni hizi, Spika maana yale *you speak so you don't speak when I am speaking, alright? (Makof)*

Ndiyo Kanuni zetu tulizozitunga ndivyo zinavyosema kwa hiyo tuzifuate, maana tumejiwekea utaratibu kama tunataka kuzibadilisha tutumie utaratibu wa kawaida tubadilishe. Tuwe tu na heshima ya kawaida kabisa, sisi wote humu ndani ni viongozi.

Kwa upande wa CCM majina yaliyokuwa yameletwa yalikuwa mengi, lakini kwa uwiano tumemaliza vizuri. Kwa hiyo, majina watakaochangia kwa upande wa CCM kesho ni Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Ajali Akbar, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia na mengine yatakayoongezeka kwa mujibu wa uwiano wa uchangiaji wa kesho.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho terehe 2Juni, 2017 asubuhi saa tatu kamili.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 2 Juni, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*